

Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA ISHIRINI

KIKAO CHA ISHIRINI NA TANO – TAREHE 12 JULAI, 2005

(Mkutano Ulianze Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI (K.n.y. WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA):

Taarifa ya Mwaka na Hesabu za Wakala wa Wakulima Wadogo wa Chai kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2004 (*The Annual Report and Accounts of the Tanzania Small Holder Tea Development Agency for the Year ended 30th June, 2004*).

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha 2005/2006.

MHE. HERBERT J. MNTANGI (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA):

Maoni ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha ulipita, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka 2005/2006.

MHE. ISAAC M. CHEYO - MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI:

Maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Nishati na Madini kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na Maoni yake kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa mwaka 2005/2006.

MASWALI NA MAJIBU

Na. 235

Kituo cha Afya - Jimbo la Muleba Kaskazini

MHE. NAZIR M. KARAMAGI (K.n.y. MHE. RUTH B. MSAFIRI) aliuliza:-

Kwa kuwa Jimbo la Muleba Kaskazini halina Hospitali ya Serikali wala Kituo chochote cha Afya hali inayofanya gharama za matibabu kuwa kubwa sana kwa wananchi wengi kuweza kuzimudu na kwa kuwa, Jimbo la Muleba Kaskazini lina eneo la Visiwa vyenye wakazi wa kudumu na kwa kuwa nilipochangia Hotuba ya Bajeti ya Wizara hii 2002/2003 nilipendekeza pamoja na mambo mengine na kuomba kwamba Jimbo hili lipatiwe walau vituo viwili vya Afya katika mwaka ujao 2003/2004 kwa lengo la kuwapunguzia wananchi gharama za Afya ambapo nilipendekeza kwa kutamka Zahanati za Izigo na Ibuga;

- (a) Je, Serikali imeanza kulifanyia kazi pendekerezo na ombi hilo la kuzipa hadhi ya Vituo vya Afya Zahanati za Izigo na Ibuga katika mwaka 2003/2004?
- (b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kuimarisha huduma za Afya katika Visiwa vya Bumbiire na Goziba kwa kuwapatia matibabu na dawa za kutosha?
- (c) Je, Serikali inafahamu kwamba Zahanati nyingi hufungwa baada ya saa 9:30 na hufunguliwa siku inayofuata hali ambayo hukosesha huduma wagonjwa katika kipindi hicho?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ruth Msafiri, Mbunge wa Muleba Kaskazini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Serikali tayari imeanza kuyafanyia kazi mapendekezo na maombi ya Mheshimiwa Mbunge, kwa kuzipa hadhi za Vituo vya Afya Zahanati za Izigo na Ibuga tangu mwaka 2003/2004. Kuanzia mwezi Februari 2004 Vituo hivyo vimeanza kupokea madawa (*drug kits*) zenyé hadhi ya Vituo vya Afya na kuongozwa na Waganga wasaidizi yaani *Clinical Officers*.

Vilevile ni vyema kueleza kwamba kwa kuwa Vituo hivi vimepandishwa hadhi kutoka Zahanati, ni dhahiri kwamba havina majengo ya kutosha. Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, inaendelea kuhamasisha wananchi na wahisani mbalimbali ili kushiriki kuongeza majengo yatakayotosheleza majukumu mapya ya Vituo hivyo.

(b) Mheshimiwa Spika, katika juhudini za Serikali kuimarisha huduma za afya kwenye visiwa vya Goziba na Bumbiire, tayari kuna zahanati katika kisiwa cha Bumbiire. Kutohana na vigezo vilivyopo katika utoaji wa huduma za afya, Kisiwa cha Goziba hakikidhi vigezo vya kuwa na zahanati. Hata hivyo kisiwa hicho hupata huduma za afya za mkoba (*mobile clinics*) kutoka zahanati ya Kisiwa cha Kerebe. Kwa kuwa Zahanati ya Kerebe inamilikiwa na Kanisa, Serikali inagharimia usafiri na posho kwa wafanyakazi wanaotoa huduma hiyo Kisiwani Goziba.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kwamba baadhi ya Zahanati Wilayani Muleba, hufungwa saa 9:30 na kufunguliwa asubuhi siku inayofuata. Hii ni kwa sababu Zahanati hizo hazina nyumba za kuishi watumishi karibu au katika maeneo ya zahanati hizo na pia upungufu wa watumishi unachangia tatizo hili kwani watumishi wachache waliopo wanapopumzika hakuna wengine wa kuwapangia zamu za kuendelea na kazi. Aidha, wakati Serikali inaendelea kuajiri watumishi ili watosheleze mahitaji, ni vyema wananchi na viongozi wao wakajipangia ili kujenga nyumba za watumishi katika maeneo ya kutolea huduma za afya.

MHE. NAZIR M. KARAMAGI: Mheshimiwa Spika, namshukuru Naibu Waziri kwa jibu lake zuri lenye matumaini kwa wananchi wa Muleba Kaskazini. Pamoja na hayo nina swali moja.

Tunajua kwamba matatizo ya afya yanakabili wananchi wengi humu Tanzania, kwa nini pasiwepo na Sera ya Serikali kila Jimbo liwe na hospitali moja ya Serikali ili kupunguza hayo matatizo na tukiangalia kama matatizo ya Muleba ni kama vile vile ya Bukoba Vijijini hatuna Hospitali ya Serikali, lakini kuna vituo kama Izimbia, Katoro vituo vya afya ambavyo tayari vina vigezo vya kuwa kama Hospitali. Kwa nini Serikali isivichukue vituo hivyo vikawa Hospitali za Serikali? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MIKOZA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Karamagi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni dhamira kwa kweli ya Serikali kama ambavyo tumekuwa tukisema mara nyingi kwamba tungelipenda kwa kiasi kikubwa kabisa matatizo ya afya yakapungua katika maeneo mbalimbali. Lakini tunakabili na mambo mengi ambayo inabidi yote twende nayo, lakini kubwa ni uchache wa fedha ambazo zinatakiwa ziongoze katika mazoezi haya. Kwa hiyo, nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge, kwamba kadri uwezo utakavyoongezeka tuna hakika kabisa kwa wale watakaokuwa na maeneo ambayo yanakidhi sifa za kupandishwa hadhi kuwa vituo vya afya au hospitali zoezi hili litafanyika tu. (*Makofi*)

MHE. PETER KABISA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa tatizo la ufunguzi wa zahanati kuanzia saa 12.00 asubuhi mpaka saa 9.00 linafanana sana na tatizo la zahanati ya Kigogo, ambako sasa hivi huduma zinatolewa kuanzia saa 12.00 asubuhi mpaka saa 12.00 jioni na usiku huwa huduma hizo hazipo na kwa vile Kata ya Kigogo huwa

inaathirika sana kwa maradhi ya mlipuko kama vile vile kipindupindu. Je, Serikali itakuwa tayari kuhakikisha kwamba zahanati ya Kigogo inapata huduma za masaa 24? Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIKOA: Mheshimiwa Spika, naomba tu nipokee rai yake tutashirikiana naye tuone namna ya kuweza kumaliza tatizo hili bila mgogoro mkubwa. (*Makofii*)

Na. 236

Lami kwa Barabara za Miji Midogo na za Vijijini.

MHE. HERBERT J. MNTANGI aliuliza:-

Kwa kuwa, jitihada za kuboresha barabara za Miji Midogo na Vijijini Halmashauri nyingi za Wilaya zimekosa uwezo wa kifedha kuziwekea lami barabara hizo ambazo ziliwahi kuwa za lami kama zile za Miji ya Muheza, Korogwe na miji mingine nchini na kwa kuwa, Serikali ilionyesha nia ya kusaidia kuzijenga upya barabara hizo ambazo zipo kwenye hali mbaya sana:-

- (a) Je, Serikali haioni kwamba ipo haja ya kuandaa na kutekeleza mpango wa kuzirudishia lami barabara hizo ambazo awali ziliwahi kuwa na lami?
- (b) Iwapo mpango huo upo. Je, jukumu la kusimamia utengenezaji wa barabara hizo utakuwa chini ya mamlaka gani?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Herbert James Mntangi, Mbunge wa Muheza, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, barabara zilizokuwa za lami Mkoani Tanga kwa ujumla kwa hazina lami zina jumla ya km. 98.8 ambapo Km. 1.5 zipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, Km. 94 zipo Manispaa ya Tanga na Halmashauri ya Lushoto km. 3.3. Uongozi wa Mkoa wa Tanga umekwishaona umuhimu wa kuzirudishia barabara hizo lami.

Halmashauri za Wilaya na Manispaa ya Tanga katika kikao cha Mkoa cha Bodi ya Barabara cha tarehe 30/10/2003 ziliagizwa kuandaa Bajeti ya ukarabati wa barabara hizo kwa kiwango cha lami na kuiwasilisha Serikali ili iweze kuingizwa kwenye mipango mbalimbali ya Serikali.

Aidha, agizo hilo baada ya kuwa limetekelawa limeonyesha kama ifuatavyo:-

- Halmashauri ya Wilaya ya Muheza itahitaji Tshs. 220,788,000/=;
- Manispaa ya Tanga itahitaji Tshs. Bilioni 1.025/=; na
- Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto Tshs. 244,760,000/=.

Hivyo, kwa ujumla Bajeti ya shilingi bilioni 1,490,548,000/= iliwasilishwa katika Serikali. Aidha, Ofisi yangu chini ya Mradi wa *N RTP* itafanya tafiti za matumizi ya lami nafuu *low cost seals* kwa ajili ya kuzirudishia lami barabara zilizokuwa na lami na kuziwekea lami barabara nzuri zinazotengenezeka ili kupunguza gharama za matengenezo.

(b) Kutokana na ukweli kwamba barabara hizo ni za Halmashauri na tayari Halmashauri zimeandaa mipango ya kukarabati barabara hizo, jukumu la kusimamia na utengenezaji pia ni la Halmashauri husika. Serikali itatoa fedha za matengenezo ya barabara hizo na jukumu la Halmashauri hizo itakuwa ni kuhakikisha fedha hizo zimetumika vizuri. (*Makofi*)

MHE. HERBERT J. MNTANGI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza swali kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa wakati barabara hizo zilipotengenezwa miji yetu hii ilikuwa ni midogo sana na kwa hivyo barabara zenyewe pia zilikuwa fupi. Je, Serikali imefikiria uwezekano wa kuziongezea urefu barabara hizo kutokana na kukua kwa kasi kwa miji yetu hii midogo?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza ndiyo ilipewa jukumu la kutazama uwezekano wa matengenezo ya barabara hizo naamini kwa swali la Mheshimiwa Herbert Mntangi Halmashauri hiyo bila shaka itakuwa imezingatia jambo hilo vile vile. Lakini kama halikufanyika bado ninashauri Halmashauri hiyo ikishirikiana na Mbunge wakae watazame ni nyongeza kiasi gani kinahitajika na kuwasilisha Bajeti yake Serikalini, Serikali itaona uwezekano wa jambo hilo kulingana na uwezo wa kifedha utakaopatikana.

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, kwa kuwa imedhihirika wazi kwamba uwezo wa Halmashauri zetu ni mdogo hauwezi kukidhi haja kwa maana ya kutengeneza barabara za Wilaya na za Vijijini na kwa kuwa suala la barabara ni nyeti na ni muhimu kwa ajili ya mawasiliano, Serikali haioni kwamba umefika wakati sasa wa kuangalia upya utengenezaji wa barabara kwa maana ya kwamba chombo kimoja tu kama vile *TANROAD* kipewe Mamlaka ya kutengeneza barabara kuanzia barabara Kuu, za Mkoa, za Wilaya na za Vijijini ili kuondoa hii kunyofoa fedha hapa peleka hapa na matengenezo ya barabara kama siyo mazuri.

Je, Serikali haioni kwamba wakati muafaka umefika *TANROADS* wapewe jukumu la kutengeneza barabara katika ngazi zote? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, suala la kubadilisha sera ya utengenezaji wa barabara za Halmashauri na Barabara Kuu na za Mikoa ziwe chini ya chombo kimoja inawezekana tu kwa kubadilisha sheria iliyounda *TANROADS*. Wanaoweza kubadilisha sheria ya iliyounda *TANROADS* ni Bunge lako Tukufu. (*Makofî*)

Na. 237

Mapunjo ya Posho, Mishahara na Nauli kwa Walimu

MHE. STEPHEN M. KAZI aliuliza:-

Kwa kuwa na kutokana na jinsi Tume ya Waziri Mkuu, ilivyofanya kazi ya kuhusiana na malalamiko ya walimu na namna maagizo yalivyotolewa ya kushughulikia jambo hilo malalamiko mengine yaliachwa nje na hadidu za rejea hususan mapunjo ya posho, mishahara na nauli kwa walimu ni ya kweli kama yalivyojitekeza kwa walimu wa Mwanza:-

(a) Je, ni lini Serikali itayamaliza matatizo hayo kabisa kwa kuwalipa walimu haki na madai yao?

(b) Je, athari za thamani ya fedha kwa malipo hayo yaliyocheleweshwa sana zitafidiwaje?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini , lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba mnamo Mwezi Agosti 2004 Mheshimiwa Waziri Mkuu, aliunda Tume iliyooongozwa na Mheshimiwa Omari Kwaangw' Mbunge wa Babati Mashariki, kwa ajili ya kuchunguza madai mbalimbali ya walimu. Aidha Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilikuwa imeunda Tume ya kuhakiki madai ya walimu na watumishi wengine wa Halmashauri.

Mheshimiwa Spika, hadidu za rejea zilizoainishwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa Tume aliyounda pamoja na ile iliyoundwa na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa zilizingatiwa. Kwa kiasi kikubwa maoni na hoja za malalamiko ya walimu kwa ujumla wake vilizingatiwa na katika kutekeleza kazi zake Tume zimejitahidi kujibu hoja hizo. Hivi sasa Serikali imeanza kuwalipa walimu madai yao mbalimbali kwa kadri yalivyojitekeza kwa walimu na Tume nilizozitaja hapa juu. Aidha madai ya walimu

yaliyohakikiwa kwa Mkoa wa Mwanza yanafikia Sh. 1,131,241,460.00 yakiwa na mchanganuo ufuatao:-

Uhamisho ni Sh. 915,527,737, fedha kwa ajili ya masomo Sh. 80,700,061, safari za kikazi Sh. 1,383,000, likizo sh. 43,491,318, gharama za matibabu sh. 39,945,956, posho ya ajira sh. 38,755,898, posho za chakula sh. 11,399,150 na madai ya waliofariki sh. 38, 340.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Wizara ya Fedha inaendesha zoezi la malipo kwa wahusika kwa uwazi zaidi kwa kutangaza wanaolipwa siku hadi siku. Hata hivyo, Serikali haijafunga milango yake kwa madai mengine yoyote ya ziada ambayo walimu wanaweza kuwa nayo na hata sasa tunaendelea kupokea maombi na madai mbalimbali.

(b) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba kumekuwepo na ucheleweshaji wa malipo ya watumishi mbalimbali wakiwemo walimu. Lakini kama nilivyoeleza katika sehemu (a) Serikali tayari imekwishaanza kushughulikia tatizo hili na kwa kweli kwa taratibu zilivyo sasa hatudhani kwamba suala la fidia kwa ucheleweshaji wa malipo hayo itakuwa ni halali kwa upande wa Serikali. (*Makofi*)

MHE. STEPHEN M. KAZI: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu yaliyojitokeza namshukuru sana Naibu Waziri, lakini suala hili na matatizo ya walimu hayajakamilika. Kwa kuwa sehemu kubwa ya malipo ambapo yamefanyika ni kuhusiana na malimbikizo ya mshahara. Haya madai yaliyobaki sehemu nyingi Mwanza walimu hawajapata. Kwa mfano ametoa mfano kwamba nauli ipo kama milioni moja, walimu ni wengi sana Mwanza, milioni ni Shilingi chache sana.

(a) Je, Serikali inasemaje kwamba itamaliza lini suala hili kabisa tunataka liishe? (*Makofi*)

(b) Kuna tatizo la walimu kudai kulipwa huu utaratibu mpya wa mafunzo, walimu wanapofanya mafunzo sehemu ya gharama inalipwa na Serikali huo ndiyo msimamo tuliuweka. Lakini wengi hawajalipwa na Waziri hakulitamka hili katika majibu yake. Je, hilo nalo watalipwa lini?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, madai haya ya walimu kama nilivyosema kupitia tume hizo ambazo nimezitaja nimesema yamezingatiwa kwa kiasi kikubwa. Lakini nimetamka wazi hapa kwamba milango ya Serikalini haijafungwa bado tunapokea madai mengine yoyote ambayo yanaweza kuwepo na yenewe yanaendelea kufanyiwa kazi.

Lakini nataka nisisitize tu kwamba madai haya yataonekana kwa sehemu kubwa yanaendelea na kuendelea kwa sababu hata baada ya malipo kufanyika bado Walimu na baadhi ya watumishi wanakuwa hawaridhiki na kile kilichotolewa na kuonekana kwamba wamepunjwa. Lakini taratibu zote zimezingatiwa kwa maana ya uhakiki unapowasilisha documents zako nyingine zinakubalika, nyingine hazikubaliki. Kwa hiyo, katika hali

hiyo walimu wasitegemee kwamba watapata kila kitu kama walivyokuwa wameomba, ni baada ya uhakiki ndipo unaweza ukalipwa kile unachostahili.

Pili, suala la fedha hizi kwa ajili ya mafunzo mimi nasema Mheshimiwa Stephen Kazi kwa upande mmoja wala siyo tatizo kubwa, lakini tatizo kwa Mwanza lipo kiasi cha kutosheleza wasilisha tu jambo hili kwetu rasmi nina hakika kabisa tutakusaidia kulisukuma mpaka liweze kumalizika. (*Makofi*)

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Spika, matatizo ya madai ya walimu ya yamekuwa ni sugu na kila siku tumekuwa tukieleza kwamba madeni yanalipwa lakini inaonekana kwamba Serikali haina utaratibu wa kusema sasa tatizo hili linatakiwa liishe. Je, Serikali ina mkakati gani kuhakikisha kwamba miaka ijayo matatizo haya hayataendelea? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kabuzi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Kabuzi, unayoyasema nina hakika na Wabunge wote ndivyo wanavyosema hivyo hivyo. Lakini nataka nikuhakikishie matamshi yaliyotaka hapa Serikalini yamekwishaanza kutekelezwa kwa maana kwamba kwa sasa tunachohangaika nacho ni malimbikizo ya madai mbalimbali ya huko nyuma na maagizo yameshatolewa kuambiwa Wakurugenzi wote hakuna kutoa mwanya wa jambo kama hili kutokea tena isipokuwa kama una fedha. Nataka nikuhakikishie kwa kweli kwa yoyote atakayekiuka maagizo haya ya Waziri tuna hakika kabisa hatua kali zitachukuliwa kwa sababu ni kero ambayo hata sisi kama Ofisi hatupendi kuiona inaendelea. (*Makofi*)

Na. 238

Mabango ya Matangazo Kando Kando ya Barabara.

MHE. KHAMIS AWESU ABOUD aliuliza:-

Kwa kuwa, yapo mabango ya matangazo ya biashara yaliyowekewa alama ya X kwa ajili ya kuyaondoa kwa sababu mbalimbali ikiwemo ya upanuzi wa barabara, ujenzi wa nyumba au kwa sababu yoyote ile ambayo Serikali inaona inafaa, yakiwa na alama hiyo na kwa kuwa, mabango mengine ni ya Serikali, mashirika mbalimbali na ya watu binafsi.

(a)Je, ni fedha kiasi gani kimetumika kama gharama za uwekaji alama mabango hayo kwa Tanzania nzima?

(b) Je, kiasi hicho cha fedha kama kingetumika kwa ujenzi wa barabara, zingejenga kilometa ngapi za barabara?

(c) Kama mabango hayo ni ya watu binafsi, Je, Serikali itawalipa gharama zao walizotumia katika kuweka mabango hayo?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Napenda kujibu swal la Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mbunge wa Mkanyageni lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, Sheria ya Barabara (*Highway Ordinance*) inakataza mtu yeote kujenga ndani ya hifadhi ya barabara, hivyo mabango ya matangazo ambayo yamejengwa ndani ya hifadhi ya barabara ni kinyume na sheria hiyo na lazima yaondolewe. Kutokana na weny mabango hayo kujenga ndani ya hifadhi ya barabara na kwa kuwa Wizara yangu ni mhusika wa kulinda hifadhi hiyo, kuweka alama ya “X” kwenye mabango hayo kunaashiria kuwa hayatakiwi kuwa pale. Kwa sasa hatuna takwimu ya gharama zilizotumika kuweka alama hiyo ya “X” kwenye ujenzi uliofanywa ndani ya Hifadhi ya Barabara kwa kuwa kazi bado inaendelea na itakapokamilika tutatoa gharama zake.

(b) Kama nilivyojibu sehemu (a) ya swal la Mheshimiwa Mbunge, fedha ambazo zingeokolewa kwa kutoweka alama “X” kwenye mabango ingesaidia kufanya shughuli zingine za maendeleo katika barabara zetu, lakini kutokana na ukiukwaji wa sheria hiyo inabidi zitumike kwa shughuli hiyo isiyo na tija. Ili fedha zetu ziweze kufanya kazi za maendeleo yanayoeleweka ni wajibu wa wananchi kuzingatia sheria za barabara.

(c) Mheshimiwa Spika, sheria iko wazi kuhusu hifadhi ya barabara, mtu anapoweka bango lake la matangazo kwenye hifadhi ya barabara anafanya hivyo kwa makusudi kuvunja sheria hivyo mtu kama huyo halipwi fidia yoyote kwa kuondoa bango hilo. Ila sheria inamtaka e ye ye ailipe Serikali kwa kuvunja sheria. (*Makofî*)

MHE. KHAMIS AWESU ABOUD: Mheshimiwa Spika, kama alivytangulia kusema kuwa mabango yamewekwa alama ya X sasa kwa kuwa mabango yamewekwa alama “X” lengo la Serikali naamini ni kuyaondoa kwa nini bado yapo si mngeyaondoa tu kwa vile mmeyaweke alama ya “X”? (*Makofî/Kicheko*)

La pili, wakati mabango yamewekwa barabarani hasa yale mabango ya watu binafsi ninachoamini kuwa kuna taasisi iliyohusika ambayo wamewaruhusu kuweka hayo mabango. Je, ni Taasisi ipi iliyowaruhusu na kama wameruhusu hawa waliowaruhusu kuweka hayo mabango watachukuliwa hatua gani? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, anayevunja sheria ni mwananchi na anayetakiwa kurekebisha sheria hiyo ni Serikali. Lakini inaporekebishwa sheria hiyo ni ili inaposimamia sheria hiyo, wanaotakiwa kujirekebisha ni hao hao wananchi.

Kwa kuwa mabango yamewekwa bila ridhaa ya Wizara, Wizara haihusiki kuyaondoa mabango hayo inamwambia mwenye mabango kaondoa mabango yake, hilo bango ulipoweka hapo siyo sahihi, ndiyo maana tunamwekea alama ya X. sasa yeze atajua kuliondoa na kuliweka. Sisi tukiliondoa tunakwenda kulitupa, lakini yeze kwake ni mali. Kwa hiyo, tunamwambia akaliondoa akaliweke kwingine.

Nani amewaruhusu, hakuna mtu aliyewaruhusu hawajaomba kibali kutoka kwetu wangeomba kibali kutoka Wizara ya Ujenzi tungewaambia ni sehemu gani ya kuweka mabango hayo. (*Makofî*)

MHE. JACKSON M. MAKWETTA: Mheshimiwa Spika, wale walioweka mabango wameruhusiwa na Halmashauri za Wilaya, kwa sababu kwa kuweka yale mabango wanalipia. Baada ya uamuzi huu yamebaki pale hawalipii kwa sababu yamekataliwa na Serikali Kuu kwa Halmashauri zinakosa fedha na huyu bado anatangaza mambo yake kinamna kwa sababu licha ya alama ya “X” bado yanasmeka.

Ni vizuri basi Serikali kwa kushirikiana na Serikali zake za Wilaya wakayaondoa wakatoa maagizo yaondolewe ili kuondoa uchafu huu wa alama ya “X” mahali popote ambapo yapo? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kama waliotaa ruhusa ni Halmashauri nawaomba Halmashauri wawaelekeze walioweka mabango haya kwenye barabara wayaondoe kwa sababu Halmashauri hawamiliki Hifadhi ya Barabara Kuu. Hifadhi ya Barabara Kuu zote zipo chini ya Wizara ya Ujenzi. (*Makofî*)

Na. 239

Kazi za Makandarasi

MHE. SEMINDU K. PAWA aliuliza:-

Kwa kuwa, Serikali imefanya kazi nzuri sana katika sekta ya barabara na madaraja nchini kote kupitia wizara ya Ujenzi na barabara nyingi za lami *trunk roads* zimejengwa:-

(a) Je, Serikali inapompa mkandarasi barabara kuu, kwa mfano ile ya Chalinze hadi Melela, kwa nini haimpi masharti kwamba asafishe nusu kilomita ya barabara ziingazio kwenye barabara kuu kama zile za Gwata – Ujembe hadi Kinonko, Mdaula – Kidugallo, Ubena – Ngerengere, Fulwe- Mikese, Mkambalani – Pangawe, Maseyu – Mazizi, Lubungo – Mikese na Fulwe – Newland?

(b) Je, kwa nini mkandarasi asitoe vibarua ndani ya Vijijini ambako barabara husika inapata?

NAIBU WAZIRI WA UJENZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swalii la Mheshimiwa Semindu K. Pawa, Mbunge wa Morogoro Kusini – Mashariki, lenye sehemu (a) na (b) naomba nitoe maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, nia ya Serikali ni kujenga kwa kiwango cha lami mtandao wote wa barabara kuu nchini na wakati huo huo kuhakikisha barabara zote za Mikoa na zile muhimu za Wilaya, Miji na Vitongoji zinakarabatiwa na kufanyiwa matengenezo muhimu ili ziweze kuitika vizuri katika majira yote ya mwaka.

Aidha ni nia ya Serikali pia ni kujenga uwezo wa ndani kifedha na kitaaluma vinavyohitajika katika kujenga na kuimarisha mtandao wa barabara zetu ili ziweze kuchangia kikamilifu katika mkakati mzima wa kupambana na umaskini yaani MKUKUTA.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo ya utangulizi sasa ninaomba kujibu swalii la Mheshimiwa Semindu K. Pawa, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, mtandao wa barabara nchini unasihamiwa na Mamlaka mbili kuu, nazo ni Wizara ya Ujenzi ambayo inasimamia barabara kuu na za Mikoa na Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambayo inasimamia barabara za Wilaya, Miji, Vijiji na Vitongoji. Hivyo utekelezaji wa ujenzi na ukarabati wa barabara kuu na zile za Mikoa unazingatia eneo la hifadhi ya barabara husika bila kuingilia mipaka na mamlaka nyine.

(b) Mheshimiwa Spika, katika kujenga taaluma na uwezo wa ndani wa kujitegemea, mikataba yetu kwa kuitia Sheria ya Kazi imeainisha wazi kwa kuwataka makandarasi kuajiri wazawa zaidi. Kwa mfano, katika mradi wa Chalinze-Melela kulikuwa na wastani wa wafanyakazi 780 kila mwezi kati ya hao asilimia 3 walikuwa ni wageni, asilimia 12 walikuwa akina mama wazawa na asilimia 85 wanaume wazawa. Wafanyakazi wengi walioajiriwa katika mradi huo walitoka Mikoa ya Pwani na Morogoro.

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kupata majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Waziri. Nina maswali madogo tu ya kusaidia barabara hizi ambazo zinatuhusu wote pamoja na Mheshimiwa Mwenegoha.

Swali la kwanza, kwa kuwa napongeza Wizara ya Ujenzi kwa kutoa fedha nydingi sana safari hii katika barabara mbalimbali nchini zikiwemo zile za barabara za Morogoro Vijijini ya Ubena-Ngerengere hadi Mkulazi na Kidunda ambayo kazi imeanza wiki ya jana.

Je, Wizara inaweza ikatusaidia lile daraja la pale Ubena ambalo lipo Jimbo la Chalinze inasaidia majimbo mawili na matatu ya kwetu Kusini na Kusini Mashariki pamoja na Kigalila, Buya na Ngerengere? Hiyo (a).

(b)Kwa kuwa mwaka jana niliomba mafuta kutoka Taasisi mbalimbali niliwaambia wasipitishie kwangu isionekane kuwa ni kampeni, wapitishie Wizara ya Ujenzi. Niliomba Taasisi nne. Niliomba Kanisa moja KKKT akiwepo Katibu Mkuu, Bwana Mwenegoha na pamoja na watu wengine ambao kama akina Patel na watu wengine. (*Makofi*)

Je, walipokea michango hiyo ya mafuta? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, kwanza kweli nakiri kwamba Wizara ya Ujenzi imetoa pesa kwa barabara ya Ubena, Ngerengere hadi Kidunda na imetoa pesa kwa barabara ya Ngerengere, Tununguo hadi Kiganila mpaka Mkulazi. Hiyo ninakiri. Lakini vile vile kuna daraja hapo la Ubena maelekezo yangu ni kama ifuatavyo:-

Halmashauri iandike hoja ya kuomba kutengenezewa daraja lile na Wizara ya Ujenzi. Wasitulee makadirio ya ajabu. Kwa sababu maombi yao ya kwanza yalitaka daraja lile litengenezwe kwa milioni 30 lakini jeshi wanaweza kutengeneza daraja lile kwa milioni 6. Sasa walete masahihisho kamili Wizara ya Ujenzi itafikiria kama ina pesa ya kutengeneza daraja hilo.

Ya pili, mafuta kokote kule ulikoomba Mheshimiwa Mbunge, tunakushukuru sana kwa kusaidia Wizara ya Ujenzi. Lakini tunaelekeza mafuta hayo Mheshimiwa Mbunge uwaelekeze uliowaomba wayapeleke Halmashauri kwa sababu hizo barabara zinazotengenezwa siyo za Wizara ya Ujenzi. Kwa hiyo, apeleke Halmashauri, Halmashauri watatumia katika kutengeneza barabara hizo.

MHE. MARIAM S. MFAKI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swalii dogo la nyongeza. Barabara zinazosimamiwa na Wizara pamoja na Mikoa wakati makondarasi wanapozitengeneza huwa mara zinakuwa na mashimo ya pembeni kwa ajili ya kuchimba na kutengeneza barabara. Huwa wanasimamia mpaka baada ya kumaliza barabara mashimo yale yanafukiwa na kuacha hali nzuri katika pembeni mwa barabara.

Lakini zipo barabara zinazosimamiwa na Halmashauri, wakati wanapotengeneza mifereji mara nyingi udongo uliochimbwa huwekwa pembeni mwa barabara na baada ya mifereji kutengenezwa udongo ule hubaki pale pale, matokeo yake wakati mvua zinaponyesha udongo ule unarudi tena kwenye mifereji ile na kuziba.

Mheshimiwa Spika, swalii. Je, Serikali iko tayari kuziagiza Halmashauri ili makondarasi wale wanapotengeneza hiyo mifereji udongo ule wauondoe na usambazwe ili usije ukarudi tena kwenye mifereji na kuziba mifereji hiyo? Ahsante. (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA UJENZI: Mheshimiwa Spika, ni kweli kama udongo ambao umechimbwa kwa kutengeneza mifereji na umewekwa pembeni ukiachwa hapo basi mvua zitakaponyesha udongo huo utarudi kwenye mifereji nakufanya mifereji kuziba. Kwa hiyo, wahakikishe ma-injinia wa Wilaya, wanaposimamia ujenzi wa barabara za Wilaya wahakikishe kwamba makandarasi wanaondoa udongo huo usirudi tena kwenye mifereji, ama siyo kazi itakayofanyika itakuwa ni kazi bure.

Na. 240

Hujuma katika Reli ya Manyoni - Singida

MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MHE. MGANA I. MSINDAI) aliuliza:-

Kwa kuwa kuna habari za kuaminika kwamba kuna watu wameanza kufanya hujuma kwa reli itokayo Manyoni – Singida kwa kung’oa viungio vyा mataruma na kuuza kwenye machimbo ya dhahabu huko Londoni:-

Je, Serikali inalifahamu jambo hilo, na kama inalifahamu ni hatua gani zimeshachukuliwa dhidi ya tatizo hilo?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swalı la Mheshimiwa Mgana Izumbe Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kuwa kuna watu wakorofi ambao wameanza kufanya hujuma kwenye reli itokayo Manyoni hadi Singida kwa kung’oa viungio vyा mataruma na kuviuza kwenye machimbo ya dhahabu huko Londoni.

Serikali imebaini kuwa, viungio hivyo hutumiwa na wachimbaji kupasulia mawe yenye dhahabu. Idadi ya viungo ambavyo vimeibiwa kwenye reli hii kwa nyakati tofauti imefikia 446.

Mheshimiwa Spika, katika kufuutilia wizi huo, tarehe 6/10/2004, Polisi walitumwa kwenda kuvamia eneo la Londoni na kufanikiwa kuwakamata watu 39 waliokutwa na viungio hivyo wakivitumia kupasulia mawe ya dhahabu. Jumla ya viungo 59 vilikamatwa na vimehifadhiwa kama vielelezo.

Upelelezi wa suala hili ulikamilika na watuhumiwa walifikishwa katika Mahakama ya Mkoa wa Singida tarehe 12/12/2004 wakikabiliwa na mashtaka ya kuharibu mali na kupatikana na mali ya wizi na kesi yao inaendelea.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue fursa hii kwa kujibu swalı la Mheshimiwa Msindai kwa kulieleza Bunge lako Tukufu kuhusu tatizo kubwa la wizi wa vifaa na hujuma inayofanywa kwenye reli ya Shirika la Reli Tanzania.

Katika mwaka 2004 jumla ya nguzo 651 na kilomita 409 za nyaya za simu ziliibiwaa. Hasara iliyopatikana ni shilingi 131 milioni. Mwaka 2004 huo huo kulikuwa na matukio 30 ya kuiba reli, mataruma na vishikizo. Shirika lilipata hasara ya shilingi milingi milioni 480 na ajali moja ya treni ilitokea. Jumla ya mabehewa 135 yalivunjwa na kusababisha madai ya shilingi 450 milioni kwa Shirika.

Shirika pia, kwa mwaka 2004 lilipata hasara ya shilingi milioni 600 kutokana na wizi wa mafuta kutoka kwenye vituo vyake vya mafuta na kwenye injini. Shirika vile vile lilipata hasara ya shilingi bilioni moja kutokana na wizi wa vifaa vya mabehewa kwa mwaka 2004, tatizo hili likiwa kwenye vituo vikubwa vya reli vya Dar es Salaam, Morogoro, Dodoma, Tabora na Mwanza. Kwa mwaka 2004 Shirika lilipata hasara ya jumla ya shilingi bilioni 2.66 kutokana na hujuma hizo.

Mheshimiwa Spika, katika kupambana na tatizo la hujuma hizi, Polisi na wafanyakazi wa reli wanaendelea kufanya doria za vijiji kando kando ya reli hiyo mara kwa mara.

Shirika pia kwa kutambua umuhimu wa wananchi katika ulinzi wa reli, limeingia mikataba ya ulinzi na vijiji hamsini na moja katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Morogoro, Dodoma, Tabora, Mwanza na Tanga.

Tunapenda kuwaomba raia wema wote waishio kando kando ya reli hiyo wasaidie kutoa taarifa pindi waonapo nyendo za watu wenye lengo la kufanya hujuma. Reli hii ni yetu, ipo kwa ajili yetu, hivyo inapaswa kulindwa na kutunzwa ili iweze kudumu na kuendelea kutuhudumia. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi chote cha miaka 5 cha uhai wa Bunge hili, naomba nirudie tena sehemu hiyo kwamba Mheshimiwa Mgana Msindai, Mbunge wa Iramba Mashariki, amekuwa mtetezi mkubwa wa wananchi wa Iramba Mashariki na Iramba yenye na Singida kwa ujumla, hasa kuhusu masuala ya miundombinu, ikiwa ni pamoja na reli, viwanja vya ndege na simu. (*Kicheko/Makofî*)

Mheshimiwa Spika, napenda nichukue nafasi hii kumshukuru kwa dhati. (*Makofî*)

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuuliza swali dogo kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa tuta la reli kutoka Manyoni kwenda Singida kuna maeneo mengi yametitia na kufanya mataruma kupinda.

Je, Serikali haioni kwamba kuna haja kufanya ukarabati wa reli hiyo ili treni iweze kwenda mwendo unaotakiwa ili iweze kufika Singida mapema kama ilivyopangiwa kinyume na sasa hivi treni hiyo inafika usiku wa manane?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, nakubaliana na yeche kwamba ni kweli kuna kutitia kwa sehemu fulani fulani za reli ya Manyoni-Singida. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kila wakati tunakuwa tunashindilia kwa kuweka kokoto.

Kwa hiyo, tutaendelea kufanya hivyo na kuboresha. Lakini nia yetu hapo baadaye ni kubadilisha zile reli ambazo ziko pauni ndogo kuweka pauni kubwa hali ya kifedha ya Shirika itakapoboresha.

Na. 241

Uwanja wa Ndege Kigoma

MHE. PHILEMON NDESAMBURO (K.n.y. MHE. DR. AMANI W.A. KABOUROU) aliuliza:-

Kwa kuwa Uwanja wa Ndege wa Kigoma umeteuliwa na Umoja wa Mataifa (*UN*) kuhudumia majeshi yake ya Amani yaliyoko *Congo (DRC)* na kwa kuwa huduma hiyo inahusisha ndege kubwa za mizigo zinazotua na kuruka mara kwa kadhaa uwanjani hapo na kusababisha uwanja huo kuharibika kwa kasi kubwa:-

- (a) Je, Serikali inafahamu kuwa uwanja huo umeharibika na kwa kiwango gani?
- (b) Je, ni kweli kwamba Umoja huo (*UN*) ulikubali kuukarabati uwanja huo kufikia katika kiwango cha Kimataifa lakini hadi sasa haujafanya hivyo?
- (c) Je, ni kweli kwamba Umoja huo ulikuwa tayari kuujenga uwanja huo lakini Serikali ikalazimisha kuwa fedha za ujenzi huo ziwasilishwe Serikalini badala ya kuuachia Umoja huo kufanya kazi hiyo kwa kutumia Mkandarasi wake na kwa sababu ya ubishi huo uwanja huo unazidi kuharibika na kuwa kero kwa watumiaji. Kero ambazo

pia zinaweza kusababisha ajali. Kama ni hivyo, kwa nini Serikali isimalize ubishi huo na kazi ikafanyika?

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla sijajibu swali la Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, napenda kutoa maelezo mafupi kuhusu kiwanja hicho kama ifuatavyo:-

Kiwanja cha ndege cha Kigoma kina miundombinu ya kukidhi kupokea ndege zenyе ukubwa wa *F.50* au *ATR 72* zenyе uwezo wa kubeba abiria kati ya 40 na 50 na uzito usiozidi tani 20. Umoja wa Mataifa katika kuhudumia majeshi yake yaliyoko *Congo (DRC)* umekuwa ukitumia kiwanja hicho kwa kuhusisha ndege aina ya *C 130* ambayo kwa uzito ni kubwa ukilinganisha na *F.50*. Kiwanja cha Kigoma kina urefu wa mita 1700. Baada ya maelezo hayo sasa napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Kabourou, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu kuwa hali ya njia ya kurukia na kutua ndege siyo ya kuridhisha kutokana na matumizi ya ndege kubwa kuzidi kiwango cha uimara wa njia hiyo.

Mheshimiwa Spika, katika mkataba ambao Serikali iliingia na Umoja wa Mataifa kuhusu Kitengo cha Umoja wa Mataifa cha kuhudumia majeshi ya Amani yaliyoko Jamhuri ya Kidemokrasia ya *Congo (MONUC)*, hakuna makubaliano yoyote ya *MONUC* kutengeneza kiwanja hicho. Hivyo basi *MONUC* haijatoa pesa kwa Serikali na Serikali haijawahi kuwalazimisha kupatiwa fedha wala kupokea fedha kutoka *MONUC* kwa ajili ya matengenezo ya kiwanja hicho. Hata hivyo baada ya kuona uharibifu uliotokea Serikali imefanya majadiliano na Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (*UNDP*) na *MONUC* kuhusu uwezekano wa wao kukifanya kiwanja hicho matengenezo mbali ya matengenezo ya dharura ambayo *MONUC* wenyewe na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege wamewahi kuyafanya.

MHE. PHILEMON NDESAMBUTO: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri lakini ningeomba kuuliza swali moja dogo. Kiwanja cha Kigoma kimeonyesha umuhimu wake kwa sababu ya kuhudumia wakimbizi. Lakini pia kiwanja kile kingeweza kupanuliwa kikawa ni kichocheo kikubwa cha utalii kwa sehemu ya kule. (*Makofî*)

Serikali haioni ilikuwa ni bora zaidi kukipanua kiwanja hiki na kuacha kutumbukiza pesa nyingi katika kiwanja cha Arusha ambapo *Kilimanjaro International Airport* iko kilometra 25 tu kutoka pale? (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, nakubaliana naye na Serikali inajua umuhimu wa kiwanja cha ndege cha Kigoma kwa uchumi wa nchi hii. Na ndiyo maana katika mipango ya mamlaka ya viwanja vya ndege kiwanja hiki kinapangiwa kuwekewa lami katika miaka mitano ijayo. Lakini

napenda nichukue nafasi hii nimwelezee Mheshimiwa Ndesamburo kwamba kiwanja cha Arusha nacho kina umuhimu wake vile vile. Kwa sababu kinachangia vile vile katika uchumi wa nchi hii. Ni kiwanja cha tatu ambacho kinaingiza mapato zaidi katika nchi hii.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kunipa nafasi hii niulize swal moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Ningependa tu kuelewa kama kuna mpango wowote wa kuingiza viwanja vidogo vya ndege kwenye mipango ya usafiri na uchukuzi ya Halmashauri za Wilaya kwa sababu kulikuwa na viwanja ambavyo vinatumika *Air Strips* kwa mfano pale Mombo kwa Mkoa wa Tanga, Wilaya ya Korogwe na Lushoto, halafu kule Ludewa kwa Mheshimiwa Kolimba, kule kuna kiwanja pale mwambao wa Ziwa Nyasa na ni muhimu sana hivi kwa ajili ya *emergency transport* hasa kunapotokea dharura na ghamama hizo iwe ile mipango kamili katika mipango ya wilaya badala ya kuiachia tu Serikali Kuu? Nashukuru sana.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge suala hili sisi tulilifkiria zamani kwamba kama Halmashauri wangeweza kuviendeleza viwanja hivi, sisi tungelifurahi sana na tulichukua hatua za kuwakabili wote kuona kwamba je, mnawenza tukupeni viwanja hivi muendeshe na wote jibu lao ni kwamba hawawezi kumudu kuendeleza viwanja. Pesa tunazozipata hazikidhi kutengeneza viwanja vyote vikubwa sembuse hivi vidogo. Lakini kama tutapata hela tuko tayari Serikali Kuu kuendelea na jukumu hilo.

Na. 242

Tatizo la Gari Sekondari ya Longido

MHE. LEKULE M. LAIZER aliuliza:-

Kwa kuwa Sekondari ya Longido ina wanafunzi zaidi ya 645 wa Bweni na haina gari la kuihudumia shule hiyo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuipatia shule hiyo gari ili litoe huduma hapo shulen?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu inayatambua matatizo ya ukosefu wa vyombo vya usafiri hasa magari uliopo katika shule nyingi za Sekondari za Serikali nchini ikiwemo Shule ya Sekondari ya Longido. Kutohana na uwezo mdogo wa Bajeti Serikali haina uwezo wa kununua magari kwa shule zake zote kwa wakati mmoja. Kati ya shule za sekondari 113 za bweni ni shule 49 tu ndizo zenye magari. Aidha Mkoa wa Arusha

wenye shule za sekondari 59 ni shule 9 tu zina magari. Magari hayo yamepangwa katika shule kwa kuzingatia hali ya kufikika, umbali kutoka barabara kuu na umbali kutoka makao makuu ya Wilaya.

Mheshimiwa Spika, wakati Serikali inaendelea kutafuta ufumbuzi wa tatizo hilo, utaratibu uliopo sasa ni gari lililopo katika shule moja ya sekondari kuhudumia pia na shule za sekondari zilizo jirani. Tutaendelea na utaratibu huu hadi tutakapokuwa tumefanikiwa kuzipatia shule zote magari. Kwa hiyo, Serikali itaipatia gari shule ya sekondari ya Longido na nyingine za aina hiyo kadri tutakavyokuwa na uwezo wa kununua magari na kuyagawa kwa kuzingatia mahitaji ya kila shule. Kwa sasa shule hiyo inaweza kuazimwa gari kwa matumizi ya muda kutoka Shule ya Sekondari iliyoko jirani ikiwa ni pamoja na Ilboru ambayo yenewe inalo gari.

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili ya nyongeza. Kwa kuwa Waziri alisema vigezo vinayosababisha shule hizo kupata magari ni pamoja na umbali wa shule kuwa mbali na makao makuu ya wilaya na Longido iko mbali sana na Makao Makuu ya Wilaya. Je, haoni kwamba inastahili kupata kwa sababu ya kigezo hicho?

Swali la pili, kwa kuwa Sekondari zote zilizoko Wilaya ya Monduli hazina magari, sekondari zote karibu 10 hawana magari. Je isingefaa kupewa Wilaya hiyo gari ili ihudumie shule zote 10 zilizoko katika Wilaya hiyo?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA K.n.y. WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI): Mheshimiwa Spika, bahati nzuri nimekaa na kufanya kazi mjini Arusha na nafahamu umbali ulioko kati ya Longido na Makao Makuu ya Wilaya ya Arusha. Nakubaliana naye kwamba kuna umbali mkubwa. Lakini tatizo la msingi ni lile tulilolisema uwezo wa kutoa gari kwa kila shule ya sekondari, uchumi wa nchi yetu haujatufikisha mahali hapo. Tutakapofika tutatekeleza wajibu wetu.

Kuhusu sekondari zote za Wilaya ya Monduli kwamba hakuna hata sekondari moja ilio na gari, ningependa niseme kwamba katika hali hiyo kwamba kati ya yale magari machache yanayopatikana, kwa kweli itabidi iangaliwe kwa namna yake kwamba Wilaya nzima sekondari zilizoko katika wilaya hiyo walau tutakapopata magari ipewe kipaumbele cha kupewa gari walau katika moja ya Sekondari za Wilaya hiyo. (*Makofi*)

Na. 243

Mikopo ya Ukarabati wa Matrekta

MHE. PASCHAL C. DEGERA aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali ilibuni utaratibu wa kutoa mikopo ya kukarabati matrekta mabovu ya wakulima nchini na kwa kuwa wakulima wengi wa Wilaya ya Kondoa wametuma maombi yao ya mikopo:-

Je, ni wakulima wangapi wa Wilaya ya Kondoa walipatiwa mikopo hiyo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swal la Mheshimiwa Paschal Degera, Mbunge wa Kondoa Kusini, kama ifuatavyo:-

Hadi mwezi wa Juni, 2005, Mfuko wa Taifa wa Pembejeo (*Agricultural Inputs Trust Fund*) ulikuwa umepokea maombi 14 kutoka Wilaya ya Kondoa kwa ajili ya kununua matrekta mapya. Maombi yote 14 yalipitishwa na Mfuko na waombaji wanakamilisha taratibu za kibenki ili kupata mikopo waliyoomba.

Aidha, Mfuko ulipokea maombi 76 kwa ajili ya mikopo ya kukarabati matrekta machakavu. Maombi manane, kati ya hayo, yalipitishwa na mfuko na waombaji watatu tayari wamepata mikopo waliyoomba.

Maombi 68 hayakupitishwa kutokana na kasoro mbalimbali. Baadhi ya kasoro zilizojitokeza ni waombaji kutokuwa na Hati Miliki au hati za viapo za mahakama za mali walizokusudia kuziweka dhamana, kutokupitisha maombi yao kwenye Halmashauri zao, maombi kutoambatanishwa na nyaraka muhimu, kwa mfano, ankara vifani za vipuri vitakavyonunuliwa, kivuli cha kadi ya trekta linaloombewa mkopo na taarifa ya tathmini ya trekta kutoka kwa Afisa Zana wa Wilaya. Waombaji wote tayari wameandikiwa barua za kuwashauri na kuwaelekeza namna ya kurekebisha kasoro zilizojitokeza ili wapate mikopo.

MHE. PASCHAL C. DEGERA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swal moja la nyongeza. Aidha namshukuru sana Naibu Waziri wa Kilimo na Chakula kwa majibu yake mazuri.

Kwa kuwa wakulima walioomba kupata pesa kwa ajili ya kukarabati matrekta walikuwa 76 na kwa kuwa wanane tu ndiyo walioweza kufanikiwa kupata mikopo hiyo, na kwa kuwa tatizo kubwa ni masharti magumu ya kupata hiyo mikopo ikiwemo na hati miliki kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri. Je, Serikali haioni kwamba kuna haja ya kulegeza masharti ili wakulima waweze kukopa matrekta hayo kwa masharti nafuu? (*Makofit*)

Kwa kuwa gharama za kufuata mikopo hiyo Dar es Salaam ni kubwa sana. Je Serikali ina mpango gani wa kuweza kusambaza huduma hiyo katika Mikoa na Wilaya? (*Makofit*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, tatizo la hawa 76 limeelezwa hati miliki ni moja na wakati mwингine wanaweza kutumia kiapo Mahakamani na Mahakama zipo katika Wilaya na hatuwezi kulegeza kwa sababu

tukilegeza masharti tutapata matatizo yaliyotukumba huko nyuma kwa kukosa kurejeshewa fedha bilioni 5. Kwa hivi haya masharti magumu ni kutokana na matatizo ya nyuma, uzoefu wa nyuma. Kwa hivi itakuwa vigumu kulegeza masharti hayo na siyo magumu sana kama una nia ya kukopa.

Na ya pili, kuhusu gharama, mara nyingi utaona mikopo hii inapitia Halmashauri ya Wilaya na Halmashauri ina uwezo wa kushughulikia masuala haya na siyo lazima kila mara kama mwombaji lazima afike Dar es Salaam. Kwa sababu Halmashauri inashirikishwa katika kuomba. Kwa hivyo tunaomba tushirikiane na Halmashauri zetu husika tuweze kutatua hili aliloliezea Mheshimiwa Degera.

Na. 244

Matrekta kwa Wakulima

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE (k.n.y. MHE. JOHN E. SINGO)
aliuliza:-

Kwa kuwa kilimo cha jembe la mkono Tanzania kimepitwa na wakati kwa sababu hakina tija kwa mkulima kwani mkulima hutumia muda wake mwingi, nguvu nyingi, uzalishaji mdogo na teknolojia duni, kwa kuzingatia na kulijua hilo:-

- (a) Je, Serikali ina mpango gani madhubuti wa kuwakopesha wakulima matrekta katika kila Wilaya?
- (b) Je, Serikali imeanzisha/imewezesha vituo vingapi vyta kukodisha matrekta katika kila Wilaya kwa lengo la kuwaondolea wakulima adha ya kutumia jembe la mkono?
- (c) Je, Wilaya ya Same imefaidika vipi na mpango huo katika sehemu ya (a) na (b) ya swali hilo?

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa John Singo, Mbunge wa Same Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

- (a) Hadi sasa hatujawa na utaratibu madhubuti na endelevu wa kukopesha wakulima matrekta. Utaratibu uliopo sasa unategemea fedha zinazotengwa kwa Bajeti ya Serikali na kiasi kinachotengwa kila mwaka kitategemea uwezo wa Serikali na vipaumbele vitakavyokuwapo. Utaratibu madhubuti utakuwapo Benki maalum ya kilimo itakapoanzishwa na vyombo vyta fedha vitakapokubali kutoa mikopo ya kununulia

matrekta na zana nyingine za kilimo kwa wakulima. Jukumu la kutoa mikopo ya kuwekeza katika kilimo inapaswa kuwa ya sekta binafsi.

Kwa wakati huu, Serikali, kupitia Mfuko wa Pembejeo, imeweka utaratibu wa kutoa mikopo ya masharti nafuu kwa wakulima kwa ajili ya kununulia matrekta mapya na zana zake na kukarabati matrekta machakavu.

Kwa utaratibu huu, maombi ya mikopo ya kununua matrekta mapya au kukarabati matrekta machakavu hawasilishwa kwenye Mfuko wa Pembejeo baada ya kupitishwa na kuridhiwa na Halmashauri za Wilaya zinazohusika. Waombaji hupatiwa mikopo kupitia kwenye benki zilizoteuliwa baada ya kutimiza masharti yaliyowekwa, ambayo ni pamoja na kuwa na dhamana inayokubalika kisheria.

(b) Serikali kupitia Mfuko wa Pembejeo, imewezesha kuanzishwa kwa vituo vitano vya kukodisha matrekta katika Wilaya za Masasi, Kilombero, Songea, Iringa na Moshi. Aidha, maopereta 20 wa matrekta katika vituo vilivyoanzishwa wamepatiwa mafunzo na serikali juu ya uendeshaji wa matrekta kibiashara na jinsi ya kuyatumia na kuyahudumia.

(c) Katika msimu wa 2003/2004, Mfuko wa Pembejeo ulipokea maombi 14 ya kukarabati matrekta kutoka Wilaya ya Same. Kati ya maombi hayo, maombi sita yalipitishwa na Mfuko na waombaji kutakiwa kukamilisha taratibu za kibenki ili wapewe mikopo waliyoomba. Hadi sasa ni mwombaji mmoja tu, Bwana Issa Mamento, aliyekamilisha taratibu zote na kupewa mkopo wake.

Aidha, Mfuko wa Pembejeo ulipokea maombi mawili tu kutoka Wilaya ya Same kwa ajili ya mkopo ya kununua matrekta mapya. Maombi hayo hayakupitishwa na Mfuko kutokana na waombaji kutotimiza masharti ya mikopo.

PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa kilimo ndio uti wa mgongo wa uchumi wa nchi hii na kwa kuwa kubadilika kwa uzalishaji katika kilimo kidogo tu kunaweza kubadilisha hali ya nchi kwa ujumla. Serikali inafikiria nini kuendeleza vituo hivi vya matrekta ya kukodisha ili vifike katika kila Wilaya na kutumiwa katika kuleta mabadiliko ya kilimo hapa nchini? (*Makofî*)

(b) Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ililetä zile *power tillers* kwa majaribio hapa nchini na pale zilipotumika zilionyesha mafanikio makubwa. Je, Serikali ina mpango gani wa kutoa ruzuku katika manunuzi ya hizi *power tillers* kama zinanunuliwa na vikundi vya wakulima au vya *SACCOS?* (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Prof. Jumanne Maghembe, kama ifuatavyo:-

Ni kweli kilimo ni uti wa mgongo nchini mwetu na kuendeleza vituo hivyo itasaidia sana kuendeleza kilimo. Lakini hata hivyo tuna sera ambayo ipo kwa mfuko ulipoanzishwa kwa kweli haukuwa kwa maana hii, ulikuwa zaidi kuhusu kutoa msaada wa ruzuku kwa *stockiest* wa mbolea za chumvi chumvi na kadhalika.

Lakini baadaye kutokana na mahitaji ya aina hii kwa ubunifu tu matrekta yalitumbukizwa. Sasa si rahisi kiuchumi kuhakikisha kuwa matrekta yanakuwa mengi kama Mheshimiwa anavyosema. Ushauri wetu ni kuwa tuombe Halmashauri za Wilaya zihamasishe wananchi wenyewe uwezo wawekeze, hii ni shughuli ambayo hasa ni sekta ya binafsi.

Pili, *power tillers* kweli zilikuwa zimeletwa lakini hadi sasa haupo mpango wa kutoa ruzuku kwa sababu hiyo hiyo, mfuko wenyewe ni finyu sana mahitaji ni mengi sana. Maana siyo tu *power tillers*, kuna matrekta ya aina mbalimbali tena *power tillers* zingine kama haulimi bondeni mlimani hazifai, zinfaaa tu kutifua kwenye mabonde yenyenye unyevu unyevu.

Lakini kwenye ardhi ngumu unahitaji matrekta yenyenye *horsepower* kama 85 na kuendelea na hayo ni gherama kubwa sana. Kwa hivyo kwa kutumia ruzuku kwa sasa ni vigumu mpaka hapo tutakapokuwa na uwezo itafikiriwa upya. (*Makofii*)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha sasa tunaendelea kama ifuatavyo. Matangazo, kuna kikao kimoja cha Kamati kilichopangwa kufanyika leo nayo ni Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala, Mwenyekiti wake Mheshimiwa Athumani Janguo, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane leo tarehe 12 mara tu baada ya kipindi hikki cha maswali katika ukumbi Na. 27.

Tangazo la pili linahusu Kamati ya Wabunge wote wa CCM, Mwenyekiti anaomba Wabunge wote wa CCM tutakapoahirisha saa 7.00 mchana huu wabaki kidogo. Ni kupokea taarifa fupi kutoka Makao Makuu ya Chama cha Mapinduzi (CCM), itachukua muda mfupi.

Mwisho, ni wachangiaji wa leo naona wamekuwa wengi karibu maombi 25 nimepata na haiwezekani wote wakapata nafasi kwa hiyo ngoja niwataje wale ambao nina hakika watapata nafasi ili wengine waweze kuchangia kwa maandishi. Ambao hawajachangia hata mara moja wako wawili ni Mheshimiwa William Shellukindo na Mheshimiwa Ponsiano Nyami. Ambao wamechangia mara moja tu ni Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba,

Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro nafikiri hao ndio watapata nafasi kwa muda tulio nao.

Waheshimiwa Wabunge, wabunge waliobaki wamechangia mara moja lakini wamechelewa kuwasilisha maombi ni Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz na Mheshimiwa Lekule Laizer. Ikitokea mtu akaenda Mtera mnawenza mkafanikiwa lakini vinginevyo kuna mashaka. Pia waliochangia mara mbili wapo, mara tatu wapo nadhani hawa wachangie kwa maandishi tu. Mwisho wa matangazo Katibu tuendelee na *Order Paper*.

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka 2003/2006

Wizara ya Nishati na Madini.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, baada ya kuzingatia taarifa iliyowasilshwa mbele ya Bunge lako tukufu na Mwenyekiti kwa Kamati ya Bunge lako Tukufu na Biashara, naomba kutoa hoja kwamba sasa Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio na matumizi ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004/2005 Bunge lako Tukufu liliondolewa na Wabunge watano. Wabunge hao ni: Mheshimiwa Abdulkarar Towegale Kiwanga - Mbunge wa Kilombero, Mheshimiwa Ahmed Hassan Diria - Mbunge wa Rahaleo, Mheshimiwa Frank Michael Mussati - Mbunge wa Kasulu Mashariki, Mheshimiwa Theodos James Kasapira - Mbunge wa Ulanga Mashariki na Mheshimiwa Margareth Bwana - Mbunge wa Viti Maalumu. Nachukua fursa hii kuwapa pole familia za Marehemu hao na wananchi wa majimbo husika.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hiki ni kikao cha mwisho cha bunge lako tukufu na ni mwaka wa mwisho wa Serikali ya awamu ya tatu, napenda nitumie nafasi hii kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na wenyeviti wako wawili kwa jinsi mlivyoongoza Bunge hili tukufu katika kipindi chote mllichoshika madaraka hayo. Aidha, mimi pamoja na wenzangu katika Wizara ya Nishati na Madini na wananchi wote wa jimbo langu la uchaguzi la Same Mashariki tunamtakia Mheshimiwa Rais Mkapa na familia yake afya njema na mafanikio baada ya kumaliza kipindi chake cha Urais. Tunamshukuru kwa kazi kubwa na nzuri aliyoifanya kwa miaka kumi ya kulijenga taifa letu na kuimarisha demokrasia.

Mheshimiwa Spika, itakumbukwa kuwa tarehe 4 Mei, 2005, Chama cha Mapinduzi (CCM) kilifanya mkutano wake mkuu na kuwapendekeza makada wa CCM ambao watagombea nafasi za Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar. Hivyo, sina budi kuwapongeza wajumbe wa Mkutano Mkuu wa CCM kwa kazi waliyoifanya ya kuwachagua wagombea hao kwa uwazi na utulivu. Taratibu za uchaguzi wa makada hao zimepongezwa ndani na nje ya nchi kuwa za demokrasia na haki. Kwa namna ya pekee nampongeza Mheshimiwa Jakya Mrisho

Kikwete kwa kuchaguliwa na CCM kugombea nafasi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Dr. Mohamed Ali Shein, kwa kuteuliwa kuwa mgombea mwenza. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Amani Abeid Karume, kwa kuchaguliwa na CCM kuwa mgombea wa Urais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar. Napenda pia kuwapongeza wanachama wote wa ccm ambao walijitokeza kwenye kinyang'anyiro hicho cha kiti cha Urais, kwani kuwepo kwoa ndiko kuliifanya CCM isifike kwa demokrasia iliyotumika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huu ni mwaka wa uchaguzi wa Rais na Wabunge hivyo napenda kuwatachia mafanikio mema wale wote watakaogombea nafasi hizo. Naomba uchaguzi uwe wa haki na amani ili kukidhi lengo letu la kuwa Wabunge wengi tulipo hapa sasa tutarejea tena mara baada ya uchaguzi wa mwezi Oktoba, 2005.

Mheshimiwa Spika, natoa shukrani zangu za dhati kwa kamati ya Bunge ya Uwekezaji na biashara chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa William Shelukindo, Mbunge wa Bumbuli, kwa kuichambua na kujadili bajeti ya Wizara yangu. Ushauri wa Kamati hii katika hatua za awali za maandalizi umesaidia kuboresha bajeti ninayowasilisha leo. Ningependa vilevile kuwapongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri ambao tayari wamewasilisha bajeti zao hapa Bungeni.

Mheshimiwa Spika, Mafanikio na Matatizo ya Serikali ya Awamu ya Tatu Katika Utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 1995 na 2000, katika kutekeleza maelezo yaliyotolewa katika Ilani ya Uchaguzi Mkuu ya CCM ya Oktoba, 1995 na Oktoba 2000, sekta ya Nishati na Madini licha ya mafanikio ziliyoyapata zilikabiliwa na changamoto kubwa ambazo ni: Bei kubwa ya nishati, ukosefu wa fedha za kupeleka ummeme vijijini, ukame na usimamizi wa leseni za madini.

Mheshimiwa Spika, Mafanikio Katika Sekta ya Nishati, kati ya mwaka 1995 na 2004, sekta ya nishati ilikua kwa wastani wa asilimia 5 kwa mwaka, ikilinganishwa na chini ya asilimia 3 mwanzoni mwa miaka ya 1990. Aidha, katika kipindi hicho, Serikali ilichukua hatua mbalimbali zilizolenga kuleta mabadiliko katika usimamizi na uendeshaji wa sekta hii. Baadhi ya hatua hizo ni:

- Kutoa fursa kwa wawekezaji binafsi kushiriki katika kuzlisha umeme (kwa mfano *IPTL* na *Songas*)
- Kuanzisha soko huria la biashara ya mafuta mwezi Januari, 2000;
- Kupitishwa Bungeni kwa Sheria ya kuanzisha chombo cha kusimamia sekta za nishati na maji (*EWURA*) mwezi Aprili, 2001;
- Kudurusu Sera ya Nishati ya mwaka 1992 na kutoka Sera ya Nishati ya mwaka 2003;
- Kupitishwa bungeni kwa Sheria ya kuanzisha Wakal wa Nishati Vijijini (*REA*) na Mfuko wa Nishati Vijijini (*REF*) mwezi Aprili, 2005;

- Kudurusu Sheria ya Umeme ya mwaka 1957 kwa lengo la kuandaa muswada wa Sheria mpya ya umeme; na
- Kuhakikisha kuwa bei za umeme Tanzania hazizidi sana au zinakuwa chini ya zile za Kenya na Uganda.

Mheshimiwa Spika, mwaka 1995 uwezo wa kuzalisha umeme (*installed capacity*) nchini ulikuwa Megawati (*MW*) 587 ikilinganishwa na uwezo wa sasa wa MW 863. Jedwali Na. 4 linaonyesha uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme nchini na umeme uliozalishwa tangu mwaka 1995 hadi 2004. Uwezo huo umeongezeka kwa zaidi ya asilimia 47. Awali mfumo wa uzalishaji umeme kwa kiasi cha zaidi ya asilimia 80 mfumo wa uzalishaji umeme kwa kiasi cha zaidi ya asilimia 80 ulitegemea nguvu ya maji ambapo kiasi hicho kitapungua na kufikia asilimia 50 ifikapo mwishoni mwa mwaka 2006. Kupungua kwa utegemezi huo kunatokana na ongezeko la umeme unaozalishwa kwa gesi ya Songo Songo na jenereta za mafuta za *IPTL*.

Mheshimiwa Spika, kukamilika kwa ujenzi wa bomba la gesi ya Songo Songo kuliwezesha kuanza kutumika kwa gesi hiyo katika jiji la Dar es Salaam mwezi Julai, 2004. Mheshimiwa Rais alifunga rasmi mradi huo mwezi Oktoba, 2004. Gesi hiyo inatumika viwandani na kwa ajili ya kuzalisha umeme. Aidha, kuanza kwa uzalishaji wa umeme kwa kutumia gesi ya Songo Songo na mradi wa *IPTL* kulilifanya Taifa kuepukana na mgao wa umeme tangu mwaka 2000.

Mheshimiwa Spika, sera ya Nishati inaelekeza kupeleka kwanza umeme kwenye makao makuu ya wilaya, miji midogo na kwenye vituo vya kuzalisha mali vikiwemo vinu vya kuchambulia pamba na viwanda vijijini. Madhumuni ya Sera hii ni kutumia umeme ili kuweka msukumo kwa maendeleo ya wananchi na katika shughuli mbalimbali za uzalishaji. Aidha, kwa kufikisha umeme vijijini taifa litafanikiwa kupunguza kasi ya utumiaji wa kuni na mkaa na hivyo kulinda misitu na mazingira yetu.

Mheshimiwa Spika, tangu mwezi Oktoba, 1995 hadi Novemba, 2005, Serikali ya awamu ya tatu imeyapatia umeme makao makuu ya wilaya 23 za Tanzania Bara. Wilaya zilizokwishapatiwa umeme hadi sasa ni Kongwa, Maketi, Sengerema, Kilwa, Iramba, Mbulu, Kiteto, Bunda, Karatu, Ileje na Ruangwa. Wilaya nyingine ni Tandahimba, Mkuranga, Meatu, Igunga, Mbarali, Sikonge, Geita, Ngara, Biharamulo. Aidha, Wilaya za Urambo Serengeti na Ukerewe zitapatiwa umeme kabla ya mwezi Oktoba, 2005.

Mheshimiwa Spika, kutokana na mafanikio hayo, Rais awamu ya nne atakabidhiwa wilaya 13 tu ambazo bado hazina umeme. Wilaya hizo ni Ngorongoro (Mkoa wa Arusha); Kilolo na Ludewa (Mkoa wa Iringa); Kasulu na Kibondo (Mkoa wa Kigoma); Simanjiro (Mkoa wa Manyara); Rufiji (Mkoa wa Pwani); Nkasi (Mkoa wa Rukwa); Bukombe (Mkoa wa Shinyanga); Kilindi (Mkoa wa Tanga); Uyui (Mkoa wa Tabora); Namtumbo na Mbanga (Mkoa wa Ruvuma). Ningependa kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kuwa Wizara yangu pamoja na *TANESCO* tutatoa ushirikiano

wa hali ya juu kwa Serikali ya awamu ya nne ili kutekeleza miradi ya kupeleka umeme kwenye wilaya hizo 13 zilizobakia haraka.

Mheshimiwa Spika, licha ya upelekaji umeme kwenye makao makuu ya wilaya, kazi nzuri imefanywa na Serikali ya awamu ya tatu kuipatia umeme miji midogo, mashamba makubwa na vijiji vingi nchini. Katika kipindi cha miaka 10 iliyopita miji midogo iliyopatiwa umeme ni pamoja na Dareda, Magugu, Oldeani, Mto wa Mbu, Kiru, Mwisi, Nkinga, Chimala, Ubaruku, Madabaga, Makuyuni na Kibakwe. Miji mingine ni Mahuta, Nanyanga, Kisamwa, Balangidalalu na mji wa Chato. Aidha, Miradi ya *TANESCO* ya kufikisha umeme kwenye miji midogo ya Sumve, Malya, Bugarama, Ilogi, Forti Ikoma, Isenye, Ilolangulu, Usoke, Tumbi, Igwange na Kibara inaendelea. Pamoja na kazi hizo nilizozitaja, mradi unaandaliwa wa kuvipatia umeme vijiji 31 vilivyoko katika maeneo linakopita bomba la gesi ya Songo Songo. Mradi huu unafadhiliwa na Benki ya Dunia pamoja na Serikali kwa gharama ya zaidi ya shilingi bilioni 10. (*Makofii*)

Mheshimiwa Spika, Matatizo Katika Sekta ya Nishati, sekta ya nishati iliendelea kukabiliwa na upungufu wa fedha zinazotengwa na Serikali kwa ajili ya miradi ya kupeleka umeme mijini na vijijini. Kwa miaka mitatu iliyopita Serikali ilitenga wastani wa shilingi bilioni 1.3 kwa mwaka, ambazo ni sawa na gharama ya mradi mmoja wa kupeleka umeme katika makao makuu ya wilaya moja tu kati ya zile zilizoonyeshwa kwenye Jedwali Na. 5.

Sekta hii pia ilikabiliwa na upungufu mkubwa wa maji katika mabwawa ya Mtera na Nyumba ya Mungu na kuifanya *TANESCO* kutegemeana zaidi uzalishaji wa umeme kwa kutumia mafuta na gesi asilia. Aidha, bei ya mafuta hapa nchini imepanda kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta hayo katika soko la dunia, kuongezeka kwa gharama za usafirishaji wa mafuta hayo na kushuka kwa thamani ya sarafu yetu.

Mheshimiwa Spika, mafanikio katika Sekta ya Madini, mchango wa sekta ya madini kwenye Pato la Taifa umeendelea kuongezeka kutoka asilimia 1.4 mwaka 1995 hadi kufikia asilimia 3.2 mwaka 2004 kama jedwali Na. 6 linavyoonyesha. Ili kuendeleza sekat ya madini Serikali ya awamu ya tatu iliweka vivutio kwa wawekezaji katika sekta hii kupitia Sera ya Madini ya Mwaka 1997, Sheria ya Madini ya Mwaka 1998, Sheria ya Fedha na takwimu za kujiolojia na madini.

Mheshimiwa Spika, tangu Serikali ilipopitisha Sera ya Madini mwaka 1997, kumekuwa na maendeleo makubwa kwenye sekta ya madini ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa shughuli za utafutaji na uchimbaji wa madini. Katika kipindi hicho, migodi mikubwa sita ya dhahabu ilijengwa kwa thamani ya dola bilioni 1.5 na imeanza kuzalisha. Migodi hiyo iko Nzega, uliofunguliwa Februai, 1999; Geita, uliofunguliwa Agosti, 2000; Kahama, ulifunguliwa Julai, 2001; Tarime, uliofunguliwa Septemba, 2002; Buhemba uliofunguliwa Januari, 2003; na Tulawaka ambaa ulifunguliwa Juni, 2005.

Kuanza kwa uzalishaji katika mgodi wa Tulawaka kunaifanya Tanzania kuwa nchi ya tatu barani Afrika Kusini na Ghana. Tanzania sasa inazalisha takriban tani 50 za

dhahabu kwa mwaka ikilinganishwa na wastani wa tani 3 mwaka 1995. Jedwali Na. 7 linaainisha migodi mikubwa ya dhahabu nchini na uzalishaji wake kwa mwaka.

Mheshimiwa Spika, Mauzo ya madini kutoka Tanzania yamekua hadi kufikia asilimia 52.1 ya mauzo yote ya nje kwa mwaka 2004. Jedwali Na. 8 linaonyesha mauzo ya madini yakilinganishwa na mauzo ya mazao mengine nje. Mapato ya fedha za kigeni kutokana na mauzo ya madini yaliongezeka kutoka dola za marekani milioni 26.4 mwaka 1998 hadi kufikia dola za marekani milioni 692.9 mwaka 2004. Pamoja na kulipa mirahaba na kodi Serikalini, kampuni za madini zinatoa mafunzo ya ajria kwa Watanzania zaidi ya 8,300 wa fani mbalimbali na wengine takriban 15,000 wanatoa huduma kwenye migodi hiyo na kujipatia kipato chao. (*Makofi*)

Kampuni hizo za madini katika miaka hii michache tangu zianze uzalishaji, zimetumika zaidi ya dola za marekani milioni 25 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kiuchumi na kijamii kama vile shule za msingi na sekondari, uchimbaji visima vya maji, vituo vya afya na barabara. Miundombinu hiyo ilitekelezwa katika Halmashauri za Biharamulo, Geita, Kahama, Musoma, Simanjiro na Tarime. Jedwali Na. 9 linatoa takwimu za gharama za huduma za jamii zilizotolewa na migodi hiyo.

Mheshimiwa Spika, matatizo katika Sekta ya Madini, pamoja na mafanikio yaliyopatikana, kumekuwa na hoja kutoka kwa wadau kuwa Taifa halijafaidika kwa kiasi kinachostahili kutokana na sekta ya madini. Kutokana na hoja hizo, mwaka 2004 Serikali iliunda Kamati ya kufuutilia malalamiko hayo. Hadidu za rejea za Kamati hiyo zilikuwa:-

Kuangalia taratibu za uwekezaji kwenye sekta ya madini; umiliki wa hisa kwenye migodi; mfumo wa kodi na vivutio kwenye sekta ya madini; namna ya kuvutia wawekezaji ili kukuza uwezo wa kuongeza thamani ya madini nchini kabla ya kuyasafirisha nje; usimamizi wa shughuli za uchimbaji na utoaji huduma kwa wachimbaji wadogo; namna ya kuondoa vikwazo kwenye biashara ya madini na kuondoa migongano kati ya wadau kwenye sekta ya madini. Kamati hiyo iliyoongozwa na Dr. Jonas P. Kipokola tayari imewasilisha taarifa yake Serikalini. Aidha, Waheshimiwa Wabune nao wamepata nafasi ya kuipatia taarifa hiyo na kutoa maoni yao. Serikali kwa sasa inafanya kazi taarifa ya Kamati na ushauri wa Waheshimiwa Wabunge kwa lengo la kuondoa matatizo na upungufu uliosababisha baadhi ya hoja hizo kutolewa.

Mheshimiwa Spika, Muhtasari wa utekelezaji wa mpango wa 2004/2005 na mpango wa utekelezaji kwa mwaka 2005/2006.

Utekelezaji wa mpango kwa mwaka 2004/2005, katika mwaka 2004/2005 Wizara iliendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2000 katika sekta za nishati na madini kwa kutoa kipaumbele kwa miradi ya umeme, gesi na makaa yam awe; usambazaji umeme katika mji mikuu ya wilaya, miji midogo na baadhi ya vijiji vinavyopitiwa na gridi ya Taifa; kuhamasisha wawekezaji wa sekta binafsi; kuongeza ufanisi kwa kuruhusu ushindani katika sekta ya nishati hususan kwenye umeme na kuboresha shughuli za TANESCO. Aidha, katika sekta ya madini Wizara iliendelea kuwakaribisha wawekezaji wakubwa; kuwasaidia wachimbaji wadogo; kuimarisha

ukusanyaji wa maduhuli kutokana na mauzo ya madini na kuboresha mahusiano kati ya wachimbaji wakubwa na wadogo.

Katika sekta ya nishati mwaka 2004/2005 Serikali imefanikiwa kufanya yafuatayo: kuanza kutumia gesi ya Songo Songo kuzalisha umeme katika kituo cha *Songas Ubungo*; kutangaza zabuni ya kupeleka umeme kwenye vijiji vilivyo kandokando ya bomba la gesi ya Songo Songo; kufufua (*re-enter*) kisima cha gesi cha Mnazi Bay kulikoonyesha kuwepo kwa gesi ya kutosha kwa ajili ya mradi wa kuzalisha umeme wa *MW 14.5* na matumizi mengine; kuondoa kodi kwenye vifaa vy'a nishati mbadala; kuipatia umeme miji ya Biharamulo na Ngara; kupitisha muswada wa kuanzishwa kwa Wakala na Mfuko wa Nishati Vijijini; na kuboresha mfumo wa umeme nchini kwa kutumia vyanzo mbalimbali vy'a fedha ikiwa ni pamoja na fedha zilizotokana na ongezeko la ukusanyaji mapato ya *TANESCO* lililofikia shilingi bilioni 21 mwezi Machi, 2005 ikilinganishwa na wastani wa shilingi bilioni 11 kwa mwezi, mwaka 2001.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya madini baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni: kuanza kwa uzalishaji katika mgodi wa Tulawaka weny'e mashapo yatakayodumu kwa miaka mitano na uwezo wa kuzalisha takriban wakia 100,000 za dhahabu kwa mwaka; kukamilishwa kwa ramani mpya inayoonyesha maeneo yenye madini mbalimbali nchini; kuanza kutekelezwa kwa mradi wa kuimarisha shughuli za utoaji na usimamizi wa leseni za madini (*Mining Cadastral Information Management System*); utoaji wa mafunzo mbalimbali kwa wachimbaji wadogo katika mikoa ya Singida, Arusha, Tanga, Mbeya, Iringa na Shinyanga; kuendelezw'a kwa vituo vitakavyotoa mafunzo kwa wachimbaji wadogo vy'a Arusha *Gemstone Carving Centre* na Matundasi – Chunya; na kuongezeka kwa ukusanyaji wa maduhuli kutoka wastani wa shilingi milioni 7.0 kwa mwezi mwaka 1995 hadi wastani wa shilingi bilioni 2.25 kwa mwezi ilipofika Machi, 2005. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mpango wa utekelezaji kwa mwaka 2005/2006, mpango wa Bajeti kwa mwaka 2005/2006 umelenga kutekeleza malengo yaliyoainishwa kwenye Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini, Tanzania (MKUKUTA).

Malengo yatakayotekelezwa yanakusudiwa kutoa nishati ya uhakika na ya kuaminika, kuwawezesha wananchi kutumia teknolojia za kisasa za uzalishaji nishati, kuongoza machango wa sekta za nishati na madini kwenye pato la Taifa, kuongeza ufanisi katika utawala na utoaji huduma na kujumuisha masuala mtambuka, kama vile UKIMWI na mazingira katika utekelezaji wa mpango.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2005/2006 sekta ya nishati imelenga kuanzisha ofisi ya Wakala na Mfuko wa Nishati Vijijini, kuendelea na utekelezaji wa miradi ya upelekeji umeme katika Makao Makuu ya Wilaya, kutangaza na kusimamai maeneo na shughuli za utafutaji wa mafuta na gesi nchini, kukusanya maduhuli, kugharamia malipo ya mitambo ya uzalishaji wa umeme (*Capacity Charge*) unaofanywa na wawekezaji binafsi ikiwemo *IPTL* na Usimamizi wa sekta ya nishati. Aidha katika sekta ya madini mpango unalenga kuimarisha mfumo wa utoaji leseni za utafutaji na uchimbaji madini nchini na kusimamia sekta ya madini kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya mpango na Bajeti ya 2004/2005 na mwelekeo kwa mwaka 2005/2006, Sekta ya Nishati, Umeme katika makao Makuu ya Wilaya. Kufuatia mazungumzo yaliyokuwa yakiendelea kati ya Wizara na Sida hadi sasa Serikali ya Sweden imekubali kutoa fedha za kufanya upenguzi yakinifu kwa ajili ya kupeleka umeme wa gridi katika Mikoa ya Ruvuma, Kigoma na Kagera. Kufuatia makubaliano hayo, *TANESCO* inakamilisha hadidu za rejea ili kazi hiyo iweze kuanza. Mshauri kwa ajili ya mradi wa kituo cha kupoza umeme cha Makambako amepatikana. Aidha Sida imeidhinisha fedha kwa ajili ya upenguzi yakinifu wa njia ya umeme ya kilovoti 132 kutoka Makambako hadi Songea.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kasi ndogo ya kutekeleza miradi ya kupeleka umeme Vijiji inayotokana na fedha chache zinazotengwa, mwaka 2004/2005 umeme ulifikishwa Biharamulo na Ngara ambako katika mwaka huu wa fedha kazi zitakazoendelea ni usambazaji wa umeme katika miji na Vijiji vya maeneo hayo. Aidha miradi ya upelekaji umeme katika Wilaya za Serengeti, Urambo na Ukerewe inaendelea vizuri. Mradi wa Ukerewe utagharimu takriban Shilingi bilioni 10, mradi wa Serengeti utagharimu jumla ya Shilingi bilioni 4.3 na ule wa Urambo utagharimu Shilingi bilioni 2.6 miradi hii inatarajiwa kukamilika mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa 2004/2005 Serikali iliingia mkataba mpya wa miaka miwili na nusu kati yake na menejimenti ya *TANESCO (Net Group Solutions)* kuanzia Agosti, 2004 hadi Desemba 2006. Chini ya mkataba huo menejimenti hiyo itatekeleza yafuatayo:- Kuongeza kasi ya kuwaunganishia umeme wateja, kuboresha huduma ya umeme na kuandaa mipango ya uongozi wa *TANESCO* kuongozwa na Wazalendo baada ya mkataba kwisha.

Mheshimiwa Spika, mradi wa gesi ya Songo Songo ulifunguliwa rasmi na Mheshimiwa Rais mwezi Oktoba, 2004 kwenye kituo cha *Songas, Ubungo*. Gesi ya songo songo inatumika kuzalisha umeme katika kituo hicho na kwenye viwanda vya Saruji *Wazo Hill, TBL, ALAF* na *Kioo Ltd*. Viwanda vingine vitatu vinafanya marekebisho ya mitambo ili viweze kutumia gesi hiyo. Viwanda hivyo ni *Bora Shoe, NIDA* na *URAFIKI (Tanzania, China Friendship Textile Ltd)*.

Mheshimiwa Spika utekelezaji wa miradi ya umeme kwenye Vijiji vilivyo karibu na mkuza wa bomba la gesi ya songo songo umeanza. Hivi karibuni zabuni ya kujenga kituo na kuweka jenereta tatu zenye uwezo wa kuzalisha umeme jumla ya MW sita kwa kutumia gesi hiyo ilitangazwa.

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha kuwa mwaka 2007 Taifa linakuwa na umeme wa uhakika *TANESCO* imeanza kutafuta mwekezaji kwenye mradi wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi ya Songo Songo ili kuongeza ushindani kwenye sekta hiyo.

Mheshimiwa Spika, Gesi ya *Mnazi Bay*, Kampuni ya Artumas ilifufua (*re-enter*) kisima cha gesi ya *Mnazi Bay* na kufanya majaribio ya uzalishaji. Matokeo ya majaribio hayo yameonyesha kuwa kisima hicho kina uwezo wa kuzalisha gesi kwa kiasi cha futi za ujazo zaidi ya milioni 10 kwa siku. Kiasi hiki kinatoshereza kwa mahitaji ya mradi wa

kuzalisha umeme kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara. Mikataba ya usambazaji na ununuzi wa gesi na umeme baina ya wadau mbalimbali inaandaliwa na masoko ya gesi ya ziada kutoka *Mnazi Bay* yanatafutwa ndani na nje ya Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Mfuko wa Nishati Vijijini, Wizara iliendesha warsha za uhamasishaji juu ya kuanzishwa kwa Wakala na Mfuko wa Nishati Vijijini. Mada zilizowasilishwa katika warsha hiyo zilihusu mtazamo na mwelekeo wa Sera ya Nishati, dira na misingi muhimu ya wakala na mfuko, muundo na mfumo wa utawala wa wakala na mfuko na rasimu ya sheria ya uanzishwaji wa wakala na mfuko huo. Aidha Muswada wa kuanzishwa kwa wakala na Mfuko wa Nishati Vijijini ulipitishwa na Bunge lako Tukufu katika kikao chake cha 19 mwezi Aprili, 2005. Kufuatia hatua hizo mwaka 2005/2006 Wizara imetenga fedha kwa ajili ya kuanzisha Ofisi ya Wakala, kuajiri Watumishi na kununua vifaa vya kufanya kazi na kuanda taratibu za kuanza kutunisha mfuko wa Nishati Vijijini.

Mheshimiwa Spika, uhamasishaji wa uwekezaji katika sekta ya nishati. Wizara ilishiriki katika mikutano mbalimbali ya kuhamasisha uwekezaji. Moja ya mikutano hiyo ni *Tanzania Business Opportunities and Investments* uliofanyika Johannesburg Afrika Kusini ambapo ujumbe wa Tanzania uliongozwa na Mheshimiwa Waziri Mkuu. Taarifa muhimu kuhusu fursa za uwekezaji zilizopo kwenye sekta hizi zilisambazwa kwa washiriki wa mikutano kwa njia ya kanda (*CDS*), vipeperushi, majarida na makabrasha mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, Mradi wa *IPTL*, Serikali iliendelea kutafuta namna ya kupunguza mzigo wa capacity charge ya mradi wa *IPTL* na kuangalia uwezekano wa kuununua. Mawasiliano na Serikali ya Malaysia kwa lengo la kuiwezesha Serikali yetu kujadiliana na wadau wakuu wa mradi wa *IPTL* (wawekezaji na wakopeshaji) ili kufikia muafaka katika masuala hayo bado hayajaza matunda. Kama nilivyolarifu Bunge lako Tukufu mwaka 2004/2005 kuwa mitambo ya uzalishaji umeme ya *IPTL* ingefanyiwa marekebisho ili iweze kutumia gesi ya Songo songo badala ya mafuta, kazi hiyo imeanza.

Usanifu kwa ajili ya marekebisho unaendelea na inatarajiwa kuwa marekebisho yataanza katika mwaka huu wa fedha na kugharimu jumla ya dola za marekani milioni 18.0. Matumizi ya gesi ya Songo Songo kwenye mitambo ya *IPTL* yatapungua kwa karibu nusu gharama ya ununuzi wa mafuta ambayo ni takriban Shilingi bilioni 5.0 kwa mwezi.

Mheshimiwa Spika, utafutaji wa mafuta. Wataalam wa Wizara na Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (*TPDC*), wameendelea na jitihada za kuyatangaza maeneo yenye uwezekano wa kuwa na mafuta na gesi. Baadhi ya mikutano iliyofanyika ni mkutano wa annual Africa Upstream 2004 uliofanyika nchini Afrika Kusini mwezi Oktoba 2004, *Third Licensing Round* iliyofanyika Uingereza mwezi Novemba, 2004 na mkutano wa pili wa *East African Petroleum Conference* uliofanyika Uganda, mwezi Machi, 2005 kwa maeneo ya kina kirefu cha maji baharini.

Mheshimiwa Spika, Bomba la mafuta Dar es Salaam hadi Mtwara, Wizara imepokea taarifa ya maendeleo ya utekelezaji wa mradi wa Bomba la Mafuta la Dar es Salaam hadi Mwanza kutoka kwa Richmond *Development Company (RDC)*. Katika taarifa hiyo, *RDC* wameainisha kuwa wako katika hatua za maandalizi kutafuta mshauri (*consultant*) wa kufanya upenguzi yakinifu wa mradi kufanya mazungumzo na vyombo vya fedha kutathmini njia itakayopita bomba, uhamishaji wa watu na fidia kwenye mradi huo. Ili kufanikisha mradi huu Serikali iko makini kuhakikisha kuwa *RDC* inafanya kazi kufuatana na makubaliano kinyume na hayo hatua za kutafuta mwendelezaji mwingine zitachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uendelezaji wa nishati mbadala, vyanzo mbadala vya nishati kama vile juu, upopo, tungamotaka, maporomoko ya maji (*hydro*), jotoardhi (*geothermal*), makaa ya mawe na kadhalika vitaendelea kuwa tegemeo la kudumu kwa maendeleo ya nchi yetu. Kwa hiyo, ni muhimu kutafiti na kuthibitisha uwepo wa vyanzo hivyo na kuviendeleza ili wananchi walio wengi zaidi wapate huduma bore za nishati. Katika mwaka 2004/2005, kazi zilizofanyika ni pamoja na uendelezaji wa matumizi ya umemenuru, uandaaji miradi mipyä na ukusanyaji wa taarifa na takwimu kuhusu vyanzo mbadala vya nishati na teknolojia muafaka ya kupikia kwa mfano majiko sanifu ambayo hupunguza matumizi makubwa ya kuni na mkaa. Aidha, Wizara iliendelea kuratibu na kusimamia utekelezaji wa Mradi wa Uendelezaji Soko la Umemenuru Mkoani Mwanza ambapo mitambo kadhaa imefungwa katika baadhi ya vituo vya afya na shule kama mkakati wa kupunguza matatizo ya nishati na kuhamasisha wananchi kuhusu teknolojia hii.

Vile vile, pamoja na Serikali kuondoa kodi ya ongezeko la thamani (*VAT*) kwa vifaa na mitambo inayotumia mionzi ya juu na nguvu za upopo, mikakati ya kuwa na viwango (*standards & codes of practice*) inatekelezwa kwa kushirikiana na nchi nyingine za Jumuia ya Afrika Mashariki.

Mheshimiwa Spika, maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa umemenuru chini ya ufadhili wa Serikali ya Swedeni yalikamilika na utekelezaji wa awali (*inception phase*) umeanza. Pia, maandalizi ya utekelezaji wa mradi wa uendelezaji nishati jadidifu chini ya ufadhili wa Serikali ya Ujerumanu yalikamilika na utekelezaji wa awali umeanza. Aidha, ukusanyaji taarifa za viashiria vya jotoardhi (*geothermal*) ulifanyika mkoani Arusha (Ziwa Natron), manyara (Ziwa Manyara), Tanga, Pwani (Ruhoi - Rufiji) na Mbeya (Songwe). Utafutaji fedha kwa ajili ya kuendelea na utafiti wa uchimbaji (*Exploration Drilling*) unaendelea. Lengo ni kuendeleza chanzo hiki kwa ajili ya kuvuna mvuke na kuzalisha umeme katika maeneo husika.

Mheshimiwa Spika, Wizara kwa kushirikiana na *UNIDO* na *TANESCO* zilifanya utafiti wa awali kuhusu uendelezaji wa matumizi ya maporomoko madogo ya maji (*small scale hydro*) katika mito sita mkoani Tanga, mto mmoja mkoani Iringa na mto mmoja mkoani Rukwa ili kuangalia uwezekano wa kuazaisha umeme.

Mheshimiwa Spika, ili kuhamasisha wafanyakazi serikalini kuhusu matumizi bora ya nishati, Wizara kwa kushirkiana na washauri, imetekeliza programu ya kufanya

ukaguzi wa matumizi ya nishati (*energy audits*) katika majengo ya Wizara nne ambazo ni Ujenzi, Nishati na Madini, Fedha na Elimu na Utamaduni.

Lengo ni kuainisha mianya ya upotevu wa nishati katika majengo husika na kutoa mapendekezo ili kupunguza upotevu huo. Katika kuhitimisha kazi hiyo, Wizara inatarajia kuitisha warsha ya wadau kujadili taarifa ya ukaguzi huo ili kuongeza uelewa wa matumizi bora ya nishati, pia kupunguza Ankara za umeme kwa kiasi cha asilimia 30 ya fedha zote zinazotumika kwa mwaka kwa ajili ya kulipia umeme.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uunganishaji wa Gridi za Umeme za Zambia, Tanzania na Kenya. Zoezi la kuajiri Mshauri atakayefanya uchunguzi wa athari za kijamii na mazingira (*Environmental and Social Impact Assessment*) katika mradi wa kuimarisha njia kuu ya usafirishaji wa umeme kutoka Mbeya hadi Singida ambayo ni sehemu ya Mradi wa Kuunganisha Gridi za Zambia, Tanzania na Kenya limekamilika. Mshauri anatarajiwa kuanza kazi mwezi Agosti, 2005 na atakamilisha uchunguzi mwezi Desemba, 2005.

Aidha, Mawaziri wanaoshughulikia masuala ya nishati kutoka Zambia, Tanzania na Kenya watakutana kujadili mkakati wa kuanza kutekeleza ujenzi wa mradi. Ni matarajio yetu kuwa kuharakishwa kwa utekelezaji wa mradi huu kutaiwesheha miradi mikubwa kama ya Mchuchuma na Ruhudji kupata soko la umeme katika nchi zitakazokuwa zimeunganishwa na gridi hiyo.

Mheshimiwa Spika, kuhusu Mradi wa *Nile Basin Initiative*, taarifa ya mwisho ya Mradi wa *Nile Basin Strategic/Sectoral, Social and Environmental Assessment of Power Development Options in the Nile Equatorial Lakes region – Stage I (Burundi, Rwanda and Western Tanzania)* imekamilika. Taarifa hiyo inatoa mapendekezo mbalimbali ya uzalishaji umeme katika eneo hilo. Moja ya miradi inayopendekezwa kuendelezwa na nchi hizo ni mradi wa kuzalisha *MW 62* za umeme kutokana na maporomoko ya mto Rusumo. Tanzania ikiwa ni mwenyeji inakamilisha maandalizi ya ofisi ya regional *Power Trade Project* na moja ya miradi itakayosimamiwa na ofisi hiyo ni mradi wa umeme wa Rusumo.

Mheshimiwa Spika, katika sekta ya majini, kuhusu utoaji wa leseni za madini, katika hotuba ya Bajeti ya Wizara yangu mwaka jana, nilitoa taarifa ya uanzishwaji wa mradi mpya unaojulikana kama *Mining Cadastral Information Management System*, unaolenga kuongeza ufanisi katika shughuli za utoaji na usimamizi wa leseni za madini nchini. Ninapenda kulifahamisha Bunge lako Tuikufu kuwa, mkataba wa utekelezaji wa mradi huo kati ya Serikali na mkandarasi, *Swedish Geological AB*, kutoka Sweden ulisainiwa mwezi Januari, 2005.

Katika mpango wa utekelezaji, mkandarasi ataboresha uwezo wa kiutendaji wa Wizara kwa kutoa mfunzo, kuweka mfumo wa kompyuta na mawasiliano wa kutumia katika shughuli za utoaji leseni, kununua vifaa, kuhakiki viwanja vya madini na kujenga masijala ya kisasa ya leseni za madini. Aidha, atapendekeza marekebisho ya Sheria ya Madini ili iendane na mfumo mpya unaotarajiwa kuanzishwa na uingizwaji wa takwimu

na taarifa za leseni za madini, biashara na vibali vilivyo chini ya Sheria ya Manini ya Mwaka 1998 na Sheria ya Baruti ya mwaka 1963 kwenye mfumo wa kompyuta vitafanyika.

Mheshimiwa Spika, Shirika la Madini la Taifa (*STAMICO*) lina leseni za madini katika maeneo ambayo linakusudia kuyaendeleza kwa ubia. Maeneo hayo ni Ileje na Malonji mkoani Mbeya yenyе madini aina ya Platinum ambapo juhudи za kuwapata wabia zinaendelea; Buhungukilwa *Gold Prospect*, ambako mbia, *Savannah Company Limited* wa kulienendeza eneo hilo amepatikana; Mahene *Gold Prospect*, ambako eneo litaendelezwa kwa ubia kati ya *STAMICO* na *TANZAM* 2000 na *Igusule Gold Prospect* ambako *STAMICO* ina ubia na *Barrick Exploration Africa Limited*. Aidha, *STAMICO* inaendelea kutafuta wabia kwenye eneo la Itetemia baada ya kampuni ya Barrick *Exploration Africa Limited* kujitoa.

Mheshimiwa Spika, katika juhudи za Wizara za kuwasaidia wachimbaji wadogo wa madini, Wizara iliendesha mfunzo kwa wachimbaji wadogo yaliyofanyika Morogoro mwezi Julai, 2004, mkoani Singida mwezi Oktoba 2004, Mbeya mwezi Desemba, 2004 na Shinyanga mwezi Aprili, 2005. mafunzo hayo yalihusu Sheria ya Madini ya mwaka 1998 na marekebishо kwa baadhi ya vifungu katika shria hiyo yaliyofanywa na Bunge mwezi februari, 2004, uchimbaji salama wa madini, utunzaji wa mazingira, matumizi salama ya baruti, utafutaji wa madini, matumizi salama na madhara ya zebaki, biashara ya madini, ulipaji wa mrabaha, uongezaji wa thamani ya madini, masual aya jinsia na kujikinga na UKIWMI.

Aidha, Wizara ilitenga maeneo maalum ya Maganzо na Kishapu mkoani Shinyanga, Londoni mkoani Singida, Kilosa mkoani Morogoro na Handeni na Kilindi mkoani Tanga kwa ajili ya wachimbaji wadogo.

Mheshimiwa Spika, kwa lengo la kuwawezesha wachimbaji wadogo kuzalisha kwa tija zaidi na kwa kuzingatia kanuni za usalama, afya na mazingira, wachimbaji wadogo wa dhahabu walio jirani na kituo cha mafunzo kwa vitendo kilichopo Matundasi wilayani Chunya wameanza kunufaika kwa huduma za ushauri wa kitaalam unaotolewa bure pamoja na ukodishaji wa vifaa na mashine kwa gharama ndogo kutoka katika kituo hicho. Kituo kilizinduliwa rasmi na Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mwezi Januari, 2005.

Mheshimiwa Spika, kuhusu suala la kuongeza thamani ya madini, katika mwaka 2004/2005 wizara yangu imeendelea na ujenzi wa Kituo cha Uchongaji na Usanifu wa Mawe na Vito cha Arusha (*Arusha gemstone Carving Centre*). Napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba, ununuzi wa vifaa na mashine husika umekamilika na tathmini ya mahitaji ya ufungaji wa mitambo ilifanyika mwezi Aprili, 2005. Kazi ya ufungaji wa mashine na majoribio ya uchongaji vitaanza mwaka huu wa fedha. Wizara imeendelea kuwahamasisha wadau juu ya umuhimu wa kukata madini hapa nchini kwa lengo la kuongeza thamani na kutoa ajira zaidi kwa Watanzania. Kwa upande wa madini ya vito (hasa *Tanzanite*) usanifu hapa nchini unaongezeka siku hadi siku. Aidha, Wizara inaendelea kuzungumza na kampuni mbalimbali zilizojitokeza kujenga mtambo wa

kuchenjua dhahabu (*gold refinery*) jijini Dar es Salaam, ambao utachangia katika kuongeza thamani ya dhahabu.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchimbaji mkubwa wa madini, katika mwaka 2004.2005 mgodi mkubwa wa dhababu wa sita nchini ulianza uzalishaji. Huu ni mgodi wa dhahabu wa Tulawaka unaomilikiwa na kampuni za *Barrick Gold Corporation* na *Northern Mining Exploration Limited* za Canada. Mgodi huo una uwezo wa kuzalisha takriban wakia 100,000 kwa mwaka. Mgodi umegharimu jumla ya dola za Marekani milioni 50 na kulingana na makisio ya sasa ya mashapo ya dhahabu yanayofikia wakia 565,000 uchimbaji utaendelea kwa muda wa miaka mitano. Baadhi ya manufaa kwa Serikali kutokana na mgodi huo yatakuwa ni pamoja na malipo ya mrabaha dola za Marekani milioni 6, kodi mbalimbali dola za Marekani milioni 3 na ajira ya moja kwa moja kwa wananchi 600.

Mheshimiwa Spika, kampuni za *Barrick Gold Corporation* na *Falconbridge Limited* zilisaini makubaliano ya ushirikiano katika uendelezaji wa maradi wa Kabanga Nickel. Katika makubaliano hayo *Falconbridge* watakuwa waendeshaji wa mradi ambapo katika miaka michache ijayo wanatarajia kutumia dola za Marekani milioni 50 kwa ajili ya utafiti zaidi kwenye mradi huo. Tangu mradi uchukuliwe wawekezaji hao wamefanya kazi zaidi za utafutaji kwenye eneo hilo. Ni matumaini ya Wizara kuwa makubaliano kati ya kampuni hizo yatakelezwa na kuufikisha mradi katika hatua ya uzalishaji.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utafutaji wa madini, katika jitihada za kuwavutia wawekezaji kwenye maeneo mengine ya nchi, mwaka 2003/2004 Wizara yangu ilikamilisha zoezi la ukusanyaji wa takwimu za kijiofizikia kwa njia ya anga katika maeneo ya Wilaya za Kahama, Bukombe, Biharamulo, Tarime na Mpanda. Kupatikana kwa takwimu mpya katika maeneo hayo kumeongeza hamasa kwa wawekezaji katika sekta ya madini kuzinunua kwa ajili ya kuboresha taarifa zitakazowasaidia katika utafutaji wa madini kwenye maeneo hayo. Baadhi ya kampuni kubwa ambazo zimeshanunua takwimu hizo ni *Barrick Exploration*, *Twigg Gold*, *Placer Dome* na *COPACABANA*.

Mheshimiwa Spika, kazi ya ukusanyaji wa takwimu za kijiolojia, kijiomeria na kijiofizikia katika maeneo ya Wilaya za Kahama Bukombe na Biharamulo zimekamilika kwa asilimia 62. katika mwaka huu wa fedha juhudi zitaelekezwa katika kukamilisha kazi ya ukusanyaji wa takwimu kwenye maeneo hayo. Aidha, katika kipindi hicho ukusanyaji wa takwimu utanza katika maeneo ya Wilaya ya Mpanda.

Mheshimiwa Spika, kuhusu *Tanzania Geological Survey (TGS)*, mwaka 2003/2004 nililiarifu Bunge lako Tukufu kuwa, kwa mujibu wa muundo wa Wizara ulioidhinishwa mwaka 2001 Kitengo cha *TGS* kinatakiwa kuwa Wakala wa Serikali.

Hadi sasa kimekubalika kuwa Wakala na kinaitwa *Geological Survey of Tanzania (GST)* na Mtendaji wake Mkuu amekwishapatikana. Katika mwaka huu wa fedha, Kitengo kitaendelea na majukumu yake ya kukusanya, kuchambua na kuhifadhi taarifa za

kijiolojia. Aidha, Kitengo kimejiimarisha kutoa huduma za kijiolojia na maabara kwa wadau.

Mheshimiwa Spika, Kitengo cha *TANSORT* sasa kinaendesha shughuli zake kama vitengo vingine vya Serikali. Kuanzia mwaka 2004/2005 Kitengo hicho kimekuwa kinapatiwa fedha za matumizi ya kawaida kupitia katika Bajeti ya Serikali na kukusanya mapato yanayotokana na tozo ya kuchambua almasi za kampuni ya *Williamson Diamonds* ili kuyaingiza katika mfuko wa Serikali. Aidha, katika kuimarisha utendaji wa kazi wa Kitengo hicho, kuanzia mwaka huu Kitengo hiki kimepatiwa kifungu cha matumizi katika bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini.

Mheshimiwa Spika, kuhucu Chuo cha Madini, kwa kuzingatia umuhimu wa ukuaji wa Sekta ya Madini nchini, Wizara yangu inakiimarisha Chuo cha Madini kilichoko katika Manispaa ya Dodoma, eneo la Mbwanga. Chuo kinatoa mafunzo ya miaka mitatu ya ufundi sanifu, *Full Technician Certificate (FTC)* katika fani za Uhandisi wa Migodi (*Mining Engineering Technology*), uchenjuaji wa madini (*mineral Processing Engineering Technology*) na jiolojia na utafutaji wa madini (*Geology and Mineral Exploration Technology*).

Chuo cha Madini kilisajiliwa mwezi Februari, 2005 na Baraza la Vyuo vya Ufundu nchini (*NACTE*). Baada ya kupata usajili wa kudumu, chuo sasa kinakamilisha taratibu za kutambulika kitaalum (kupata *accreditation*) kwa Baraza la Vyuo vya Ufundu nchini. Aidha, Wizara iko katika zoezi la kuajiri walimu na watumishi wengine ili kuongeza idadi ya watumishi chuoni. Katika mwaka 2005/2006 Chuo kitaendelea kujenga miundombinu muhimu inayohitajika katika kukiimarisha. Maendeleo ya Utumishi, Wizara inao watumishi 603 ambao wameajiriwa katika fani mbalimbali. Kutohana na kupanuka kwa shughuli za Wizara, Serikali imeidhinisha watumishi wapya 81 waajiriwe katika mwaka wa fedha 2005/2006. Katika kujenga uwezo wa kutimiza majukumu yake, mwaka 2004/2005 wizara iliwapeleka katika mafunzo ya muda mrefu na mfupi watumishi 72. Katika mwaka wa fedha 2005/2006 wizara imetenga fedha kwa ajili ya mafunzo kwenye kila idara na kitengo.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2005/2006 wizara itatoa mafunzo ya mapitio na upimaji wa wazi wa utendaji wa kazi (*OPRAS*) kwa watumishi wote wa Wizara ili waweze kujua utaratibu mpya wa upimaji utendaji kazi wao. Wizara tayari imeunda Kamati ya Jinsia yenye ujumbe kutoka idara na vitengo mbalimbali vya Wizara ili kusimamia masuala ya jinsia sehemu za kazi. Pia, Kamati Maalumu ya Ajira imeundwa ili kushughulikia ajira, kupandisha vyeo na kuthibitisha kazini watumishi mbalimbali Wizarani. Aidha, Wizara imeanza kuwassaidia kwa kuwapatia mahitaji muhimu kiafya waliojitokeza kuwa waathirika wa UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, ushirikiano wa Kimataifa, katika mwaka 2004/2005 sekta za nishati na madini zilinufaika na misaada ya wafadhili mbalimbali. Hivyo, kwa niaba ya Serikali napenda kutoa shukrani kwa Serikali za nchi na mashirika ya kimataifa kwa ushirikiano na misaada waliyotoa kwa ajili ya kuendeleza sekta hizo. Naomba nizishukuru Serikali za Australia, China, Denmark, Finland, Hispania, India, Japan,

Canada, Marekani, Norway, Sweden, Ubelgiji, Ufaransa, Uholanzi, Uingereza na Ujerumanii. Aidha, natoa shukrani kwa Umoja wa Mataifa (*UN*) na Umoja wa Nchi za Ulaya (*EU*), Benki ya Dunia, Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB*), Benki ya Rasilimali ya Ulaya, *DANIDA*, *Global Environment Facility*, *IAEA*, *IMF*, *KFW*, *NDF*, *NORAD*, *Sida*, *UNDP*, *UNESCO*, *UNIDO* na *USAID*. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hili ndilo Bunge letu la mwisho la awamu ya tatu, ningependa kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa ushirikiano wao mkubwa tangu mwaka 1995 nilipoingia Bungeni kwa mara ya kwanza. Ni matarajio yangu kuwa Wabunge wengi tulipo hapa sasa tutarejea tena mara baada ya uchaguzi wa mwazi Oktoba, 2005. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru viongozi wenzangu ambaa kwa pamoja tumeweza kufanikisha shughuli za Wizara kwa mwaka 2004/2005. Kwanza napenda kumshukuru Mhe. Dr. Ibrahim Msabaha, Naibu Waziri kwa msaada wake mkubwa alionipa katika kusimamia shughuli za Wizara. Napenda pia kuwashukuru Katibu Mkuu, Bwana Patrick Rutabanzibwa, Makamishna, Wakurugenzi na Wakuu wote wa Idara na Vitengo, viongozi wa mashirika yaliyo chini ya Wizara wakiwemo Wenyeviti na Wajumbe wa Bodi na Watendaji Wakuu. Kamati zinazosimamiwa na Wizara na wafanyakazi wote wa Wizara ya Nishati na Madini.

Kabla sijatoa majumuisho ya hotuba yangu ningependa kuishukuru familia yangu kwa kuniunga mkono kikamilifu kwa miaka yote 10 ambayo nimekuwa mwanasiasa. Aidha, nawashukuru wananchi na wapiga kura wote wa jimbo la Same Mashariki kwa kunichagua mara mbili kuwa Mbunge wao tangu 1995 hadi sasa 2005. Katika miaka 10 hiyo tumeshirikiana na kubadili sura ya jimbo hilo kwa kiwango kikubwa kimaendeleo hasa katika kuboresha huduma za jamii na za kiuchumi. Ni matumaini yangu kuwa kutokana na uzoefu huo tutaendelea kujenga jimbo letu kwa kasi kubwa zaidi katika miaka ya usoni. (*Makofî*)

Hotuba hii ina majedwali ambayo yanatoa taarifa au takwimu zaidi kuhusu baadhi ya mambo niliyoyagusia. Nawaomba Wabunge wayasome ili wapate uelewa zaidi. Sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali na kuidhinisha mapendekezo ya Bajeti ya Sh.131,914,614,631,000 kwa ajili ya matumizi ya Wizara na mashirika yake kwa mwaka 2005/2006. Mchanganuo wa Bajeti hiyo ni kama ifuatavyo:-

- (i) Bajeti ya Maendeleo ni Sh.101,361,504,500 ambazo kati yake Sh.5,900,000,000 ni fedha za hapa na Sh.95,461,504,500 ni fedha za nje; na
- (ii) Bajeti ya Matumizi ya kawaida ni Sh.30,553,126,500 ambapo Sh.1,280,126,000 ni kwa ajili ya mishahara (*PE*) na Sh.29,273,000,500 ni matumizi mengineyo (*OC*).

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

WAZIRI WA AFYA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MHE. HERBERT J. MNTANGI (k.n.y. MHE. WILLIAM H. SHULLUKINDO - MWENYEKITI WA KAMATI YA UWEKEZAJI NA BIASHARA): Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, naomba kutoa maoni na mapendekezo ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara, kuhusu mapendekezo na malengo ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, naomba kutoa shukrani kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara, kuhusu mapendekezo ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2005/2006, kwa mujibu wa kanuni Namba 81(1) ya mwaka 2004.

Wizara ya Nishati na Madini ilipangwa kukutana na Kamati tarehe 31 Mei, 2005, tarehe hiyo Kamati haikuweza kuchambua bajeti hiyo kwa vile ilihitaji kupata ufanuzi katika masuala yafuatayo: Kwanza, Shirika la Maendeleo ya Petroli Nchini (*TPDC*), kutotengewa fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Pili, Jengo la Mafuta (*Mafuta House*), lililojengwa kwa pamoja na Mashirika ya *TPDC* na Shirika la Nyumba Tanzania (*National Housing Corporation*), kutolewa bure kwa Shirika la Hifadhi ya Jamii (*NSSF*). Tatu, taarifa rasmi ya Serikali kuhusu Mradi wa kuzalisha Umeme wa *IPTL*. Nne, Taarifa rasmi ya Serikali kuhusu mapato yanayotokana na mchakato wa mchango huko Japan unaotoka kwenye machimbo ya dhahabu.

Mheshimiwa Spika, Wizara ilifika tena mbele ya Kamati tarehe 6 Juni, 2005 ikiwa na ufanuzi wa masuala hayo na hivyo kuiwezesha Kamati kuchambua mapendekezo ya Wizara hiyokwa mwaka 2005/2006. Kamati imeridhishwa na hatua mbalimbali zilizofikiwa na Wizara katika kutekeleza ushauri uliotolewa na Kamati wakati inachambua Bajeti ya Wizara hii katika mwaka 2004/2005. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sote tunaelewa umuhimu wa madini katika uchumi wa Taifa letu na pia mahitaji makubwa ya nishati tuliyonayo na faida kubwa inayoweza kupatikana kutokana na kuuza mafuta gesi asilia. Ili kusimamia utekelezaji wa mambo hayo muhimu, Wizara na Mashirika yake imeomba iidhinishiwe fedha chini ya Fungu Namba 58 kama ifuatavyo: Fedha za matumizi ya kawaida shilingi 30,553,126,500/= na fedha za matumizi ya maendeleo shilingi 101,361,504,500/. Jumla ya maombi yote ni shilingi 131, 914, 631,000/=.

Mheshimiwa Spika, baada ya kupata maelezo ya Wizara kuhusu vipengele vilivyotajwa vilivyo hitaji ufanuzi, pia baada ya kuitia mapendekezo ya bajeti ya mwaka 2005/2006, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

Kwanza, Shirika la Maendeleo ya Petroli (*TPDC*), kisheria lina wajibu mkubwa wa utafutaji na uendelezaji wa nishati ya petroli nchini, pamoja na kuiwasilisha Serikali kwenye maeneo ya uchimbaji wa bidhaa za mafuta ya petroli na gesi asilia. Hivyo basi,

Kamati inashauri kuwa, Shirika hilo lipewe fedha shilingi bilioni mbili ilizoomba kwa mwaka 2005/2006 ili liweze kutekeleza majukumu ya kutafiti na kutafuta mafuta.

Pili, Shirika la Maendeleo ya Petroli (*TPDC*) na Shirika la Nyumba la Taifa (*National Housing Corporation*), yote ni Mashirika yanayoendelea na majukumu yaliyoundiwa. Mashirika hayo mawili yaliingia ubia ili kujenga jengo la mafuta (*Mafuta House*), lakini Serikali iliamua kulitoa jengo hilo bure kwa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (*NSSF*). Hadi Serikali inafikia uamuzi wa kulitoa Jengo hilo kwa *NSSF*, mashirika hayo ya umma yalikuwa yamewekeza kwenye jengo hilo kama ifuatavyo: *TPDC* shilingi 14,121,537,308/= na *National Housing Corporation* shilingi 1,673,577,456=/. Jumla ni shilingi bilioni 15,795,114,764=/. Aidha, madeni ya *TPDC* na *National Housing Corporation* yaliyohamishiwa *NSSF* ni shilingi 4,267,295,322=.

Mheshimiwa Spika, Kamati haikubaliani na uamuzi huo wa kulitoa bure jengo hilo kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, *TPDC* na Shirika la Nyumba ni Mashirika ya Umma yanayomilikiwa na Watanzania wapatao milioni 35 na yanatoa gawiwo kwa Serikali wakati *NSSF* ni Taasisi ya Kijamii yenye wanachama 346,664 tu na haitoi gawiwo kwa Serikali. Hivyo, si busara kuwanyang'anya Watanzania milioni 35 mali yao na kuigawa kwa wanachama wachache. (*Makofî*)

Jengo la *Mafuta House* sehemu ya chini ilijengwa kwa minajili ya kuhifadhi takwimu muhimu zinazohusu utafiti wa mafuta. Hivyo, ni vizuri sehemu hiyo ikaendelea kwa matumizi hayo yaliyokusudiwa ili kuepukana na gharama kubwa za kutunza takwimu hizo nje ya nchi. Hivi sasa takwimu hizo zimesambazwa katika nchi mbalimbali zikiwemo Canada, Italia, Ufaransa, Norway na Uingereza. Thamani ya takwimu hizo kwa kuhifadhi ni dola za Kimarekeni 595 milioni kwa mwaka. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kamati ina taarifa kwamba, siku za awali *NSSF* iliombwa kuingia ubia kwenye ujenzi wa jengo hilo lakini ilikataa kwa kueleza kuwa haikuwa na mahitaji nayo.

Mheshimiwa Spika, Mashirika yote hayo yaliundwa kisheria, hivyo, uamuzi wa kugawa mali zao, ungefanywa kisheria vilevile. Aidha, vitabu vyta hesabu vyta *TPDC* na Shirika la Nyumba, vinaonesha kwamba, bado wamewekeza kwenye Jengo la Mafuta maana utaratibu wa kuhamisha uwekezaji wa mali za shirika unatakiwa kufanywa kisheria na Mhifadhi wa Mali ya Taifa (*Custodian of Government Assets and Properties in Parastatal Enterprises*), ambaye ni msajili wa Hazina. Hivyo basi, Kamati inashauri yafuatayo:-

Kwanza, kwa kuwa mashirika ya *TPDC* na *National Housing Corporation*, yamewekeza kiasi cha shilingi bilioni 15.7 katika Jengo la Mafuta, basi fedha hizo zigeuzwe kuwa hisa na kuendelea kuwa mionganoni mwa wenyewe miliki katika kitega uchumi hicho. (*Makofî*)

Pili, kama ushauri katika sehemu hiyo ya kwanza hapo juu haukuliki, basi *TPDC* na *National Housing Corporation*, warejeshewe fedha hizo na kwamba, madeni ya shilingi bilioni nne yaliyochukuliwa na *NSSF*, yakatwe kwenye marejesho hayo ya shilingi bilioni 15.7.

Tatu, kuhusu eneo la Jengo la Mafuta, ambalo liliwekwa mahususi kwa ajili ya kuhifadhi takwimu na miamba ya nishati ya mafuta, lipewe Serikali ili litumike kwa madhumuni yaliyolengwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Serikali imeeleza hatua zilizochukuliwa na zinazoendelea kuchukuliwa ili kuweza kununua mitambo wa kuzalisha umeme wa *IPTL*. Kununua mitambo hiyo kutaipushia Serikali kulipa *Capacity Charge* ya zaidi ya shilingi bilioni 2.6 kila mwezi. Kamati imefurahishwa na jitihada hizo za Serikali, ikiwa ni pamoja na mkakati wa kubadili mitambo ya *IPTL* kuanza kutumia gesi asilia badala ya mafuta, hatua ambayo itawezesha kupunguza gharama za kuendesha mitambo hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kamati pia inaishauri Serikali, ifuatilie kwa makini, makubaliano ya Mikataba ya *Songas* ili mitambo zaidi ya uzalishaji wa umeme ijengwe kwa nia ya kutimiza azma ya kuwa na umeme wa ziada, ambao utaweza kuuzwa nje ya nchi. Kamati imeridhishwa na utaratibu uliowekwa na Serikali katika kuratibu na kudhibiti mapato yatokanayo na mchanga toka kwenye machimbo ya dhahabu na kufanyiwa mchakato zaidi huko Japan. Serikali imeeleza kuwa kutokana na mchakato huo, toka mwaka 2001 imepata mapato kama ifuatavyo: Kutokana na Shaba dola za Kimarekani 35,214,320.26; kutokana na Fedha dola za Kimarekani 300,498,216.98; kutokana na Dhahabu dola za Kimarekani 247,485,395.29 na kutokana na Mrabaha dola za Kimarekani 7,440,438.8.

Kwa vile kumekuwa na minong'ono mingi mionganoni mwa Watanzania kuhusu mchanga huo unaopelekwa Japan, Kamati inaishauri Serikali ichukue hatua za kuelimisha Wananchi kuhusu hali hiyo. Pamoja na hayo, Kamati inaishauri Serikali izishawishi nchi za Kusini Mashariki mwa Afrika, kuititia Taasisi ya *Southern and Eastern African Mineral Centre (SEAMIC)*, ili ziweze kuyashawishi makampuni yajenge kiwanda cha kufanyiwa mchakato wa mchanga katika kanda hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kamati imeridhishwa na hatua za Serikali ya kuiweka *Tanzania Government Diamond Sorting Organization (TANSORT)*, iliyoko London Uingereza kuwa ni kitengo katika Wizara hiyo. Hatua hiyo inatarajia kuliongezea Taifa mapato zaidi kutokana na udhibiti wa shughuli zake. Kamati inaishauri Wizara iharakishe uteuzi wa Mtendaji Mkuu wa Taasisi hiyo.

Mheshimiwa Spika, Kampuni ya *At rib Resources* ya Canada, imeshindwa kuendelea na kazi ya utafutaji wa mafuta huko Tanzania Visiwani kutokana na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kutaka kwanza yafanyike mazungumzo ili shughuli za mafuta ya gesi asilia isiwe suala la Muungano. Kamati inazishauri Serikali hizi mbili, zihakikishe katika kumaliza mazungumzo na kufikia makubaliano kwa kuzingatia kwamba, Kikatiba suala la mafuta na gesi asilia ni suala la Muungano. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inapendekeza kwamba, Serikali iifanyie marekebisho Sheria ya *Petroleum Exploration and Production* ya mwaka 1980 ili iendane na hali ya sasa ya utafutaji wa mafuta. Ni vizuri Serikali pia iyapitie marekebisho ya Sheria hiyo. Kwa vile sasa shughuli za utafutaji wa mafuta ya gesi asilia umekuwa dhahiri, Kamati inashauri itungwe sheria itakayoshughulikia masuala ya gesi asilia na hivyo kuhusisha vipengele vingi zaidi vinavyohusu gesi asilia.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na mgogoro wa mara kwa mara kati ya Kampuni ya *Williamson Diamonds Limited* na Kampuni ya *Hilary Minerals Limited*. Kamati inashauri Serikali isimamie na kusuluuhisha migogoro hiyo haraka ili isiathiri uzalishaji wa Almasi nchini.

Mheshimiwa Spika, vilevile Sekta ya Madini imeanza kukua kwa kasi kubwa, si vizuri kuwepo na Maafisa wanaokaimu katika nafasi zao, hivyo, Kamati inaishauri Wizara kuwa nafasi ya Kamishna wa Madini ijazwe haraka ili mhusika aweze kutumia Sheria kwa kujiamini katika shughuli hizo za madini.

Mheshimiwa Spika, napenda kumshukuru Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Daniel Yona, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Katibu Mkuu, Ndugu Patrick Rutabanzibwa na Wafanyakazi wote wa Wizara, kwa maandalizi mazuri ya taarifa na pia katika ushirikiano ambao wameutoa kwa Kamati hii, wakati wote tukiwa tunashughulikia masuala ya Wizara hii. Aidha, tunamshukuru Waziri, kwa kuwezesha baadhi ya Wajumbe wa Kamati hii, kwenda Namibia na Botswana ili kuona jinsi Serikali za nchi hizo zinavyoendeleta shughuli za madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maoni na ushauri uliotolewa umetokana na juhudi na bidii ya Wajumbe wenzangu wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, ambao walitoa michango yao kwa umakini mkubwa. Napenda kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo:-

Mwenyekiti wa Kamati hii ni Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mheshimiwa Salome Joseph Mbatia ni Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Khamis Awesu Aboud, Mheshimiwa Fatma Said Ali, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Omar Chubi, Mheshimiwa Ismail Iwatta, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Aisha Magina, Mheshimiwa Freeman Mbewe, Mheshimiwa Ali Machano Mussa, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Nazir Mustafa Karamagi, Mheshimiwa Mohamed Ali Said, Mheshimiwa Dr. James Wanyancha, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Christopher Wegga, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Marehemu Mheshimiwa Margareth James Bwana na mimi mwenyewe, Mheshimiwa Herbert James Mntangi.

Mheshimiwa Spika, naomba pia nimshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Damian S. Foka, kwa kuiwezesha Kamati hii kufanya kazi zake vizuri, vile vile napenda kumshukuru Ndugu Aggrey Nzowa, kwa kuihudumia vizuri Kamati hii wakati inachambua Bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kamati ya Uwekezaji na Biashara, naunga mkono hoja na ninaomba kuwasilisha. (*Makofii*)

MHE. ISAAC M. CHEYO - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Spika, kwa mwaka mwininge tena wa kujadili bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini, nasimama hapa kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, kutoa maoni yetu kwa mujibu wa Kanuni za Bunge kifungu cha 43(5) (b) (c), toleo la 2004.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri na Wataalam, kwa kuiandaa bajeti yao ya kutuomba tuwapeSh. 30,553,126,500/= za kutekeleza na kusimamia mipango iliyopangwa chini ya ofisi yao kwa kipindi cha mwaka 2005/2006 kama matumizi ya kawaida na Sh.101,361,504,500/= kwa matumizi ya kuendeleza miradi ya maendeleo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2005/2006 na hivyo ufanya jumla ya Sh. 131,914, 631,000/=.

Mheshimiwa Spika, kama kuna nchi ambayo Mwenyezi Mungu, alijali na kuipa kwa wingi vyanzo vya nishati, hakuna nchi zaidi ya Tanzania katika bara hili la Afrika. Tuna maporomoko ambayo hayajaendelezwa, tuna gesi, tuna wanyama ambao wanawenza kutoa *biogas*, tuna taka za kila aina, ambazo zikitumika tunaweza kutengeneza nishati kwa matumizi mbalimbali mijini, vijijini, majumbani na viwandani. Pamoja na vyote hivi, Watanzania zaidi ya asilimia 90 bado wanatumia nishati mkaa. Madhara ya nishati mkaa wote tunayafahamu. Hawa ndiyo walipa kodi na wazalishaji wa mazao ya kilimo. Mchango wao kwenye Pato la Taifa ni mkubwa kuliko sekta nyingine za uzalishaji. Kwa akili ya kawaida, maendeleo yao yanekua kwa haraka zaidi kama kungekuwa na mabadiliko ya nyenzo nishati huko waliko.

Mheshimiwa Spika, tukiangalia maendeleo ya nishati, yameelekezwa zaidi kwenye miji kuliko kwenye maeneo ya vijijini wanakoishi Watanzania wengi. Kwa maneno mengine, wanaochangia kwa asilimia kubwa katika uchumi wa nchi hawapati mgawo wa kuwarahisishia maendeleo yao, kwa kuwajengea miundombinu nishati ili na wao waonje raha ya kuwa na umeme.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba, umeme umeelekezwa mijini na maeneo machache ya vijijini, ujenzi wa miundombinu hiyo ni wa aghali sana, ukilinganisha na endapo Serikali ingeendeleza miundombinu ya nishati mbadala kwa kutumia vyanzo vingine kama vile umeme wa sua, umeme wa *biogas/biomass* na kadhalika. Huu ni umeme ambao hautakuwa ghali kwa matumizi ya vijijini.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004 tulipitisha Sheria hapa ya kuunda wakala wa umeme vijijini, ukiwa na malengo ya kurahisisha upatikanaji wa nishati umeme vijijini. Lakini hadi leo hakuna dalili zinazoonesha *Rural Energy Agency* yoyote iliyopewa leseni ya kujenga na kuendeleza miundombinu ya umeme vijijini. Tunaamini hili likifanywa

haraka, Wananchi wetu huko vijijini, watafaidi na kupata unafuu kwa maendeleo yao. Tumetunga sheria na kukaa kimya.

Mheshimiwa Spika, Serikali sharti ibadilike katika kutekeleza mipango yake. Serikali lazima ikubali kuwa ukiritimba wa kibashara umepitwa na wakati. Sasa ikubali na kuwasaidia watu binafsi na wabia kujenga na kuendeleza miundombinu ya nishati umeme kibashara. Awe mtu binafsi au mbia, aruhusiwe kutafiti na kujenga miundombinu hiyo popote pale vijijini anapoona anaweza kufanya hivyo na kupata faida na Wananchi wakapata nishati hiyo kwa bei nafuu. Ukiritimba wa kila kitu kifanywe na *TANESCO* ni kuchelewesha kuwapatia umeme Wananchi wetu huko vijijini. Tutumie mawakala kufikisha umeme vijijini, hili liwe la kwanza katika mipango yetu.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wote tunafahamu umeme wote unaouzwa na *TANESCO* ni kwa ajili ya Watanzania wasiozidi asilimia 10, licha ya gharama kubwa za ujenzi wa miundombinu hiyo. Shirika la Umeme (*TANESCO*) ni Shirika linalotakiwa kujiendesha lenyewe bila ya Serikali kukopa fedha nyingi na kuzipeleka *TANESCO*. Sote tunajua kama Shirika ni la kibashara na linatengeneza faida, Shirika hilo linawezza kujiendesha lenyewe bila ya Serikali kukopa fedha za kuliendesha. Ili kuliendesha Shirika la *TANESCO*, Serikali imekopa shilingi milion 620, busara ya kawaida haikubali kuwa, Serikali inakopa ili kuliendesha Shirika linalotengeneza faida, hapa kuna walakini!

Mheshimiwa Spika, kuna mrija unaitwa *IPTL* ndani ya *TANESCO*, kila Mtanzania anafahamu ujio na sababu za kuwepo kwake. Hatuna sababu ya kurudia maelezo ya kwa nini *IPTL* ipo, kinachotupa tatizo ni nani hasa anaimiliki. Kama *IPTL* ni kampuni binafsi na kwamba ina Mkataba wa kuuza umeme kwa *TANESCO*, basi gharama za kuiendesha *IPTL* au kuibadili kutoka hali iliyonayo ya kuzalisha umeme kwa kutumia mafuta kwenda kwenye kutumia gesi, mabadiliko hayo ni lazima yafanywe na mwenye mali, yaani *Independent Power Tanzania Limited (IPTL)*, kwa gharama zake na siyo kwa gharama za mteja.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa kupitia *TANESCO* ni mteja wa *IPTL* na Serikali inalipa mabilioni ya fedha kwa *IPTL* kila mwezi. Hivyo, siyo halali kwa Serikali kukopa shilingi bilioni 16 kwa ajili ya kubadili mitambo ya *IPTL* kutoka matumizi ya mafuta kwenda matumizi ya gesi.

Mheshimiwa Spika, kuna mashaka juu ya *who owns IPTL*. Kuna kitu kimefichwa, Watanzania hatukijui. Kama *IPTL* ni mali ya Serikali, hatuna sababu ya kuuliza maswali mengi lakini kama *IPTL* ni *Private Company*, tuna kila sababu ya kuhoji kwa nini Serikali itumie shilingi 16 bilioni kubadilisha mitambo ya *IPTL*? Pesa hiyo ingeelekezwa kwenye ujenzi wa njia ya umeme Makambako - Songea ambako hadi leo wanatumia *Thermol Power*.

Mheshimiwa Spika, Miji ya Ngorongoro, Kilolo na Ludewa, wanahitaji shilingi bilioni 12.72 kwa ujumla wao. Miji ya Kasulu, Kibondo na Simanjiro, wanahitaji shilingi bilioni 10.2 kwa ujumla wao na pia Nkasi, Rufiji na Kilindi, wanahitaji shilingi bilioni

8.92 kwa ujumla wao; kwa nini isiwe ni *priority* katika miji hiyo kwanza badala ya kupeleka shilingi bilioni 16 kwa *IPTL*?

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004 tulisema sana juu ya utafiti wa mafuta mwambao wa Pwani ya Tanzania, pamoja na ule wa baharini. Tulielezea jinsi makampuni yaliyopewa leseni na *TPDC* ya kutafiti mafuta katika bahari na hasa huko Pemba kuwa, yameshindwa kufanya hivyo kwa sababu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, haitaki makampuni hayo yafanye tafiti hizo kwa kisingizio kuwa mafuta siyo suala la Muungano.

Mheshimiwa Spika, Watanzania wote tumekubali kwamba, mambo yote ambayo ni ya Kimuungano yatafanywa na makampuni ya Kimuungano. Utafiti wa mafuta ni suala la Kimuungano kufuatana na jedwali la nyongeza ya kwanza iliyoko katika Katiba yetu. Leo iweje jambo la Kimuungano ambalo limo kwenye Katiba inayoheshimiwa na Serikali zetu, lizuiwe na upande mmoja wa Jamhuri?

Mheshimiwa Spika, kuzuiwa kwa makampuni yaliyopewa leseni na *TPDC* kufanya utafiti wa mafuta, ni kuchelewesha shughuli lakini kwa upande mwingine, kutokuruhusu kufanyika kwa shughuli hizo ni kuvunja Katiba. Katika ibara ya nne ya Katiba, yametajwa mambo ambayo ni ya Muungano. *Item* ya 15 katika *schedule* inasema, mambo ya Muungano ni pamoja na maliasili ya mafuta, mafuta yasiyochujwa ya motokaa na mafuta ya aina ya petroli na aina nyinginezo za mafuta au bidhaa za gesi asilia

Mheshimiwa Spika, kama kweli Serikali mbili zilikubaliana hivyo, kwa nini leo upande mmoja wa Muungano uone kama siyo sahihi kwa *TPDC* kutoa leseni ya utafiti? Hili ni suala tulilokubaliana sote. Tunaitaka Serikali itoe ufanuzi ili kutoa mashaka kwa upande wa pili wa Jamhuri Muungano kuwa suala la mafuta halikuingizwa kinyemela kwenye mambo ya Muungano na Kamati imeshaonesha pale.

Mheshimiwa Spika, Muungano wetu tunaupenda na tungependa udumu, njia ya kufika hapo ni kuondoa maeneo yote yanayoleta shaka. Serikali ikae ilette Muswada wa kurekebisha kasoro hizo kwa manufaa ya Watanzania wote. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, suala la *Mafuta House*, naona sina sababu ya kulizungumzia kwa sababu Kamati imelizungumzia. Kwa hiyo, tunategemea Mheshimiwa Waziri, atalipa Bunge hili sababu maalum. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, mpango mzima wa Jeshi letu kuingia Mkataba wa uchimbaji madini siyo tatizo. Tatizo ni jinsi MEREMETA ilivoingia na baadae kujibadili kuwa kampuni ya kuchimba madini sawa na kampuni nyingine kwa kupitia mgongo wa Jeshi.

Mheshimiwa Spika, MEREMETA ilipoanzishwa kwa mara ya kwanza, malengo yake yalikuwa ni kuwa, mbia na Jeshi wa kununua dhahabu kutoka kwa wachimbaji wadogo wadogo, pamoja na kuwapatia vitendea kazi ili kurahisisha shughuli zao. Jambo hili lilimfurahisha kila mwananchi, pia Jeshi lilifaidika na mpango huu.

Mheshimiwa Spika, miaka ya karibuni, MEREMETA imejitoa katika malengo yake ya awali na kuwa kampuni ya uchimbaji madini huko Kyabakari, imeacha majukumu yake ya awali na kuwaacha *solemba* wachimbaji wadogo wakiwa hawana tena mtu wa kuwasaidia na wala Serikali haizungumzii tena kuwa nani atawasaidia wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, lingekuwa jambo la busara kwa meremeta kuendelea na kutoa huduma hiyo kwa wachimbaji wadogo wadogo kwa kuwapatia nyenzo na soko kwa madini wanayochimba.

Mheshimiwa Spika, suala la dhahabu ya *Kahama Mining* kupelekwa Japan, limeendelea kuzua mjadala kwa Watanzania wengi. Leo nchi ina machimbo mengi ya dhahabu, yaani huko Geita, Bulyankhulu, *Afrika Mashariki Gold Mine* (Musoma), Lusu (Nzega), Kyabakari (Musoma) na kadhalika; mbona dhahabu ya Bulyankhulu pekee ndiyo inasafirishwa kwenda Japan kwa ajili ya kutenganishwa, mbona dhahabu toka migodi mingine haipelekwi huko? (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, Mgodi wa Kahama ambao asilimia 100 unamilikiwa na *Barrick*, una dhahabu nyingi kuliko mgodi mwingine wowote hapa nchini. Tunategemea kama dhahabu yote inayochimbwa Kahama na kuuzwa kama ilivyo katika machimbo mengine, pato kupitia mrabaha lingekuwa ni kubwa kuliko ambalo leo tunatangaziwa. Dhahabu inayosafirishwa kwenda Japan hatuna *control* nayo, isipokuwa ni kupewa taarifa ya utenganisho wa madini (*copper, silver, sulphur and gold*). Hatuna uthibitisho wa dhahiri ni kiasi gani cha dhahabu kimepatikana baada ya kuchujwa, kiasi gani kimepatikana kutokana na madini mengine kama *silver, copper* na kadhalika, baada ya kutenganishwa. Hata mrabaha uliopatikana hatuna uhakika ni kiasi gani kimepatikana kutokana na mauzo.

Mheshimiwa Spika, kwa kupitia Bunge lako Tukufu, tunapendekeza yafuatayo: Kuwepo na *monitoring team*, ambayo itajua ni kiasi gani cha dhahabu inayopatikana baada ya kutenganishwa na madini mengine na yameuzwa kwa bei gani na nchi imepata nini na Makampuni yote ya madini yawe *partly owned* na nchi. *At least 25 percent* ya milki ya machimbo iwe ya Serikali, hili lazima liwekwe kisheria ili kila kampuni inayochimba madini, wajue kwamba, yana ubia na Serikali ya Tanzania kwa manufaa ya nchi.

Mheshimiwa Spika, madini ni mali inayokwisha, siyo mali inayoweza kumea tena baada ya kuchimbwa, hivyo basi, tuyachimbe, tuyasafishe na tuyauze lakini asilimia 25 ya kinachopatikana, kiwe kwa ajili ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, dhana tunayopewa kila siku eti tunafaidi kwa mrabaha, ajira na kodi, hii ni sawa na kutoa mshahara mdogo kwa wachungaji na kuondoka na mali zote. Ukipachukua mali, wao wanabaki fukara na hawajui kulikuwa na nini, wataoneshana mashimo na kubakia na historia kuwa kulikuwa na madini, pia na wao wanabakia na mshangao kwa nini tuko maskini.

Mheshimiwa Spika, juzi hapa, Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais, anayeshughulikia Mazingira, alikuwa akijibu swalii la Mbunge aliyetaka kujua, kwa nini barabara huko Geita ilihamishwa na kupelekwa porini. Mheshimiwa Waziri alijibu kwa kejeli na kusema barabara lazima ipite porini. Jibu hili sidhani kama ni sahihi kwa Wananchi wa Geita. Hawa ni watu maskini, licha ya kuwa mgodi wa dhahabu uko Wilayani kwao, ukihamisha barabara na kuipeleka mbali, maana yake unawaongeza nauli na unawapeleka mbali na huduma.

Mheshimiwa Spika, hivi ni kweli hakuna uwezekano wa kujenga barabara ya kupita karibu na machimbo; mbona Mwadui wana barabara inayozunguka mgodi kwenda kwenye vijiji vya karibu na hawakuipeleka barabara hiyo porini?

Mheshimiwa Spika, Watanzania hawakuchagua kuwa maskini, Watanzania hawakuchagua kuwa karibu na machimbo haya, Wawekezaji wamewakuta na si sawa kunyanyaswa na wawekezaji hao. Pia siyo sahihi kwa Serikali kubariki unyanyasaji huo. Kama jibu la Waziri alilolitoa, Mheshimiwa Mbunge alikuwa anatafuta ni namna gani watu wake wafike Mjini Geita kwa urahisi na kwa gharama ndogo. Tunaitaka Serikali ilione tatizo hilo la watu wa Geita na kulipatia ufumbuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwisho, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani katika Bunge lako Tukufu. Nitakosa shukrani kama sitowashukuru Wananchi na wapiga kura wa Jimbo langu la Bariadi Magharibi, kwa kunipa vipindi viwili vya kuwawakilisha. Natumaini mategemeo yao nimeyafikisha na kwamba, sasa tunaingia kwenye uchaguzi mwingine, nitaendelea kuwaomba tushirikiane na tuiendeleze Bariadi na kuendeleza ushindi kwa mwenendo ule ule na *speed* ile ile iliyotumika katika chaguzi zilizopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hali inaonesha tutashinda na tutakutana tena mwezi Novemba, 2005. Mungu atulinde na tufike hapo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. Ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili na mimi nichangie hoja hii ya Waziri wa Nishati na Madini. Awali ya yote, napenda kusema kwamba, ninaunga mkono hoja hii kwa sababu Kamati yangu ya Uwekezaji na Biashara, imeunga mkono, isipokuwa nitapenda tu kusisitiza katika maeneo machache.

Jengo la Mafuta (*Mafuta House*) ni kitegauchumi kwa hiyo Mashirika mawili ya *TPDC* na *National Housing Corporation*, yalidhamiria kufanya hivyo. Sasa ni vizuri dhamira yao hiyo iheshimike. Pamoja na kwamba, Serikali ilichukua hatua za haraka kulinusuru jengo hilo, kwa sababu uwezo wa *TPDC* ulikuwa mdogo kuweza kuendelea kulimaliza jengo hilo. Lakini tatizo liko katika mkakati uliotumika (*strategy*) ya kulitoa bure.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono jinsi kabisa walivyolichambua na ushauri ulitolewa. Kamati imefanya vizuri kwa sababu haikusema jengo hilo lirudishwe *TPDC*, hapana. Tunataka hilo lieleweke waziwazi. Tunasema *NSSF* wana uwezo mkubwa wa fedha, kwa hiyo, Taasisi hii inaweza kushirikiana na Taasisi nyingine. Kwa hiyo, yale machaguo au *options* zifikiriwe. Ile ya kwanza ya kuheshimu hisa hizo ni mojawapo kama haikubaliki, nakubaliana na Kamati kwamba, waende ile ya pili ya kurudisha fedha hizo kwa wale waliowekeza hapo na sisi kama Kamati ya Uwekezaji na Biashara, tungependa taratibu hizi kwa kweli zitumike. Ni vema heshima ya kuwekeza kwa kweli iheshimiwe. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni hili la Gesi Asilia. Imedhihirika waziwazi kabisa kwamba, nchini kuna gesi ya kutosha kabisa. Imeshagunduliwa Songo-Songo na imeanza kutumika. Sasa hivi kuna mkakati wa kuhakikisha kwamba, ile gesi iliyoko *Mnazi-Bay* nayo inatumika.

Katika uchambuzi na utafiti tuliofanya, tumeona wazi kabisa kwamba, matumizi ya gesi yana gharama ndogo sana katika uzalishaji wa umeme na katika uzalishaji wa bidhaa. Kwa mfano, katika Kiwanda cha Sementi cha *Wazo Hill*, kwa kutumia umeme unaotokana na gesi, wameweza kupunguza gharama za uzalishaji kwa karibu dola milioni tano, ikiwa na maana kwamba, wakutumia mafuta (*jet fuel*), wanatumia dola milioni nane na walivyotumia gesi kwa muda wa miezi 10, wametumia dola milioni tatu tu, ikiwa ina maana kwamba, hapo kuna upungufu au kuna tofauti ya dola milioni tano. Kwa hiyo, tunaishauri Serikali kwa kweli ijitalidi zaidi kuhakikisha kwamba, tunapata gesi zaidi ili tuweze kupunguza gharama za uzalishaji wa umeme. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, tukiangalia Mtambo wa Uzalishaji Umeme Ubungo, kwa kutumia mafuta (*jet fuel*) kwa muda wa miezi 10, wanetumia dola za Marekani milioni 133. Lakini katika miezi 10, kwa kutumia gesi kuzalisha umeme wametumia dola milioni nne tu kwa maana ya kwamba, kuna tofauti hapo ya gharama ya uzalishaji kwa dola milioni 129. Kwa hiyo, hii ni nishati yenye nafuu kubwa sana. Kwa hiyo, tunaomba kwa kweli katika mipango yetu ya nishati, suala hili litiliwe maanani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema kwamba, gharama hizi zimepungua, tunataka kujuu kama bei ya umeme unaotoka Ubungo kwa gharama ndogo nao umepungua?

Mheshimiwa Spika, la pili, kwa kuwa uzalishaji wa sementi pale *Wazo Hill* kwa gharama ndogo, je, bei ya sementi ya *Wazo Hill* imepungua? Kama haikupungua, kwa kweli wenye viwanda lazima wawe waaminifu na wakweli. Kama gharama zimepungua basi na wao lazima wapunguze gharama za bidhaa zao ikiwa ni pamoja *TANESCO* vilevile. Isije ikafikia mahali kwa kweli Serikali inayafanyia Mashirika haya kazi nzuri, lakini gawio linakuwa dogo na nafuu ya gharama inakuwa kubwa zaidi kwenye Mashirika hayo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, sehemu ya tatu, ninayotaka kuchangia ni hili suala la uchimbaji wa madini hapa nchini. Inaelekea wawekezaji wengi sasa hivi wanakuja kuchimba madini. Serikali haijawekeza kwenye madini mahali popote na sasa hivi

hakuna uwezekano wa Serikali kuwekeza kwenye madini. Lakini ni vizuri Serikali iwe na vyombo vingine hapa nchini, ambavyo vingeweza kuwekeza kwa niaba yake. Kwa mfano, Shirika la Maendeleo la Taifa (*NDC*), lingeweza kujengwa kwa njia ambayo ingekuwa ni chombo cha kushiriki katika uwekezaji. Shirika la Maendeleo ya Mafuta (*TPDC*), nalo lingetumika kama chombo cha kuisaidia Serikali uwekezaji katika maeneo ya gesi na mafuta. Tusipofanya hivyo, tutashindwa kuelewa ndani kule kuna nini kwa sababu hatutashirikishwa kwenye maamuzi na taratibu na kubadilisha sera za wawekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, si vizuri tukakaa nje tu, tukawaachia tu wawekezaji waingie huko ndani kwenye machimbo wachimbe wala hatujui wamefika mpaka umbali gani chini ya ardhi? Wanaweza kuchimba wakafika mpaka Dar es Salaam sisi hatuna habari, kwa sababu hatuhusiki, wakaguzi wetu wa mambo ya kodi hawana ile nguvu ya kuingia ndani ya migodi. Lakini kama tunashiriki kwenye Bodi, tutaweza kujua nini kinafanyika. Nafikiri imefika wakati, maadam sasa hivi Sera ya Madini inaangaliwa upya, haya masuala yatazamwe kwa kweli na sisi tunashauri kabisa kwamba, huu ndio wakati mzuri wa kuangalia yale makosa ambayo tumeyafanya na ambayo hatukuyafanya kwa makusudi ila ni kwamba hatukuwa na uzoefu tuyarekebishe. Madini si sekta ya kawaida kwa watu wa kawaida wa Tanzania. Sisi kazi yetu ya kawaida ni kilimo tu, tunalima juu ya ardhi, wenzetu wamejifunza kuingia kutafuta utajiri chini ya ardhi, ambapo tulikuwa hatuna uwezo huo. Kwa hiyo, hili lingetazamwa hapo upya kisera ili nchi ishiriki kwa kurumia *NDC*, *TPDC* na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, upande wa pili wa uchimbaji wa madini nadhani imefika wakati sasa tutumie uhuru wetu wa kusema ni kipi kifanyike na kipi kisifanyike. Kuhusu madini, napenda kushauri kabisa kwamba, suala la uchimbaji wa vito vya thamani (*gemstones*) liwe ni kwa Wazalendo tu. Nasema hivi kwa sababu hakuna gharama kubwa sana ya uwekezaji. Ni kufukua fukua tu. Hivi mtu aje awekeze kwenye kufukua fukua tu. Tuachenii tufukue fukue wenyewe tu, kazi hiyo tunaiweza hata kwa kutumia majembe ya mkono na sururu. Tunaweza kutumia vito hivi vikasaidia kupunguza umaskini. Hasa nazungumzia wachimbaji wadogo wa Mererani. Kamati ya Uwekezaji na Biashara ilitembelea huko, tuliona hali ilivyo mbaya kwa wachimbaji wadogo. Kazi ile wanaweza kuifanya kwa kusaidiwa nyenzo kidogo, wanaweza kuunganishwa kwenye vikundi wakawenza kusaidiwa hata kuchukua mikopo ili wafanye kazi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, napendekeza kabisa na ninaomba Waheshimiwa Wabunge, mniunge mkono kwamba, vito vya thamani viwe ni kwa ajili ya Wazalendo tu. Almasi, dhahabu na *tin*, hayo tuwaachie wakubwa kwa sababu uwekezaji wake ni mkubwa zaidi. Lakini vito vidogo vidogo, hivi pale Jimbo la Bumbuli, Wananchi walikwenda kwenye Msitu wa Hifadhi wakafukua fukua na kupata dhahabu. Hivi tulete mwekezaji kweli kutoka nje? Tuweke mazingira watu wale wafanye kazi kwenye maeneo ambayo siyo ya kuhifadhi mazingira, watiwe hamasa, wasaidiwe na wawezeshwe. Tumepitisha Sheria ya Uwezeshaji. Nadhani eneo moja ambalo tungelitilia mkazo la uwezeshaji ni hili la mitaji ya uwezeshaji katika uchimbaji wa madini. Kwa sababu kuna zana ambazo zinahitajika kuchukuliwa kama mashine za

kuvuta maji na mashine za kuchimba. Kwa njia hii tutafanikiwa kupunguza umaskini katika nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa mimi nimeshiriki vilevile kwenye Kamati yangu, nilichofanya kwa kweli ni kusititiza kwamba, hayo tuliyoyatoa, tumeyatoa kwa dhati kabisa. Tunaomba Serikali ikubali ushauri wetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru na ninaunga mkono hoja hii tena. (*Makofî*)

MHE. PONSIANO D. NYAMI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia. Awali ya yote na mimi naomba niungane na wenzangu, kutoa salamu za rambirambi kwa familia za ndugu zetu, ambao wamefariki katika Bunge hili; Marehemu Mheshimiwa Margareth Bwana, Marehemu Mheshimiwa Abu Kiwanga, Marehemu Mheshimiwa Ahmed Hassan Diria, Marehemu Mheshimiwa Frank Mussati na Marehemu Mheshimiwa *Capt.* Theodos Kasapira. Mwenyezi Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi. *Amin.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwanza kabisa, napenda niunge mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Lakini na mimi nitakuwa na mawili, matatu ya kuboresha hoja yake. Nianzie na eneo la madini. Katika eneo la madini ninahisi kwamba, Tanzania hatujafaidika vizuri, kama wapo waliofaidika ni wachache na faida zao binafsi. Kwa muda mrefu, Awamu ya Kwanza ilikuwa ni vigumu sana kuruhusu makampuni kuja kuchimba madini na vito kwa nia kwamba, Watanzania bado hatujawa na uwezo wa kutetea kilicho chetu ni wazi wangetuibia zaidi. Lakini wakati ulivyozidi kwenda, imefika wakati ambapo ni lazima tuchimbe madini yetu, lakini nami nasema bado tunaibiwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu uchimbaji huo, unawatetea zaidi wawekezaji wakubwa na siyo watu wetu (Wazalendo). Hata katika migodi hiyo, ukienda na sisi wengine tunafanya utafiti, wakiambiwa Mheshimiwa Waziri, anakwenda kwenye mgodi fulani au labda Kamishna wa Madini au Viongozi wakubwa, wale wanaohusika na migodi hiyo, huweka mazingira ya kuwafurahisha wakubwa hao na kuwapeleka katika maeneo ambayo wao wanajua kwamba, hayataweza kuwaathiri wao kama wawekezaji na maeneo yale ambayo ni nyeti hata kama angekuwa Mheshimiwa Waziri hapelekwi huko ng'o.

Mheshimiwa Spika, mfano ni mzuri tu kwamba, wale Wazalendo wetu walioajiriwa katika migodi hiyo hata kama angekuwa na uwezo wa kuajiriwa katika nafasi fulani ya unyeti wa masuala ya madini, hawekwi huko, wanawaweka wageni na kuwapa tahadhari kwamba, kila wanachokiona huko wakifiche. Katika maeneo machache walipoajiri Watanzania wenyewe ujuzi huo huo mmoja, *degree* ni ile ile moja, kwa sababu tu huyu ni Mtanzania hawamlipi mshahara mzuri na wala hawamwekei mazingira mazuri ya kazi yake, tofauti na yule anayetoka nje. Hiyo ipo hata kama mtu angeweza akabisha, hiyo ipo na fanyeni utafiti. (*Makofî*)

Mheshimiwa Spika, kuna watu ambao wamefanya kazi huko wametuambia na wanatuambia tuje tuseme, malalamiko yamefika Wizarani na yamefika kwa Kamishna wa Madini, lakini wanafumba macho, ndugu zangu nyie ni Watanzania msifumbe macho kwa Watanzania wenzenu. Unapomua Mtanzania mwenzako ni sawasawa na kumuua mtoto wako. Angalieni maslahi ya Watanzania, hao wanaotoka nje kesho na kesho kutwa watarudi huko nje na watafaidisha huko nje na sisi tutabaki na umaskini wetu hapa nchini, ni lazima tuwe wajanja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wanapoambiwa mchanga unapelekwa kwenda kufanyiwa utafiti nje, hivi kwa akili ya kawaida, hatuwezi tukaona kwamba hapo tunaibiwa. Kama wameamua kuja kufanya utafiti hapa Afrika, kwa nini wasijenge vitu hivyo hapa Afrika. Kama wanaona hawana faida kwa nini wanabeba mchanga kwenye meli, sijui kwenye ndege, eti wanakwenda kufanya utafiti Ulaya? Kwa akili ya kawaida tu mtu utajua kwamba unaibiwa. Sasa tuwe wajanja sisi Watanzania. Sisemi kwamba, pengine baadhi ya wanaohusika wanapewa fedha au mali au matumaini na kuruhusu hilo. Hebu waulizeni hao kwamba, katika kwenda kufanya utafiti huko kama kuna Watanzania wetu ambao wanajua utafiti huo, waambatane na mchanga huo wakafanye utafiti kule kama watawakubali, ni wazi watakataa. Lakini kama mlisshawahi kufanya hivyo, kuna Watanzania waliambatana nao kwenda huko na nyie wachunguzeni Watanzania waliokuwa wamekwenda kule, waliwekwa kwenye mazingira yepi wakati wanachunguza huo mchanga.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi matokeo yanapokuja, nadhani au nahisi kwamba, hakuna matokeo mazuri kwamba tumepata moja, mbili, tatu. Ninahisi matokeo yanayokuja mara nyingi si mazuri. Maana nakumbuka hata wale waliokuwa wanatengeneza reli ile ya *TAZARA*, kuna kipindi walipokuwa wanafukua ile milima eti walikuwa wanapeleka mchanga huko kwao kwenda kuchunguza ni aina gani ya mchanga ili waone ni jinsi gani ya kuitisha reli. Sasa kwa akili ya kawaida, unaona vitu hivi siyo vya kweli.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninashauri kwanza, tuzingatie uzalendo wetu na tuitazame nchi yetu kwamba, ni yetu na si ya mtu mwingine. Lazima tutazame maslahi ya Taifa ya kizazi chetu cha leo na cha kesho na cha kesho kutwa. Mheshimiwa Isaac Cheyo, amesema wanachimba na mashimo hayo hayatapelekwa Ulaya wala katika nchi nyingine yoyote ile iwe Asia au wapi, yatabakia Tanzania. Uharibifu wa mazingira uliopo utabakia Tanzania na madini yaliyopo Tanzania yanafukuliwa na kupelekwa kufaidisha huko nje, tutabaki na umaskini wetu hapa. Ni lazima tuwe wajanja na tuwe Wazalendo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi ni nani ambaye anampenda mtoto wako zaidi kuliko unavyompenda wewe, hata akamlea mwanao vizuri zaidi kuliko unavyomlea wewe na kwa hiyo, akawa na uchungu na mwanao zaidi kuliko wewe ulivyo na uchungu. Tusiongee nao lugha za kigeni tukaona na sisi tumefanana na wao. Kwa upande wa madini niishie hapo. Yapo mengi kwa mfano, wachimbaji wetu wadogo wadogo, tumesahau hata kuwapa vifaa vidogo vidogo kwa ajili ya kuwaondolea umaskini, tumejipendekeza zaidi kwa wawekezaji. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Spika, tunaposema kuondoa umaskini, tunauondoaje umaskini jamani? Ama umaskini unaondoka kwetu sisi viongozi tuliopo madarakani, tunawaacha hao walioko pembedi! Mbona tunaimba kuondoa umaskini, kuondoa umaskini, tunauondoaje umaskini? Kwetu sisi viongozi au tunaondoa umaskini kuwajali wenzetu hao wa daraja la chini. Tuwe Wazalendo zaidi tusipapatikie wageni sana. Nendeni kwao hivi ninyi mpapatikiwa? Kama anakupapatikia kuna kitu anachokitaka, kwani sisi hatujasafiri tukaona. Mnapokwenda kuomba misaada, mnatukanwa, wanapokuja kwetu kutaka chetu, wanatubembeleza tuonekane wa maana kama wao. Wanatulamba miguu, kumbe wanatafuta ulaji wao, wanasema mtumikie kafiri upate ujira wako. Tuwe Wazalendo zaidi kuliko kujali ubinafsi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu umeme, eneo hili linasikitisha na kama hatutaki kuwatumia wasomi wetu kikamilifu na ushauri wao, tutakwama. Nasema hili kwa maana kwamba, ingawa nitalaumu hapa, lakini kwanza, nipongeze nisilaumu tu bila kupongeza. Katika Wilaya zaidi ya 110 za Tanzania, takriban Wilaya 100 zimekwishapata, umeme haya nai mafanikio makubwa sana na hii ni pongezi kubwa sana. Hongera sana. Lakini bado Wilaya kama 13 hazijapata umeme na wakati huu zingekwishapata umeme, kwa sababu ya upendeleo. Mimi nadhani kama kila Wilaya ingekuwa imekwishapata umeme, ingekuwa ni faraja kubwa. Lakini upendeleo uliopo ni kwamba, baada ya baadhi ya Wilaya kupata umeme, wanakimbilia kupeleka umeme kwenye vijiji zaidi huko, kutumia mabilioni ya fedha kupeleka umeme vijijini na kuacha Wilaya nyingine ziko hoi hazina umeme.

Mheshimiwa Spika, sioni sababu kwa mfano, Wilaya kama vile ya Nkasi, ambayo ni kilomita kama 96 kutoka Sumbawanga kwenda pale, wamekwishaleta nguzo ziko Sumbawanga na nyingine ziko Namanyere. Lakini bado mnapata kigugumizi gani kutokuleta umeme Nkasi na wao walinihidi mapema tu, kama nguzo wameleta na nyingine ziko pale Sumbawanga ni tatizo gani linawapa kigugumzi cha kutoleta umeme pale Wilayani Nkasi? Lakini mnaelewa kwamba, ili tuweze kuboresha mazingira yetu ni lazima kuhakikisha kwamba, umeme unapatikana katika maeneo mengi ya Tanzania. Kutegemea umeme wa maji kwa wakati tulionao haifai, maana maji yanapungua, vyanzo vya maji vinakauka, mvua hazitoshi, hivi tutaendelea kufikiria suala la kutegemea umeme wa maji mpaka lini?

Kuna teknolojia nzuri tu ya umeme wa makaa ya mawe na wala usitegemee kwamba, eti kuweka *generator* itakayoweza kutumia makaa ya mawe ni lazima tuchimbe makaa ya mawe, hapana, tunaweza tukaagiza nje makaa ya mawe, ni rahisi tu. Zambia hapa karibu yapo, Malawi yapo, Tanzania tunaweza tukachimba, ni rahisi sana, tumia watalamu wako wanatuambia hivyo, lakini ninyi mnakuwa na kigugumizi cha kutegemea maji ambayo yatakauka kesho. Sasa hivi megawati ambazo tumezizalisha Tanzania hazizidi 700. Lakini ukiweka *generator* moja tu ya kuweza kufua umeme kutumia makaa ya mawe, unaweza ukazalisha zaidi ya *watt* 1,000 na nchi nzima ikafaidika na umeme na pengine tukapeleka nje. Ni kweli, leo hii wenzetu wa nchi za Ulaya sasa wanaungana ili kuhakikisha kwamba, wanatumia *nuclear fusion*, wanaondoka na *nuclear fusion* ile ya kutenganisha. Wanafanya utafiti mkubwa kwa kuungana ili

nuclear fusion iungane izalishe zaidi umeme kwa kiwango kikubwa zaidi, ikiwezekana kisima kimoja au viwili, vitosheleze Ulaya nzima, ndiko wanakokwenda wenzetu.

Sisi tunafikiria maji ambayo yanakauka kesho. Kidatu maji hayatoshelezi, Mtera maji hayatoshelezi, Kihansi maji hayatoshelezi, tunakazania umeme wa maji, hatu-*plan* mambo mengine mapya. Sasa huu ni upungufu. Umeme wa *IPTL*, kwa mfano, Mheshimiwa Rais, aliwahi kupendekeza kwamba, tuununue, lakini suala hili bado linasuasua. Hivi ninyi wakubwa huko, mna *interest* gani mnayopata faida kule *IPTL*, mtuambie? Muwe Wazalendo zaidi jamani. Kwa nini suala hili linasuasua, Rais ameshauri tununue hiki kitu, ninyi mazungumzo, sijui hajafanyaje na nini? Hebu acheni mambo ya namna hii jamani, mnatumaliza. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, unajua tunasema vitu vingine vinauma kwa sababu gani? Ukiichunguza hii nchi sana ni sawa sawa na kumchunguza kuku na manyoya yake, unaweza ukashindwa kumla. Wakati umefika wa kujali uzalendo wa Tanzania na sio kujijali sisi wenyewe, tujali umma.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja hii, nakushukuru sana. (*Makofi*)

MHE. MOHAMED H. MISSANGA: Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa shukrani zangu za dhati kwako, kwa kunipa fursa nami nichangie katika hoja iliyo mbele yetu. Lakini nikushukuru zaidi kwa kweli kwa kunipa nafasi ya awali kabisa ya kuweza kuchangia.

Mheshimiwa Spika, nilishatoa rambirambi zangu na pongezi kwa wale wote wanaohusika sikusudii kurudia. Lakini nitumie nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, pamoja na Watendaji wote kwa ujumla, kwa kazi nzuri wanayoifanya katika Wizara hii. Ni Wizara nyeti, kwa hiyo, lazima itakuwa na kashkash za hapa na pale na sisi kwa sababu tunawawakilisha watu, lazima tuseme hizo kashkash na tuwaambie pale ambapo tutawakwaza basi watusamehe lakini nia ni kusema ule ukweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina hakika kuwa Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha na Mheshimiwa Daniel Yona, watakuwa wanafahamu kwamba, lazima nizungumzie suala la umeme wa Ihanja. Kwa sababu wamenidanganya na wamewadanganya Wananchi wa Ihanja kwa miaka kadhaa. Wamewahadaa kwa maana kwamba, wamewapelekea nguzo toka mwaka 1998 na kuwatamanisha umeme na wasipate mpaka hii leo. Nguzo hizo sasa nyingine zinazuwa na kazi iliyopo pale asubuhi wakiamka Wananchi wanakwenda kuzisalimia, *asalaam aleykum* na jioni pia *asalaam aleykum*, ndiyo kazi iliyopo kwa sababu hazina manufaa yoyote.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri na hasa Mheshimiwa Naibu Waziri, nakumbuka mwaka 2004, wakati Bunge lako limekaa kama Kamati ya Matumizi, aliponisiji na kuniomba nisichomoe hata senti tano na kwamba, suala langu la umeme kule Ihanja hasa katika Sekondari ya Ufundsi ya Ihanja, ingepatiwa umeme mapema iwezekanavyo. Baada ya kudanganywa toka mwaka 1998, lakini mpaka sasa kila

nikifuatilia na yeche ni shahidi, nimemsumbu wakati mwingine hata naona haya kumsumbu sana, lakini kwa sababu ni kazi ya watu, imebidi kumwomba mara kwa mara na hadi sasa hakuna kitu ambacho kimefanyika. Wananchi wa Ihanja, wanajiuliza wameikosea nini Serikali yao ya CCM na kama unavyofahamu, Mkoa wa Singida ni mkoa wa CCM sasa tatizo nini? Wamefanya makosa katika hali hiyo? Inasikitisha sana na nilishasema kwamba, Sekondari ile ya pale inaendeshwa na madhehebu ya Kikristo na wamepata msaada kutoka Marekani wa kupatiwa vifaa vya kiufundi, kompyuta na kadhalika, ili shule ile ifanye kazi vizuri au watimize lengo lao, lakini mpaka leo hata wale wenzangu nao wanaanza kukata tamaa na mimi kama Mbunge wao, wanansikitikia sana.

Mheshimiwa Spika, kwa uchungu sana naomba niwasilishe tena masikitiko yangu kwa Wizara hii, kwa hadaa ambayo imefanywa kwa Wizara hii kwa Wananchi wa Ihanja, kwa kosa ambalo wenyewe hawalijui. Wangependa kuelezwu ni kosa gani wamefanya? Sababu gani mradi huu unatoka Puma unakwenda pale kilomita 12. Awali wataalam walisema shilingi milioni 120, sasa hivi wataalam hao hao wanakuja tena wanasema shilingi milioni 200. Iko miradi mingine ambayo imetumia zaidi ya shilingi milioni 400, 500 na ni miradi mipyä imepewa fedha, lakini huu mradi wa zamani au mradi kiporo haupewi fedha. Hapa nadhani *justice* haifanyiki. Ningemwomba Mheshimiwa Waziri, awaambie wenyewe atakapokuwa ana-sum up, kosa lao ni nini na kama hawapati umeme basi wajue cha kufanya.

Mheshimiwa Spika, napata wasi wasi kwamba, inawezekana upo upotoshaji kwa baadhi ya watendaji pale *TANESCO*, hasa wanaosimamia umeme vijijini. Nina wasi wasi, kwa sababu iko barua moja imeandikwa na mtaalam mmoja anasema umeme wa kwenda Ihanja unatoka Ikungi, uko wapi umeme unaotoka Ikungi? Umeme wa Ihanja unatoka Puma, kilomita 12. Yeye anasema unatoka Ikungi kilomita zaidi ya 30. Hii ni hujuma, huku ni kupotosha ili kuonekana kwamba, suala hili ni gumu halifanyiki. Wako pale *TANESCO* Makao Makuu. Ushahidi wa mazingira uliopo ni kwamba, wao makwao wamepeleka umeme ingawa kwa gharama kubwa sana. Wao wako pale kwenye Kitengo cha Umeme Vijiijini, makwao wamepeleka umeme na ni mbali lakini Ihanja kilomita 12 ni karibu. Hii sio haki, watende haki, wako pale kwa niaba ya watu sio kwa niaba yao binafsi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, sina hakika nani hasa anahusika na uamuzi wa kuamua umeme uende wapi pale *TANESCO*, ni kikundi cha wachache, ni Mkurugenzi na wasaidizi wake au ni nani hasa. Kwa sababu kama kweli suala hili lingekuwa linatazamwa kwa ujumla wake na kwa umuhimu wake na kwa ahadi ambazo zimeahidiwa, nina hakika Wananchi hawa wa Ihanja wangkuwa wameshapata umeme. Nimwombe sana Mheshimiwa Waziri, alitolee kauli suala hili kwa sababu linanitia kichefuchefu na linaleta hisia kwamba, kuna upotoshaji, kuna hujuma inafanywa na watumishi pale *TANESCO* kwa sababu ambazo mimi zisielewi.

Mheshimiwa Spika, ningemwomba basi sambamba na suala la umeme pale Ihanja, lakini pia nimeshawasilisha maombi ya umeme kule Sepuka. Sasa tumeambiwa kwamba kuna mpango wa Benki ya Dunia sijui unaanza lini? Basi niwaombe sana kwamba, pale

Sepuka nako na sehemu nyinginezo katika jimbo langu la Singida Kusini, nao wapate umeme, hasa kama huo mpango wa Benki ya Dunia utaanza mwaka 2006, kwa sababu Waziri amesema jana, mapema mwaka 2006, sasa mapema *it can be October, it can be January*, mapema tu. Sasa hizo ni vague statements ambazo mtu anatafuta mahali pa kukimbilia. Ningependa kujua huo umeme ambao unazungumzwa na wafadhili wa Benki ya Dunia, unaanza mwaka 2006 wakati gani?

Mheshimiwa Spika, mwenzangu aliyemaliza kuchangia sasa hivi amezungumza habari ya *IPTL*, kwa hiyo, sina sababu ya kuzungumza sana. Lakini ni kweli kwamba ni suala ambalo linasumbua na limezungumzwa muda mrefu na kama Mheshimiwa Rais alishasema, nadhani kauli ya Mheshimiwa Rais hata akisema, hayo ni maelekezo. Kwamba, ni vizuri Serikali ikaangalia uwezekano wa kumiliki yenyewe ile *IPTL* kulikoni kuendelea kutumia fedha chungu nzima za kuwalipa wale. Sasa kuna kigugumizi gani, kuna tatizo gani, kuna *interest* gani katika *IPTL*? Sisi hizo sababu za nyuma huko, tumeshasema tuyaa che hayo mambo ya nyuma, ilikuwaje, nani ameingia Mkataba, kwa maslahi gani, haya tuyaa chilie mbali. Turekebishe kwa kuhakikisha kwamba, *IPTL* inakuwa *owned* na Serikali. Sasa hilo nalo linakuwa kigugumizi kwa sababu gani? Ningedhani ni vizuri Serikali itafute njia zozote zile hata kama ni kupata mkopo au mfadhili, tuondokane na hii adha ambayo kwanza, inatia kasoro katika Serikali yetu ya CCM.

Mheshimiwa Spika, gesi ya Songo Songo imeanza kutumika na matazamio ya Waheshimiwa Wabunge na Wananchi kwa ujumla, wakati tunazungumza suala la Songo Songo ilikuwa kwamba, itakapoanza kutumika gesi ya Songo Songo kutakuwa na nafuu kubwa ya matumizi ya gesi hiyo na kwa ajili hiyo, gharama za umeme viwandani na majumbani zitapungua. Lakini pamoja na kwamba, zimeanza kama alivyosema Mheshimiwa Waziri, kule *Wazo Hill* au *Twiga Cement*, kuna *ALAF* pale wameanza lakini gharama hazijapungua, ndiyo kwanza gharama za uzalishaji ama zinaongezeka au wenzetu wale wenye viwanda vile vya *ALAF* na *Twiga Cement* wanatuuhadaa kwa maana ya kwamba, mfuko wa saruji bei iko juu, bati bei iko juu, sasa Wananchi wanatuuliza mnataka tushiriki katika kujilettea maendeleo wakati mfuko wa saruji Singida sasa hivi ni zaidi ya shilingi 10,000, wakati bati Singida ni zaidi ya shilingi 9,000/=, huyo mwananchi wa kawaida atapata shilingi 10,000/= wapi na atapata wapi shilingi 9,000/= anunulie bati ili aweze kujenga nyumba nzuri, kama inavyohimizwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, nina wasi wasi kwamba, wenzetu hawa kwa sababu bei zao zikishafika pale hata wakipata jambo la maana ambalo linasaidia kupunguza bei hawawezi kupunguza bei. Ningeiomba Serikali kwa kweli hebu ifanye tathmini, ijue hasa uzalishaji wa wale wenzetu uko vipi ili yale matumaini ambayo Wananchi walikuwa nayo kwamba, gesi ya Songo Songo ikianza na umeme utapungua bei ama viwandani au majumbani ipatikane, vinginevyo itakuwa tunawafaidisha wenye viwanda lakini Wananchi wa kawaida hawafaidiki na hiyo ya Songo Songo hata ikianza hiyo ya *Mnazi Bay* hadithi itakuwa ni ile ile. Ningependa Mheshimiwa Waziri, atakapokuwa anafanya *sum-up*, kwa mfano, atueleze hivi gharama halisi za uzalishaji ni kiasi gani kwa hiyo ya

Songo Songo na vile vile gharama ya kuuza sasa ni shilingi ngapi ili tujue na Wananchi wajue tuweze kujua nani mkorofsi katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, kupanda kwa bei holela kwa mafuta ni tatizo. Naiomba Serikali iliangalie pamoja na kwamba sasa hivi kuna mtu anaitwa *regulator*, lakini kwa kweli bei ya mafuta inatisha na matokeo yake ni kwamba, bei za vitu zinapanda siku hadi siku na Wananchi wanazidi kulalamika, hivi tunashindwa nini kuliangalia suala hili. Kweli kuna soko huria, lakini sasa katika hali ambayo Wananchi wanaathirika kiasi hicho, tunang'ang'ania tu soko huria bila hata huyo mdhibiti ambaye amewekwa kuangalia sawa sawa, kila siku bei ya mafuta inapanda. Naomba hilo nalo Serikali iweze kuliangalia.

Mheshimiwa Spika, kule Singida kuna dhahabu katika sehemu ambayo iitwayo Sambaru, Kata ya Mang'onyi. Wananchi na hasa wachimbaji wadogo wadogo, wanajitahidi sana kuchimba na wanafanya kazi nzuri sana. Sasa Wizara nafikiri inajua kwa sababu nimeshazungumza na mwakilishi wao pale mkoani, anafahamu na ameshakwenda na mimi pia nimeshakwenda. Kwa hiyo, ningeomba sana wasaidiwe kikamilifu, kwa sababu wanayo matatizo kadhaa pale machimboni Sambaru. Miiongoni mwa matatizo waliyonayo ni vitendea kazi duni, uwezo wao ni mdogo kwa maana ya mikopo, halafu baadhi yao wengine hawajapata leseni na akina mama pia wanasema na wao wanaweza wakachimba na wako pale, wanataka nao wafikiriwe sambamba na wanaume, nao wapewe leseni, wachimbe hayo madini na kadhalika kadhalika. Kwa hiyo, ningeomba Mheshimiwa Waziri, atupie macho pale Sambaru na wasaidiwe wale Wananchi kwa hali na mali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, ni kuhusu *Net Group*, ningependa kujua Mkataba unaisha lini? Nadhani sasa hakuna haja ya kuongeza tena Mkataba wa *Net Group*, kwa sababu matatizo yale yale ambayo yalikuwepo bado yapo, pamoja na kwamba wamewezeshwa, wamepewaa fursa. *TANESCO* zamani hawakuruhusiwa kukata umeme jeshini wala hospitali, lakini *Net Group* wanakata. Pamoja na kusaidiwa namna hiyo, bado matatizo yako pale pale, umeme unakatika ovyo, bei ya umeme iko juu na kadhalika, wa nini sasa hawa kuendelea nao au kuna mtu anapata maslahi juu ya *Net Group* kuwepo pale? Kwa hiyo, nadhani wakati umefika sasa, *Net Group* waondoke na ubinafsishaji wa *TANESCO proper* ufanyike. Kama Mashirika mengine au Taasisi nyingine ambazo zilikuwa zinafanya kazi vizuri zimebinafsishwa, hivi *TANESCO* wanangoja nini? Kwa nini *TANESCO* isibinafsishwe? Wakati umefika sasa ibinafsishwe kwa sababu hakuna lolote, hatufaidiki kwa chochote na *Net Group* kuendelea kuwepo pale bali ni adha ya siku hadi siku.

Mheshimiwa Spika, ningeiomba Serikali iondoe kigugumizi, inatosha miaka mitatu, minne, wameshafaidika kiasi cha kufaidika na sasa hatua *proper*, ambazo walisema zitafuatia baada ya *Net Group* kufanya kazi yake ya ubinafsishaji, nazo ziweze kuchukuliwa ili kama yalivyobinafishwa Mashirika mengine na kwa tahadhari ile ambayo tumeeleza wakati tukielezea zoezi la binafsishaji kwa ujumla, nasema sasa *TANESCO* nao wabinafsishwe, tuangalie wengine kwani wao wameshindwa. Sasa kama wanashindwa kupeleka umeme kilomita 12, wa nini hawa kuwepo hapa. Kilomita 12 tu

inawashinda sasa watakuja kuweza kilomita 120 kama wanavyosema Wilaya gani sijui na ndiyo maana haiwezekani. Nina hakika kama *TANESCO* wetu wale wa zamani wangekuwepo, sasa hivi tumefika mbali. Kwanza, ni bahati mbaya mipango yote ambayo ilikuwa imepangwa na *TANESCO proper* ile ya zamani, hawa wenzetu wamekuja wameitupilia mbali, kitu ambacho sio sawa sawa.

Mipango ile ilikuwa imebarikiwa na Serikali na nilidhani kwamba, kazi ya kwanza ingekuwa ni kuheshimu mipango ile na kuiendeleza lakini wao wamekuja wameitupilia mbali, wakaanza ya kwao na ndiyo maana baadhi ya Wilaya mpaka leo hazijapata umeme na miradi mingine ya awali ambayo ilikuwepo kama huu wa Ihanja, imekuwa kiporo, wengine wamepata, wengine wanasema bado haijakamilika, ni kwa sababu ya udhaifu wa *Net Group*. Wakati umefika sasa waondoke na *TANESCO* ibinafsishwe.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia. (*Makofi*)

MHE. STANLEY H. KOLIMBA: Mheshimiwa Spika, naomba kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuzungumza kidogo kuhusu hoja hii ya bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini.

La kwanza, napenda kuwashukuru sana watu wa Wizara kwa kutenga shilingi milioni 400, kwa ajili ya mtandao wa umeme katika Mji wa Ludewa. Kwa kweli tangu uhuru wa nchi hii na tangu Wilaya ya Ludewa ianze, kuhusu sekta ya umeme hatujawahi kupata chochote, hii ndiyo mara ya kwanza kupata. Kwa niaba ya Wananchi wa Ludewa naomba kuwapongeza sana. (*Makofi*)

Vile vile naomba nimpongeze Waziri mwenyewe binafsi, kwa sababu katika mjadala wetu ndiye aliyependeka kwamba, tuandike barua na kuomba Wizara ya Fedha, kwa hiyo, Wizara ya Fedha nao nawapongeza na Wizara inayohusika naipongeza. Vile vile nampongeza sana Meneja wa *TANESCO*, kwa sababu ndiye aliyefanya *survey* ya kwanza haraka iwezekanavyo. Nadhani kama tutatumia *speed* aliyotumia katika nchi hii, tunaweza tukafaidika kwa sababu ilikuwa ni mwezi mmoja baada ya kumwambia mwezi wa pili alikamilisha kazi na akatoa makisio yote ya mji wa Ludewa na mtandao wake. Kwa hiyo, naye nampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa kawaida mtu unapokuwa kwa chifu unasema yote siku hiyo hiyo, kwa hiyo, nafikiri hapa niseme yote.

SPIKA: Haya sema?

MHE. STANLEY H. KOLIMBA: Baada ya pongezi hizo, nafikiri vile vile niwaombe ndugu zetu wa *TANESCO*, ambao kwa kweli walishaanza kuleta nguzo za umeme pale Ludewa, tayari nguzo 75 zilifika, palihitajika nguzo 75 nyingine, tungeomba ile kazi iliyozubaa zubaa pale katikati, sasa ingekuwa ndio wakati wake huu wa kumalizia zile nguzo zilizobaki kutoka Mafinga zije Ludewa ili tuweze kukamilisha ile

kazi. Sasa hivi kama walivyosema wenzangu, nguzo zote ziko pale, ukiwaaambia watu wanasema kwamba, nguzo hazisaidii kitu. Kwa hiyo, nadhani kama pangekuwa na *activities* zinaendelea pale na kwa sababu fedha zimepatikana, nadhani kazi hii ingeanza mara moja, Mheshimiwa Waziri pengine ungefanya msukumo.

Mheshimiwa Spika, lingine nilikuwa napenda kuwaeleza kwamba, pamoja na kupata Mji wa Ludewa ule mtandao pale wa umeme, lakini tulikuwa tunafikiri iko haja ya kupeleka umeme kwa Wilaya ya Ludewa. Wilaya ile ni ya siku nyingi sana toka mwaka 1975 imenzishwa na sisi tulitegemea kwamba, walipopata Makete tukajua watashusha kutoka Makete na sisi ni majirani. Kwa hiyo, tulifikiri umeme wetu utatoka Makete utashuka kwenda Ludewa, lakini hata hivyo, halijafanyika hilo. Sasa tumeona hapa kuna shilingi bilioni sita zinawatisha pale lakini tunaomba sana umeme uende Ludewa, kwa sababu ni moja ya Wilaya ambayo imeanza siku nyingi kuliko Wilaya nyingine ambazo kwa kweli zilikuwa zimekuja nyuma yetu. Hatusemi mmependelea, nadhani sisi kwa sababu tunakaa *remote* kule kwa hiyo, pengine hiyo ni hoja lazima tupate fedha nyingi, lakini basi tuwemo. Lakini tunashukuru katika maelezo mnaeleza kwamba, Serikali ya Awamu ya Nne, mtaikabidhi Wilaya hizi 13 zilizobaki. Sasa hilo sijui ni agizo, sijui ni Mkataba au sijui ni makubaliano, je, maana yake si lazima niwe mimi, Mbunge mwenzangu anayekuja au mimi mwenyewe nikibaki, nimwambie kwamba, Mkataba huu umekubaliwa kwenye Bunge au vipi?

Baada ya kueleza hayo, vile vile tunahitaji umeme sana kwa sababu tunataka kuibadilisha Wilaya ya Ludewa kwa kweli. Ilikuwa Wilaya ya kilimo sasa iwe Wilaya ya viwanda na maeneo mengi, kwa mfano, sasa hivi tumepata *High School* pale, kwa hiyo, inahitaji umeme, iko kule Malangali. Tuna maeneo ambayo *Secondary Schools* zimejengwa nyingi, tunazo karibu 10 na tuna kopyuta na kadhalika, sasa tunaona ni heri sasa hivi kuwepo na mpango mzuri zaidi wa kuleta umeme katika Wilaya ya Ludewa. Kwa hiyo, tunaiomba Serikali ifanye hivyo.

Lakini nilikuwa na wasi wasi na mipango ya nchi kidogo. Nilikuwa nafikiri kwamba, lengo la umeme katika nchi hii, iwe kupata umeme nafuu kuliko tu kupata umeme. Nimewahi kusikiliza hapa semina nyingi sana zilizokuwa zinaendeshwa kwa ajili ya Afrika Mashariki, *SADC* na kadhalika. Lakini tatizo ninaloliona ni kwamba, Tanzania itashindwa kushindana katika soko kwa sababu umeme wetu ni ghali mno. Sasa ningefikiri wataalam, mngezamisha vichwa kwenye tatizo hili mkajua ni umeme upi unaweza kuiokoa nchi hii ishindane katika soko. Kwa uzoefu wangu, nafikiri kwamba, umeme mmojawapo unaoweza kusaidia kuleta mapinduzi na kushindana katika soko la bidhaa katika dunia ni umeme wa makaa ya mawe, kwa sababu historia inaeleza.

Watu wote walioendelea katika nchi za dunia, Amerika, Ulaya, Uingereza, Afrika Kusini, Australia na kadhalika, wameendelea kwa kutumia umeme wa makaa ya mawe. Sasa sisi ni tofauti gani? Kwa hiyo, nilikuwa nafikiri hapa suala lisiwe tu kupata umeme. Ndiyo unaweza kupata umeme mwingi duniani hapa, lakini umeme huu ni nafuu na unaweza kutuvusha katika nchi hii. Hilo ndilo swalii?

Sasa wakati napitiapitia hii hotuba ya Mheshimiwa Waziri hapa, ameelezea habari ya umeme mbadala. Katika kipengele kile sijaona mbadala wa makaa ya mawe pale na ukapewa uzito. Kama itakumbukwa mwaka 2004, Waziri alisimama katika Bunge hili na akaeleza kwamba, sasa Serikali ya Tanzania, imekubali makaa ya mawe ya Mchuchuma uwe ni mradi unaoweza kutekelezeka na wawekezaji wake waendeleze shughuli hiyo. Sasa humu mbona hakuna, wala kugusia tu kama upo Wizara ya Viwanda na Biashara lakini kugusia humu kwamba nao ni mradi mbadala. Pengine Waziri atatupa jibu na kutuelekeza ni lipi linafanyika. Kwa hiyo, nafikiria kwamba, katika mambo ambayo tunaweza kufikiria kwamba ni nishati nafuu nilikuwa nafikiria makaa ya mawe ni nishati nafuu na uchambuzi umefanywa.

Kulikuwa na *argument* kule kwenye *Standing Committee* ya *Mtwara Corridor*, wataalam wa kutoka Wizarani wanazungumzia kwamba, makaa ya mawe yanaweza kuwa ghali kuliko aina nyingine ya mbadala. Sasa nilikuwa nafikiria kwamba, hizi *arguments* zingine zimekaa mno kitaaluma taaluma tu, lakini ukitazama zaidi utaona kwamba, ule mgogoro unatokana na hii miradi kutokuwa chini ya Wizara moja.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kuna tatizo la mgogoro kati ya Wizara na Nishati na Madini na mgogoro kati ya Wizara ya Viwanda na Biashara. Pengine huu mradi ungekuwa kwenye Wizara moja, pasingekuwa na majadiliano ya ajabu ajabu haya. Sasa watu wanazungumzia *costing* zake, watu wa huku wanazungumza lingine, sasa utaalam wa wapi huo. Kwa hiyo, nilikuwa nafikiria tusuluhishe hii migogoro, tuanze kujenga na vile vile labda tuliondoe jini hili. Hapa linaonekana kuna jini linalozua mradi huu. Sasa kama hili jini lipo, kwa nini tusitafute mganga, hili jini kiwete anasema Mheshimiwa. Tutafute namna ya kuliondoa hili jini ili mradi huu kila siku usisukumwe nyuma tu. Unasukumwa nyuma kila siku kwa nini, hili jini liko wapi, liko Wizara ya Nishati na Madini au liko Wizara ya Viwanda na Biashara? Kwa hiyo, tunaomba Serikali iwe *serious* na jambo hili. Tunafikiria kwamba, makaa ya mawe ni nishati nzito katika nchi hii. Tupende tusipende katika miaka ijayo, historia inaweza kutuhukumu sisi kwa kuchelewesha mradi huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hivyo, nilikuwa nafikiria niende labda kwenye vyanzo vingine. Kulikuwa na chanzo cha Kitawaka kule kuna maporomoko mazuri tu, sasa sijui maendeleo yake yamefikia wapi na *TANESCO* nadhani walishafanya *survey*, sasa sijui kama kuna maelezo yoyote yanayoweza kutolewa kuhusu chanzo hiki.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nilikuwa naomba nizungumzie habari ya wachimbaji wadogo. Mara nyingi sana wenzetu mnafikiria kwamba, maeneo ya huko juu, kwa mfano, Mwanza, Shinyanga na kadhalika, ndio kuna wachimbaji wadogo. Lakini sisi Ludewa tunao wachimbaji wadogo mmewasahau. Wako kule Amani wanachimba dhahabu, ushauri hakuna. Tunaomba tembeleeni hata hizi Wilaya nyingine ambazo zina wachimbaji madogo.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba, nilikuwa nataka kuwakumbusha tu miaka ya 1958, kulikuwa na *Williamson*, alikuja Ludewa sehemu ile ya Chiulungi kuchimba au kutafiti almasi. Kwa hiyo, tulikuwa tunaomba pengine mwendeleze wazo lile pale

Chiulungi. Sisi tunaamini kwamba, pale pana almasi ya kutosha na alikuwa na *interest* kubwa na alijenga hata kiwanja cha ndege pale, kwa nini msitazame jambo hili kule chini.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naipongeza tena Serikali kwa Mradi ule wa Liganga wa Chuma, kwamba kuna juhudzi zinafanyika pale, kuna wawekezaji wameonesha *interest*, hawa watu wa *MM Integrated Steel Mill Limited*, wamekwenda pale kajaribu kuweka kiwanda cha kutengeneza chuma cha nondo, *medium size industry*. Kwa hiyo, tunaishukuru sana Serikali kwa kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nilikuwa nataka tu kuwakumbusha na kuwapongeza, kwa kazi nzuri mnayofanya, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

MHE. DR. AARON D. CHIDUO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie katika kujadili hoja ya Waziri wa Nishati na Madini. Nianze kwa kusema kwamba, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama Mjumbe wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, Kamati yetu imetoa maoni yetu, nami nilishiriki kwa ukamilifu, kwa hiyo, sitakuwa na mengi ya kusema, nayaunga mkono yale maoni yetu lakini kwa upande wangu, nitazungumzia kidogo juu ya sekta ya madini na hasa kuhusu wachimbaji madini wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, kama tunavyoolewa, sekta ya madini ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi na kuongeza Pato la Taifa na vilevile kuinua kipato cha wachimbaji madini. Kulingana na sera ya madini, uwekezaji kwenye madini tunavyoolewa umeachiwa sekta binafsi na tunaambiwa jukumu la Serikali ni kuweka mazingira mazuri na vivutio ili tuwapate wawekezaji kwenye madini. Lakini tukiangalia kwa makini tunaona kwamba, mazingira hayo mazuri na vivutio, yameelekezwa zaidi kwa wachimbaji wakubwa wageni, lakini wachimbaji wadogo hawajawekewa mazingira mazuri wala vivutio vya kutosha na hata hawajaelezwa juu ya utaratibu bora wa kuingia katika uchimbaji wa madini, wenye mpangilio bora na wa kisasa. Sana sana tunachokiona, wanahangaika hangaika tu, wakisikia mahali kumegundiliwa madini, basi wanakimbilia huko kwa wingi, kunakuwa na msongamano katika maeneo hayo bila kuwa na huduma zinazofaa. Kusema kweli, wanachimba katika mazingira magumu na katika maeneo hayo ukweli wa mambo ni kwamba, katika msongamao huo vile vile unakuta wanaeneza virusi vya UKIMWI, ndiyo ukweli wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka 2004 nilielezea juu ya wachimbaji wadogo waliokuwa wanachimba katika Jimbo langu, wanaoitwa *Fed Spar*. Mimi sikuelewa *Fed Spar* hasa ina faida gani au inakazi gani, mpaka nilipotembelea Taasisi ya *Southern and Eastern Africa Mineral Centre (SEAMC)*, iliyoko kule Kunduchi, Jijini Dar es Salaam. Ukweli wenyewe hata wale Wananchi waliokuwa wanachimba yale madini, walikuwa hawajui madini yana faida gani na kwa wale waliokuwa wanawalangua tu. Sasa huo sio utaratibu mzuri na kwa utaratibu kama huo, wachimbaji hawa wa madini hawawezi kufaidika. (*Makofi*)

Katika Milima ya Ukaguru katika Jimbo langu, kuna madini ya vito vya thamani, niliwahi kuchukua ramani hapa katika kituo chetu cha madini hapa Dodoma, kilichoonesha wazi kwamba, katika milima ile yako madini ya vito, lakini hakuna juhudzi zozote za makini zinazochukuliwa kuona kwamba Wananchi wa maeneo yale wanasaidiwa kuyachimba madini hayo.

Nimekuta kikundi cha wachimbaji wadogo hivi karibuni, wamekodisha *bulldozer* kwa ajili ya kuchonga barabara ya kwenda kwenye maeneo ya Kishapu na Chagongwe katika Tarafa ya Nongwe, kuchimba madini ya vito wakitumia zana duni kabisa. Hawa wanastahili kusaidiwa waweze kupata zana bora na waweze kupata uwezo wa fedha. Wenyewe wanasema wako tayari kabisa kupewa mikopo ya kuweza kununulia zana lakini hawaelewi zana hizo watazipata wapi. Kwa hiyo, utaona kwamba, kama nilivyosema, nao wanahangaika

Mheshimiwa Spika, wachimbaji wadogo wanahitaji utalamu wa ugunduzi wa maeneo yenye madini, wanahitaji kufundishwa namna ya uchimbaji bora wa madini, kwa utaratibu unaofaa, bila kuhatarisha maisha yao. Kuna sehemu moja katika eneo hilo hilo, mchimbaji mmoja alifukiwa akafa akitafuta hayo madini. Wachimbaji wadogo hawa wanahitaji miuondombinu na hasa barabara za kuweza kuyafikia maeneo yao hayo yaliyo na madini. Kama nilivyosema, wanahitaji vifaa na zana bora na wazipate kwa bei nafuu, vile vile wanahitaji masoko yanayoaminika na yanayokidhi mahitaji yao. Hawa wachimbaji wadogo wanahitaji kusaidiwa waunde makundi rasmi ya kuchimba madini, inaweza kuwa ni vikundi vinavyoolekea kwenye vyama vya msingi vya ushirika. Ingefaa vilevile waundiwe mfuko rasmi wa fedha, utakaochangiwa na Serikali na wachimbaji wakubwa kuwasaidia hawa wachimbaji wadogo. Kwa kufanya hivyo, tutakuwa tunawasaidia wachimbaji wadogo nao wajitoe katika umaskini wa kipato.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hali ya kuiachia sekta binafsi kuwekeza kwenye sekta ya madini, Serikali isiache jukumu lake la kusimamia kwa ukamilifu, kuona kweli tunafaidika na madini ambayo tunayo hapa kwetu. Madini ni yetu na lazima tufaidike na hii mali asili yetu tuhakikishe kwamba, pamoja na kwamba, hawa wachimbaji wakubwa nao watachimba kwa kupata faida na kwa kweli tumewapa uhuru wa kupeleka fedha kutokana na faida wanayopata, waitoe nje ya nchi lakini vile vile na sisi kwa mapato yanayotokana na uchimbaji wa hayo madini, nchi yetu na sisi tupate sehemu kubwa ya mapato ili tubadili hali yetu ya maisha na sisi tuondokane na umaskini.

Mheshimiwa Spika, kwenye Wilaya zenye madini inafaa kuwepo Maafisa wa Madini. Katika Halmasahuri ya Kilosa, hatuna mtaalam wa madini, tunategemea mara moja moja tuone mtaalam akitoka Morogoro. Sasa hiyo kwa kweli haitusaidii sana na vile vile Wananchi wanastahili kuelezwu utaratibu mzima uko vipi. Wanawenza kumiliki maeneo ya madini na maeneo hayo wakayapatia hati miliki ili wasidhulumiwe na wajanja wachache amba wakati mwengine ndiyo wenye utalaam wa kujua namna ya kupata hati miliki za migodi na kwa maana hiyo, Wananchi wanakuwa kama vibarua tu, lakini wanaonufaika zaidi ni hao wanaoelewa utaratibu mzima wa jinsi ya kupata hati miliki. Kwa hiyo, nimegeomba sana, hasa kwa Jimbo langu na hasa katika Milima hii ya Ukaguru, vito vile visaidie kubadili hali ya maisha ya watu wa Tarafa ya Nongwe.

Mheshimiwa Spika , kuhusu *TPDC* na *Mafuta House*, wenzangu wameshaeleza kwa ukamilifu na mimi naunga mkono kabisa mawazo yao na natumaini, Serikali itatilia maanani na kubadili maamuzi ambayo yalikwisha kufanywa ili haki ipatikane. Vile vile juu ya *capacity charge* ya *IPTL*, wote tunaelewa kabisa jinsi ambavyo huwezi kusema kwamba, Serikali inanyonywa, lakini kwa upande mwengine, inakuwa kama inanyonywa kwa sababu ni fedha nyingi ambazo zinatolewa kila mwezi ambazo zingeweza kutumiwa kuleta maendeleo katika sehemu nyingine na kama tulivyotoa ushauri vile vile ni kwamba, Serikali itazame vizuri hatma ya *IPTL*, kama ni kuinunua au kwa njia yoyote ile, tuondokane na deni hili kubwa la kulipa kila mwezi, ambalo kwa kusema kweli linatia huzuni kwa sababu ni fedha nyingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, kama nilivyo sema, nilikuwa mmoja wao katika Kamati na Kamati imeshatoa mawazo yetu, nasema tu kwamba, nampongeza Waziri na wasaidizi wake wote, kwa hotuba yao nzuri na nina hakika, tutawapatia fedha ili watekeleze wajibu wao.

Mheshimiwa Spika, nasema tena kwamba, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyopo mbele yetu. Napenda nianze kwanza, kwa kuunga mkono hoja. Nilikuwa kati ya Wajumbe waliodurusu Sera ya Madini, hivyo nitaunga mkono zaidi kama utekelezaji wa maelekezo yetu ambayo tulitoa kwenye Kamati hiyo, kama Wizara hii itayafanya kazi na nchi yetu tuna matumaini kwamba itafaidi.

Mheshimiwa Spika, ningependa kwanza, nijielekeze kwenye hili suala la mrabaha na mimi ni kati ya wale wanaolalamikia suala hili. Kwa kweli kiasi cha asilimia tatu ni kidogo sana. Lakini katika uchunguzi nilikuwa naangalia sana na kwa makini, tumezunguka katika nchi hii na nchi nyingine zinazozalisha madini, asilimia tatu ni kama kiwango ambacho kimewekwa karibu *standard* na kuna nchi nyingine hazipati mrabaha huo, kwa mfano, Afrika ya Kusini, mrabaha sehemu ndogo tu ya mapato.

Katika madini kuna sehemu tatu za mavuno, mapato mengi yanakwenda ambayo ni kati ya asilimia 70 mpaka 80 kwenye *operating costs*, asilimia 20 unakuta ndiyo ya wale wenye mali na mrabaha. Sasa nchi kama Afrika Kusini haitozi mrabaha kwa sababu yenye inapata mapato yake kwenye asilimia 70 na 80 na hii unakuta imejikita kwenye utendaji zaidi, viafaa vyote vinavyofanya kazi migodini vinatoka humo humo ndani ya nchi, kwa hiyo, inafaidika zaidi. Watumishi, karibu kila kitu kinatoka pale na Canada ni hivyo hivyo.

Botswana wenye wameingia mapema, kwa hiyo, wanapata *share* kubwa sana, sasa sisi hapa Tanzania, kwenye *operating costs* ambako ndiko kuna hela nyingi, utakuta ni kiasi kidogo tunachofaidika pale, kwa hiyo, hatufaidiki chochote ndiyo tunalilia ile asilimia tatu. Sasa Serikali inabidi iangalie katika hii asilimia 80, tutaingiaje? Kuna mianya ambayo tunaweza kuingia japokuwa ni kazi kubwa kwa sababu kazi ya migodi inahitaji mtaji mkubwa na inahitaji vifaa vizito, ambavyo mara nyingi vinatoka nje, lakini kwa kazi nyingine, nadhani Serikali inahaja ya kuanza kuangalia kwenye hii asilimia 80,

sisi tutapata nini na tumependekeza kwamba, sasa Serikali ianze kuweka mikakati. (*Makofi*)

India na Sri-Lanka, mwekezaji hawezi kungia bila kuwa na *local partner*, lazima wawepo washirikiane, kama hauna *local partner* hakuna. Sisi anakuja anaingia, tuwe na utaratibu huo, nafikiri tunaweza kuanza kuliangalia hilo. Halafu wanaajiri wale watu ambao wanaona kwamba, hawakuweza kupatikana nchini, sisi hili hatujaliangalia, nafikiri tunaweza kulingalia hilo. Kwa mfano, Nyamongo, tumekuta walinzi ni wa-Nepal, sasa kuna mtu anaweza akalinda kuliko Mkurya, maana yake Wakurya ndiyo kazi yao, hawaulizani unafanya kazi gani, anauliza wewe ni jeshi gani hata kama ni mwalimu, wale wanajua kazi ile. Kuna kazi ambazo wanaweza wakazifanya watu wetu. (*Kicheko/Makofi*)

Hata kuagiza mafuta tunaweza kuangalia makampuni yetu ndiyo yanaweza kuagiza badala ya mafuta kuagizwa na *TOTAL* ya Kenya yakapitia hapa yakaingia, kwa hiyo, fedha inakuwa imebaki hapa. Ajira tunaangalia kwanza wazawa kuna kazi ambazo wanaweza wakaingia hapa sio watu watoke nje, unakuta wameajiriwa watu kutoka Ghana wakati mwingine watu wetu wanajua zaidi.

Mheshimiwa Spika, wanasema vyakula vyenu ni *sub-standard*, lakini nafikiri kwa sababu kuna *loophole* ya kuweza kuleta vyakula kutoka nje, vyakula vinaweza vikawa vinatoka nje kwa sababu kuna nafasi hiyo. Kwa sababu watu hawa tunakutana nao kwenye nyama choma, vikiletwa kule wanasema ni *sub-standard*, lakini kwenye nyama choma tuko pamoja nao. Nadhani kuna haja ya kuangalia ni sehemu gani tunaweza kuingilia tuweze kushirikiana na watu hawa. Maana yake tuking'ang'ania kwenye ile asilimia 20, tutabaki pale pale lakini tuangalie hapa ambapo kuna nyama kubwa sisi tuaingiaje? (*Makofi*)

Hata vipuli wanaweza akapatikana watu wa hapa wenye uwezo wakaagiza vikaingia kwa kupunguziwa kodi, sio kwamba vikiagizwa na Mzungu ndiyo vipunguziwe kodi lakini Mwafrika akiagiza vinapandishwa kodi. Hata karatasi kupeleka karatasi pale Geita kutoka Mgololo zimebekewa kodi lakini zikitoka nje hazikuwekewa kodi, sasa maana yake nini? Baadaye tukiwaliza wanatuambia sasa kwa nini ninunue hapa wakati za kutoka nje ni bei nafuu. Kwa hiyo, lazima tuviwezeshe viwanda vya ndani, ndiyo maana Afrika Kusini wameondoa, kwa sababu ile migodi iko pale kuweza kuinua viwanda vingine ndiyo wanapata faidi hiyo. Nilipenda nilieleze hilo kidogo kwamba, lazima tuangalie wapi fedha inapatikana.

Wakati tunazunguka wengine walikuwa wanasema huwezi ukalinganisha maendeleo ya Tanzania na Afrika ya Kusini au na Ghana, ambazo zimechimba migodi miaka mia moja, hiyo ni *wrong conception*, kwa sababu *technology* ya miaka mia moja iliyopita sio ya leo. Leo *technology* iliyopo ni ya kuibua sio mchezo, ni *weak* ile ya miaka mia moja, ni miaka mitano ya sasa hivi watu walioko kule wanachimbua hasa na wanafanya kazi saa 24. Kwa mfano, Tulawaka ni miaka minne, uangalie walichochukua kama wangefanya kwa miaka mia moja iliyopita pale wangekaa zaidi ya miaka hamsini. Kwa hiyo, lazima tuangalie tunakokwenda, ndugu zangu suala la madini linahitaji

kufanyiwa marekebisho haraka. Ningependa nimwombe Mheshimiwa Waziri katika hili, najaribu kufanya haraka haraka mambo ambayo wameambiwa yarekebishwe haraka ni vizuri yarekebishwe.

Mimi niliangalia mahusiano ya Wananchi na migodi inapokuja na nchi nyingine, sisi nadhani hatujaweka utaratibu mzuri, hatuna utaratibu kwamba, huyu anayehama asiende na manung'uniko, ndiyo maana hata anayefanya *exploration* anaweza akaenda kwenye shamba la mtu, akaendesha greda lake akaliungurumisha huko mtu amelala usingizi na linapita kwenye shamba la mtu ili mradi amepewa ile leseni ya kufanyakazi kwenye eneo lile. Watu wa *East African Mining* wanaenda wanazunguka kwenye mashamba ya watu, wanakuwa na nguvu kuliko mwenye shamba, mahusiano yanakuwa ni mabaya na wanafanya hivyo kwa sababu hata wakidaiwa *compensation* inakuwa ni kidogo. Hatujaangalia sana watu waliopo pale. Wenzetu Ghana wana utaratibu wa *resettlements*, wanaangalia atakayehamishwa atakayekuwa *compensated*, wanahakikisha wanaangalia akakae wapi, wanamwekea makao.

Lakini *experience* niliyopata Kahama na Geita ni chukua hela uende, na hela zenyewe ni kidogo, nitatoa mfano hapa, naona aibu hata kuzitaja, kuna *schedule* ya malipo hapa, anaitwa Vumilia Mhelo Mkandi, wememlipa shamba la viazi shilingi 840, *DC* kasaini, *Regional Commissioner* kasaini, yaani shilingi 840 ni viazi vingapi hivi, shamba la viazi hili, nafikiri kuna tatizo hapa. Shamba la viazi na *land officer* kapiga sahihi hapa, sasa tunatarajia nini kinachotokea hapa. Watu wanaendelea kulalamika hapa. Halafu kuna mwingine huyu angalau amelipwa shilingi 48,000 kwa shamba la viazi na ye. Kwa hiyo, utaratibu wa kufidia mtu bado ni tatizo, mtu anaondolewa kwenye nyumba wanasesma hii ni nyumba ya nyasi, sawa, anaambiwa lakini tunasahau kwamba huyu anayehama inatakiwa ijengwe nyumba mpya anakokwenda kule akaanze maisha upya. Ni vitu ambavyo vinahitaji kurekebishwa. (*Makofi*)

Kingine ninachoomba Mheshimiwa Waziri, hili suala tulilopendekeza kwenye Mikataba liangaliwe upya. Mikataba kweli hebu kaeni muiangalie, kuna vitu ambavyo havipendezi. Kwa mfano, kuna *contradiction*, Mikataba unasesma walipe dola 200,000 kwa Halmshauri huku Sheria inakuja inapinga, fedha zisilipwe sasa hata ile Kamati ilikuwa inajiliza tufanye nini sasa. Je, kama walitaka kuwalipa watawapa? Kwanini lisirekebishwe hili haraka haraka. Naomba *Attorney General* naye aangalie Wanasheria wake wanafanyaje kazi?

Halafu lingine kwenye Sheria, inakuwaje Mikataba yote ifanane, jaribu kuliangalia kwa kuwa tumeshalieleza kwenye Kamati, ninachoomba mkalifanyie kazi. Kwa mfano, dola 200,000 ni *fuel revenue* kwa migodi yote, *why flat rate* wakati Kahama na Geita ni migodi mikubwa sana na Lusu, Nyamongo na Tulawaka ni migodi midogo? Wote wanalipa *fuel revenue* dola 200,000, sijui ni *criteria* gani waliitumia hapa? Kuna haja ya kuangalia upya, vitu hivi vyta haraka haraka na tunavyochelewa kama nilivyosema, kulikuwa na uchimbaji wa kiwango cha juu itafikia mwisho kabla utekelezaji wake haujaanza. Tunaomba Mheshimiwa Waziri, mliangalie sana

Lingine ni la wachimbaji wadogo, wananyanyasika sana, wanapata shida, kwa mfano, kuna wachimbaji wa Kwamarwa wametumia karibu miaka mitano kuomba leseni,

mimi nimeingia Ubunge bado wana-*apply* leseni, ndiyo wamepata juzi, wengine wemeshatawanyika, wengine wameshakufa ndiyo leseni inapelekwa.

Jamani wasaidieni wapeni eneo lao, wapewe thamani na misaada, kuwe na mikakati ya kusaidia wachimbaji wadogo hawa ndiyo watakao tuondolea umaskini, kwa sababu mchimbaji mmoja anaweza kuchukua watu zaidi ya 500 wakafanya kazi. Kwa mafano, mchimbaji kama Kadeo au Ahmed, hawa wanakuwa na watu nyuma na kuwasadia wasiuze mashimo yao kwa sababu wakiiza ndiyo migogoro inaanza kwa sababu anawaacha wale wengine hoi. (*Makofi*)

La mwisho, napenda nizungumzie kuhusu matumizi ya fedha zinazopatikana kwenye migodi, tafadhali tunaomba zitumike vizuri. Kwa sababu dhahabu inakwisha, madini yanakwisha, tutabaki hatuna kitu, tuige kama Botswana wanavyofanya, kwenda kwenye miundombinu na tunaomba sasa Serikali ione aibu, kule kwenye machimbo iweke miundombinu. Nilipokuwa nazunguka nilikuwa na mtu mmoja anatoka Moshi katika Kamati, akaniuliza hivi huku ndiyo mnakotoka Wasukuma, ndiyo kwenye dhahabu huku?

Nikawa nataka kujificha chini ya kiti cha gari, kwa sababu nyumba zinatisha, mashamba ya ajabu, lakini mashine zinaunguruma pembeni za kuchimba dhahabu. Sasa oneni aibu kwamba, wale watu wanahitaji msaada kwa sababu katika bajeti zote, sikuona upendeleo wowote kupeleka kwenye maeneo yale. Serikali sasa ione aibu au basi wekeni Sheria, Waziri asitokane na Wabunge ili tubanane vizuri, wote tuwe jiwe moja hapa, tunaomba tafadhali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. PHILIP S. MARMO: Mheshimiwa Spika, ahsante. Hii ni nafasi yangu ya pili kujiunga na mjadala katika Mkutano huu wa Bajeti ya mwaka 2005/2006. Nilishatoa rambirambi kwa wale waliotutoka na niliwapongeza wale walioleuliwa kugombea nafasi ya juu katika nchi yetu. Isipokuwa hapa katikati bahati mbaya Mwenyezi Mungu alimchukua Mbunge mwenzetu, mashuhuri na mahiri sana, Hayati Margareth Bwana. Mwenyezi Mungu aiweke roho yake mahali pema Peponi, Amina.

Mheshimiwa Spika, huu sio wakati wa kukandiana. Tunakwenda kwenye mashindano makali ya kisiasa; ingawaje mimi sina tatizo kubwa sana, kuna dalili nitashinda. Lakini pamoja na hayo mimi nafikiri kuna haja ya kuzingatia kanuni za kuendesha shughuli katika nyumba hii. Hivyo kabla sijaanza ningeomba utupe mwongozo wako kwamba magazeti ya leo, yote, haturuhusiwi kusoma magazeti humu ndani, mimi nimeoma kule nje. Hotuba ya Wizara hii ilikuwa imesomwa nchi nzima toka usiku wa manane. Kwa upande wa Kanuni, naomba mwongozo wako lakini kwa upande wa Serikali wanaelewa wenyewe kwamba hii si halali kwa sababu hata taarifa zetu za Kamati zinakuwa wazi tukiweka mezani hapa. Lakini baya zaidi kama Wabunge tunaona wananchi kusoma huko nje, asubuhi leo sisi tukiwa hapa ndani. Kwa lugha ya Kiingereza tunasema wame-*pre-empty* tunayojadili hapa na athari yake ni kubwa sana kwa wale

ambao tunawawakilisha ambao wamesoma hotuba hii toka usiku wa manane. Kwa hili, kwa sababu huu sio wakati wa kukandiana sana, utusaidie baadaye kutoa mwongozo wako.

Mheshimiwa Spika, Wilaya yangu pia ina madini. Lakini kwa sababu wengi wenye kufahamu eneo hili kwa undani wamelisemea vizuri na siyo tatizo na kero kwa wananchi ninaowawakilisha hapa, mimi nitakwenda moja kwa moja kwa upande wa nishati hasa umeme.

Jana niliuliza swal la nyongeza, liko kwenye *Hansard* kuhusu eneo hili. Leo nimeogopeshwa zaidi na kutishwa na maneno mazito ya uchungu yaliyosemwa na Wabunge wenzangu kuhusu namna ambavyo umeme unasambazwa katika nchi yetu. Nimetiwa uchungu zaidi na mjadala wa Mheshimiwa Ponsiano D. Nyami, Mbunge wa Nkasi, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mbunge wa Singida Kusini na wengine. Sio vyema kwa nchi inayoheshimika kama nchi yetu, nchi inayoendesha mambo yake kistaarabu na kufuata haki; inasikitisha maneno mazito kama haya kusemwaa katika nyumba ya heshima kama hii.

Ni imani yangu wanaohusika wote, Mheshimiwa Waziri na wenzake wote, Waziri na wenzake wote wanalelewa jambo hili kama ambavyo limesemwa kwa uchungu sana na wenzetu. Hili lisichukuliwe kwamba ni kwa sababu ni wakati wa uchaguzi, hapana. Jambo hili limeanza kufuatiliwa toka miaka ya mwisho ya 1960, toka tulipomaliza mradi wa Mtera. Nitalielezea zaidi baadaye.

Mheshimiwa Spika, katika mtiririko huo na kwa kufahamu kwamba vianzio vyetu vya nishati vimeduwa vichache sana, sasa tumeanza kutumia gesi. Lakini vianzio ambavyo tumevitegemea zaidi ni maji na kupata nishati kutoka nje ya nchi ambalo ni jambo zuri.

Mheshimiwa Spika, kwa taarifa, Utumishi wangu katika Umma niliuanza katika Mkoa wa Kigoma, Mkoa tajiri, wenye rutuba na ungelisha nchi hii kwa mazao ya viwanda na kilimo. Hakuna Mkoa ambao nishati ya umeme uko karibu kama Kigoma. Nchi za Afrika ya Kati, *Congo*, Burundi na Rwanda zina vianzio vya uhakika vya nishati.

Maelezo ya Serikali kwamba umeme kutoka Burundi usingeingia Tanzania, hayana msingi hata kidogo. Pamoja na migogoro yote iliyokuwa Burundi na Kongo, njia za nishati, njia za umeme ambazo zinatikanya kwenye mipaka yetu, kwenye mashamba ya miwa, hata mara moja haijadhuri, ziko salama muda wote. Kwa hiyo, mimi bado ni mmojawapo wa wanaoamini kwamba haki haitendekei kwa maeneo kama haya muhimu sana.

Mheshimiwa Spika, nataka kusema machache kwa undani, kuhusu *TANESCO*, uendeshaji wake na miradi iliyoko na nisingependa kuongelea bila kumsaidia Waziri na Naibu Waziri kwa sababu baadaye hapa tutachukua muda mrefu sana katika vifungu. Naomba Mheshimiwa Waziri asaidiwe na Maofisa wa Wizara yake kuhusu mchanganuo wa fedha hizi. Kwanza, fedha ambazo zinatakiwa zitumike na *TANESCO* kama

matumizi ya kawaida, kwa mfano kasma ndogo ya 3195, Menejimenti ya *TANESCO*; uendeshaji wa *TANESCO* Shilingi milioni 620 ambayo tunapewa na Sweden, huu ni mkopo. *Managers* nafikiri wanapewa fedha zao kutokana na biashara ya umeme wanayoifanya.

Pili, Waziri apate maelezo ya kutosha kuhusu umeme Vijijini. Hili ni chanzo cha wananchi na Wawakilishi wao kusema kwamba eneo hili haki haitendeki tofauti na MMEM, tofauti na MMES, tofauti na *PADEP* na miradi mingine ambayo inaendeshwa katika nchi yetu. Tuna mikopo na mikopo hii tutalipwa wote. Tuanze na mkopo wa *African Development Bank* ambaao ni wa *Electricity 4*; ile kasma 3190, Shilingi bilioni 2.4. Lakini pia kuna mkopo mwingine wa *African Development Bank* kasma 3.3293 *rural electrification*, mkopo kutoka *ADF* Shilingi bilioni 1.1. Hizi fedha ni za mkopo na fedha hizi tunatakiwa tupate mchanganuo wote ili tujue ni kwa nini wananchi wanunung'unika, kwa nini tunasema kwamba haki haitendeki.

Awali nimesema sisi ni watu tuliostaarabika, watu ambaao tunatenda haki, lakini kwa wakati kama huu ambapo mlango umekuwa wazi, njia imeonyeshwa na wenzetu wa Wizara ya Elimu, Wizara ya Kilimo, Wizara ya Mifugo hapa na barabara. Kwa nini inakuwa ni *discretion* ya watu wachache kugawa fedha ambazo hatimaye tutalipa wote? Kwa hiyo, ningependa kabla ya kusimama hapa wakuandalie mchanganuo wa fedha hizi za mikopo kutoka *African Development Bank*, hizo kasma mbili nilizozitaja.

Lakini pia kuhusu umeme Vijijini, tunafahamu kuna mpango wa umeme wa Ukerewe, umeme wa Serengeti na umeme wa maeneo mengine. Tuseme wazi kwamba kasma hii ni ya umeme wa kwenda Serengeti, umeme wa kwenda Urambo, umeme wa kwenda Ukerewe kwa sababu Sweden hapa kwa umeme Vijijini inajitokeza karibu mara tano. Kasma tano tu kwa ajili ya Sweden, zinakwenda wapi? Umeme Vijijini, mkopo kutoka Spain, tunataka mchanganuo. Shilingi bilioni 20 ni fedha nyingi sana, zinakwenda wapi?

Mheshimiwa Spika, hili litamsaidia Mheshimiwa Waziri kujibu hizi, hoja za uchungu za Waheshimiwa Wabunge, kwa sababu siyo kwamba fedha hakuna, fedha zipo. Sasa haya ni mambo machache ambayo kwa ajili ya kuhifadhi muda wakati wa Kamati, ni maeneo machache ambayo Waziri angweza kusaidiwa na wenzake mchanganuo mzuri ili na sisi tupatiwe majibu na hasa mimi ningependa kupata majibu kwa sababu mbili:-

Kwanza, Wilaya mimi ninayotoka, upande wa Magharibi iko chini ya Meneja wa *TANESCO* wa Singida na umeme umeingia katika Mji wa Haidom miaka kama 25 iliyopita na biashara na viwanda vya Mji huu vinachangia sehemu kubwa sana katika pato la Taifa, Biashara ya *Regional Manager* Singida. Lakini kwa miaka 25 hata kilometra moja ya kupanua umeme haijawezekana. Mwananchi wa maeneo hayo akitaka kuona umeme lazima aende Singida au Iramba Vijijini. Lazima aende kuona umeme kule! Toka mwaka wa 1980 hata kilometra moja iliyoongezewa kutoka Haidom. Upande wa Mashariki Meneja wa Wilaya yetu anatoka Arusha na hivi sasa ni miaka kadhaa alikuwa

anaendesha mradi unaoitwa *Electricity 4* ambao pia nimeutaja mwaka huu 2005 umechangiwa Shilingi bilioni mbili, ni mkopo.

Lakini katika *Electricity 4*, ukiacha Makao Makuu ya Wilaya kwa miaka 10 iliyopita, hakuna hata kilometa moja iliyotengwa, lakini kwa Wilaya nyingine zote ikiwa ni pamoja na Kiteto, Simanjiro, Monduli, Hanang, Babati zote zimetengwa zaidi ya kilometa 60, kilometa 40, kilometa 30, Mbulu hamna hata kilometa moja. Kwa nini wananchi wasijiulize kuna nini?

Tuliahidiwa kilometa 20 pengine, ni kidogo sana, lakini hata hizo baadaye zilindolewa. Baadaye nitamwomba Mheshimiwa Waziri, uamuzi wa kuondoa kilometa 20 katika Mradi wa *Electricity 4* ambao ungekuwa utekelezwe Wilaya ya Mbulu, kwanza uamuzi wa kuondoa hizo kilomita 20 ulichukuliwa na nani na ni lini na kwa sababu gani?

Kwa kweli mimi nasikitika. Sio wakati wa kuvutana sana katika Bajeti hii, lakini angeniambia ule *mradi wa Electricity 4* utarudishwa. Miji ambayo imepelekewa *Electricity 4* katika Mikoa niliyotaja, ni Miji midogo sana, unaweza ukaunganisha Miji mitano ndiyo unapata Dongobeshi. Dongobeshi siyo kwa Shule moja, Shule kadhaa za Sekondari, viwanda kadhaa lakini kilometa 20 haipelekwi kule. Sio kwamba hatukuomba, tumeomba sana.

Mimi huwa nawaambia wananchi hali halisi ndiyo maana wananielewa. Yawezekana chochote hunatolewa, mimi sina uwezo wa kutoa chochote. Kwa sababu kama ni kuomba tumeomba, hoja imejengwa na tuna sifa zaidi ya Miji mingi ambayo imepelekewa umeme huu. Sasa tatizo ni nini?

Mheshimiwa Spika, kwa nini niunge mkono hoja hii? Ahsante sana. (*Makofî*)

MHE. MBARUK K. MWANDORO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana na mimi kunipa fursa ya kuchangia katika hoja hii.

Awali ya yote, ningependa kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Wataalam wa Wizara hii kwa kazi nzuri ambayo wanafanya na kwa hotuba nzuri waliyoandaa kwa ajili ya Kikao hiki.

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo imeelezwa na Waheshimiwa Wabunge waliopita na kama ambavyo imeelezwa katika ripoti ya Wataalam iliyongozwa na Dr. Kipokola, Sekta hii ya Madini na Nishati ina nafasi nzuri sana ya kuweza kuchangia katika maendeleo ya nchi yetu. Ni kweli kwamba mchango wa Sekta ya Madini na Nishati umekua kwa haraka katika miaka hii michache iliyopita.

Lakini vile vile ni ukweli kwamba huko huko kunaweza kuongezeka kukasukumwa zaidi na hali endelevu zaidi. Haya yamejidhihirisha siyo tu kutokana na taarifa ile ya Kamati ambayo ilikwenda huko na taarifa hiyo ambayo imetolewa hapa tukaifanyia semina, lakini hata sisi baadhi ya Wabunge wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara tulipata fursa ya kwenda nchi hizo na kujionea hali hiyo.

Ukweli wa mambo ni kwamba, dhana ya Serikali ya kujitoa katika shughuli za uzalishaji, lazima tuiangalie vizuri katika masuala kama haya. Nchi kama Botswana, Afrika Kusini na Namibia zinafaidika sana kwa sababu Serikali yenyeWE inaingia kwa ndani zaidi, inawekeza katika shughuli mbalimbali na kwa hiyo, kuweza kuangalia uzalishaji unakwendaje, kusimamia kwa karibu zaidi, kudhibiti kwa karibu zaidi na kutegemea zaidi mapato ambayo yanatokana na shughuli hizo pengine kuliko mrahaba au masuala mengine kama hayo.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninapendekeza kwamba ni vizuri Wizara hii ikazingatia kwa makini taarifa ile ambayo imetolewa na Kamati ya Dr. Kipokola na kuitekeleza kwa makini. Naamini kwamba ile tukiitekeleza ipasavyo, nchi yetu itawenza kufaidika sana katika suala hili na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, masuala mengine yamezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge, lakini si vibaya na mimi nikarudia. Suala hili la kuongeza thamani kwa bidhaa. Ni muhimu sana hasa bidhaa za madini. Tumeona wenzetu kule Botswana wanavyofaidika na kuongeza thamani ya bidhaa yao ya Almasi. Almasi yao wanaichimba wenyeWE pale na kuisafisha wenyeWE. Kwa hiyo, wameWEza kupata faida kubwa sana. Mimi nashukuru kwamba Tanzania tumeanza hatua ya awali ya ile ya *TANSORT* London kuitoa kwa *Williamson Diamonds* tukaileta kwetu. Nafikiri hii ni hatua moja nzuri ambayo itatupeleka pazuri.

Ni jambo la kuhuzunisha kwamba hawa *Williamson Diamonds* tumekuwa nao lakini Mgodi wa Almasi wa Mwadui, miaka nenda miaka rudi wanasema hawa jamaa wanapata hasara. Wanaendelea kuwepo na zaidi ya kuendelea kuwepo wanataka wachukue hata ardhi ambayo haiko kwao. Wawekezaji wengine na wananchi wanataka kuchukua wao. Sasa hili jambo linasikitisha sana. Kwa nini wawe wanapata hasara kwa kuendelea kuwa hivyo?

Wizara ilitufahamisha kwamba ilikuwapo Kamati ambayo imeundwa kuchunguza juu ya suala hilo au wataalam ambao wameWEkwa. Nafikiri ipo haja wataalam hawa wahimizwe wafanye shughuli hiyo haraka iwezekanavyo ili tuweze kujua ukweli wa mambo kwa sababu haiwezi kuwa ni kweli kwamba hawa wamepata hasara na miaka nenda miaka rudi unaweza kuwapo na unataka kuchukua ile ardhi, unataka kuwachukulia wale wananchi wengine kule. Si kweli, jambo hili na nashukuru Wizara imechuka hatua hiyo na ihimize hatua hiyo na hatua zinazostahili zichukuliwe.

Ni kweli kwamba hisa zetu ndogo na labda pengine na sisi wenyeWE hali yetu ya uchumi ni ndogo, lakini ikiwezekana tuweze kuongeza hisa katika migodi hii mbalimbali. Wenzetu katika sehemu tulikokwenda siyo migodi ya almasi tu na dhahabu, migodi mingine yote wana hisa kubwa zaidi na hata mfumo wao wa kodi ni mzuri. Pamoja na kusema kwamba tunapenda kulinda kwamba sisi tumo katika ushindani, lakini wenzetu hawa walioko katika ushindani wameWEza kupata nafuu.

Mwenyekiti wetu Mheshimiwa William H. Shellukindo, alieleza vizuri kwamba bahati mbaya pengine kihistoria ndiyo ilitokea hivi sisi tukawa tumeangukia hali hii iliyyotujia. Kwa sababu mambo haya yalitokana na Ukoloni. Lakini kwa sisi wenyewe tumeingia, ni vizuri tukaitizama upya hii Mikataba ili tuone vipi tutaweza kufaidika na madini yetu haya.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la kufurahisha sana au jambo la faraja kubwa kwamba kila kunapokucha tunazidi kugundua madini zaidi na mafuta na gesi zaidi. Hili ni jambo la kufurahisha sana. Lakini kitu kimoja ni vizuri tukazingatia kwamba, shughuli za utafiti wa mafuta na gesi ni shughuli ambazo zinahitaji fedha nyingi sana. Ukitazama takwimu na ripoti za *TPDC* ni kwamba wao wanatumia fedha nyingi sana.

Bahati nzuri nilibahatika kwenda katika Kikao kimoja Entebe ambapo nchi za Afrika na nchi nyingine za Mashariki ya Kati zilikuwa zinazungumzia masuala ya Uwekezaji katika Sekta ya Nishati. Pale tuliona jinsi gani nchi mbalimbali wenzetu kama Kenya kwa mfano, wao hawana maliasili hii kama tuliyonayo sisi lakini wanatumia fedha nyingi sana ili kuweza kutafuta haya. Sisi ambao tumeona dalili nzuri ya mafuta, dalili nzuri ya gesi ya kutosha na tumeona jinsi gani inaweza kutupunguzia gharama ya kuagiza mafuta kutoka nje kwa faida kubwa sana, takwimu zimetolewa za kutosha.

Kwa hiyo, mimi nashauri Wizara na Serikali nzima kwa ujumla kusema ukweli, ilipe suala hili umuhimu na kipaumbele cha hali ya juu na kuweza kutoa fedha za kutosha kuiwezesha *TPDC* na vyombo vingine vinavyoshirikiana nao, siyo tu waweze kufanya utafiti unaostahili, lakini pia waweze kushiriki katika uwekezaji mkubwa zaidi kuliko hivi sasa. Hii ni kwa *TPDC* na nashukuru kwamba *STAMICO* inaundwa upya.

Hali kadhalika nayo *STAMICO* vile vile iweze kupewa uwezo mkubwa wa kuweza kutafiti, uwezo mkubwa wa kuweza kuwekeza ili tusiwaachie hawa wenzetu toka nje, kweli tunawaamini, tunawavutia waje, lakini ni vizuri na sisi wenyewe keki yetu hii tukaifaidi kidogo siyo tu wenzetu wakaila keki hiyo kwa ukubwa zaidi. Kwa hiyo hili ni suala, kuna maombi mengi hasa kuhusu suala la *Mnazi Bay* tulipata maombi mengi sana. Wizara inajua takwimu zake, Serikali inaelewa. Haya ni masuala ya kusaidia hizi Taasisi ili tuweze kufaidika kwa nguvu zaidi. (*Makofit*)

Mheshimiwa Spika, nashukuru kwamba Wizara hii imejitahidi kwa kadri inavyoweza kusambaza umeme. Ndugu zangu wamezungumza kwa uchungu mkubwa sana matatizo ambayo sehemu mbali mbali tunapata.

Nashukuru kwamba vile vile tumeweza kutengeneza hii Taasisi ya umeme vijijini pamoja na mfuko wa umeme vijijini. Hili tulifanya na wakati tulipopitisha sheria zake hizi tuliomba sana Wizara kwamba urasimu usitumike kama vile ambavyo umetumika kuianzisha *EWURA*. *EWURA* tumeipitisha siku nyingi sana lakini mpaka leo haijafanyika. Sasa hii, hii Taasisi ya umeme vijijini na Mfuko wa umeme vijijini tunaomba nayo isije ikachelewa kama zilivyochelewa hizi.

Lakini pamoja na kuchelewa huko, mimi naamini kwamba Serikali kama alivyosema Mheshimiwa mmoja aliyepita hapa kwamba ziko fedha nyingi kutoka Sweden, kutoka sehemu nyingine mbali mbali zipo kwamba wakati huu kama *TANESCO* yenye we haiwezi kufanya kazi hiyo, Serikali kupitia mifuko yake hii mbali mbali inaweza kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, yako maeneo mengi sana ambayo tumekuwa na maombi muda mrefu. Jimbo la Mkinga, Wilayani Muheza ni mahali ambako kusema kweli umeme hauko katika Vijiji muhimu. Hili suala linafahamika vizuri sana kwa viongozi wengi. Ahadi nyingi zimetolewa na Mawaziri wengi kuanzia Mheshimiwa Dr. Abdallah Omar Kigoda alipokuwa Waziri kule, wakaja wengine mpaka mwisho ndugu yangu Dr. Ibrahim Msabaha akapita pale, akawatania Wazee wa Kidigo watani wenzake akawaahidi Vijiji vya Daluni, akaahidi Vijiji vya Gombero, Kijiji cha Kwale, Kijiji cha Mkinga kwamba tutaleta umeme haraka iwezekanavyo. Mpaka sasa haujaja.

Tulijua kuwa kuna matatizo lakini maombi haya ni ya miaka mingi sana na kule kwetu tuna nafasi nzuri sana ya kuendelea kwa sababu si tu uzuri wa rutuba ya ardhi tuliyonayo, lakini madini tunayo kwa wingi na bidhaa nyingine kwa wingi. Kwa hiyo, uwekezaji ni kitu ambacho kina nafasi nzuri sana, lakini uwekezaji hauwezi kufanyika bila umeme. Sasa hivi tuna wawekezaji wamekuja sehemu za Kwale na sehemu nyingine, lakini wanashindwa kuendelea na shughuli hizi kwa sababu ya suala hili.

Tuna Shule zetu za Sekondari ambazo zinahitaji umeme nazo zinakwama. Tuna Vituo vyetu vya Afya ambavyo vinahitaji umeme, vinakwama na haya masuala na mimi ningependa kuuliza kama walivyouliza wenzangu, sijui kosa ni nini? Watu wetu wa Jimbo la Mkinga wanalamika sana sana sana. Wamekosa Wilaya, sasa wanasesma hata umeme pia jamani mnatunyima! Wilaya haya tuna elewa kwamba labda kuna gharama kubwa, sasa umeme ambao kwa sehemu kubwa hauko mbali sana toka Vijiji mbalimbali. Upita katika mashamba ya mkonge na katika gridi kubwa ile ambayo inapita kwenda kuungana na Kenya. Sasa ningeomba Mheshimiwa kwamba suala hilo Wizara ilifikirie kwa bidii na kuweza kutuondolea kero hii ambayo tumekuwa nayo kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, nikirudi katika masuala ya madini, nafikiri wenzangu wameeleza, lakini sio vibaya nikigusia kwamba wachimbaji wadogo wadogo wanapata taabu sana. Wanapata taabu kwanza, kutambuliwa *rights* zao; pili, kupewa leseni; tatu, kutokuwa na taalauma ya kutosha.

Mheshimiwa Spika, sasa haya mambo wenzangu wameeleza, lakini na mimi ningependa kusisitiza kwamba ni vizuri Wizara hii ikawa na mipango mizuri ya kuwabaini hawa wachimbaji wadogo wadogo kuwawekea taratibu nzuri za mafunzo, kuwawekea taratibu nzuri za kuwapatia leseni, kuwapatia taratibu nzuri za kuwapatia vifaa mbalimbali. Wengi hawa wanachimba kienyeji bila utaratibu mzuri, lakini wakipata vifaa tutakuwa tumewasaidia. Mimi naamini kwamba chini ya MKUKUTA, Wizara hii iweke utaratibu maalum ambao utaweza kuwasaidia wachimbaji wetu wadogo waweze kuendelea katika shughuli hii.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo napenda kuunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja na nashukuru sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge kama nilivyowataja waliokuwa wamejiandikisha kuchangia hoja hii, kulikuwa na wawili amba walishachangia mara moja tu na amba vile vile niliwataja. Sasa nilishaeleza siku za nyuma kwamba tunaweza kuendelea na mjadala ikibidi mpaka saa 11.30. Kwa hiyo, hawa wawili waliobaki watachangia mchana saa 11.00 mpaka 11.30, nao ni Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz na Mheshimiwa Lekule Laizer. (*Makofi*)

Baada ya hapo Mheshimiwa Philip Marmo aliomba mwongozo kuhusu jambo ambalo limetokea. Kwa jumla mwongozo ni kama ifuatavyo:- Jambo hili huwezi kulikuta kwenye Kanuni, yaani huwezi kulisoma ndani ya Kanuni. Lakini ni taratibu, mionganoni mwa taratibu ambazo zinakubalika na kuheshimiwa sana katika mwenendo wa Bunge, zinaitwa *Convention* kwa Kiingereza. Ni taratibu ambazo zina nguvu ile ile sawa na Kanuni. Sasa hizi taratibu huwa tunazijadili kwenye Mikutano ya Maspika wa *Commonwealth*.

Tunapokutana ni kwamba wakati Bunge linakutana, kama Bunge liko *in session*, mawasiliano yoyote ya kutoka Serikalini kwenda kwa wananchi lazima yapitie kwa Wawakilishi wao Bungeni, yaani lazima Serikali izungumze na Wabunge kwanza kabla haijazungumza na wananchi kupitia Vyombo vya Habari. Ni *convention* iko hivyo. Kama Bunge haliko katika Vikao, hiyo tofauti.

Lakini kama Bunge lipo, linakutana, ni Serikaliitazungumza na wananchi kupitia kwa Wawakilishi wao Bungeni. Ndiyo maana kuna Kanuni ya Kauli za Mawaziri ili kutoa nafasi kwa Serikali kama kuna jambo linatakiwa lijulikane haraka kwa wananchi, Waziri anapewa nafasi, anatoa kauli hapa Bungeni.

Sasa kilichotokea leo nimekwishamwuliza Mheshimiwa Waziri, anakiri kwamba ilikuwa ni kosa la kiutendaji. Ni afadhalii nikasoma maelezo niliyopewa ili yaingie kwenye *Hansard*. Anasema:-“Mheshimiwa Spika ni dhahiri hiki kilichotokea ni kosa la kiutendaji. Hatujaua kosa hili limetoka ndani ya Wizara au limetokea kule kule kwenye magazeti. Kilichokusudiwa ni kwamba hotuba hiyo ilipaswa ichapishwe kesho, yaani baada ya kusomwa Bungeni na siyo leo. Ndiyo utaratibu waliojiwekea Mawaziri, kwamba wakishasoma Bungeni, hotuba inaonekana kwenye magazeti ili wananchi nao wapate fursa ya kuisoma. Sasa anasema Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri wanaomba radhi kwa kosa hilo na watalifuutilia na kuchukua hatua pale itakapohitajika kuchukuliwa.

Kwa hiyo, ilikuwa ni bahati mbaya Mheshimiwa Philip S. Marmo, tuhesabu kwamba jambo hili limekwisha. Nimeishasoma kwamba wameomba radhi, si lazima itoke mdomoni kwa Waziri mwenyewe.

Sasa, nikumbushe tu kwamba Kikao cha Waheshimiwa Wabunge wa CCM kinafuata mara baada ya kusitisha shughuli za Bunge. Baada ya maelezo hayo sasa nasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 jioni.

(*Saa 06.56 mchana Bunge lilifungwa mpaka Saa 11.00 jioni*)

(*Saa 11:00 jioni Bunge lilirudia*)

Hapa Naibu Spika (Mhe. Juma J. Akukweti) Alikalia Kiti.

MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kukushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie katika hoja iliyoko mbele yetu. Naomba nianze kwanza kuwapongeza Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Naibu wake na Watendaji wao kwa hotuba yao nzuri.

Aidha, nitoe pongezi nyingi kwa Mwenyekiti wa Kamati Biashara na Uwekezaji kwa hotuba yake nzuri ambayo kwa kweli kwa jumla naiunga mkono sana. Naomba nianze kwanza kwa kusema kwamba naunga mkono hoja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende katika maeneo machache ambayo naomba Serikali itufanyie uamuzi au ufanuzi ambao tutauelewa wengi. Naomba nianze na jengo la Mafuta House (*TPDC*) na *National Housing* waliwekeza pesa zao pale, lakini yale majengo yako matatu, Serikali imeamua kuchukua yote na kuwapa *NSSF* bure, lakini yako majengo mengine ambayo wenyewe walioanzisha walishindwa kuyamaliza, kwa mfano jengo la *NIC* kule Ubungo, Serikali ikaagiza waingie ubia *NSSF* lakini bado *NIC* wanayo haki na majengo yale. Kwa nini haiko hivyo kwa Mafuta House? (*Makofî*)

Lakini kama vile haitoshi, lile jengo limejengwa sehemu maalum kwa ajili ya kutunza *data* za mafuta ambazo nyingi ziko nje ya nchi. Kama ilivyoandikwa kwenye hotuba ya Kamati, nyingine ziko pale nje zinaharibika tu, kwa nini hatuipendi nchi yetu? Kwa nini Serikali haiko tayari kutoa eneo lile kwa ajili ya kutunza kumbukumbu zile ambazo ni muhimu sana kwa nchi yetu? Kikwazo ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli napata wasiiasi na utaratibu mzima ule wa kuhamisha miliki hii ya jengo kutoka *TPDC* kwenda *NSSF*. Ukiangalia pale mwanzo *TPDC* walikuwa wanahitaji Shilingi bilioni 15 jengo lile limalizike lakini *NSSF* wanatumia Shilingi bilioni 30 kwa jengo hilo hilo. Kidogo hapa wanantia wasiiasi. Naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa *ana-wind up* anieleze, kwa nini Serikali haitaki kutoa lile eneo kwa *TPDC*? Kama siko sahihi atuambie leo kwamba lile eneo limetolewa kwa Shirika la Maendeleo ya Mafuta, vinginevyo nadhani kidogo itakuwa taabu kukubaliana huko mwishoni tunakoelekea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio kwamba natishia hapa, ni ukweli tu kwamba tupate maelezo ya kueleweka kwamba jengo limejengwa kwa kazi hiyo, Serikali haitaki kutoa kwa nini. Naomba nipate maelezo kidogo ya kuridhisha na kama inashindikana yote,

basi angalau wapeni *tower* moja ile wachukue mbili hawa NSSF lakini sio kuwanyang'anya kabisa wakati wengine ambaao wanashindwa wanaingia ubia hawa hawaingii ubia. Kuna nini hapo ndani yake? (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba vilevile nizungumzie kuhusu gesi asilia. Nianze na gesi ya Songo Songo. Gesi hii imeanza kutoa manufaa makubwa kwa viwanda ambavyo vinaitumia. Gharama nadhani zimepungua kwa matumizi ya hii gesi. Lakini gharama zimepungua kwa wenye viwanda peke yake, hakuna faida ambayo inaonekana. Kwa mfano, bei za vitu hazipungui, wala watumishi hawaongezewi mishahara. Sasa sielewi faida hii. Nadhani ni vizuri hawa ambaao sasa hivi angalau gharama zimepungua wangejaribu kutenga fungu kwa watumiaji wengine ama kwa wafanyakazi wao au kushusha bei ambazo sasa hivi wanazalisha, kwa sababu sasa hivi zile bidhaa wanazalisha chini ya gharama kuliko hapo awali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie gesi ya asilia hiyo hiyo kwa upande wa gesi ya *Mnazi Bay*. Gesi ya *Mnazi Bay* ndio inatazamiwa kutoa umeme kwa Mikoa ya Lindi na Mtwara, lakini kwa sisi kule lazima uunge Lindi, Mtwara na Tunduru kwa sababu Tunduru ni karibu sana na Mtwara kuliko Songea. Lakini nataka kujua kwa sababu nimepata habari kwamba umeme ule utakuwa ghali kuliko umeme mwingine wa maeneo mengine ya nchi yetu.

Sasa hapo nataka nizungumzie Mikoa ile ya Lindi na Mtwara kwamba kwa muda mrefu imekuwa nyuma kimaendeleo. Sababu zipo za kihistoria sitaki kuzirudia, tunataka umeme sasa ili tuweze kupata maendeleo ya haraka tupate wawekezaji, tupate viwanda ili na sisi tupate maendeleo. Kutuletea umeme wa bei ya juu kuliko maeneo mengine ya nchi, hatuko tayari kukubali hilo, kwa sababu umeme huo utakuwa upo lakini wananchi watashindwa kuilipia. Hakuna mtu atakayekuwa tayari kuwekeza Lindi na Mtwara kwa sababu umeme ni ghali. Kwa hiyo, umeme ule utakuwa ni hasara kwetu kuliko faida. (*Makofî*)

Naomba Mheshimiwa Waziri atupe uhakika kwamba umeme ule utakuwa na bei inayolinga na maeneo mengine ya nchi yetu. Kama ni umeme wa bei ya juu ya kuliko ulivyo sehemu nyingine, kwa kweli hauna maana yejote kwetu na itakuwa ni mpango tu wa Serikali kuendelea kutuzuia maendeleo kwa sababu umetupa umeme ambaao haununuliki, umeme ambaao wananchi hawauwezi, viwanda hawawezi kulipia, viwanda havitakuja vitaendelea kujengwa maeneo yale yale ambayo viwanda viko vingi na ambako kutakuwa na umeme rahisi. Kwa hiyo, sioni sababu kwa nini katika nchi moja bei za umeme ziwe mbili tofauti kati ya eneo na eneo.

Ningependa kutoa tahadhari tusiunde *IPTL* nyingine, tuwe na hakika kabisa kwamba umeme huu utakuwa na bei sawa na sehemu nyingine na kwa maeneo mengine, kwa vile sisi tulikuwa nyuma kimaendeleo kwa muda mrefu, kwa sababu ya vita na hivi Serikali ilistahili sisi tupewe umeme rahisi kuliko sehemu nyingine kwamba ninyi mlikuwa kwenye vita basi, umeme senti nne au pengine senti sita ili watu wengine wavutike kuja kwetu kule.

Lakini mkituwekea umeme wa juu ni kuendelea kutuumiza na kwa kweli Mheshimiwa Waziri naomba nitoe tahadhari kwamba kwa kweli hatutakuwa tayari kupokea umeme ambao una bei ya juu kuliko maeneo mengine ya nchi yetu.

Kama ni lazima, basi Serikali yenyewe itoe *subsidy* kutuongeza pale, lakini sisi tuuziwe umeme kama wanavyouziwa wengine. Vile vile, ningeomba wataalamu wetu wawaangalie wawekezaji hawa gharama wanayoweka kama ni sawasawa na ni ya lazima. Kwa sababu wengine wanawekeza kwa gharama kubwa kwa matumizi ya baadaye, lakini walipaji tuwe sisi. Leo naomba tuwe waangalifu katika eneo hilo, tuone kwamba wanawekeza yale ambayo yanatakiwa kwa sasa sio wawekeze kwa matumizi ya baadaye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Nabu Spika, tatizo lingine katika eneo hilo, ni nani anayesambaza huu umeme? Umeme wetu katika nchi hii unasambazwa na *TANESCO*. *IPTL* umeme wao wanawauzia *TANESCO*, *Songas* wanauzia *TANESCO*, ndio watu wasambazao umeme Tanzania. Umeme wa ATUMAS nani anasambaza? Tungependa umeme ule uendale kusambazwa na *TANESCO* na kama haiwezekani tuambiwe kwa nini haiwezekani? Kwa sababu wao ndio Shirika la Kusambaza Umeme hapa Tanzania. Sasa nataka tuelewe. Msiwape kila kitu wao na gharama zikawa kubwa sana tukashindwa kuzimudu.

IPTL imekuwa ni gumzo kila sikukwa ajili hii kupitia Bunge, naomba kuipa Serikali tahadhari kwamba tusijilingize katika *IPTL* nyininge. Mheshimiwa Waziri, Naibu wake na Watendaji wao wawe waangalifu sana, naomba hili walione. Sio kwamba mnamatiliza huu Ubunge ndio mnasema kwamba itakuwa mimi sipo, utakuwepo hapa hapa, tutawaona humu ndani au kwenu tunakujua tutawaambia, jamani nyie mlituponza! Nawaombeeni kila la kheri mrudi tena humu Bungeni na mrudi hapo hapo mlipokuwepo lakini tunasema tunataka umeme Lindi, Mtwara na Tunduru, lakini tunataka umeme wenye bei inayolingana na maeneo yote yaliyopo hapa nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la mrabaha. Kuhusu mrahaba wa madini, kumekuwepo na malalamiko mengi sana kuhusu asilimia ndogo ambapo Serikali inapata asilimia tatu. Kweli ni ndogo. Nilikuwa ninaomba Serikali ione, hivi hakuna uwezekano wa kukaa wakapitia Mikataba ile upya wakairekebisha kwa mujibu wa Sheria? Sio kwa kutumia ubabe, hapana. Kwa mujibu wa Sheria.

Haiwezekani wakaa wakaangalia upya ile Mikataba kuona jinsi gani nchi yetu inapata manufaa zaidi kuliko ilivyo sasa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nilikuwa naomba niunge mkono hotuba ambayo alitoa Mheshimiwa Shellukindo pale mapema kwamba uchimbaji wa vito uachwe kwa wazawa peke yake, hawa wakubwa wachimbe migodi mikubwa mikubwa almasi na dhahabu, lakini biashara ya vito, rubi, tomalini na vitu vingine tuwaachie wananchi wenyewe Wazalendo ili waweze kujiendezeza.

Mimi nafikiri wanaweza, kama Serikali itaamua kuwasaidia kupata nyezo ili waweze kuchimba hivyo vito, tuwatafutie masoko ili waweze kuuza hivyo vito. Lakini kuwaachia wageni wafanye kila kitu, tutawaacha Watanzania hapa nchini hawana shughuli ya kufanya, kwa sababu wenzetu wana mitaji mikubwa, kwao Benki yapo wanakopesha mapesa huko, kwetu sisi hapa hakuna pesa.

Kwa hiyo, hawawezi kushindana nao. Lazima tuwapendeelee kwa namna fulani na upendeleo wao ni huo kwamba ni wao peke yao ndio waruhusiwe kuchimba madini ya vito ndani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru, lakini naomba Mheshimiwa Waziri ayafikirie vizuri niliyoongea na baadaye anijibu vizuri ili nisipate taabu ya kusimama hapa tena kwenye vifungu kuuliziaulizia.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kusema, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini. Lakini mimi sitangulizi kuunga mkono hoja hii na pamoja na kuwa najua tu kwamba itapita, lakini sio vibaya ikipita bila mimi kuunga mkono. Siungi mkono kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba zote za Wizara ya Nishati na Madini kwa miaka kumi nikiwa hapa Bungeni, kila hotuba nimechangia na nikichangia, ni kwa ajili ya kuomba umeme katika Jimbo la Longido. Mheshimiwa Rais mwaka 1996 alikuja Longido na Namanga, akaahidi kabisa kwamba umeme utafika maeneo ya Jimbo la Longido, lakini mpaka sasa amemaliza muda wake na naamini kwamba Rais alitaka umeme ufile huko, lakini Watendaji hawakutaka.

Mwaka 1999 akiwa Waziri Dr. Abdallah Kigoda, niliuliza swali hapa Bungeni, nilisimama wakati wa vifungu akaomba akasema kwamba mwisho wa mwaka huo 999 umeme utakuwa umefika Namanga. Lakini haujafika mpaka leo.

La pili, Mheshimiwa Waziri alitaja Wilaya ambazo hazina umeme, hakutaja Monduli kwa sababu Monduli ina umeme, lakini ukitaka kusambaza umeme Monduli, katika Vijiji vya Vilaya hiyo haiwezekani kabisa umeme wa Monduli ukaenda Longido.

Sisi tunapakana na Rombo, umeme umefika Rombo lakini haukufika Vijiji vinavyopakana vya Jimbo la Longido, umeme unafika Hai, Siha tunapakana nao lakini umeme umeishia huko, haufiki Jimbo la Longido; umeme umefika Arumeru tunapakana nao lakini umeme haukufika Jimbo la Longido. (*Makofi*)

Kwa hiyo, unakuta Jimbo la Longido ni giza. Kwa sababu hiyo, nasema siungi mkono hotuba hii. Niliunga miaka tisa mfululizo, sasa huu mwaka wa mwisho nasema kwamba siungi mkono kabisa. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kila mwaka kuna swali langu kuhusu umeme Longido na Namanga, cha ajabu wataalamu wameandika *proposal* nzuri sana waliyopeleka *World Bank* na Mkurugenzi wa Umeme Vijijini yuko hapa anafahamu kabisa, ilipopelekwa Wizara ya Fedha wakaenda kukataa kuipitisha. Ni hayo ndio yananikera nisiunge mkono hoja bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, sisi hatuna umeme, lakini misitu ya Jimbo langu imeisha kutokana na kuchoma mkaa na huo mkaa unapelekwa Arusha Jimbo la Longido linabaki kuwa jangwa hatuna umeme, hatuna misitu, yote imeisha kwa ajili ya kupeleka mkaa Mjini Arusha wale wale watu wenye umeme. Kwa hiyo, nasema, hata nikiunga mkono kwa kweli wananchi wa Jimbo langu watanicheka kabisa kwamba sikuchangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika maeneo yote, vijana wanahangaika hawana kazi, umeme ni kitu kimojawapo ambacho kitaleta ajira katika maeneo yote.

Kwa hiyo, vijana wa Mji wa Longido na Mji wa Namanga, wangepata ajira wangefungua viwanda vidogo vidogo, sasa hakuna. Kwa hiyo, hili linaonyesha upendeleo mkubwa uliopo katika Wizara hii. Kama kuna Wizara yenye upendeleo katika Serikali ya Jamhuriya Muungano ni Wizara hii. Wanabagua maeneo, wanabagua Wabunge, kunawanaosikilizwa na kuna wengine hata ukilia hausikilizwi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naona kama umeme umekuwa wa upendeleo kana kwamba nimeomba fedha kwa Mheshimiwa Waziri, itakuwa ni mshangao. Nimesema miaka kumi niliyopiga kelele hapa, miaka kumi niliyoandika maswali kuuliza umeme Namanga ni kwamba Mawaziri, kuanzia Waziri Shija, niliomba akiwa Waziri Shija akiwa Waziri wa Wizara hii, Mawaziri wote waliopita niliwafuata Ofisini, hawa waliopo sio mara moja nilikwenda kwao, hakuna jibu lolote nililopata.

Kwa hiyo, napenda kusema kwamba, kwa hili na kwa upendeleo mkubwa ambao Serikali imeonyesha kwamba kuna maeneo ambayo yanabaki kuwa maskini, yanabaki nyuma kimaendeleo ni pamoja na Jimbo la Longido ambayo maeneo yote, Wilaya zinazonguka Jimbo la Longido wana umeme lakini wamekataa katakata kwamba umeme usifike Longido. Kwa hiyo, nasema kwamba kwa hilo na mimi sitaunga mkono hoja hii, hata ikipita na ipite bila mimi kuunga mkono. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

MICHANGO KWA MAANDISHI

MHE. EDSON M. HALINGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichagie hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa bajeti ya mwaka 2004/2005 Waziri aliniahidi mbele ya viongozi wa *TANESCO* wa Mkoa wa Mbeya kwamba umeme

utafikishwa Iyula ambako nguzo zilikuwa zimesimikwa tayari mwezi wa kumi. Mpaka leo hii ni nguzo tu na hakuna matumaini wala Waziri hajasema lolote katika bajeti yake ya leo ya mwaka 2005/2006. Hatujaamini kuwa ahadi zilikuwa ni klinikanyanya tu. Naomba majibu ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilayani Mbozi kumejitokeza wachimbaji madini wasiofufuta utaratibu wa sheria na wamesababisha uharibifu wa mazingira na kuharibu mali za wananchi bila fidia. Wizara ina taarifa zote lakini hakuna maelezo yoyote kuhusu suala hili katika hotuba ya Wizara. Naomba Wizara itoe tamko kuhusu hali hii.

Mheshimiwa Naibu Spika,kuhusu umeme Mbozi umekuwa si wa uhakika, huzima wakati wowote na kusababisha kuunguza vifaa kama majokofu, mashine za kusaga, mita na kadhalika. Hasara hizi zinapotokea *TANESCO* husema hawahusiki. Nani awajibike katika hili? Na hatua gani zichukuliwe?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kucheleva kuanzisha kutoa umeme wa makaa ya mawe Mchuchuma, kunalimbikiza umaskini katika nchi hii suala la kusema eti umeme utakuwa mwingi zaidi si la kweli, kwa sababu haja ya umeme katika nchi ni mkubwa sana. Wazo la kuuza umeme wa ziada nje ya nchi, haliwezekani kwa vijiji vingi kwani baadhi ya Wilaya hazina umeme. Naomba hili liangaliwe kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Wizara ielewé kuwa bila umeme kufikishwa vijijini, hali ya umaskini haitakabilika. Naunga mkono hoja kwa kutegemea kuwa nitajibibiwa mashaka yangu.

MHE. DIANA M. CHILOLO: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Daniel Yona, Mbunge, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Mbunge, Katibu Mkuu na Watendaji wote walioshiriki katika kuandaa bajeti hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali pamoja na kuuliza maswali hapa Bungeni, mara kadhaa juu ya upelekaji wa umeme Taarifa ya Ihanja katika Jimbo la Singida Kusini. Serikali imekuwa ikitoa ahadi nzuri kwa zaidi ya miaka miwili bila utekelzaji hadi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali, kuitia bajeti hii itamke rasmi umeme utapelekwa lini katika Tarafa ya Ihanja ili taasisi mbalimbali zinazotoa huduma humu ziweze kuboresaha huduma zao kwa wananchi, ili wananchi waweze kuwa na imani na Serikali yao ya CCM kwani wameanza kukata tamaa kwa nguzo kukaa muda mrefu hadi zimeanza kuibowi kwa matumizi mengine ambayo haikuwa azima ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nishauri Serikali juu ya *Net Group Solution* kwani toka uongozi huu upewe dhamana ya kusimamia suala zima la umeme nchini, hatujaona matunda yake au mafanikio yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi huu umekuwa na kiburi, kwani wamekuwa wakikata umeme hovyo, hovyo, hata taasisi muhimu mfano, hospitali, kambi zote za jeshi

na kadhalika, bila kujali kwamba hizo ni sehemu nyeti hazistahili kukatiwa umeme hata kidogo. Naomba maelezo ya Serikali inasema nini kuhusu udhaifu au mapungufu haya makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kutamka kwamba kati ya mikoa iliyobahatika kuwa na madini ni pamoja na Singida na nina furahi kusema kwamba kati ya wananchi wanaojishughulisha na uchimbaji wa madini ni pamoja na wanawake, katika machimbo ya Sambalu. Kata ya Mang'onyi, Kijiji cha London, Manyoni Mashariki, Machimbo ya Mlima Sekenke, Iramba Magharibi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iwape kipaumbele wanawake wanaojitahidi kuondokana na umaskini kwa kuwakopesha fedha za kununulia vifaa vya kisasa kwa ajili ya uchimbaji wa madini. Vile vile pamoja na soko huria la madini ningeishauri Serikali iwatafutie wananchi soko kwani wananchi wanauzu madini kwa walanguzi kwa hasara ambao sio rasmi. Vile vile wanawake wapewe leseni kwa ajili ya uchimbaji ikiwa ni njia mojawapo ya kumkomboa mwanamke anayejitahidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukumbushia kauli ya Serikali juu ya kununua mtambo wa umeme kutoka *IPTL* iliyotoa hapa Bungeni kwani mpaka sasa hatuoni utekelezaji wala kauli yoyote ni nini kinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kauli hiyo ya Serikali, wananchi waliifurahia sana kwani tungeondokana na hasara kubwa inayotokana na mkataba kati ya Serikali na *IPTL* wa kulipa shilingi bilioni 3.6 kila mwezi.

Mwisho, napenda kutamka rasmi kuwa naunga mkono hoja hii asilimia mia kwa mia. Nasubiri maelezo ya hoja zangu hapo juu.

MHE. ALI SAID SALIM: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia suala la utafutaji na uzalishaji wa gesi asilia umekuwa dhahiri. Mimi ushauri wangu kuhusu masuala ya gesi asilia iwepo sheria itakayoshughulikia masuala ya gesi hiyo na hivyo vihusishwe vipengele vingi zaidi vinavyohusu gesi asilia.

Pili, kuna suala ambalo ningeshauri lifanyiwe marekebisho Sheria ya *Petroleum (Exploration and Production Act* ya mwaka 1980). Marekebisho hayo yatakafanyika itaendana na hali ya sasa ya utafutaji mafuta ni vizuri Serikali ingepitia marekebisho ya Sheria hiyo yaliyoahirishwa mwaka 2002.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia suala la utengenezaji wa barabara hasa kwa kupita eneo la machimbo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni hayo tu nilipenda kuchangia. Ahsante sana.

MHE. JANETH E. MASHELE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini kwa hotuba yake nzuri na mwelekeo unaoeleweka. Kwanza kabisa napenda kuzungumzia suala la migogoro mbalimbali inayotokea huku migodini mfano suala la kampuni ya *Williamson Diamonds Limited* na

El-Hial Minerals Limited ni jukumu la Serikali kusimamia na kusuluhiha migogoro hiyo haraka ili isije ikaleta athari ya uzalishaji wa almasi nchini.

Suala lingine ni suala la utafutaji na uzalishaji wa gesi asilia umekuwa dhahiri na jukumu la Serikali kutunga sheria itakayoshughulikia masuala ya gesi asilia na hivyo kuhusisha vipengele vingi zaidi vinavyohusu gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia suala la machimbo ambayo yapo hapa nchini kwetu ni ya kwetu Watanzania. Hao wanaokuja kuwekeza siyo ya kwao. Hao nao ni wenyeji wawe na heshima. Hivyo ni lazima nao wenyeji wao waliangalie hilo kwa makini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nazungumzia suala la kuzurura kwa makampuni. Leseni kufanya utafiti wa mafuta ni uchelewesha shughuli lakini kwa upande mwengine tunavunja Katiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hayo niliyoyaona kwenye mchango wangu.

MHE. RAPHAEL N. MLOLWA: Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu juu ya hotuba ya Mheshimiwa Daniel Yona, Mbunge, Waziri wa Nishati na Madini kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Fedha ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2005/2006 utalenga maeneo machache yafuatayo:-

Kwanza katika aya ya 11 Waziri amezungumzia vigezo vinavyotumika kupeleka/kusambaza umeme nchini, kwamba msukumo unapelekwa kwenye makao makuu ya Wilaya, Miji Midogo na kwenye vituo vya kuzalisha mali. Naomba sera ya nishati ifikie kuongeza kusambaza umeme kwenye vikao vya afya kwani hivi ni vituo muhimu kwa kuimarisha huduma za afya nchini.

Pili, nimesoma kwa makini matatizo katika sekta ya nishati kama anavyofafanua Waziri kwenye aya ya 13. Nadhani matatizo hayo yawe fundisho kubwa juu ya udhaifu wa mipango yetu wa kutenga nishati inayotokana na mafuta ambayo haina uhakika. Maji mara nyingi yanategemea mvua. Pakiwa na ukame, panakuwepo na uhaba wa nishati ya maji. Kwa upande mwengine, gharama za mafuta zikipanda katika nchi yanakotoka mafuta gharama za nishati ya umeme nazo zinapanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Nishati na Madini ina dhamana kubwa kwa Watanzania kusaidia kupunguza gharama za uzalishaji wa mali na huduma *goods and services* nchini kwa kuhakikisha nishati ya bei nafuu. Kwa kuzingatia dhamana hiyo, inashangaza kabisa kwamba Mheshimiwa Daniel Yona hakuzungumzia chochote juu ya mradi wa nishati kutoptana na makaa ya mawe. Kulikoni mradi wa umeme wa mkaa wa mawe wa Mchuchuma Mheshimiwa Waziri?

Tatu, nimerejea jedwali Na. 9 linaloonyesha michango ya makampuni makubwa sita kiuchumi nchini. Utaona kwamba michango ya makampuni katika huduma za jamii vijijini ni ya kusuasua. Inapenda na kushuka kila mwaka na haitabiriki. Tunategemea

fadhila za viongozi wa migodi waliopo. Huku nyuma, mimi nimelisemea sana suala hili, kwa masikitiko na kutoa tahadhari juu ya athari za mwenendo huu. Kwa uzoefu wangu wa kuwa karibu na uendeshaji wa kampni ya Dhahabu ya Kahama (*KMCL*) na pengine na ile ya Geita, suala la kampuni na haya hayana nia yakinifu kusaidia jamii zinazozunguka migodi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima pawepo utaratibu unaoamimika, unaotabirika na wa uhakika katika utoaji wa misaada ya makampuni ya madini kwa jamii katika maeneo yao. Utaratibu huo budi ubuniwe na kusimamiwa na Serikali Kuu, badala ya kuachiwa Halmashauri za Wilaya/Miji ambazo hazina uwezo wa kufikia mikataba yenyе maslahi kwao hasa zinapopambanishwa na makampuni haya ya Kimataifa yenyе uzoefu wa muda mrefu wa mikakati ya kuweka mbele faida kuliko kitu kingine chochote.

Mwisho katika aya ya 37 Mheshimiwa Daniel Yona anazungumzia suala la mwekezekaji *Richmond Development Company* katika mradi wa Bomba la Mafuta Dar es Salaam hadi Mwanza na hakuzungumzia kabisa mwekezaji mzalendo aliyepo kwenye mradi - *Afrocommerce International Limited*.

Katika majadiliano yaliyofanywa kati ya Waziri na Kamati ya Fedha na Uchumi ambaye mimi ni mjambe, ninavyofahamu ni kwamba maelewano yalikuwa kusaidia *Afrocommerce International Limited* ifanikishe uendelezaji wa mradi huo. Inasikitisha kwamba Waziri hajatolea maelezo yoyote kuhusu hatua ya *Africommerce International Limited* juu ya mradi huu!

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. DR. MILTON M. MAHANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa jitihada na kazi nzuri iliyofanyika katika sekta ya nishati na ile ya madini.

Kilio changu kikubwa Jimboni Ukonga ni mradi wa umeme wa kutoka Pugu kwenda Chanika. Mradi huu umesimama kwa zaidi ya miaka mitano sasa ingawa *TANESCO* wananieleza kwamba kwa sasa hawana fedha, naomba Wizara itoe kipaumbele cha kipekee ili mradi huu ukamilike kabla ya Oktoba mwaka huu. Eneo la Chanika limekua kwa haraka na kero kubwa ni umeme!

MHE. KABUZI F. RWILOMBA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Naomba umeme maeneo ya Nyakagwe, Bukuli, Nyarugusu, Rwamgasa, Kaseme, *Tembo Mine* na Katoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa kupeleka umeme Bukombe tokea Kakoka (Kahama) upitie maeneo hayo ya machimbo. Maeneo hayo ni maarufu kwa uzalishaji mazao ya kilimo na madini. Umeme ni muhimu kwa kazi ya uchimbaji.

MHE. BAKARI M. MBONDE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwanza kuwapongeza Waziri na Naibu wake na pia kuwapeni pole kwa majukumu mazito mliyo

nayo katika kusimamia Wizara hii ya Nishati na Madini ambayo ina matatizo mengi ya kiutendaji. Pamoja na yote naomba kuchangia yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Rufiji ni moja ya Wilaya ambayo Rais wa Awamu ya Nne atakabidhiwa, ambayo haina umeme. Pamoja na fidia wanazolipwa wananchi kwa sababu ya kutekeleza mradi wa umeme wa gesi ya Songo Songo katika Wilaya ya Rufiji hakuna popote katika bajeti ya mwaka 2005/2006 panapo zungumzia utekelezaji umeme makao makuu ya Wilaya ya Rufiji, Utete na Vijiji vyake. Je, hii tuamini kwamba kauli ya Serikali kwamba utekelezaji wa mradi wa umeme katika Mji wa Utete haikuwa sahihi au ilikuwa danganya toto?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa *IPTL* ni mali ya nani? Ibara ya 35 ya hotuba ya Waziri anazungumzia kukwama kwa mazungumzo na wadau wakuu wa mradi wa *IPTL*. Lakini wakati huo huo Serikali inawekeza Serikali inawekeza shilingi kufanyia marekebisho umeme wa *IPTL* ili uweze kutumia gesi ya Songo Songo. Kwa nini Serikali inajipa jukumu hili kama *IPTL* sio mali ya Serikali na wakati huo huo mawasiliano na Serikali ya Malaysia bado hayajaza matunda.

Suala la *Mafuta House*, mimi sidhani maoni ya Kamati ni kwa maslahi ya Taifa. Inaelekea kuna ubinafsi kati ya baadhi ya wajumbe na watendaji wa *TPDC*. *TPDC* na *NHC* hawana uwezo wa kulikamilisha jengo lile. Hakuna mbia ambaye yupo tayari kuendeleza jengo lile. Ama liachwe, lioze kwani halina thamani.

Lakini la msingi kwa nini Serikali haitaki kutoa hali halisi? Je, suala la kuwakabidhi *NSSF* jengo halikuwa kwa maslahi ya umme? Je, suala hilo halikuzungumziwa kwenye *Cabinet* au lilikuwa ni uamuzi wa mtu mmoja? Je Waziri anaona kigugumizi gani kuhusu hili?

Mimi naamini ilikuwa sahihi kuwapa tena bure Shirika la *NSSF* ili kuokoa mali ya umma ili mradi *NSSF* wamekubali kuwapa *TPDC* eneo la ghorofa ya chini mahususi kwa ajili ya kuhifadhi takwimu na miamba ya nishati ya mafuta. Ni vyema *TPDC* na Kamati ya Bunge ikaacha kuupotosha umma kuhusu *Mafuta House*. Aidha, watendaji wa *TPDC* wawajibishwe kama kweli wanakaidi uamuzi wa *Cabinet*.

Kuhusu gesi ya *Mnazi Bay*. Mradi huu ni mmoja wa miradi iliyokumbwa na ubinafsi wa watendaji wa Wizara ya Nishati na Madini. Kuna tuhuma kwamba si kweli kwamba mikataba ya usamabazaji na ununuzi wa gesi na umeme inaandaliwa, bali watendaji ndiyo wanakwamisha utiaji saini mikataba hiyo.

Je, Waziri atakubaliana na wale wanaodai kwamba kusuasua kwa mikataba inayohusu mradi wa *Mnazi Bay* inatokana na tuhuma kwamba umeme utakaozalishwa na gesi ya *Mnazi Bay* utakuwa na gharama ya chini sana kwa wateja kuliko ule utakaozalishwa na gesi ya Songo Songo na hivyo kuitia aibu Serikali na watendaji wa Wizara kwa gharama za juu za mradi wa gesi ya Songo Songo. Ni nyema Serikali ikatoa ufanuzi wa jambo hili na kuueleza umma kwa nini mikataba ya mradi wa gesi ya *Mnazi Bay* inahusishwa na kigugumizi cha watendaji wa Wizara ya Nishati na Madini?

MHE. ARIDI M. ULEDI: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nitachangia katika maeneo machache ya hoja ya Waziri wa Nishati na Madini. Matatizo ya sekta ya umeme yatakwisha lini? Matatizo hayo ni haya yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kushindwa kusoma mita za wateja kila mwezi hivyo kutoa bili za umeme kila mwezi bila kukadiria, kukatika umeme mara kwa mara kwa muda mwangi bila *TANESCO* kutoa taarifa yoyote, bila kiwango cha umeme kubadilika badilika mara kidogo mno na mara nyingine mwangi mno hivyo kuathiri vifaa mbalimbali vya wateja, gharama za umeme kwa *unit* moja kubadilika badilika mara kwa mara hivyo kutoa mwanya wa wateja kulipishwa zaidi na madai ya rushwa kutoka kwa wafanyakazi wakati wa kuunganishiwa umeme kwa maombi mapya na baada ya kukatiwa umeme au kuunganishiwa kwenye *line* zingine zenyе umeme wa uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo yote hayo yalikuwapo kabla ya Menejimenti ya *Net Group Solutions* haijaanza na wala sasa matatizo hayo bado yanaendelea. Hivyo kuna haja gani kuwa na Menejimenti hiyo wakati imeshindwa kuondoa kero hizo zote. Bado Menejimenti hiyo mpya inategemea ruzuku ya Serikali katika kuendesha *TANESCO*. Naomba Serikali kuangalia upya mkataba wake na *Net Group Solutions*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara nyingi nimekuwa naomba umeme uliopo Masasi upelekwe pia Jimbo la Nanyumbu. Kumekuwepo na sababu mbalimbali zinazotolewa na Serikali ambazo wakati mwagine zinapingana. Mara umeme hautoshi wakati umeme huo umesambaa hadi Wilaya kadhaa za Mikoa ya Mtwara na Lindi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini umeme huo ushindwe kufikishwa Jimboni Nanyumbu umbali wa kilometra 10 na kuendelea wakati umepelekwa zaidi ya kilometra 100 hadi Tandahimba! Naomba Serikali ianze mipango ya kupeleka umeme Nanyumbu ili kuondoa kero hiyo kubwa. Miradi mingi ya maendeleo inakwama kupelekwa Nanyumbu kwa kukosa umeme. Viwanda vya mbaao, nafaka, vimeshindikana kuanzishwa kwa kukosa umeme. Aidha, shule za sekondari, vituo vya afya, zahanati vinakosa kupata huduma mbalimbali za kisasa kwa kukosa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu madini nichangie tu juu ya eneo la chini la Mto Lumesule ambapo huko nyuma wananchi walikuwa wanachimba madini hapo lakini baaadaye waliondolewa kupisha uanzishwaji wa hifadhi ya pori la akiba la Lukwika-Lumesule. Hali hiyo imewakosesha wananchi kupata mapato kutokana na uchimbaji wa madini.

Naomba Serikali ingefikiria tena kuruhusu eneo lenye madini ambalo ni dogo sana wananchi wachimbe madini ili kuwasondolea umaskini. Kwanza eneo kubwa kuzunguka pori la akiba hilo linaathirika na wanyama ambaao hushambulia mazao. Hali hiyo huwaacha wananchi hao wakiwa maskini siku zote. Uchimbaji wa madini ungesaidia sana kuwaondolea umaskini huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango huo niseme tu kuwa naunga mkono hoja moja kwa moja.

MHE. SIJAMINI MOHAMED SHAAME: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii maalum kwanza kumshukuru Mungu kwa kuiunga mkono hotuba hii muhimu kwa asilimia mia moja. Aidha, niwapongeze sana Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu Waziri, Katibu Mkuu wa Wizara hii kwa kuonyesha kuwa wamekuwa saa zote wanafanya kazi zao kwa ushirikiano mkubwa na maelewano.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi binafsi na nina hakika hata wapiga kura wangu wa Kitope tunapata taabu kubwa kusikia kuwapo na malumbano ya aina yoyote kati ya Zanzibar na Tanzania Bara Kikatiba. Ninaloliomba kwa Wizara hizi mbili ni tendo la kuimarisha mambo yanayohusu Muungano wetu, kwani kuna nini na hili suala limeanzia wapi? Nadhani hili suala halina uhusiano wowote na mambo ya msongamano au adha za Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, waasisi wa Muungano wa Zanzibar na Tanganyika wengine bado wapo, hali na maadili ya Muungano wetu wanayaelewa na sisi tumekuwa tunaambibiwa. Hivyo ni kweli hawa wazee ambao tayari wako mbele ya haki (akhera) tunawapelekea zawadi gani? Nadhani viongozi wetu ambao mko hai na ambao mmepewa dhamana ya kuendeleza nchi hii tunashindwaje kukaa pamoja na kuona nini tatizo la faida ya mazungumzo yetu. Hakuna lisiloweza kuzungumzwa ila ni budi tutambue kuwa hii nchi ni moja, Taifa moja lenye kutarajia maslahi kwa nchi zetu zote mbili Zanzibar na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar ni yetu sote na Mungu katujaalia kuwa na visiwa na maskini sana na kwa maana hiyo nawaomba sana mtambue kuwa pale tunaposema lolote kuhusu hali yetu basi ni vyema mtuelewe na katu msituchoke. Kwa hiyo basi, Serikali zetu mbili ziache tabia ya kupata kigugumizi kuongea mambo yenu. Mimi sioni kama kitendo cha huu mzozo wa kutofanya utafiti wa mafuta kule Zanzibar si kitendo cha kukinaiyana ndugu wawili wa damu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri sana tena kwa haraka mkae pamoja na muangalie kwanza maslahi ya Taifa letu na tujaribu sana kurejea maudhui ya Muungano wetu na kwa nini Muungano umezaliwa hapa Tanzania. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa hapa Tanzania Bara afanye kila linalowezekana kumwona mwenzake wa Zanzibar na wafahamiane kwa kutowanyima haki Wazanzibari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mimi nina imani na Wizara hizi zote mbili nina hakika wana uwezo wa kuondosha suitafahamu hizi tena kwa muhimu. Najua kuwa Zanzibar wao hawana tabia ya kuzozana kwani wao Wazanzibar ndiyo waliobuni wazo la kutaka Muungano wa nchi mbili zilizokuwa na haki sawa sawa za kufaidi matunda ya Muungano yaani watu wa Zanzibar na Jamhuri ya watu wa Tanganyika. Maana ya Tanzania ni haki sawa kwa Zanzibar na Tanzania Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, namaliza kwa kuunga mkono hotuba hii kwa udhati wa moyo wangu, upendo mkubwa sana na naunga mkono hoja kwa asilimia kwa mia.

MHE. MUDHIHIR M. MUDHIHIR: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii. Mchango wangu unahusu kilio changu cha miaka yote kuhusu kupatiwa umeme katika vijiji vya Mchinga na Ng'apa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukipewa maneno matamu kila kipindi cha bajeti kinapofika. Mwaka 2004/2005 nilijibiwa humu Bungeni kuwa suala hili linashughulikiwa. Katika ufuutiliaji naambiwa nisubiri umeme wa *Mnazi Bay*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sitaki kuamini kuwa ndani ya Wizara ya Nishati na Madini au *TANESCO* yupo mtu au kikundi cha watu chenye visa na mimi binafsi au na watu wa Mchinga. Lakini kwa hakika inauma sana.

Namwomba Mheshimiwa Waziri leo awatamkie wananchi wa Mchinga kuwa ikiwa Wizara haina huruma na watu wa Jimbo hili, kwa nini inatoa ahadi za matumaini kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, sinayo maneno mazuri yanayokidhi kuelezea uchungu wangu juu ya suala hili.

MHE. LEONARD N. DEREFA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Naomba kutoa ushauri kwa masuala yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, uwezekano upatikane wa kujenga *Wind Turbines* sehemu za Same kwa kuwa kuna upepo wa kutosha huko. Utaratibu huu ni *environmental friendly*. Utafiti ufanywe wa kuwa na *Wind Turbine Farm*. Bado madini mchango wake kwa uchumi haijaridhisha. Niliona takwimu za dhahabu ya mchanga unachimbuliwa Japan kwa miaka mitano ni *US\$ 286 million* Serikali ililipwa *US\$ 7.40 million!* Hii ni balaa! Ni vyema sheria ikaboreshw. *Factors of production* ni tatu, moja ardhi, mbili *labour* na tatu ni mtaji. Sasa kama ardhi ni yetu kwa nini hatukupewa *shareholding* kwenye makampuni ya uchimbaji madini? Kweli huu sijui ni ujinga kiasi gani. Nitapenda maelezo kwa nini wawekezaji wa madini hawatoi *shareholding* kwa ardhi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchimbaji *petroleum* ukitazama ramani kule kunakochimbwa mafuta katika Bahari ya Hindi hakuna mafuta yanakochimbwa. Ila ni *SUMATRA*, India na kadhalika. Pamoja na bahati ya kupata gesi mwambao wa *Indian Ocean*, Tanzania. Nchi za Sudan na Uganda wamefanikiwa kupata mafuta ndani ya nchi hasa katika mabonde ya Ufa, *Wembele Plains* na kadhalika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mtaalam mmoja wa Japan amewahi kuandika kuwa mwanzo wa kupata mafuta mengi yanayopatikana Uarabuni ni *Salt Lakes* za *East Africa* kwa mfano, *Lake Eyasi*, *Lake Natron*, *Lake Manyara*, *Lake Kitangiri*, *Lake Balalaugila - Kateshi Area* na kadhalika. Ukweli huu ni vyema ukachunguzwa. Mtaalam huyo alidai kuwa mito ya chini (*underground rivers*) kama Mto Nile. Kwa sababu hiyo ndiyo kuna Oasis ndani ya *Sahara Desert*. Kutokana na joto kali la *Sahara Desert* ambalo ndiyo

kinapika mafuta hayo, kwa sababu hiyo ndiyo maana maziwa ya chumvi yote yana utaratibu wa kukauka wakati wa kiangazi kwa mfano, *Lake Eyasi* na kadhalika.

Kuhusu *NDC*, *STAMICO* na *TPDC* waendelee kupewa fedha za kutosha za kuwekeza kwa niaba ya Watanzania katika madini, viwanda vya madini na utafutaji mafuta. Kuhusu madeni ya *TANESCO* kwa muda mrefu kwa sasa wananchi wangu wa Shinyanga Mjini wanavyodaiwa madeni ambayo hayaeleweki. *TANESCO* Shinyanga wamewabambikiza madeni watu wangu na kuwatishia kuuza nyumba zao.

Nakuletea makala za madeni hayo. Hivi mtu anawezaje akatumia umeme wa nyumbani hadi shilingi 1,317,759.70 pasipo kukatwa! Wapo watu Mjini Shinyanga wanaonyanyaswa na watu wa *TANESCO* kwa mfumo huu, wanavivurugia kura zangu. Kama *TANESCO* walifanya uzembe kama huo mimi sielewi. Nililetewa malalamiko ya baadhi ya wananchi wafuatao: -

Ndugu Issa Iddi Mrisho, deni 1,317,759.70/=, Ndugu Juma Rashidi deni 422,591.56/= na Ndugu Kassim Abdala deni 358,272.95=/. Nitaomba maelezo kuhusiana na tatizo hili na kwa nini wavuruge watu wetu wakati wa uchaguzi? Mwenye kampuni ya *SUBIA* ni mtu wa *CUF*.. Nitashukuru kwa maelekezo.

MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ: Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itoe kauli kwa nini haitaki kuwapa *TPDC* lile eneo ambalo limejengwa mahsus kwa kutunza kumbukumbu za utafutaji mafuta. Kwa nini majengo kama *Ubungo Plaza* ambalo lilikuwa mali ya *NIC* limemalizwa na *NSSF* lakini *NIC* ni wabia katika jengo hilo kwa nini sio kwa *TPDC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Mnazi Bay* bei ya umeme isiwe tofauti na maeneo mengine kwa maana ya bei kuwa kubwa kwa sababu ya umaskini wa Mikoa ya Kusini na kukosa wawekezaji kwa muda mrefu. Serikali ipunguze bei ya umeme kwa kutoa *subsidy at least* ya 25% ili kuvuta wawekezaji katika Mikoa lyra Kusini na kuiendeleza kwa haraka mikoa hiyo.

Kuhusu mikataba ya madini kiasi cha 3% tunachopata ni kidogo sana. Serikali iangalie uwezekano wa kuipitia upya mikataba hiyo ili kuona namna ya kuongeza asilimia hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaunga mkono baada ya kujua hatma ya *Mafuta House*, bei ya umeme wa *Mnazi Bay* na sio vinginevyo.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napongeza sana kwa hotuba nzuri yenye ufanuzi wa kina kuhusu Wizara ya Nishati na Madini. Pili naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Pamoja na kuunga mkono naomba kuchangia maeneo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wizi wa nyaya za umeme ni tatizo kubwa pamoja na wizi wa mafuta ya *transforma* hapa nchini. Je, wizi huo umeisababishia

Serikali/Shirika hasara kiasi gani kwa kipindi cha mwaka 2004/2005? Je, Serikali imeweka mkakati gani kudhibiti hali hiyo ili umeme uendelee kutoa huduma kwa Watanzania? Je, ni watu wangapi wamekamatwa katika hujuma hiyo?

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Naibu Spika, bado Wizara hii haijawatendea Watanzania haki ya kufaidika na raslimali za madini katika nchi yao. Mgawanyo wa *royalties* (mrahaba) hasa kwenye maeneo yenye migodi utaendelea kuwa ni kilio cha kudumu kutoka kwa wananchi. Kiwango cha 3% kwa dhahabu na 5% kwa almasi ni kidogo ikilinganishwa na nchi nydingine kwa mfano, Eritria.

Mheshimiwa Naibu Spika, usombaji wa mchanga kupeleka Japan kwa nini unaendelea? Kwa nini isiwe katika nchi za Afrika ya Kusini, Ghana na Botswana, nchi hizo zinafanya nini? Upatikanaji wa umeme katika Wilaya ya Nzega hasa katika Tarafa ya Pege eneo la Nkimiziwa, Puge na Ndala. Je, ile ahadi ya Rais maandalizi yake ni nini? Kuna utaratibu gani wa kuanza ili iwepo ratiba maalum ya kupata umeme?

MHE. SEMINDU K. PAWA: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Wizara ya Nishati na Madini, ipokee pongezi za dhati kabisa toka kwangu kwa kazi nzuri zinazoonekana machoni kwetu Watanzania. Hongera sana Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, *DAP*, Wakurugenzi wa Wizarani hapo, Wakuu wa Idara, Taasisi zote ndani ya Wizara hii, hongereni sana. Apongezwe sana Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha Mbunge anatujibu vizuri maswali ya watani zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu wizi wa madini, udhibiti wake ukoje? Tunayo taaluma ya kufuatialia wizi wa aina hii hadi sasa wezi wangapi waliokamatwa kwa kutorosha madini yetu nchini?

Pia mrabaha, kwa nini mrabaha unakuta unawekewa vikwazo mara kwa mara? Natoa maoni kwamba wachimbaji wakubwa badala ya kujenga vitu wanavyovitaka kama vile shule, zahanati, pengine vipaumbele vyao wananchi siyo hivyo. Kwa sasa tuna MMES, MMEM, *TASAF* na MKUKUTA. Vitu vingi vitajengwa na mipango hiyo. Hivyo mrabaha uwe na fedha siyo vitu. Huo ni ushauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, jengo la mafuta (*Mafuta House*). Kwa nini jengo lile lilinyang'anywa toka kwa aliyelijenga na kupewa bure au kwa bei ya chee Taasisi ambayo inamiliikiwa na wanachama wachache wa Taasisi hiyo, nashauri basi warejeshewe fedha zao za ujenzi na gharama zao au eneo la chini ambalo ni hifadhi na maktaba ya mafuta wapewe warejeshewe basi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu makao ya Wizara. Wizara hii kwa umuhimu wake naomba sana itafute eneo zuri. Kwa nini baada ya kumalizia jengo la *Mafuta House* Wizara ishirikiane na *TPDC* imalizie jengo hilo ni Wizara ihamie hapo. Sekta ya Mafuta, *flow meter* imesaidiaje kupunguza bei ya mafuta?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini bei ya mafuta ya taa iwe inapanda mara 12 kulingana na bei ya mwaka 1995. Mnayo habari wanavijiji wanapapasana ndani hawana

uwezo wa kununua mafuta ya taa? Giza, giza majumbani. Shirika la umeme lina matatizo yafuatayo:-

Kwanza malipo ya kununua nguzo ni ghali mno wananchi wameshindwa kumudu. Kwa nini *tariff* yetu iko juu sana na Kidugallo, Mikese na Mkuyuni Kiroka, Matombo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji hivi wanaomba mradi wa umeme Vijiji Serikali inasemaje? *Bill* za umeme. *Bill* zinakuwa kubwa ukilinganisha na matumizi halali inakuwaje?

MHE. OSCAR T. MLOKA: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutanguliza kuunga mkono hoja ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa asilimia mia moja.

Pamoja na kuunga mkono hoja hii nina maoni na ushauri kwa utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Suala la huduma ya umeme katika Miji lina unyeti mkubwa sana. Miaka miwili iliopita niliomba usambazaji ufanywe ndani ya Jimbo langu la Morogoro Mjini kwa maeneo ya Bigisa na Konga.

Napenda kulishukuru Shirika la *TANESCO* kwa kutimiza ombi hili pale Bigwa lakini bado naomba wakamilishe eneo lililobaki la Konga katika Kata ya Mzinga kwa kuweka *transformer* kwenye umeme unaokwenda Mzumbe wenyewe Msongo wa 33 KV. Tayari nilishamkabidhi Meneja wa Mkoa majina ya wateja zaidi ya themanini na sita ambaao wamejiorodhesha kuhitaji huduma hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ni lalamiko langu binafsi kwa shirika la umeme, kulikuwa na hitilafu ya kiufundi kwenye *transformer* ya *Kola Hill Area* inayosambaza umeme hadi nyumbani kwangu. Nikitoa taarifa kwa Meneja wa Mkoa mwenyewe Ndugu Kamoleka ambaye aliwatuma mafundi. Mafundi walikiri kuwepo kwa hitilafu hiyo yaani waya wa *neutral* ulikuwa unasoma umeme hadi kufikia 140 volts kiwango ambacho hata Marekani hakitumiki (110 volts). Hitilafu hii imeharibu vifaa kadhaa vinyavolinda badiliko lolote haya la umeme kama *RCD*, *voltage stabilizer*, *cut out* na kadhalika ndani ya nyumba yangu na kuwasilisha gharama pamoja na vifaa vyenye vivilvyoharibiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza ni pale uongozi wa Mkoa ulipokubali hali hiyo na kuiwasilisha Makao Makuu ya *TANESCO* kwa fidia, lakini kuletewa jibu la kukataa eti kwa nini uharibifu huo utokee kwangu tu na siyo na wengine. Kwa hakika hauhesabu huu kuwa ni ubabaishaji kwa sababu uthibitisho umefanywa na Mkoa hivi huyu anayekalia kiti pale Dar es Salaam anawezaje kutoa sababu za ajabu kama hizi?

Naomba suala langu litazamwe kwa uangalifu kwani nalichukulia kuwa mimi nimetukanwa kuwa ni mwongo mbele ya shirika ukizingatia kuwa mimi ni kiongozi niliyeapa kulilinda na kulitetea Taifa hili. Hivi kama mimi ambaye ni kiongozi nimewenza kutendewa haya, mwananchi wa kawaida ambaye namwakilisha anawezaje akapata haki

yake kutokeapo hitilafu za kiufundi kama hizi? Kwa nini tunatafuta kesi zisizo za msingi kufikisha mbele ya vyombo nya sheria?

Mheshimiwa Naibu Spika, malalamiko haya nilishayafikisha nakala ya barua kwa Naibu Waziri wa Nishati na Madini, naomba sasa suala hili lifikie tamati kwa kumhusisha Meneja wa Mkoa wa Morogoro ndugu Nicolaus Kamoleka, aliyethibitisha tatizo hili kuititia kwa mafundi wake kama nilivyowataja kwenye barua zangu za malalamiko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyo tangulia kusema sina matatizo na Bajeti ya Wizara iliyowasilishwa hapa, hivyo narudia tena kwa kusema naiunga mkono mia kwa mia.

MHE. KHALID S. SURU: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kutoa fursa hii. Pili nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Daniel Yona na Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, kwa bidii zao kazini. Pia na usikivu wao kwa Waheshimiwa Wabunge. Nilipowaandikia barua kuwaeleza shida ya umeme Jimboni, haraka Naibu Waziri alitembelea Jimbo na Wilaya kwa ujumla. Nawashukuru na kuwapongeza. Kufika kwake kulisaidia Vijiji vifuatavyo kuwekwa katika programu ya utekelezaji 2005/2006.

Kijiji cha Choka, Mji Mdogo wa Kolo , Mji Mdogo wa Mnienia, Mji Mdogo wa Pahi, Mji Mdogo wa Kingale, Mji Mdogo wa Tyoli, Mji Mdogo wa Haubi na Gereza la King'ang'a. Ni mategemeo yangu na wananchi wa Jimbo la Kondoa Kaskazini kwamba kazi inaanza mara moja. Wananchi wamenituma kwamba nimwambie Mheshimiwa Daniel Yona na Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, wanataka kuona kazi, siyo maneno.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuikumbusha Serikali kilio cha wananchi wa Vijiji vifuatavyo kwa muda mrefu sasa yaani takribani miaka 8 hivi bila umeme japo njia au nyaya za umeme zinapita juu ya Vijiji hivyo. Vijiji au Miji hiyo ni Kijiji cha Puhi, Mji Mdogo wa Bereko, Kijiji cha Salanka, Kijiji cha Masawi, Kijiji cha Bukulu, Kijiji cha Kwadinu, Kijiji cha Kolo, Kijiji cha Choka na Kijiji cha Gubali, wapeni umeme ni haki yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme unaopita humo ni kutoka Babati - Kondoa - Kiteto tangu mwaka 1998 umeme wa gridi. Kwa nini wananchi wa Vijiji hivyo visipewa umeme hadi leo? Nahitaji maelezo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ni umeme ni ghali sana. Punguzeni gharama za umeme kwa faida ya wanyonge. Wakala wa umeme Vijijini (Sheria ya Bunge) waanze kusambaza umeme Vijijini haraka. Umeme huo unaweza kuwa nafuu sana pengine ni *solar* (jua) au jenereta.

MHE. PASCHAL C. DEGERA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuchangia hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini. Nianze kwa kumpongeza sana Waziri kwa hotuba yake nzuri. Aidha, nampongeza Waziri, Naibu

Waziri, Katibu Mkuu na Watumishi wote wa Wizara hii kwa kazi nzuri sana wanayofanya katika sekta zote wanazosimamia za Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru kwa namna ya pekee Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, kwa kufanya ziara katika Wilaya ya Kondoa na hususan Jimbo la Kondoa Kusini na kufanya kazi nzuri sana ya kuhimiza maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi kwa juhudi yake ya kusambaza umeme nchini. Kutokana na juhudi hizi Makao Makuu ya Wilaya ya Kondoa imekwisha unganishwa na Gridi ya Taifa (Umeme wa Taifa). Wananchi wa Wilaya ya Kondoa na hususan wa Jimbo la Kondoa Kusini wanashukuru sana kwa kazi hiyo nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Vijiji vya Mondo, Kelema Maziwani, Jenjeluse, Goima, Songolo, Chandama, Mrijo Juu, Mrijo Chini na Olboloti wanatoa shukrani za kipekee kwa Serikali kuwapatia umeme wakati wa utekelezaji wa mradi wa *Electricity IV*. Umeme umekuwa changamoto kubwa ya maendeleo katika Vijiji hivyo. Hivi sasa viwanda vidogo vidogo vya kusindika mazao vimeanza kujengwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ujenzi wa nyumba bora umeshamiri katika Vijiji hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutoa pongezi na shukrani zangu sasa naomba nichangie hotuba kwa maombi. Lengo la kufikisha umeme katika maeneo mbalimbali nchini ili umeme huo usambazwe kwa watumiaji. Nasikitika kusema kuwa pamoja na Serikali kufanya kazi kubwa na nzuri ya kufikisha umeme wa Gridi ya Taifa katika Jimbo la Kondoa Kusini lakini mpaka sasa ni wananchi wachache sana wanaonufaika na nishati hii kwa sababu Serikali haijafanya juhudi ya kusambaza umeme tangu mradi wa *Electricity IV* ukamilike miaka zaidi ya mitano iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusubiri muda mrefu Vijiji vifuatavyo vimeniomba nifikishe maoni yao kwa Waziri. Kwa ajili ya kumbukumbu ninaomba nivitaje; Pongai, Waida, Cheku, Sori, Kelema Balai, Dalai, Piho, Tandala, Mtakuja, Kinkima, Churuku, Jinjo, Jangalo, Itolwa na Mlongia katika Tarafa ya Mondo. Vingine ni Makamaka, Mirambo, Igunga, Hamai, Madaha, Mapango, Soya, Mwailanje, Mwaikisabe, Nkulari, Isusumya, Songambele, Mogasa, Msaada na Machiga katika Tarafa ya Goima.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Vijiji hivi vipatiwe umeme. Ukiacha hivi Vijiji karibu na njia ya umeme, kuna Vijiji ambavyo viko mbali na siyo rahisi kuvifikishia umeme kutoka chanzo hicho. Vijiji hivyo viro katika Tarafa ya Farkwa na Kwamtoro. Naomba Vijiji hivi vipatiwe umeme wa juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mchango wangu mdogo naomba niunge mkono hotuba ya Waziri wa Nishati na Madini.

MHE. ERNEST G. MABINA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa kabla ya yote naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja. Sitakuwa na maneno mengi ya kuchangia ila nataka kujuaya yafuatayo:-

Kwanza kuna mwekezaji ambaye amechukua eneo la Munguru ambalo lina matatizo kati ya wananchi na mmiliki wa mwanzo ambaye ni Kampuni ya *Chipaka Mining Co. Ltd.* Mwekezaji huyu kabla ya kumaliza mgogoro huu ameamua kuweka uzio eneo lote la machimbo ambapo wananchi wameleta malalamiko haya kwangu kuilalamikia Kampuni ya *Shanta Mining Co. Ltd.*

Je, Serikali inatoa tamko gani la kusimamisha shughuli zote za Kampuni hii mpaka shauri lao litakapoisha kule Mahakamani?

Pili, uwekezaji ni Sera ya Taifa kwa ujumla lakini kwa takwimu zinavyoonyesha katika sehemu mbalimbali nchini wawekezaji hawa wameamua kuijingiza katika masuala ya kisiasa ambapo shughuli za jamii zinazohitajika zitolewe na Kampuni zinageuzwa kuwa anayeota ni hiari yake wale siyo sera ya Serikali, kitendo hiki kinapigwa debe na mashabiki kisiasa ambacho wananchi wanalahaiwa na kuwaona wawekezaji hawa wanafaa kuliko wawakilishi wao. Je, Serikali natoa tamko gani kwa wawekezaji hawa wanaojingiza kwenye masuala ya siasa?

Tatu, malipo ya fidia wanayopewa wananchi haziendani na wakati kwa mfano wananchi wa maeneo ya Nyametagata, Nyamalembo, Katoma na Magema. Kuna wananchi waliolipwa kiasi cha shilingi 840 wenyewe hazifiki hata 50,000. Malipo ya sehemu za Nyamatagata hayaendani na watu wenyewe, kulikuwa na wananchi 110 lakini waliopata fidia ni 39 tu je, wengine itakuwaje na Serikali inawaambiaje wananchi hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Magema walisalia wakati wa Kijiji cha Mtakuja kilipovunjwa na wananchi wake kuhamishwa kupisha mgodi lakini Magena kilikuwa Kitongoji, je, Serikali inasemaje kuhusu wananchi hawa ambao wanaambuliwa kwa kukosa maji, barabara, mlipuko ya mara kwa mara inasababisha ugonjwa wa moyo, mimba zinaharibika hata wengine vifo na kupata ugonjwa wa kifua kikuu kwa baadhi ya wananchi kwa ajili ya mavumbi.

Je, Serikali inasemaje kuwahamisha wananchi hawa kwa kuwapa fidia yao ili waondokane na adha hii?

MHE. RICHARD M. NDASSA: Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono kwa asilimia mia mia hoja hii.

Mheshimiwa Niabu Spika, kuptia Wizara naomba kuipongeza *TANESCO* kwa kuanza kusimika nguzo za umeme kutoka Kisese hadi Mji wa Sumve, lakini pia kwa kwanza au kuonyesha nia ya kuweka nguzo kuanzia Mji wa Ngudu hadi Mji wa Malya. Najua inawekana *TANESCO* wanayo matatizo ya kifedha, lakini umuhimu ni kitu cha muhimu, si vizuri kwanza mradi halafu ukasimamia kwa zaidi ya mwaka huko ni kuzika hata kile kidogo ulichonacho.

Hivi suala la umeme Sumve na Malya imekuwa nditi? Naulizwa hivi sasa imekuwa hoja ya wapinzani kuwa hiyo ilikuwa danganya toto. Siyo vibaya nikapata majibu ya kuridhisha kabla sijakukoromea kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini.

Naiomba Serikali iliombi *TANESCO* na kwa sababu Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, alipotembelea Mji wa Sumve aliwaahidi wananchi kuwa umeme katika mji wenu utawaka mwezi Aprili, leo ni mwezi Julai na tunaelekea Uchaguzi Mkuu, kazi hiyo waimalizie pamoja na ukwasi walionao kwani eneo la Sumve umeme unahitajika si kwa kisiasa bali ni kwa kibiashara hata Katibu Mkuu ndugu Patrick Rutabanzibwa, anafahamu kwani ameshafika pahali hapo. Sambamba na hilo Mji wa Malya ni Mji mkongwe na unahitaji huduma ya umeme basi Shirika la Umeme lisiishie tu kuweka nguzo chini, limalizie kazi ili kuondokana na maswali ya mara kwa mara ya Sumve na Mji wa Malya. Tunaipongeza sana *TANESCO* kwa kazi nzuri inayofanya pamoja na kwamba mahitaji ni mengi lakini uwezo haufanani na maombi hii ni kutokana na fedha kutotosheleza kwa mara moja kukamilisha miradi yote, lakini bado naleta ombi kwenu kuwa mradi wa Sumve na Malya vipewe kipaumbele. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia moja.

MHE. TATU M. NTIMIZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Wizara kwa kazi nzuri katika sekta zote zinazoongozwa na Wizara hii. Nitashukuru kama maandalizi ya upelekaji umeme katika Jimbo la Igalula utaanza wakati wa utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ndani ya kipindi hiki.

Miji midogo ya biashara inakua kwa haraka hasa Kijiji cha Kigwe ambako barabara kuu ya Dodoma - Manyoni - Itigi - Tabora inapita. Kijiji cha Igalula ndiyo Makao Makuu ya Jimbo penye Shule ya Sekondari ya Mchakana, Kituo cha Reli na Kituo cha Polisi. Maeneo ya aina hii umeme ni muhimu. Kijiji cha Goneko chenye wakazi wengi wafanyabiaishara, kituo cha reli na nyumba nyingi. Kijiji cha Muswaki kiko Kanda ya Kaskazini mwa Jimbo na kwenye mpaka wa Wilaya ya Igunga ni wakulima wakubwa na zao la mpunga na zao ambalo linalisha maeneo mengi ya nchi hadi Pemba na Unguja. Kina wakazi wengi na majengo mengi ya kudumu. Umeme katika eneo hili halitakuwa na mjadala kwani uwezo wa wananchi wanaona pia mradi wa umwagiliaji unashughulikiwa kwa kuendelea ukuzaji wa ukulima na mpunga.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitashukuru kupata jibu la matumaini na wananchi na maeneo hayo wasikie ili waanze kuijandaa. Katika miaka ya 1989 hadi 2001 wawekezaji walifika katika Kijiji cha Loya na Ture katika utafiti wa madini, ingawa wananchi hawa hushirikiana sana wataalam/wawekezaji hao walichimba udongo huo na kubeba kwenye magari kupeleka Dar es Salaam kwa utafiti zaidi. Inasemekana Kijiji cha Ture, kuna uwezekana na kuchimba dhahabu na almasi. Kijiji cha Loya, kunaonekana madini ya dhahabu na almasi na ya aina nyingine. Sasa ni kipi kinaendelea kwani wananchi walipoona kimya hasa huko Kijiji cha Loya wao wameanza kuchimba na kutoa wanachokitoa bila utaratibu.

Naomba Serikali ieleze ili wananchi wasikie na wajipange. Pamoja na yote ya kungojea jibu, naunga mkono hoja na Bajeti hi ipite ili itekeleze hayo.

MHE. OMAR MJAKA ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naitumia fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Kamishina wa Madini, maafisa, watendaji na wafanyakazi wote wa Wizara kubwa, nzito na muhimu kwa uchumi na maendeleo ya nchi yetu hii ya Tanzania, kwa uongozi wao mzuri, wenyе bidii, hekima, uvumilivu na usimamizi ulio makini sana kwa Wizara zao pamoja na kuwasilisha Bajeti yao hii nzuri, iliyo wazi na yenye kuleta matumaini makubwa ya maendeleo ya kiuchumi katika nchi yetu hii ya Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kuwapongeza sana viongozi hawa Wakuu wa Wizara hii na naunga mkono Bajeti hii asilimia mia moja.

Katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri, inatueleza kuwa sera ya nishati inaelekeza kupeleka kwanza umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya, Miji Midogo na kwenye vituo vya kuzalisha mali. Kwa kweli naipongeza sana Wizara hii kwa kuwa na sera hii ya msingi kwa maendeleo ya Taifa letu. Naiomba sana Wizara hii na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kusimamia vizuri sera hii ili iweze kufanikisha malengo yote yaliyokusudiwa katika sera hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba hii tunaelezwa kuwa mauzo ya madini kutoka Tanzania yamekuwa hadi kufikia asilimia 52.1 ya mauzo ya nje kwa mwaka 2004. Naipongeza sana Wizara na Serikali yetu kwa ongezeko hili lakini pia tunasikia kuwa pamoja na ongezeko la mauzo haya ya madini Serikali yetu haifaidiki na ongezeko hili. Ni sababu gani zinazosababisha hali hiyo ya Serikali yetu kutokufaidika na ongezeko hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tunasikia kuwa Madini ya *Tanzanite* yanapatikana na kuchimbwa Tanzania tu lakini kuna baadhi ya nchi zinajitangaza kuwa wanazalisha madini hayo, je, sababu kubwa ni nini? Je, Serikali yetu inasemaje juu ya suala hili? Je, ni hatua gani zitachukuliwa na Serikali yetu juu ya suala hili ili kuieleza dunia kuwa *Tanzanite* ni ya Tanzania?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaelezwa katika Bajeti hii kuwa mpango wa Bajeti kwa mwaka 2005/2006 unalenga kutekeleza malengo yaliyoanishwa kwenye Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA). Ni jambo la faraja sana kuwepo kwa mpango huu katika Bajeti hii na kwa kweli nawatachia mafanikio mazuri ili uweze kufanikiwa kama ulivyopangwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile mpango huu unalenga pia kuiweza nchi yetu kufikia katika maendeleo leo makubwa kuanzia sasa hadi mwaka 2020. Tunaelezwa kuwa Kampuni ya *Artumas* ulifufua (*re-enter*) kisima cha gesi cha *Mnazi Bay* na kufanya majaribio ya uzalishaji. Matokeo ya majaribio hayo yameonyesha kuwa kisima hicho kina uwezo wa kuzalisha gesi kwa kiasi cha futi za ujazo zaidi ya milioni.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana hatua hii tulioifiki nchi yetu kwa kuwa mmoja wa wazalishaji wa gesi hapa duniani. Kutokana na mafanikio haya makubwa ya kimaendeleo, naiomba Serikali yetu kupitia Wizara yake hii ya Nishati na Madini kuongeza juhudhi zitakazowezesha kapatikana kwa gesi zaidi na mafuta katika nchi yetu ambayo inasemekana kuwa vitu hivi viwili yaani gesi asilia na mafuta tunayo mengi sana hapa nchini petu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutaka kulifanikisha suala hili kwa maendeleo ya Taifa letu hatuna budi kuondoa tofauti na kasoro za aina yoyote zilizojitokeza kama zipo. Sheria zilizopo kuhusu suala la mafuta katika nchi yetu ya Tanzania ni lazima zifuatwe ili kuleta maendeleo ya kweli ya nchi yetu. Mafuta ni chanzo kikuu cha uchumi mkubwa kwa nchi yoyote ile hapa duniani. Kwa hivyo, tuondoe tofauti zetu haraka iwezekanavyo ili tuweze kutafuta mafuta na gesi asilia katika maeneo yetu yote ya Jamhuri yetu ya Muungano wa Tanzania. Siyo vizuri tukafanye makosa a kichelewesha nishati hii kama tunayo kama ilivyofanyika kwa gesi ya *Mnazi Bay* ambayo tunasikia kuwa iligunduliwa mnamo miaka ya 1980 lakini uzalishaji wake umefanyika mnamo mwaka ya 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusifanye mzaha kwa suala la uchumi na maendeleo ya Taifa letu na kwa wananchi kwa ujumla. Naomba sana suala hili lishughulikiwe ipasavyo na kwa mujibu wa sheria na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kama zilivyotungwa na kuwekwa hapa mwanzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naipongeza sana Bajeti kwa kuona kuwa ndani ya Bajeti hii yameelezwu malengo ya kuwawezesha wachimbaji wadogo kuzalisha kwa tija zaidi na kwa kuzingatia kanuni za usalama. Katika ukurasa wa 32 katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini inelezea juu ya ushirikiano wa Kimataifa. Nikinukuu sehemu hii inasema kuwa: "Katika mwaka 2004/2005 sekta ya nishati na madini zilinufaika na misaada ya wafadhili mbalimbali."

Naipongeza Wizara yetu hii kwa kuwa na ushirikiano mzuri na wafadhili mbalimbali na pia nawapongeza sana wafadhili hawa kwa kuwa na ushirikiano mzuri sana na Wizara yetu hii pamoja na Serikali yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli nalazimika pia nitoe pongezi zangu za dhati kwa Wizara hii ya Nishati na Madini ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali yetu ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na Serikali ya Norway na Shirika lake la misaada la *NORAD* kwa kusaidia mradi wa kusambaza umeme katika Vijiji 62 vya Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile tunapongeza msada wa kufanyiwa matengenezo kwa mashine za umeme Kisiwani Pemba. Vile vile naitumia fursa hii kuipongeza Serikali ya Norway na shirika lake la misaada la *NORAD* baada ya kusikia kuwa wataalam kutoka Norway kuwasili Zanzibar kwa ajili ya kufanya utafiti wa kutoa umeme kutoka Tanga kwenda Pemba kupitia chini ya bahari. Hii ni taarifa ninayoinukuu kutoka taarifa ya habari ya tarehe 16 Mei, 2005 na kipindi cha habari za magazetini leo

cha *Radio Tanzania* cha tarehe 17 Mei, 2005 asubuhi kwa kweli mlifarijika sana na taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, naziomba Serikali zetu mbili ya Muungano na ya Zanzibar kulisimamia na kulifanikisha suala hili kwa maendeleo ya Pemba na Tanzania kwa ujumla na naunga mkono asilimia mia moja.

MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutamka naiunga mkono hoja ya Wizara hii. Pamoja na kuunga mkono nahitaji Wizara ya Nishati na Madini, inieleze kwa nini sasa inakaribia takribani miaka minne bado haijatekeleza maombi iliyopewa Mheshimiwa Rais Benjamin William Mkapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipotembelea Jimbo la Kilosa katika Kata ya Berega pamoja na kazi alizozifanya katika Kata hii aliombwa akubali kuongeza dawa hospitali ya Berega inayoendeshwa na Kanisa la Anglikana na kupatia hospitali hii umeme. Hospitali hii inahudumia Mikoa minne ambayo ni Mikoa wa Manyara, Tanga, Dodoma na Morogoro. Hospitali hii ina kiwanja cha ndege kuwezesha *flying doctors* kutoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia aliombwa kupeleka umeme, katika maombi hayo Mheshimiwa Rais alitoa ahadi ya kuiongeza dawa hospitali hii. Ahadi hiyo ameitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umeme alisema angepeleka maombi hayo kwa Wizara ya Nishati na Madini. Kufuatia maombi hayo Wizara ya Nishati na Madini ilimtaka Meneja wa *TANESCO* wa Mkoa wa Morogoro kufanya tathmini kama mradi huo ungelipa kutokea Dumila, Maguha, Magubike na Berega. Meneja wa *TANESCO* wa Mkoa wa Morogoro tathmini yake ilionyesha gharama ilikuwa 600,000,000/= na alitamka mradi huo unalipa. Sasa imepita karibu miaka minne bado maombi iliyopewa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hayajatekelezwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kupata maeleo kwa nini Wizara imeshindwa kutekeleza maombi iliyopewa Mheshimiwa Rais na imekaa kimya bila kutoa taarifa ingawa mimi nikiwa Mbunge wa Jimbo la Kilosa mara kwa mara nimefuatilia hoja ya suala hili kwa Waziri pamoja na Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Berega ndiyo hospitali kubwa peke yake kwa njia ya kutoa Morogoro hadi Dodoma. Hivyo ombi la kupatiwe umeme hospitali hii ambayo pia ina kiwanja cha ndege si jambo la anasa. Bali ni jambo muhimu sana katika maendeleo ya Taifa letu. Hoja ya uhaba wa fedha kwa uzito wa maeleo ya hoja hii haina msingi kwa sababu umeme huo hautotokwa bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ziara yake hivyo Mheshimiwa Rais, alitoa ahadi ya kujenga *library* na kutoa magodoro mia mbili kwa Sekondari ya Mgugu. Nafurahi kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa ahadi zote hizo alizozitoa Mheshimiwa Rais ameteketeleza. Kilichobaki ni umeme tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hoja hii Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Naibu Waziri wa Nishati na Madini na yeze alifanya ziara kwa sehemu zote alizopita Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, alikiri kwa kukubali mradi huo wa umeme unalipa (*the project is viable*). Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, alitoa ahadi ya kupeleka dawa katika Kituo cha Afya cha Magole kilichopo Magubike na ahadi hiyo alitekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla ya kuunga mkono hoja hii ni vizuri Wizara ya Nishati na Madini, itoe maelezo ya wao kushindwa hata baada ya *studies* zote zilizofanywa.

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Waziri wa Nishati na Madini na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Katibu Mkuu na watendaji wote kwa kazi nzuri ya kuendesha Wizara pamoja na kuandaa hotuba nzuri ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizi muhimu napenda tu leo kuchangia hoja ya nishati ya umeme na hasa kwa umeme Vijijini kwa Jimbo la Busega.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Mheshimiwa Waziri atoe kipaumbele kwa utekelezaji wa mradi wa umeme wa kutoka Lamadi na Nyashimo kama ifuatavyo: umeme kutoka Lamadi - Kalemera - Nyamikoma hadi Nyashimo, umeme kutoka Lamadi - Mkula Hospitali hadi Malili na Ngasamo, umeme kutoka Nyashimo - Shigala - Nyangili na umeme kutoka Nasse - Mwanangi hadi *Ginery* ya *Alliance*.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi hii ni muhimu sana kwani ikikamilika itasaidia kupatikana umeme wa nishati kwa ajili ya vinu vya kuchambulia pamba ya Ngasamo na *Alliance*. Pia hospitali kubwa ya Mkula pamoja na huduma kwa wateja wengi wao wakiwa wafanyabiashara

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imejitahidi kuanzisha mradi huu hapo sasa yapata miaka miwili mradi umesimama licha ya ahadi ya Serikali ya kuutekeleza mradi huu muhimu kwa mwaka huu wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuititia bajeti hii Mheshimiwa Waziri atoe tamko juu ya utekelezaji wa mradi huu muhimu kwa jamii, maendeleo na uchumi wa nchi. Naunga mkono hoja.

MHE. PROF. MARK J. MWANDOSYA: Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kuchangia kwa kuunga mkono hoja ya Waziri wa Nishati na Madini, kwa asilimia mia moja . Nawapongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Daniel Yona, Waziri wa Nishati na Madini na Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Naibu Waziri wa Nishati na Madini. Wamekuwa mstari wa mbele katika kuelezea, kufafanua na kusikiliza kero, mapungufu, mafanikio na mwelekeo wa sekta hizi mbili muhimu katika maendeleo ya uchumi wa nchi na maendeleo ya jamii. Si kazi rahisi kwani kama wawakilishi tungependa katika kila Tarafa, kila Kata, kila Kijiji na kila Kaya katika majimbo yetu, umeme upatikane. Hii

ndiyo dhamira ya Taifa ambayo hakika tutafanikiwa kufikia iwapo tutatimiza malengo yaliyo katika Dira ya Taifa 2025.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za Mawaziri zinarahisishwa na kazi nzuri za watendaji, hivyo basi nawapongeza watendaji wote wa sekta za Nishati na Madini, wakiongozwa na Katibu Mkuu, Ndugu Patrick Rutabanzibwa. Nilipata bahati ya kufanya naye kazi na wengi wao, nilipokuwa Kamishna wa Nishati na Petroli na baadaye Katibu Mkuu wa iliyokuwa Wizara ya Maji, Nishati na Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu leo utajikita katika masuala miwili, moja la kijimbo na moja la Kitaifa. Naanza na suala la umeme na maendeleo yake Wilaya ya Rungwe na hasa maeneo ya Rungwe Mashariki. Kwa niaba ya wananchi wa rungwe Mashariki naishukuru *TANESCO* kwa ushirikiano mkubwa waliowapa wananchi na mimi katika kuendeleza umeme Rungwe Mashariki.

Hata hivyo, kuna maeneo machache ambayo tayari yako katika mipango ya *TANESCO* lakini imechukua muda mrefu kuitekeleza. Dalili za utekelezaji zipo kwani katika maeneo nitakayoyataja nguzo zimesimikwa na katika maeneo mengine hata nyaya zimeletwa ama zimefungwa au zipo zipo tu. Hii imechukua miaka zaidi ya mitatu. Inaleta vishawishi vya hujuma kama vile wizi wa nyaya. Maeneo haya ni Ntaba mpaka Ipinda - Njia hii ni kiungo mbadala cha umeme kati ya Wilaya ya Rungwe na Kyela. Nguzo ziliwekwa miaka mitatu iliyopita na nusu ya urefu wa lami hiyo ya KV33 imewekwa nyaya kila tunapouliza mara nyaya hazitoshi. Zikipatikana gari bovu, zikipatikana fedha za kuwalipa mafundi hakuna, ili mradi maelezo ni mzunguko. Tunaomba *TANESCO* ikamilishe ujenzi wa laini hii, Kandete - Luteba, tayari nguzo zipo na wananchi walihusika kutoa nguvukazi katika kusimika nguzo hizo. Tunaomba *TANESCO* wakamilishe ujenzi wa mradi huu wa muda mrefu, Kandete - Mpombo, nguzo zilisimikwa miaka minne iliyopita, Isange - Mbigili, nguzo zilisimikwa miaka minne iliyopita. Hapa kuna mteja wa kudumu, *Mobitel* wana mnara Mbigili. *TANESCO* wangefanya haraka kupeleka umeme Mbigili ili kumpata mteja huyu, mbali na wananchi na taasisi nyingine na Kandete- Matamba, napo hapa nguzo tayari zimesimikwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la Kitaifa ni lile la jengo la *Mafuta House*. Usanifu wa jengo hilo utililia maanani mahitaji mahsusisi ya *TPDC* kuhusu utunzaji wa kumbukumbu na sampuli za uchimbaji na utafutaji wa petroli na gesi nchini. Sampuli hizi zinatuzwa Norway na maeneo mengine duniani.

Si jambo zuri na wafadhili wanafanya hivyo kwa hisani tu. Ndiyo walitushauri kama nchi tuwe na mahali kama hapo. Hili ni suala la msingi sana. Sitaingilia uhalali wa maamuzi yaliyopelekea *TPDC* na *NHC* kuyanyang'anywa uwekezaji walioufanya. Ingekuwa vema kama fedha walizotumia zingekuwa ni sehemu za uwekezaji wao wa pamoja na *NSSF*. Tunaamini Wizara italitafakari suala hili ili lisiletu utata au kuleta hisia potofu hasa kutokana na kazi kubwa na nzuri ambayo inafanya na *TPDC* na Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kurudia tena kuunga mkono hoja ya Waziri wa Nishati na Madini.

MHE. FATMA SAID ALI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Waziri, Mheshimiwa Daniel Yona, Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, pamoja na Katibu Mkuu Bwana Patrick Rutabanzibwa. Naunga mkono hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *TANESCO*, nashukuru juhudi za *TANESCO* za kuwaunganishia umeme wateja na kuandaa mipango na mikakati ya kuendeleza *TANESCO* na wazalendo mkataba ukiisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalı langu ni kwa nini bado umeme wa *TANESCO* ghali? Mbona gesi ipo nyigi hadi inataka kusafirisha umeme gesi Kenya?

Mheshimiwa Naibu Spika, ombi langu ni bei ya umeme ipunguzwe ili wananchi wengi waweze kuutumia na wafaidi maliasilia yao ya gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ufuatilaji wa mafuta. Naipongeza *TPDC* kwa kazi yake nzuri ya utafiti ya ufuatilaji wa mafuta Zanzibar bado hajaeleweka kwa nini Zanzibar wakatalie makampuni hayo ilhali tunataka kuondoa umaskini? Naomba Serikali ilieleweshe waziwazi tatizo lipo wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, tuunde Tume ya kuchunguza suala hilo. Mimi najitolea kufanya kazi hiyo ili tusaidie Wazanzibari kukwamuka na tatizo la umaskini. Naamini litaweza kutapa *solution*.

Mheshimiwa Naibu Spika, dalili za kupatikana mafuta baharini, naomba *TPDC* ipewe uwezo mkubwa ili wafanye utafiti kupatia visima vingi na kutafuta wawekezaji haraka bahari imetuzunguka Visiwani Zanzibar. Je, lini na sisi tutavuna mafuta kwenye bahari hiyo?

MHE. ATHUMANI S. M. JANGUO: Mheshimiwa Naibu Spika, naanza kwa kumpongeza Waziri, Naibu Waziri wake Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Katibu Mkuu na wasaidizi wao kwa hotuba nzuri yenye matumaini kwa Watanzania. Lakini nawapa pole kwani bado matatizo yapo mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa makusudio miwili ya kuzalisha umeme vijijini na kwenye vituo vya kuzalishia mali na viwanda vijijini. Katika hili, napenda kuwakumbusha kuwa katika Mkoaa wa Pwani umeme unahitajika sana vijijini ili kuendesha viwanda vidogo vidogo vya kubangua korosho na kusagisha matunda ambayo yanaaoza hovyo.

Pili azma ya kufikisha umeme vijijini ili kupunguza matumizi ya kuni na mkaa ili kulinda misitu na mazingira ni nzuri. Nashauri kuwa kipaumbele kiwe kwenye misitu inayozunguka miji mikubwa kama ilivyo misitu ya Kisarawe na Jiji la Dar es Salaam ambako matumizi ya kuni na mkaa sana yanakaribisha majangwa kwenye maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mategemeo yangu kwamba kwenye kuvipatia umeme vijiji vilivyoko kwenye maeneo linakopita bomba la gesi ya Songosongo, umeme

huo utafikishwa hata kwenye vijiji vya jirani ili azma hii ya kuzuia majangwa ifanikishwe. Naipongeza Wizara na *TANESCO* kwa umuhimu uliowekwa kwenye maeneo yanayotajwa katika Ibara ya 21 ya hotuba ya Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wananchi hawaelewi kwa nini matatizo ya kukatika katika umeme na gharama kuwa kwa watumiaji bado ziko juu.

Katika ibara ya 22 ya hotuba tunaelezwa mafanikio ya ongezeko la ukusanyaji maduhuli kutoka shilingi 11 bilioni kwa mwezi mwaka 2001 hadi bilioni 21 mwezi Machi 2005. Hongera! Lakini mafanikio haya hayamfikii mtumiaji wa umeme kwa kupunguziwa bei. Isitoshe mwananchi analazimika kununu kila kitokacho viwandani kwa bei ya juu kwa sababu ya gharama kubwa za umeme. Vipi?

Kuhusu taarifa muhimu zilizotolewa kwa wawekezaji kwenye mkutano wa Johannesburg, Afrika ya Kusini, nashauri kuwa ili twende na wakati na tuweze kuwfikia watu wengi zaidi, taarifa zetu kama hizo sasa yafaa pia zipite kwenye tovuti. Kuhusu mradi wa *IPTL*, ni bahati mbaya kuwa nchi yetu imegharimia mradi huu kwa bei ya juu sana, hasa baada ya kulazimika kuwafidia wawekezaji wa mamilioni baada ya amri ya mahakama. Kwa kuwa sasa yapo matumaini ya mitambo ya *IPTL* kutumia gesi ya Songo Songo na kupunguza gharama ya ununuzi wa mafuta kwa kiwango cha karibu nusu, ni mategemo yangu na ya wananchi wengine kuwa hili likifanyika, gharama za umeme kwa mtumiaji zitashuka kidogo. Pamoja na maoni yangu haya naunga mkono hoja na nawatakia kila la kheri. Ahsante sana.

MHE. CYNTHIA HILDA NGOYE: Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri.

Mheshimiw Naibu Spika, kwanza ni kuhusu madini. Tanzania imejaaliwa kuwa na madini mengi ya aina mbalimbali. Kama madini yanepewa kipaumbele katika uwekezaji, nchi ingepata uchumi wa kutosha. Maeneo mengi hayajafanyiwa utafiti bado. Nashauri Serikali iendelee kuwasukuma watafiti kufanya utafiti katika Milima ya Livingstone kando kando ya Ziwa Nyasa. Inaaminika maeneo yale ni maeneo yenye utajiri mkubwa. Idara ya utafiti itangaze maeneo yaliyofanyiwa utafiti na kuwashawishi wawekezaji kuyachimba maeneo haya.

Pili ni kuhusu umeme. Watu wenye uwezo, wapewe msaada wa Serikali kuwekeza katika maporomoko ya maji tuliyonayo hapa nchini kwa mfano Kiwira, Wilayani Rungwe, Kikuletwa Wilayani Hai na kadhalika. Hii itatusaidia kupata umeme zaidi na kuongeza nguvu ya umeme wa Gridi. Wapo watu walioonyesha nia ya kufanya kazi hiyo lakini wanahitaji msukumo wa Serikali.

Naomba Serikali katika mpango wake wa mwaka 2006/2007 ijitahidi kuipatia Wilaya ya Ludewa ambayo ni Wilaya kongwe ipatiwe umeme, walau hata vijiji vyake vibrate umeme ambao wanausikia tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maeleo hayo machache naunga mkono hoja hii asilimia mia moja.

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri haikuueleza mradi wa nishati ya umeme wa *ERT*. Wakati wa *ku-wind up* naomba afafanue na kueleza nafasi ya mradi wa Kongwa/Narco hadi Mkoka ambaa tumeomba kila mwaka bila mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wa Pandambili wameomba *TANESCO* kuvutiwa umeme hadi katika kisima chao cha maji. Wanadaiwa 12 milioni, umbali wa *150 metres only*. Huduma ya maji ni muhimu kwa uhai wa watu na mifugo yao. Tunaomba huruma ya Serikali kupunguza madai hayo na *TANESCO* wakubali kulipwa *monthly*, ili mradi kwa sasa huduma hiyo ipelekwe katika chanzo hicho cha maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kumtaka mteja kulipia nguzo, vikombe, posho za vibarua, waya na kadhalika ili kuvutiwa umeme si mzuri ikizingatiwa kuwa mtu anazinunua bila ya huruma halafu vitu vyote hivyo vinabaki kuwa mali ya *TANESCO*, *is it fair?* Tunaomba majibu wakati wa *winding up*.

Mheshimiwa Naibu Spika, mikataba yote ijayo ya madini, Serikali yetu *i-insist* katika *equity participation and board representation* kama ilivyo kwa Botswana. Kwa miradi mikubwa *Government participation* iwe katika *range* ya 15 hadi 25% *issued free of cost*. *Management* inaweza kuachwa kwa *private sector*.

Mheshimiwa Naibu Spika, sheria ya madini irekebishwe na mikataba ya awali ifumuliwe yote. Nashauri Serikali ikusanye *royalties to Government as percentages of gross market value in the following order, Precious Stone 15%, Precious metals 6.5% na other minerals and mineral products 5%*. *Government shareholding* iwe ni 20% *for all minerals including Gold issued free of cost*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi zote *Direct and Indirect* ziangaliwe upya, *export taxes, fees na dividends and royalties*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *mineral revenues* ziwe na *1:1 function* katika maendeleo ya Watanzania kwa kuboresha huduma muhimu za barabara, maji, elimu, afya, *reduced mortality*, mishahara bora, *a stable Tanzania shillings, exchange rate* na kadhalika hiyo ndiyo changamoto yetu sote hasa ninyi wenzetu mliopo Wizarani kwa niaba yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *it can be done...*

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. PAUL P. KIMITI: Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kwanza nimshukuru Mheshimiwa Daniel Yona, Naibu wake Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, Katibu Mkuu Ndugu Patrick Rutabanzibwa, Makamishna, Wakurugenzi na watumishi wote kwa kazi ya nzuri ya kusimamia Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2000 kwa hali ya juu. Naunga mkono hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo mengi ambayo ni vizuri yakawekwa wazi katika sera zetu. Haya ni pamoja ya mgao na mrabaha kwa maeneo yenyne madini; mrabaha kwa maeneo yenyne mafuta na kadhalika. Hivi Serikali kwa kuendeleza mtizamo huo, itafikia hatua ya kila Wilaya yenyne utajiri wa asili, iamue mgao mkubwa wa raslimali na wasiokuwa nacho, waendelee kuwa omba omba kwa wengine. Nchi hii tuangalie tusije tukaanza kuimega vipande vipande. Tumeanza kusikia kilio cha wenzetu wa Zanzibar kuhusu mafuta na Kusini kuhusu gesi. Sera yetu iwe wazi juu ya hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri sasa Serikali ikalimaliza tatizo la *IPTL* na *TANESCO* ili kumaliza tatizo la gharama kubwa na mzigo amba *TANESCO* inabeba kila mwaka. Je, uamuzi wa Serikali wa kununua mtambo huo (*IPTL*) umeishia wapi? Kwa nini Serikali ya awamu hii, isiimalize kabisa hoja hii ili isiendelee na Serikali ya awamu ya nne? Tusingoje matatizo haya. *yaka-spil over to the next Government.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Sumbawanga Mjini, imebahatika kuwa na madini ya *Emerold*. Ningombwa Wizara itume wataalam ili wathibitishe kiasi kilichopo ili tuanze kuwatafuta wawekezaji wa nje wasadiane na wachimbaji wadogo wadogo kwa nia ya kuendeleza wananchi kiuchumi na kibiashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, mpaka sasa sheria ya kuunda wakala wa umeme vijijini katika utekelezaji wake imefikia wapi ili tuelzee kwenye majimbo yetu wakati wa kampeni. Pia ningeshukuru kama kuna jithada zipi za Serikali kuwapata wawekezaji azma hii nzuri kwa wananchi wetu na hasa vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni nini tatizo la umeme toka Zambia hadi Sumbawanga kukatika katika? Tungependa kama tatizo liko upande wa Zambia, basi Serikali iingilie kati haraka iwezekanavyo kwa sababu adha hii siyo vizuri ikaendelea na inaweza ikadhaniwa ni sabotage ya upande wa pili wa nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini kila mara kwenye migodi mikubwa, kumekuwa kila mara na migogoro kati ya wachimbaji wadogo na wakubwa. Je, maandalizi huwa hafifu au mipango ya kusimamia taratibu zake huwa haiendani na hali halisi ilivyo kwenye maeneo husika? Unaposikia ugomvi au hata kudhulumiana kati yao wachimbaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru Waziri na Serikali yote kwa kukubali ushauri wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*PAC*) kwa kuiweka *TANSORT* kuwa kitengo cha Wizara ili kudhibiti shughuli zinazoendeshwa na kitengo hicho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa ujenzi wa *Mafuta House* ulifanywa kwa pamoja kati ya *TPDC* na *NHC*, ni kwa misingi ipi jengo hilo limetolewa kwa *NSSF*? Hili tulilijadili kwenye *PAC* lakini maelezo hayakupatikana. Ni vizuri likatolewa maelezo angalau kwa ufupi kwa faida ya wananchi wote, maana tunajua kuwa *NSSF* ni ya wananchi pia, lakini walio wanachama wakati *TPDC* na *NHC* ni taasisi ya umma wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, narudia kumpongeza Waziri, Naibu na watusika wote na Wizara ya Nishati na Madini kwa jitihada za kuteleza Ilani ya Uchaguzi ya mwaka 2000.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja hii kwa nguvu zote.

MHE. DANHI B. MAKANGA: Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umeme wa Gridi, *Alliance Ginnery*. Hii *ginnery* iko Wilaya ya Bariadi, Wilaya ambayo inazalisha pamba nyingi kuliko Wilaya zote nchini. *Ginnery* hii ni kubwa na ya kisasa kabisa katika ukanda huu wa pamba. Kwa muda mrefu sasa *ginnery* hii imeendelea kutumia umeme wa *generator* ambao una gharama kubwa sana. Uongozi wa kiwanda umekubali kuchangia gharama za kupeleka umeme wa gridi hadi *ginnery*, lakini bado mipango ya *TANESCO* inasua sua.

Mheshimiwa Naibu Spika, uongozi wa kiwanda na mimi Mheshimiwa Mbunge tumewasiliana na Wizara mara kwa mara, lakini utekelezaji bado. Sasa ni lini mradi huu utakamilika? Kwa kuwa utafiti ulibainisha umeme uchukuliwe toka Magu, je, tunaweza kubadilisha umeme uchukuliwe toka Bariadi Mjini hadi *Alliance Ginnery* ili vijiji vya njiani navyo vipate faida hiyo kama vijiji vya Mbiti, Ngulyati, Nyanguge, Kilalo na kijiji cha Kasoli? Ni *ginneries* ngapi nyingine ambazo hazina umeme wa gridi na lini zitapatiwa?

MHE. PHILIP S. MARMO: Mheshimiwa Naibu Spika, nitajadili hotuba ya Wizara hii wakati wa kipindi cha maswali. Niliuliza kuhusu vigezo vya kusambaza umeme kwenye Miji Midogo pale inapowezekana, kwamba kuna dalili zote za upendeleo ambapo siyo jambo zuri. Yaonekana eneo hili ni *discretion* (ya nani?) kwa kisingizio kuwa kipaumbele kwa yale Makao Makuu ya Wilaya ambayo bado hayajapata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa vile kila Mji Mdogo ulio karibu na njia ya umeme una haki ya kupata umeme, nisingependa kutaja majina miji hiyo katika mchangano wangu leo. Lakini wananchi hujiuliza (hasa kwa miradi inayoendelea sasa huko Arusha na Manyara), Miradi ya Karatu - Endabash (40 km), Makuyuni - Mto wa Mbu, Katesh - Balangda, Magugu - Minjingu (60 km) Dareda Bashnet (30 km) na kadhalika. Mradi huu ni mkopo, lakini kwa shughuli za uchumi huduma za jamii na kadhalika. Ukubwa wa mji wa Dongobesh ni zaidi ya Endabash, Makuyuni na Bashnet ikiwekwa pamoja. Lakini maombi yetu ya umeme Dongobesh (Kutoka Mbulu km 40) au toka Bashnet (km 20) hayakabaliki. Hii maana yake ni nini?

MHE. DR. WILLBROD P. SLAA: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Waziri na timu yake kwa kazi wanayofanya. Hata hivyo, pamoja na pongezi hizo naomba kuchangia maeneo yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza katika Wilaya ya Karatu kuna machimbo ya madini katika maeneo ya msitu wa Marang' na eneo la Mang'ola Barazani katika Tarafa ya Eyasi. Je, Wizara inaweza kueleza Bunge hili ni madini ya aina gani yanachimbwa katika maeneo hayo kwani kimsingi leseni (*Prospecting License*) inatolewa na Wizara na

Wilaya haifahamu ni kitu gani kinafanyika na wahusika wakiulizwa wanakuwa wakali na kusema wamepewa leseni na mamlaka husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi huu, je, tuna uhakika gani kuwa raslimali ya nchi yetu inatuletea kweli manufaa kama hatu uongozi wa Wilaya haifahamu ni madini ya aina gani katika eneo lao yanachimbwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Tarafa ya Eyasi katika Wilaya ya Karatu inatoa umeme kwa njia ya *windmills* kutokana na upopo mwangi ulioko katika eneo hilo. Je, Serikali inafahamu kuwepo kwa uwezekano huo wa kutengeneza umeme kutokana na upopo? Kama haina, je, iko tayari kufanya upembuzi wa kina na hasa kwenda kujifunza kwa Mapadri wa Kanisa la Katoliki (*Spanish*) ambao wametengeneza umeme wa upopo ambao unatumika katika kuendesha huduma zote katika eneo zima la Parokia hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua kuwa *TANESCO* kwa ratiba yake itachukua muda mrefu hadi kufikia vijijini, mathalani Tarafa ya Eyasi katika Wilaya ya Karatu. Umeme huo wa upopo siyo tu utakuwa mkombozi wa maeneo kama hayo, lakini pia utaongeza nguvu na uwezo wa umeme katika gridi ya Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Naibu Spika, nampongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu pamoja na watumishi wa Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mchango wangu nataka kueleza masikitiko yangu kwa Wizara hii kwa kutotekeleza ahadi yake iliyotoa Bungeni tarehe 6 Agosti, 2003 kutokana na hoja yangu binafsi niliyotoa kuonyesha kutoridhika na mwenendo wa utekelezaji wa Wizara ya Nishati na Madini wa kutopeleka umeme vijiji vya Mwema, Chikundi, Chigugu, Chikukwe, Namakongwa na Malambo. Mradi huu haujatekelezwa kwa muda wa miaka 15!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi Waziri alijibu kwamba: "Mheshimiwa Spika, nafurahi kumwarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa miradi hii itakayogharimu shilingi milioni 85 itatekelezwa kipindi cha mwaka 2003/2004. Sehemu ya Ndanda - Nangoo - Nanganga itatengewa shilingi milioni 660. Fedha hii inatarajiwa kupangwa kwenye bajeti ya Serikali mwaka 2004/2005 na kuendelea hadi 2005/2006. (*Makofi*)"

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo zimetolewa *transfoma* tu katika maeneo ya vijiji nilivyotaja na hakuna kazi nyingine yoyote iliyofanyika!

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji hafifu namna hii unaleta aibu kwa Waziri mwenyewe na Wizara yake. Kwa nini anaahidi Bungeni kwa niaba ya Serikali halafu watumishi wake hawatekelezi na yeze mwenyewe hafuatilii? Wananchi hawa wasubiri miaka 15 mingine ili mradi huu ukamilike? Kwa nini Waziri atoe kauli Bungeni na watekelezaji wake (watumishi) wasitekeleze? Hii ni dharau kwa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba nafasi wakati wa Kamati ya Bunge Zima ili Serikali ieleze kwa nini hawataki kutekeleza mradi huu na kwa nini Serikali haiwatendei haki watu wa Kusini. Aidha, sitaunga hoja mkono npaka yawepo maelezo ya kuridhisha kutokana na aibu hii ya utekelezaji.

MHE. KILONTSI M. M. MPOROGOMYI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze Waziri wa Nishati na Madini, Mheshimiwa Daniel Yona, Naibu wake, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha na Katibu Mkuu, Ndugu Patrick Rutabanzibwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawapongeza sana kwa kuleta bajeti hii na kwa mambo mengi ambayo yamefanywa chini ya Wizara hii. Naunga hoja mkono.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ni kama ifuatavyo: -

Kwanza, Mheshimiwa Rais Benjamin Mkapa alipotembelea tarehe 7 na 8 Agosti , 1997 alisaini *a joint communiqué* na Rais Yoweri Museveni. Katika mambo waliyokubaliana ni pamoja na kuunga mkono Bomba la Mafuta ya Petroli toka Dar es Salaam - Mwanza mpaka Kampala, Uganda. Katika hili walikubaliana kuwahamasisha wawekezaji wa nchi hizi mbili (*Ugandan and Tanzania Entrepreneurs*) wawekeze katika mradi huu. Bahati mbaya *Africommerce International Limited* ambao wamekuwa wakiendeleza mradi huu wameondolewa wakati ambapo ndipo wamepata mwekezaji/wawekezaji na kumchukua mtu ambaye shughuli hiyo hajui sawa sawa na lazima aanze moja kushughulikia mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa nini Waziri hakubali kurejesha mradi huu kwa wazalendo wa *Africommerce* ambao tayari wana mwekezaji ili kujenga *confidence* ya Watanzania kwamba Serikali yao inajali maendeleo ya raia wake kwa kuwapa nafasi kuendesha miradi mikubwa kama hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, kutochukua mwekezaji aliyepatikana inapunguza imani kwa Serikali yake kwa jinsi ambayo Wizara haitaki kutoa uamuzi kuhusu jambo hilo. Naomba maelezo kwa nini tuendelee kumkumbatia mtu ambaye ni *nonentity* katika biashara hiyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, jengo la *TPDC* la *Mafuta House* limegaiwa kwa *NSSF* bila utaratibu unaoeleweka sawa sawa. *TPDC* na *NHC* tayari walikuwa wamewekeza kiasi cha fedha kinachozidi shilingi bilioni 15. Kwa nini Serikali haikuwaruhusu *TPDC* na *NHC* wawe na hisa katika jengo hilo au wawalipe fedha zao walizowekeza katika jengo hilo? Naomba maelezo sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tumewaruhusu wachimbaji wa gesi ya Songo Songo na *Mnazi Bay* bila mpango wowote kwa kuwashirikisha Watanzania hususan Shirika letu la *TPDC* kwa utaratibu wa *production sharing?* *Allow TPDC participation* kwa niaba ya Watanzania na hii itakuwa *beneficial* kwa Taifa hili.

Nne, wakati *Songas* walipoanza, Serikali ilitoa shilingi bilioni 50 zilizowekwa kwenye *ESCROW Account City Bank*. Je, wale walipouza fedha hizo walichukua na kama hawakuchukua ziko wapi na zimetumikaje?

MHE. STEPHEN M. KAZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia hoja ya Wizara ya Nishati na Madini kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu nimpungeze sana Waziri wa Nishati na Madini kwa hotuba nzuri na ya kimapinduzi, Naibu Waziri wa Nishati na Madini kwa ushirikiano wake, Katibu Mkuu wa Wizara, Makamishna wote wafanyakazi wote ndani ya Wizara kwa ushirikiano wao na kuhakikisha kwamba hotuba hii inakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mambo mawili ambayo ningependa nipate majibu.

Kwanza, kumekuwa na kilio cha kwamba Makampuni ya Migodi ya Madini kwanza yajiorodheshe kwenye chombo cha *Stock Exchange* cha Dar es Salaam (*DSE*) ili wao pia wauzie hisa Watanzania katika Kampuni kama vile *Tanga Cement, Twiga Cement, Tanzania Cigarette Company* na nyingine nyingi zinazofanya hivyo. Kwa hiyo, Kampuni ya Madini zinapohitaji mtaji basi wapate pesa hizo kwa kuuza hisa kwa Watanzania kupitia *DSE*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kwa utaratibu wa kusambaza umeme namwomba Waziri wa Nishati na Madini awasiliane na ofisi ya *TANESCO* Mwanza ili wafikishe umeme eneo la Kijiji cha Kishili kati ya Igoma kwenye Jiji la Mwanza. Nguzo za umeme ziko mbali kutoka kwenye kijiji hicho na wananchi wanashindwa kuunganisha umeme kutoptana na umbali huo. Kwa kweli Wizara ya Nishati na Madini inafedhehesha juhudzi za maendeleo kwenye eneo hilo kutoptana na kutojali Wananchi kupitia Shirika lake la *TANESCO*. Nasema haya kwa kulinganisha juhudzi zilizofanywa na Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo kupitia Shirika lake la Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Mwanza kufikisha mtandao wa maji safi kwenye kijiji hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri wa Nishati na Madini anipatie majibu ya matatizo haya mawili ambayo naona yako chini ya uwezo wake. Naomba leo njue hatma ya matatizo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja.

MHE. BERNADINE R. NDABOINE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuchangia Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kuhusu umeme Mkoa wa Kigoma. Inasikitisha kuona kuwa ingawa Serikali ina dhamira ya kupeleka umeme vijijini Makao Makuu ya Mikoa, Mkoa wa Kigoma hakuna umeme wa uhakika. Wakati tukisubiri Serikali ya Sweden kufanya upembuzi yakinifu, basi tuongezewe *generator* ili *TANESCO* iweze kutoa umeme wa kutosha kusukuma maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni kuhusu Wilaya ya Kasulu. Mheshimiwa Rais Ali Hassan Mwinyi aliahidi kuwapa umeme, mpaka sasa bado. Alipokuja Rais Benjamin Mkapa akatoa ahadi tena, naye ahadi yake haikutekelezwa. Nina wasiwasi wananchi hawatakubali kudanganywa tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ni kuhusu Wilaya ya Kibondo. Mbona katika mpango wa Wilaya zitakazopatiwa umeme imesahaaulika?

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ni kuhusu upatikanaji wa madini. Serikali imefanya utafiti gani kuhusiana na uchimbaji wa madini huko Kagera - Nkanda Wilayani Kasulu? Ni madini ya namna gani yanayopatikana sehemu hizi? Je, Serikali inayo habari kuwa wananchi hupunjwa wanapouza madini haya kwa shilingi 2,000/= kwa kilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, huko Gombe kuna madini aina ya *Titanium* ambayo hutumika katika matengenezo ya ndege. Je, Serikali ina habari hizi? Ni kiasi gani cha madini haya kinachowenza kupatikana ili hatma za uchimbaji zianze na hivyo kuwaongezea wananchi kipato? Je, ni kiasi gani cha dhahabu kinachopatikana katika machimbo ya huko Kibondo na Serikali imewasaidiaje wachimbaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa unao utajiri wa madini, lakini bila umeme wa uhakika hatuwezi kuendeleza mkoa. Je, mpango wa Wabunge kwenda Burundi kuona uwezekano wa kupata umeme umeishia wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni tegemeo langu nitapewa majibu sahihi na ninaunga mkono hoja.

MHE. PHILEMON NDESAMBURO: Mheshimiwa Naibu Spika, kuna tatizo la msingi kule Mkoani Kilimanjaro. Mito yote inaanzia Mlimani Kilimanjaro. Mito hii inajaa maji kipindi chote cha masika na jadi ya wakazi wa Kilimanjaro huchimba mifereji ya maji toka kwenye hii mito na kuyatumia kwa kumwagilia mimea, kahawa na migomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa *TANESCO* ina hatimiliki ya maji yote katika mito hii kwa *project* ya *Nyumba ya Mungu Dam* pamoja na *Hale Project*, kwa ajili ya kutoa umeme. Kufanya Kilimanjaro kuwa *desert* kwa umeme hii siyo haki hata kidogo, kwani tuna vyanzo vingi vya umeme *IPTL*, *Songas* na hata *Solar Power* na makaa ya mawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka kurudisha ile hali ya neema chini ya Mlima Kilimanjaro na hii itawezekana tu. Kama tungekuwa na mpango kabambe wa kujenga *mini dams* katika mito yote na kuzuia maji yanayokwenda baharini ili yaweze kutumika kuleta neema Kilimanjaro. Mpango huu hautagharimu Serikali pesa zozote kwani malighafi ni mawe na udongo. Hivi vyote viro na nguvukazi ipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sijaridhika kabisa ni vipi umiliki wa *Mafuta House* ulihamishiwa *NSSF*. Shirika la Mafuta ni mali ya Watanzania wote na sisi wote tuna haki ya kupata haki yetu kutoka Shirika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, *NSSF* ni mali ya wanachama wa *NSSF*. Hapa je, haki iko wapi? Naomba Waziri alihakikishie Bunge lako Tukufu kuwa haki inatendeka na sisi Watanzania tupate haki yetu.

MHE. PROF. SIMON M. MBILINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Wizara kwa kazi nzuri na hotuba nzuri ya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu ni kwamba, kwanza, kazi ya *geologist* ipanuliwe ili waweze kutoa makisio ya kiasi cha madini wanayogundua kwa mfano tuna chuma na shaba nchini, ni kiasi gani hatujui!

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Shule ya *Geology* ya Dodoma ifundishe pia ufundi wa uchimbaji wa migodi mikubwa na ya kat. Hivi sasa kuna wachimbaji wadogo sana na wakubwa kabisa, hakuna wa kat.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, kuwe na shule za kuwafundisha wachimbaji wadogo kila Mkoa nchini. Hivi sasa wachimbaji wadogo wanatoka Wilaya chache tu na husafiri nchi nzima kuchimba vito na dhahabu.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, umeme wa gridi kwenda Songea toka Makambako umeanza kujengwa?

MHE. PROF. PIUS P. MBAWALA: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naunga mkono hoja ya Waziri wa Nishati na Madini kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo naomba kujua ile *tender* ya kuhakiki barabara ya Msongo wa umeme wa *KV 132* toka Makambako hadi Songea (Misufini) na Namtumbo itakamilika lini na mwezi upi katika mwaka huu wa 2005?

Mheshimiwa Naibu Spika, ujenzi wa *line* hiyo ya umeme toka Makambako hadi Namtumbo kuitia Songea utakamilika lini? Naomba hiyo tarehe itajwe ili wapigakura wangu wa Namtumbo wawe na matumaini ya uhakika.

Mheshimiwa Naibu Spika, je, Wilaya ya Namtumbo imo katika *Priority Districts* ya *Rural Electrification Programme*? Mradi ambao unaanza hapo 2006 kama ilivyotajwa jana katika jibu lihusulo programu hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ningeomba kujua yale makaa ya mawe yaliyoko Mto Njuga, Wilayani Songea, pia makaa ya mawe yaliyoko *Selous Game Reserve*, Wilaya ya Namtumbo, yanafaa kwa matumizi ya nishati ya kupikia au kutoa/kuzalisha umeme?

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, katika kuokoa misitu yetu kwa nini mipango isiwepo kuyapoza makaa ya mawe ili yafae kwa kupikia badala ya kutumia umeme ambaao siyo rahisi kutumika kwa kupikia kutokana na gharama zake?

MHE. OMAR S. CHUBI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote napenda kutoa pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na timu yake yote ya Wizara kwa kuandaa hotuba nzuri ambayo ni ya kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kueleza machache kuhusu ziara ya Kamati yetu kwa nchi za Namibia na Botswana. Mimi nilikwenda Namibia. Tuna sababu nydingi za kuiga kwa wenzetu katika maeneo yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ujenzi wa jengo la Wizara. Wenzetu wamepiga hatua kabisa. Wana jengo la kisasa ambalo ghorofa ya chini wameweka sehemu ya kuonyesha aina mbalimbali ya madini na bidhaa mbalimbali za madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine la kuvutia ni ujenzi wa Shirika la Maendeleo la Petroli mfano *Mafuta House*. Ujenzi wa jengo hili ni muhimu sana. Hivyo, uamuzi wa kuwanyang'anya *TPDC* jengo lao na kuwapa *NSSF* si uamuzi wa busara. Serikali iwarudishie jengo hilo mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Wizara iandae *Exchange Programme* kati ya wafanyakazi wa Wizara hii kwenda Namibia, Angola na Botswana na wa nchi hizo kuja Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

MHE. IRENEUS N. NGWATURA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii kuchangia hoja iliyowasilishwa mezani ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, napenda kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watendaji wote waliohusika katika kutayarisha bajeti hii kwa umakini mkubwa sana. Hongereni sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia utendaji wa Wizara kwa mwaka 2004/2005 ambaao una mwelekeo mkubwa wa kuridhisha, naunga hoja mkono kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa lengo la kuboresha hoja, napenda kuchangia maeneo yafuatayo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni kuhusu *IPTL*. Nashauri Serikali ichukue hatua za haraka kumaliza tatizo hilo kwa kununua mitambo hiyo. Kama mnaona ugumu bomoeni hiyo mitambo kwa sababu mitambo hiyo siyo tena kitega uchumi bali ni kinyonya uchumi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, kuhusu tatizo la wachimba madini wadogo Masuguru Mbinga, napenda nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa kutuma Tume ya Ushauri wa Madini kwa lengo la kupata taarifa sahihi kuhusu mgogoro uliojitokeza kati ya wachimbaji wadogo wa madini na wachimbaji wakubwa. Nitamwomba Mheshimiwa Waziri atoe tamko kuhusu matokeo ya Tume na maamuzi ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, naipongeza sana Serikali yetu kwa kushirikiana na Serikali ya Sweden kuititia Shirika lake la *SIDA* kwa kukubali kutoa fedha za kufanya upembusi yakinifu kwa ajili ya kupeleka umeme wa gridi ya Taifa Mkoa wa Ruvuma. Naomba kasi ya kupeleka umeme Wilaya kongwe ya Mbinga iongezwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, Chuo cha Madini Dodoma kutokana na umaarufu wa madini nchini, nashauri chuo hicho kipandishwe hadhi na kutoa *technical degrees* kwenye fani ya madini kama heshima kutokana na mchangano wa Mheshimiwa Benjamin William Mkapa, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Katika Sekta ya Madini, chuo hiki kipewe jina la *Benjamin William Mkapa School of Mines*.

MHE. JACKSON M. MAKWETTA: Mheshimiwa Naibu Spika, natoa pongezi kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, vipi utekelezaji wa mradi wa kushusha umeme Makambako na kuusambaza Makambako Mjini, Njombe Mjini na Vijiji vya Lupembe kazi itanza lini na itakamilika lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, Ibara ya 26 ukurasa wa 15 hotuba inasema: “Mshauri amepatikana.” Vipi mtekelezaji wa mradi ndani ya Njombe? Suala la upembusi wa kilovoti 132 ni kwa umeme wa kwenda Songea na siyo suala la Makambako au Njombe tena. Je, nielewe hivyo?

MHE. JEREMIAH J. MULYAMBATTE: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali kuwa na mpango mahsusini wa kupeleka umeme katika shule za Sekondari hapa nchini. Wilaya ya Meatu tunazo Shule tatu za Sekondari ambazo hazina umeme nazo ni Kimali Sekondari, Nyalanja Sekondari na Nghoboko Sekondari. Shule za Sekondari kukosa umeme ni kasoro kubwa na baadhi ya masomo hukosa kabisa kufundishwa na wanafunzi hukosa nafasi ya kujisomea wakati wa usiku. Naishauri Serikali kupeleka umeme katika hizo Shule za Sekondari Wilayani Meatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba/kuishauri Serikali kuwa na utaratibu wa kuwatambulisha wale wote wanaotumwa kuja Wilayani kutafuta madini hapa nchini kwani wao hawawatambui viongozi wa ngazi za Wilaya wala Mkoa. Hili ni tatizo na kero mbaya sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

MHE. TALALA B. MBISE: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na timu ya watendaji wa Wizara hii muhimu sana katika maendeleo

ya nchi yetu. Aidha, naomba kuwasilisha salaam za shukrani kutoka Jimbo la Arumeru Mashariki kwa Wizara, hususan kupitia kwa Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha, kwa juhudzi zake za kila hali kuhakikisha matatizo na masuala ya nishati tuliyopeleka Serikalini yanapata usikivu na utatuvi pale ilipowezekana. Sote jimboni tunamwombea kuendelea na kupata makubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati fulani mwaka 2001 timu ya wawekezaji wa *Tanzanite* Mererani walifika Dodoma wakati wa Mkutano wa Bunge. Kwenye kikao cha pamoja na wadau wa maeneo ya *Tanzanite* na Wizara waliahidi wangejenga kiwanda cha kusafisha *Tanzanite* na kufundisha Watanzania pale *Kilimanjaro Airport*. Mpango huu uliishia wapi au ilikuwa danganya toto?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la wachimbaji wadogo wadogo bado halijapata mfumo mzuri wenye utaratibu usio na mgogoro. Ni vizuri Wizara ikaendelea kulivalia suala hili njuga.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanaapolo kwenye migodi ya madini sehemu nyingi kama vile Mererani wanateseka na kuteswa kama vile wao hawana haki wala fursa kwenye raslimali za nchi hii. Kuweka ukuta au ulinzi ili wazuiwe wasiingie kwenye maeneo ya mgodi nadhani siyo suluhu, inaongeza uhasama. Wizara ishirikiane na Wizara nyingine zenye dhamana za Jamii, Vijana, Ajira, Afya na kadhalika kuweka na kutekeleza mikakati ya suala la Wanaapolo.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba na mimi nichukue nafasi hii kuchangia hoja ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Kabla sijaendelea napenda kusema kwamba naunga mkono hoja mia kwa mia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niungane na Waheshimiwa Wabunge wenzangu katika kutoa rambirambi kwa Waheshimiwa Wabunge wenzetu ambao wametutoka, hususan Mheshimiwa Abu Kiwanga na Mheshimiwa Margareth Bwana. Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema Peponi. Amen.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajaribu kupitia baadhi ya maeneo ambayo mimi nimeweza kuyaandaa kwa kupitia na maeneo mengine atayapitia Mheshimiwa Waziri. Nitaanza na suala zima la usambazji umeme nchini. Waheshimiwa Wabunge wamezungumza sana juu ya uwezekano wa kuwepo upendeleo kwenye suala la usambazaji umeme nchini. Hii ni hoja nzito na Serikali kwa ujumla haiwezi ikaichukulia kirahisi. Labda niseme tu kwamba katika suala zima la usambazaji wa umeme, kuna suala la kufikisha umeme kwenye Makao Makuu ya Wilaya, halafu kuna masuala ya kufikisha umeme kutoka ndani ya Makao Makuu ya Wilaya kwenda kwenye sehemu nyingine za Wilaya.

Kufikisha umeme Makao Makuu ya Wilaya, kwa kawaida ni kazi inayofanywa kwa fedha zinazopatikana ama kutoka Serikalini kwa kiasi kidogo au kwa kiasi fulani na fedha za Wafadhili. Hii ndio sehemu kubwa ya fedha zinazofikishwa huko kwa ajili ya

kufikisha umeme katika Makao Makuu ya Wilaya. Kuhusu usambazaji wa umeme ndani ya Wilaya ni kazi inayofanywa ama kwa fedha za Serikali inayotoka kwa *TANESCO* au kwa fedha za *TANESCO* kuitia bajeti yake yenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, napenda niseme kwamba, tunajitahidi kadri tuwezavyo kuhakikisha kwamba suala la usambazaji umeme linakwenda kwa mujibu wa mipango inayopangwa kila mwaka pale Wizarani na ndani ya Serikali na kwa mujibu wa Bajeti inayopatikana ama bajeti ndani ya Serikali yenyewe na bajeti ya Serikali pia inayojumuisha fedha za Wafadhili. Lakini nataka niseme tu kwamba kwenye maeneo ambayo usambazaji wa umeme unatoka kwenye Makao Makuu ya Wilaya kwenda kwenye sehemu nyingine za Wilaya, hii inakuwa ni kazi ya Shirika. Shirika la Umeme *TANESCO* nchini linajitahidi sana, limefanya kazi kubwa nchini ya kusambaza umeme, lakini pia linatazama vigezo mbalimbali hasa yale maeneo ambayo yanaweza pia yakalipatia kipato Shirika ili kuliwezesha kufanya kazi yake hii muhimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kwamba, kuna maeneo nchini yamepata umeme miaka mingi iliyopita katika Makao Makuu ya Wilaya zao na kwa ajili hiyo basi, usambazaji wa umeme katika maeneo hayo yasiyokuwa Makao Makuu ya Wilaya unaendelea kutokana na bajeti ya *TANESCO* ya mwaka hadi mwaka kwa Wilaya zake na Mikoa yake. Kwa mfano Jiji kama la Dar es Salaam ambao unatumia zaidi ya nusu ya umeme wa nchi nzima unazalishwa, lakini pia unatoa mapato zaidi ya nusu ya mapato ambayo *TANESCO* inapata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kwamba Shirika hili katika kuhakikisha kwamba linajiweka sawa kifedha, huwa wanahakikisha kwamba kwenye maeneo ya viwanda wanapoomba umeme na maeneo mengine wanafikisha umeme na ndio hivyo kwa Wilaya nyingine ambazo zimepata umeme zamani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika michango ya Waheshimiwa Wabunge, palitajwa maeneo mahsusili hapa, ama michango ya maandishi au michango ya kuzungumza juu ya maeneo ambayo hayajafikishiwa umeme. Tukianza na maeneo ya Makao Makuu ya Wilaya, Mheshimiwa Mbonde kwa mfano amezungumzia suala la Rufiji kama litakuwa limefikishiwa umeme mwaka huu 2005 na akadhani kwamba halikutajwa katika bajeti ya Mheshimiwa Waziri. Lakini napenda nimhakikishie kwamba suala la kufikisha umeme kwenye Wilaya ya Rufiji kwenye Miji ya Utete, Ikwiriri, Kibiti na maeneo mengine, ndio linafanyiwa kazi sasa ya kupeleka umeme.

Pia, kuna maeneo mengine ambayo pamoja na kwamba yameorodheshwa katika Wilaya kumi tatu au zaidi ya hapo lakini yamo katika utaratibu wa usasa wa kuanza kufikishiwa umeme. Hizi ni Wilaya za Simajiro na Bukombe ambayo tuna uhakika kwamba katika muda mfupi ujao tunaweza kufanikiwa kukamilisha masuala ya fedha yanayohusu upelekaji wa umeme katika maeneo haya kama ambavyo Wizara tayari imetenga fedha Shilingi milioni 400 za kusambaza umeme kwenye Wilaya hii ya Ludewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yametajwa maeneo mengine kwa uchungu kabisa na Mheshimiwa Missanga kuhusu umeme kwenye Shule ya Sekondari ya Ihanja. Napenda nimhakikishie Mheshimiwa Missanga kwamba anayosema kwamba amekuwa akizungumzia suala hili kila wakati ni kweli amekuwa mfuatiliaji mzuri wa suala hili. Lakini napenda nimhakikishie kwamba umeme wa maeneo haya ambayo ameyataja zimeingizwa sasa katika mradi huu wa *ERT*, yaani wafikishaji umeme, *Energiezing Rular Transformation* ambayo kama ambavyo nimewahi kujibu hapa Bungeni unaanza mwakani.

Mheshimiwa Ndassa naye amezungumzia katika mchango wake wa maandishi juu ya suala la umeme wa Sumve. Pia, napenda kusema tu kwamba mradi ule unajengwa sasa hivi na kwamba kilichobakia ni kupata vifaa vinavyoitwa *conductors* ambavyo sasa hivi havipo hapa nchini na Shirika hili la Umeme *TANESCO* wanashubiri tu, wakipata vifaa hivyo basi kazi hiyo itaendelea kwa awamu kama ilivyopangwa awali. Hivyo hivyo kwa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge wengine kwa mfano Mheshimiwa Mudhihir, amezungumza sana juu ya suala la umeme wa Mchinga hadi akasema kwamba watu wa Mchinga wamekosa nini?

Mheshimiwa Mudhihir, napenda niwaambie wananchi wa Mchinga kwamba umekuwa ukilifuatilia suala hili kwa kasi kubwa na kwa hakika hii ndio imepelekea mradi huu sasa wa Mchinga kuwekwa katika mpango huu wa *ERT* kuanzia mwakani na mimi nina imani watakapokuchagua tena mwaka huu utaendelea pia kulifuatilia suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *IPTL*, niliulizwa swali hapa kwamba, kwa nini Serikali inashughulika na ubadilishaji wa mfumo wa uzalishaji wa huu mtambo wa *IPTL* kutoka kwenye mafuta hadi kwenye gesi? Sababu ni kwamba, kama mnavyofahamu pale kuna mambo mawili. Kuna kitu kinaitwa *capacity charge*, kulipia tu ile mitambo yenye wekuwe pale na *energy charge*, gharama ambayo tunalipa kwa kununua ule umeme. Zote kwa pamoja ni karibu Shilingi bilioni nane kwa mwezi, *capacity charge* bilioni tatu na *energy charge* ni Shilingi bilioni tano.

Mkataba wa *IPTL* unaruhusu *TANESCO* kubadili mfumo wa uzalishaji kwa maana ya kutumia gesi badala ya mafuta ambayo ni ghali na *IPTL* kama Kampuni ukilinganisha na *TANESCO* haiwezi kuwa kuvutio, yaani haiwezi kuwa na *incentive* (kwa Kiingereza) kutumia gesi badala ya mafuta kwa sababu hawa kwa kweli hawawezi kujishughulisha sana na hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, wao kwa vyovypole vile wanapata mapato yao kwa sasa hivi. Kwa hiyo, basi ni Serikali na *TANESCO* ndio ambayo inaweza kuwa na tamau kubwa na kuwa na haja kubwa ya kubadili huu mfumo wa uzalishaji na ndio maana kwa sababu imo katika Mkataba, tumeona ni vizuri mitambo ile ibadilishwe itumie gesi ambayo tunayo hapa badala ya mafuta ambayo ni ghali mmo. Bila ya kubadali mfumo huu, maana yake ni kwamba tutaendelea kulipa fedha hizi. Lakini ikibadilishwa badala ya kulipa *energy charge*, kwa mfano bilioni tano tunaweza tukajikuta tunalipa *energy charge* bilioni moja kwa mwezi.

Kwa hiyo badala ya kulipa Shilingi bilioni nane kwa mwezi yaani *capacity charge* na *energy charge* tukajikuta tunalipa Shilingi bilioni nne na kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamechangia na Serikali inatambua kwamba jambo la msingi kabisa kuhusu mtambo huu wa *IPTL* ni kuununua, napenda niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge kwamba sasa hivi Serikali inafanya mpango ihakikishe kwamba mtambo huu wa *IPTL* unanunuliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya ruzuku kwa *TANESCO*, Waheshimiwa Wabunge wameulizia hapa kwa nini Serikali inatoa ruzuku kwa *TANESCO*? Kwanza niseme kwamba ruzuku ambayo imepata *TANESCO* hapa nyuma ni Shilingi bilioni 40 kutoka Serikalini na Shilingi bilioni 50 kutoka Benki ya Dunia. Hii imetokana na mfululizo wa hali ya ukame nchini kwa miaka mitatu na hivyo kukausha mabwawa ambayo ndio yalikuwa yanatumika zaidi kwa uzalishaji wa umeme. Bila ya ruzuku tungekabiliwa ama na mgao kama ilivyokuwa Uganda na Kenya na ambao ungekuwa na athari kubwa kwa uchumi wetu au ingebidi *TANESCO* ipandishe bei ya umeme kwa asilimia 25 ili kuweza kufidia namna ya kuweza kupata uzalishaji wa umeme kwa njia nyingine. Ndio maana katika kutathmini suala zima la kuhakikisha kwamba uchumi wetu hautetereki, Serikali ikaona ni vyema kutoa ruzuku kwa Shirika hili ambayo ni mia kwa mia ni Shirika la Serikali.

Kama ambavyo baadhi yetu tunafahamu, ni kwamba bei za *TANESCO* hapo awali hazikuwekwa kutokana na bei ya mafuta, ziliwekwa zikitegemea uzalishwaji wa umeme unaotokana na maji. Sasa ilivyotokea ukame, uzalishaji wa maji ulivyopungua ikawa sasa hakuna njia nyingine isipokuwa kutoa ruzuku ili waweze kuendelea kuzalisha umeme ama vinginevyo kama nilivyosema awali ingebidi kwenda kwenye mgao wa umeme au kuongeza bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, juu ya kutumia gesi zaidi katika kuzalisha umeme ambayo imezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge akiwemo Mheshimiwa William Shellukindo kwa kweli ni mkakati. Kwanza tunakubaliana naye na pia ni mkakati wa Serikali kuchanganya vyanzo vya uzalishaji umeme, yaani ultumia maji na gesi na kujaribu kuepukana sana na uzalishaji wa umeme kutumia mafuta kwa sababu ya gharama za mafuta. Songa sasa hivi pale Ubungo tayari ina uwezo wa kuzalisha megawati 184 na *turbines* ya tano na sita ziliwekwa haraka ili kuhakikisha kwamba tunaweka mfumo bora zaidi wa uzalishaji umeme kwa kutumia gesi ili kuepukana na gharama za uzalishaji umeme.

TANESCO wana mpango wao wenyewe pia wa kuzalisha umeme wa megawati 50 katika muda mfupi ujao kwa kufanya wao wenyewe hiyo kazi badala ya kuiachia Songas. Kwa hiyo, lengo zima la kutokuiachia Kampuni moja kuhodhi uzalishaji wa umeme, kiwango kikubwa ni megawati nyingi na baadaye pengine pakitokea tatizo katika uzalishaji pale inakuwa nchi nzima inapata matatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni hivyo hivyo ndio maana basi hata Serikali imekuwa ikihakikisha kwamba gesi ya *Mnazi Bay* inatumika katika kuzalisha umeme na kama ambavyo tunesema mara nyingi hapa Bungeni, awamu ya kwanza ya kutumia gesi hii

huenda ikatumia kuzalisha kama megawati 15 na ipo gesi ya kutosha kuna *cubic feet* bilioni 79 za gesi na katika hizi *cubic feet* milioni 10 tu ndio zinaweza kutumika kwa siku. Lakini ile Kampuni iliyopo ya *TUMAS* wanaweza kutumia kama *cubic feet* milioni mbili hadi tatu kwa siku.

Kwa maana nyingine ni kwamba ni mradi ambao una gesi nyingi unaweza kuzalisha umeme kwa zaidi ya miaka 20. Sasa Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz sasa hivi wakati anachangia amezungumzia sana umuhimu wa kutazama; je, bei ya umeme katika mradi ule itakuwaje? Nataka niseme jambo moja kwamba kwa muda wote huu kwanza Serikali imekuwa ikichangia au ikitoa ruzuku kwa njia moja au nyingine katika kuhakikisha kwamba wananchi wa Mikoa ya Lindi na Mtwara ambao hawakuunganishwa na *grid* kama ilivyo baadhi ya Mikoa mingine ambayo haikuunganishwa wanalipa bei ya umeme inayofanana na wenzao.

Suala la bei ni la msingi na ninapenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba sasa hivi Serikali inafanya majadilino na Kampuni hii ya *TUMAS* kwa ajili ya bei. Serikali hii ni makini sana kuhakikisha kwamba wananchi wetu wanapata bei ambayo inaendana na uwezo wao wa kulipa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu viwanda kupunguza bei ya bidhaa baada ya kutumia au kuuziwa gesi ya Songo Songo kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wamezungumza, ni kweli kwamba ni matumaini yetu kwamba viwanda hivi baada ya kutumia gesi, tunawatarajia au tunawategemea kwamba wataweza kupunguza bei ya bidhaa. Bei ya mafuta walijotumia kama tunavyofahamu ni moja tu ya vigezo ambavyo vinapanga bei katika Makampuni haya na wenyewe nadhani sasa hivi wanasema wanajaribu kwanza kurejesha gharama za kubadili mfumo, yaani kutoka kwenye kutumia mafuta na kwenda kutumia gesi katika uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sisi kama Wizara tunatoa wito kwa viwanda hivi kama ambavyo Waheshimiwa Wabunge wengine wamezungumza kwamba ufike wakati basi matumizi ya gesi haya yaweze kuonyesha dalili nzuri kwa bei za bidhaa ambazo wananchi wanazinunua kwenye viwanda hivi mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mkataba wa *Net Group*, kwanza Mkataba huu unaisha Desemba, 2006 na nimeshawahi kujibu hapa Bungeni juu ya mafanikio ya Kampuni hii na hasa kwenye upande wa kifedha kwa kuibadili Kampuni. Lakini katika Mkataba huu wa sasa wametakiwa waandae mpango mahsus wa kukabidhi madaraka kwa wazalendo wakati Mkataba huu utakapokwisha. Pia, tayari kama ambavyo Mheshimiwa Waziri amesema katika hotuba yake, Mkurugenzi wa Uzalishaji ni Tanzania, tungependa pengine nafasi ziwe zaidi ya hapo, lakini tutaendelea kulifuatilia kwa karibu kuhakikisha kwamba Kampuni hii inaweka mpango na inatekeleza mpango wa kuwezesha au *capacity building* ndani ya *TANESCO* ili wakati utakapofika wazalendo waweze kukabidhiwa madaraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utafutaji wa mafuta, ni kweli tunavyofahamu kwamba hili ni suala la Muungano. Pamekuwa na majadiliano ya ndani baina ya Serikali mbili kuhusu suala hili. Ni jambo la kawaida. Pameundwa Kamati ambayo

imeshawasilisha taarifa kwa viongozi wetu na mimi naamini kabisa kwamba ufumbuzi wa suala hili utapatikana ili Kampuni hizi ambazo zinakuja kutafuta mafuta ziweze kufanya kazi zake kwa ukamilifu juu ya utafutaji mafuta. Pia, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu inafanya mpango wa kuhakikisha kwamba linaleta hapa Bungeni Muswada wa Sheria mpya ya mafuta ili kubadili Sheria ya mwaka 1980 ili kuendana na wakati. Mwaka 1980 na mwaka 2005 ni vipindi tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mikataba ya Madini ambayo Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba amezungumza na Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Madini pamoja na Msemaji wa Kamati ya Uwekezaji na Biashara, kwanza niseme kwa ujumla kwamba, kama ambavyo mnafahamu, ripoti ya Mwenyekiti wa Kamati ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu aliiunda, Dr. Kipokola aliwasilisha hata kwetu sisi Wabunge kwa majadiliano. Ipo Serikalini na Serikali itaifanyia kazi taarifa hii kwa uzito kabisa kuhakikisha kwamba yale ya msingi yanatelezwa. Ninakubali kama alivyosema Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba kwamba kuna maeneo ambayo yana mgongano kati ya Sheria ya Madini ya mwaka 1998 na Mikataba ya Madini na Sheria zetu nyine hasa zinazohusu suala la kodi. Niseme tu kwamba Serikali inafanya kazi suala hili ili baadhi ya mambo kwa mfano kama yale yaliyozungumzwa ya malipo ya Dola mbili kwa mwezi yaweze sasa kupata ufumbuzi na kulipwa kwenye Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine lilihusu misaada kwa wachimbaji wadogo wadogo amba wamezungumza Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo na wengineo. Serikali inafanya kazi mapendekezo ya Kamati ya Madini kama nilivyo sema awali. Pili, sisi tunakubaliana nanyi juu ya umuhimu wa kuwawezesha wachimbaji wadogo. Najua kurekebisha makosa ya nyuma kwanye masuala ya Sekta ya Madini labda nirejee tu kwamba kimsingi kama ambavyo Mheshimiwa William Shellukindo aliwahi kusema, ni kwamba wakati tunaingia katika suala la uchimbaji madini na uwekezaji madini, hii imekuwa ni sekta mpya na kwa vyovypote vile mnapoanza kuna mambo yanaweza yakajitokeza kwamba yanahitaji marekebisho. Ndio maana basi, Mheshimiwa Waziri Mkuu aliunda Kamati ikapitia mambo haya na ikawasilishwa Serikalini. Ni imani yangu kwamba tutawenza kuifanya kazi vizuri taarifa hii na taarifa nyine ambazo zimetolewa kuhusu suala zima la madini. Ninakubaliana na Waheshimiwa Wabunge juu ya umuhimu wa Taasisi zetu kama *STAMICO*, *NDC*, *TPDC*, *SIDO* na wengine waweze kuwezesewa waingie katika uwekezaji katika Sekta ya Madini ili hata kama mfumo wetu ni kwamba Serikali yenye we haiingii. Lakini zipo Taasisi muhimu za Umma ambazo zinaweza kuingia katika suala la uwekezaji katika Sekta ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda tu niseme kwamba pamoja na Taasisi zetu kuingia katika uzalishaji au uchimbaji wa madini au uwekezaji katika madini, lazima tukubali kwamba bado tunahitaji mitaji kutoka nje kwenye uchimbaji wa madini na kwenye kuongeza thamani ya madini. Kwa hiyo, kama Serikali, nadhani tuna wajibu wa kuhakikisha kwamba tunaweka mazingira bora ya kuvutia wawekezaji katika Sekta hii muhimu ya Madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala la kupanda kwa bei ya mafuta, tumewahi kusema hapa Bungeni kwamba sababu kubwa kwa sasa hivi ni suala la vita vya Iraq na matumizi makubwa ya nchi kama Uchina, India na Marekani kwenye masuala ya mafuta. Ni jambo ambalo Serikalini tunalifahamu, tunalishughulikia, lakini si jepesi. Lakini nataka kusema tu kwamba ni suala ambalo linashughulikiwa katika kuhakikisha kwamba uchumi wetu hautetereki sana. Lakini nadhani faraja kubwa tunaipata pale Mwenyezi Mungu atakapotujalia na sisi tukaweza kupata mafuta. Kwa hali ilivyo hivi sasa, bado hatujagundua mafuta, lakini tunaendela kutafuta.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu umuhimu wa kuteuwa viongozi katika Idara badala ya kuendelea kukaimu kwa mfano Kamishna wa Madini, Mkuu wa *TANSORT* London na kadhalika, sisi tunakubaliana kabisa na mawazo ya Waheshimiwa Wabunge kwamba lazima tupate viongozi haraka iwezekanavyo kwa mujibu wa taratibu zilizopo na kazi hiyo inafanyika hivi sasa na ni muhimu basi katika kujenga uwezo wa watumishi wetu kuwa na watumishi ambao wamedhibitishwa, lakini pia katika kuwa watumishi ambao wanapata mafunzo muhimu na kazi ya mafunzo pale Wizarani sasa hivi inaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu kubwa ni kwamba Sekta hii ya Madini imekuwa haraka kuliko kasi ya kujenga uwezo na ni jambo ambalo limeonekana hata katika tafiti mbalimbali ikiwemo kazi ambayo imefanywa na Kamati ya Dr. Kipokola.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, kama nilivyosema awali kwamba, kuna mambo mengi ambayo yamechangiwa na Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa Waziri atakuja kuchangia mengine, lakini nina hakika pia pamoja na hayo hatutawenza kuyajibu yote hapa. Tutayafanya kazi, tutawapa Waheshimiwa Wabunge kwa njia ya maandishi haraka iwezekanavyo ili kuhakikisha kwamba yale ambayo wameyasema, yamewekwa katika kumbukumbu zetu ili na sisi tutakapokuja kukabidhi, basi tukabidhi kwa hawa wanaokuja kazi ambayo inapaswa kufanywa kwa mujibu wa hoja ambazo zimetolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Baada ya kusema hayo ambayo nimeyasema, napenda nichukue nafasi hii kwanza nitoe shukrani nyingi sana kwa Wapigakura wangu wa Jimbo la Kibaha ambao katika miaka 10 nilipata bahati ya kuchaguliwa nao mara tatu. Mwaka 1995 katika uchaguzi mdogo, mwaka 1999 na mwaka 2000 na kila waliponichagua, walinchagua kwa kura nyingi zaidi. Kwa hiyo, nawashukuru sana kwa kuniwezesha kuingia katika Bunge hili.

Pili, napenda nimshukuru Mheshimiwa Rais kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kulitumikia Taifa, ye ye pamoja na wasaidizi wake, Mheshimiwa Makamu wa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu na mimi nimejitahidi kadri nilivyoweza kwa nafasi ambayo nilikuwa nimepewa. Lakini pia pamoja na haya, kama tungkuwa tunatoa maneno au kuunda maneno, tungeweza kusema katika Bunge hili kwamba pamekuwa na kitu tunaweza tukasema *Mwando sya doctrine*. Amezungumza jambo hapa juu ya umuhimu wa kushukuru familia zetu na mimi napenda niungane na Waheshimiwa Mawaziri wote waliopita waliokuwa wakifanya hivyo hivyo kama alivyokuwa akifanya ye ye.

Nami namshukuru mke wangu na familia yangu kwa nafasi ambayo wamenipa muda wote na kunivumilia kwa kweli mara nyingi ambapo sipo nyumbani. Lakini napenda pia nimshukuru sana ndugu yangu, kaka yangu Mlamuwa hapa Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. (*Makofi*)

Nimefanya naye kazi kwa upendo mkubwa na kwa ushirikiano mkubwa na mimi namtakia yeje kila la kheri kama ambavyo ninaamini na yeje ananitakia mimi kila la kheri katika kuhakikisha kwamba tunarejea hapa Bungeni. (*Makofi*)

Lakini si yeje tu, napenda nimshukuru Katibu Mkuu, Kamishna wa Nishati, Kamishna wa Madini aliyeondoka ambaye sasa hivi yuko kwenye Taasisi yetu ya *STAMICO* na aliyeopo sasa hivi, Mkurugenzi Mkuu wa *TPDC*, Mkurugenzi Mkuu wa *TANESCO*, *STAMICO*, *TGS*, Chuo cha Madini na wengineo.

Napenda pia niwashukuru watumishi wote wa Wizara ya Nishati na Madini na wasaidizi ambao tumekuwa nao sisi karibu pale Ofisini pamoa kwa kuhakikisha kwamba katika kipindi chote ambacho nimekuwa Wizarani wamenifundisha, nimejifunza vizuri ninaamini. Nimeweza kusimama hapa kwa niaba yao kujibu kwa niaba ya Serikali mbele ya Bunge. Nimekuja kwenye Wizara hii nikitoka kwenye eneo lingine kabisa ambalo halihusiani na madini, lakini siku hizi naweza nikazungumza habari ya mashapo naweza nikazungumza mambo mengi tu. Ninawashukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda nimshukuru Mheshimiwa Spika ambaye sasa hivi hayupo na Naibu Spika na Wenyeviti kwa kulifanya Bunge hili kuwa ni mahali ambapo hata katika mjadala mkali sana mnaweza mkakaa mkaamua mambo kwa ufasaha kabisa na kwa utulivu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba nichukue nafasi hii niwashukuru wajukuu zangu wa kisukuma na wanyamwezi waliopo katika Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wao kama unavyofahamu wamefanya mijadala katika Bunge hapa kuwa michangamfu kabisa na mara nyingi na ndio maana nimeanza kumshukuru Mheshimiwa Spika na Naibu Spika, kwa sababu na wao wametambua umuhimu wa jadi au mila katika kuendesha Taasisi nzito kama hii, kwamba kuna wakati baki ya kuchangia mambo mazito kabisa, lakini pia utani wa kimila unakuwepo katika kusawazisha mambo. Ninawashukuru sana wajukuu zangu na ninawatachia kila la kheri, lakini msisahau kuja kutambika kule nyumbani kwenu. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya haya, sasa napenda nichukue nafasi hii na mimi niseme tena kwamba naunga mkono hoja hii muhimu ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini. Ahsante sana. (*Makofi*)

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kuniruhusu kuja kumalizia hoja yetu leo jioni na nianze kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri ambayo ameshayatoa. Lakini kabla sijaendelea na yale ambayo hakuyagusia, naomba niwatambue

Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia katika hotuba yetu leo kwa kuzungumza na waliochangia kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge ambao wamechangia kwa kuzungumza ni 12, nao walikuwa ni Mheshimiwa Herbert Mntangi, Mheshimiwa Isaac Cheyo, Mheshimiwa William Shellundo, Mheshimiwa Ponsiano Nyami, Mheshimiwa Mohamed Missanga, Mheshimiwa Stanley Kolimba, Mheshimiwa Dr. Aaron Chiduo, Mheshimiwa Faustine Rwilomba, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Mbaruk Mwandoro, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz na Mheshimiwa Lekule Laizer. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge walichangia kwa maandishi ni 47 nao ni Mheshimiwa Richard Ndassa, Mheshimiwa Danhi Makanga, Mheshimiwa Philip Marmo, Mheshimiwa Dr. Willbrod Slaa, Mheshimiwa Raynald Mrope, Mheshimiwa Kilontsi Mpologomyi, Mheshimiwa Stephen Kazi, Mheshimiwa Bernadine Ndaboine, Mheshimiwa Philemon Ndesamburo, Mheshimiwa Simon Mbilinyi, Mheshimiwa Pius Mbawala, Mheshimiwa Omar Chubi, Mheshimiwa Ireneus Ngwatura, Mheshimiwa Jackson Makwetta, Mheshimiwa Jeremiah Mulyambatte, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Oscar Mloka na Mheshimiwa Kharidi Suru. (*Makofi*)

Wengine ni Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Ernest Mabina, Mheshimiwa Hilda Ngoye, Mheshimiwa Tatu Ntimizi, Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Alhaj Abdallah, Mheshimiwa Fatma Said Ali Mchumo, Mheshimiwa Job Ndugai, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni, Mheshimiwa Prof. Mark James Mwandoysa, Mheshimiwa Edson Halinga, Mheshimiwa Diana Chilolo, Mheshimiwa Ali Said Salim, Mheshimiwa Janeth Mashele, Mheshimiwa Raphael Mlolwa, Mheshimiwa Dr. Milton Mahanga na Meshimiwa Faustine Kabuzi Rwilomba. Wengine ni Mheshimiwa Bakari Mbonde, Mheshimiwa Aridi Uledi, Mheshimiwa Sijamini Mohamed Shaame, Mheshimiwa Mudhihir M. Mudhihir, Mheshimiwa Leonard Derefa, Mheshimiwa Mohamed Abdulaziz, Mheshimiwa George Lubeleje, Mheshimiwa Lucas Selii, Mheshimiwa Talala Bana Mbise, Mheshimiwa Andrew J. Chenge na Mheshimiwa Athumanji Janguo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yake ambayo ameyatoa jioni kwa hoja mbalimbali ambazo zilitokana na mjadala wa Bajeti yetu ya leo. Amegusia maeneo mbalimbali na kwa kweli kama tutakavyoona wachangiaji walikuwa wengi hasa wa maandishi na wengine waliandika hizi karatasi wakarudia mara mbili mbili, yaani *page five, six* hivi na hoja zote hizo kwa bahati tumeweza kuzinasa mchana huu tangu tutoke asubuhi na tumejaribu kuzijibuhapa. Lakini ni majibu mafupi sana na ili nisije nikasahau, niseme kabisa kuwaahidi kwamba tutatoa haya majibu kwa maandishi vizuri zaidi tumpelekee kila Mheshimiwa Mbunge ambaye alitoa hoja, tumpekelee majibu ya kutosha katika wiki mbili zijazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kama kuna hoja ambayo nitaiacha kwa sababu ya muda, siyo kwa sababu tumeidharau au siyo nzito, lakini ni kwa sababu muda

haututoshi na kwa hiyo, nitaanza na zile hoja ambazo nadhani nitapata nafasi ya kuzizungumzia kwa sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze na hoja ya Mradi wa Mchuchuma. Waheshimiwa Wabunge wengi wamezungumzia umuhimu au faida zinazoweza kutokana na kutumia makaa ya mawe katika kuzalisha umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, makaa ya mawe ni kweli yanazalisha umeme nchi nydingi na nchi ambazo zimeendelea sana za Ulaya walianza na kuzalisha umeme wa makaa. Lakini kwa hapa kwetu makaa ya mawe yapo. Kazi kubwa au shida kubwa au upungufu mkubwa ni fedha za kuweza kuyatoa makaa ya mawe hayo ardhini na kuyageuza yawe umeme. Serikali tumeshindwa kwa miaka 40 hii kuwa na fedha za kutosha kufanya kazi hiyo, siyo kwa sababu hatutaki, lakini kwa sababu hatuna fedha katika Bajeti ya kuweza kufanya shughuli hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tumejaribu kwa miaka yote hiyo *over the years* kuwawutia wawekezaji na katika sehemu ya Mchuchuma ambapo tunaamini kuna makaa mengi tumepata wawekezaji ambao wameonyesha nia ya kuwekeza pale. Wawekezaji ambao sasa hivi tunazungumza nao ni *Siemens*. Ni kundi ambalo linaongozwa na *Siemens*, Kampuni kubwa sana ya Kimataifa ambayo inafanya shughuli hizo *South Africa* na Ulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, shida tuliyonayo ni kwamba ili mradi uwe *viable*, maana wale ni wawekezaji wanaowekeza fedha zao wenyewe ili mradi uwe wa faida, ni lazima kuwe na soko la kununua huo umeme ambao utatokana na mradi huo. Umeme ambao tungeweza kuununua sasa hivi kama mradi ungefanya kazi kama umeme ungezalishwa megawati 400 ambazo tunafikiria zinaweza kuanzishwa kwa mara moja.

Umeme huo tusingeweza kuutumia kama nchi kwa mara moja, hatuna uwezo wa kuutumia umeme huo. Kwanza uzalishwe pale Mchuchuma na kuusambaza kuupeleka kule ambako unahitajika ufile kama Kigoma, Ruvuma, Kagera na Rukwa sehemu zote hizo lazima uwe na mtandao mkubwa sana. Kwa hiyo unahitaji fedha nydingi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana mradi huo wa Mchuchuma unaonekana kama unasitasita. Wanafanya nini hasa wawekezaji, tumepatana nao watafute soko siyo ndani ya nchi tu, lakini nije ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana tunazungumzia kuunganishwa kwa *grid* yetu na nchi za jirani, huu ndio uchumi wa siku hizi kuunganishwa, siyo kwenye *computer* tu na utandawazi, lakini ni kwenye miundombinu vilevile. Mheshimiwa Magufuli anazunguzia barabara ambayo tunaunganisha sasa hivi na Kenya na Uganda ili tuweze kufanya biashara zetu vizuri, lakini hata kwenye umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, umeme ni biashara. Sisi Tanzania tunaweza kuzalisha umeme mwangi sana kuliko tunavyohitaji, lakini tuwe na soko. Soko lipo Kenya, Kenya hawana maji mengi, hawana vianzio vingi kama gesi, hawajapata bado wanatafuta. Kwa

hiyo, mradi wa kuunganisha Kenya, Tanzania na Uganda ni muhimu sana na Serikali inahimiza ili uweze kukamilika na ukishakamilika, basi mradi wa Mchuchuma nao utakuwa na *viability*. Utakuwa sasa unaweza kuanzishwa, mwekezaji anaweza kupatikana akawekeza fedha pale ukazalishwa umeme ukauzwa Kenya na Uganda na siyo kuuza tu wakati tukiishiwa na umeme sisi, *you never know* siku zijazo na sisi tunaweza kununua kutoka kwa wenzetu. Kama ninavyosema, ni biashara ambayo ina fedha na ina faida kubwa sana. Nchi za Ulaya na nchi za Waarabu wanauziana umeme mara kwa mara kwa sababu wameunganishwa.

Kwa hiyo, Mchuchuma hilo ndilo tatizo lake kubwa. Tunahitaji kama Dola milioni 600 sasa hivi uanzishe mradi ambao ni *viable* ambao unaweza ukasimama peke yake. Njia nyine ni kuanzisha kwa awamu, wawekezaji wanasema hawako tayari kufanya hivyo, wanafikiria, lakini bado hawako tayari kufanya hivyo. Hilo ndio sababu mradi wa Mchuchuma unachelewa na ndio sababu makaa ya mawe hatujaanza kuyatumia kwa kuzalisha umeme. Tunagemea gesi tunayo na gesi hiyo sasa hivi ya *Mnazi Bay* pamoja na hii ya Songo Songo tunaitumia kwenye kuzalisha umeme kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile kwenye viwanda tunajaribu, hata gesi ya *Mnazi Bay* ambayo haijatoka ardhini, lakini tunajua ipo, wameshaanza wawekezaji kutafuta masoko ya kuanzisha kwa mfano viwanda vya mbolea kama ambacho Mheshimiwa Leonard Derefa anazungumzia wakati wote, tuweze kuweka ile gesi kwenye *container* na kuiuza Uarabuni. Masoko ya kununua gesi hiyo kwenye viwanda vidogo vidogo inatiwa kwenye *container* halafu inapelekwa Mwanza, Singida na kwingine ambako hakuna mabomba ya gesi. Waheshimiwa Wabunge, yote hayo Serikali inaangalia pamoja na wawekezaji ili kuhakikisha kwamba raslimali hizi zinatolewa ardhini na zinaanza kutumika kutuletea faida katika vita vyetu dhidi ya umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna habari ya Mheshimiwa Naibu Waziri alizungumzia bei za umeme kwamba; Je, kwa nini bei bado ni ghali wakati tunatumia gesi yetu sasa hivi? Gesi kweli ni rahisi kuitoa ardhini pale, lakini tukumbuke mradi wa Songo Songo kwa mfano uligharimu karibu Dola 270, 280 na ziliwekezwa pale na Serikali pamoja na Sekta binafsi. Sasa wale waliwekeza pale wanahitaji kurudisha fedha zao na ndio maana ya *investment*. Ndio maana ya uwekezaji. Kwa hiyo, hatujafikia hatua ambapo unaifu tunaoupata na gesi yetu kwa miaka hii miwili, mitatu ya kwanza tunaweza ku-*translate* au kuupitisha kwa mtumiaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kama alivyosema Dr. Msabaha Serikali imehakikisha kwamba bei za umeme nchi nzima ziko sawasawa, mkitizama lile jedwali letu katika kitabu cha hotuba mtaona bei za umeme kwa mafungu mbalimbali hapa Tanzania, Kenya na Uganda. Mtaona tunavyolinganishwa watu wakisema Tanzania bei ya umeme ni ghali kwa hiyo viwanda haviji siyo sawa kwa kweli, siyo ukweli kabisa kuna sababu zingine labda.

Bei ya umeme peke yake kama *a source of energy* hapa kwetu inafanana fanana na ya Kenya na Uganda na kwa watumiaji wadogo wa majumbani sisi ni nafuu kabisa

kwa sababu tuna *subside* kama Serikali tunawajari wananchi wetu hasa wale ambao ni wa hali ya chini ili waweze kutumia umeme na kujipatia maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali sasa hivi inazungumza na wale wanaozalisha gesi hii kuona kwamba bei tunayopata, kodi tunazopata, mrabaha kwenye gesi ni mkubwa sana kuliko mrabaha kwenye madini. Kwenye gesi na mafuta tunapata asilimia 12.5 siyo ile tatu kama kwenye dhahabu au 5 kama almasi.

Kwa hiyo tunalinda sana maslahi yetu, lakini tunazungumza nao kuhakikisha kwamba bei hizo zinakuwa za maslahi katika Taifa letu na hatukaangwi na mafuta yetu kwa sababu ni raslimali iliyopo hapa. Lakini vilevile tunatambu kwamba wamewekeza fedha zao, fedha za *shareholders* wa huko kwao ni lazima wapate mapato ili tuweza kuvutia wengine ambao wako tayari kuja kuwekeza kutusaidia kutoa raslimali hii hapa ardhini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna swalii kila wakati ninaulizwa hivi madini ni mali ya nani? Gesi ni mali ya nani? Ni mali yetu kwa kweli lakini kama samaki, kama misitu kabla hujaitoa kule porini lile gogo au samaki hujamtoa baharini kwa kweli hakusaidii chochote hata ukisema samaki wangu huyu, we unakula mchicha unalala na njaa, mpaka umtoe pale kama huwezi kumtoa basi unatafuta mvuvi, mvuvi unamlipa ndiyo maana tunakuwa na hawa wawekezaji na tunapatana tunaingia kwenye mikataba watusaidie kutoa raslimali hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejaribu raslimali hizi kuziendeleza wenyewe kwa miaka yote hii na tumefika mahali ambapo kwa kweli tunahitaji msaada wa kutoka nje lakini wakati wowote tunajilinda katika mikataba yetu.

Ndiyo maana ushauri wa Waheshimiwa Wabunge, ushauri wa Dr. Kipokola kwamba tuwe macho Serikali inausikiliza na tutautekeleza kabisa kulinda maslahi yetu na kuyaboresha baada ya muda baada ya kuwavutia wengi wakiisha ingia nchini basi tunaweza kukaa nao sasa na kuzungumza kwamba jamani sasa na sisia hebu boresheni maslahi ambayo tunapata ukilinganisha na yale ambayo tulipatana hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni bomba la Mafuta kutoka Dar es Salaam kwenda Mwanza. Hili limezungumziwa na ni mradi ambao kwa kweli ungetusaidia sana kurahisisha usafirishaji wa mafuta kwenda Mwanza, lakini Kampuni ambayo ilikuwa na mradi huu kwa muda wa miaka 18 Waheshimiwa Wabunge inaitwa *AFRICOMMERCE* ni ya wazalendo wenzetu. Miaka 18 mimi nimekuta wana haki hiyo inaitwa *Exclusivity Right* walijopewa tangu siku za Mwalimu Nyerere inaongezwa tu kila mwaka na Wizara yangu inaongezwa tu ikiisha inaongezwa hiyo *Exclusivity Right* ya kuendeleza mradi huo.

Tulipofika mwaka jana tukaona hawa jamaa miaka 18 hawafiki popote tujaribu mwekezaji mwingine, tukatafuta Kampuni nyingine tukawapa siyo miaka 18 ni miezi 18

tu tikawaambia sasa hatumpi mtu muda mrefu sana tunampa muda mfupi mfupi tuona kama anaweza ama hawez.

Mheshimiwa Naibu Spika, hilo tumelifanya kwenye madini vilevile, leseni ya madini ukiipata au ya kutafuta mafuta ina muda ina *life space* ukishindwa tunakunyang'anya au tunapunguza ile sehemu tuliyokupa sasa hawa jamaa wa Bomba la kupeleka mafuta Mwanza baada ya kushindwa tukawapa wengine miezi 18 inaisha Desemba mwaka huu.

Kama hawakuja na *feasibility study* na *right up* nzuri ambayo inaonyesha wana uwezo, fedha zipo na tutanufaika kama Taifa na mradi huu tunawanyang'anya tunampa mwininge, inawezekana tukawarudishia walewale *AFRICOMMERCE* kama wakati huo watakuwa wako tayari.

Lakini tulikuwa tunaambiwa labda Wizara haipendelei wazalendo inawapa hawa wageni. Kwa kweli nia yetu ni kuchangamsha maendeleo tusikalie *resources* ambazo tunaweza kuzigeuza zikatusaidia kujenga uchumi wetu na kupambana na umaskini kwa kupendeleana tu kusema aha! Kwa sababu ni ndugu yetu au ni Mjomba yetu au ni rafiki yetu au ni mdogo wetu. Nadhani tuwe na mtazamo huo ili raslimali zimekuwa hapa tangu Adamu na Hawa walipokuwa hapa kwa hiyo ni wakati sasa wa kuweza kuzigeuza zikaanza kutufanya kazi na kutuletea manufaa katika maisha yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kuhusu huu mchanga unapelekwa nchi za nje. Naomba nirudie tena na Kamati yetu ya Biashara ya Mheshimiwa Shellukindo ilituagiza tuipe maelezo na tukaleta maelezo naamini waliridhika kwa sababu yalikuwa maelezo kwa kweli yanayoonyesha sababu za kuchukua ule mchanga.

Kwanza tuelewane katika kuchimba dhahabu siyo migodi yote siyo maeneo yote yana mashapo au miamba ambayo inafanana, pale Bulyankulu ni peculiar yaani ni kwa aina yake tu, ndiyo maana hata mgodi wa pale ni wa chini. Migodi mingine hapa hapa Tanzania ni ya *Open Cast* kwa sasa hivi lakini dhahabu iliyoko pale imeshikamana na *Copper and Silver* vimeshikamana kabisa huwezi kuvitoa kwa mashine zilizoko pale huwezi kuvitenganisha ni lazima upeleke kwenye mitambo mikubwa ambayo inaghari mu fedha nyingi sana na ipo Japan kwa mfano na sehemu nyingine. Siyo sisi peke yetu tu kuna nchi nyingi ambazo zinapeleka mchanga wao kule kwenda kuchambuliwa ili watenganeshe dhahabu, *copper* au *silver* (fedha).

Mheshimiwa Naibu Spika, wakiisha tenganisha tunajua kabisa ni kiasi gani tuna watu wetu wanaochunguza siyo kwamba wanapeleka tu wenyewe sisi hatujui, kuna *inspectors* wetu wanachunguza na tunaletewa takwimu zinarudi hapa tunapata kodi zetu zote ambazo tunastahili kuzipata na wale wenye mali hizo wanachukua mali yao kama kawaida. Ni *process* kama vile ukienda hospitali wakati mwininge unachukuliwa *specimen* wanakuambia tunaipeleka kwa mfano kwa kule Same Kijiji unaambiwa inapelekwa KCMC au inapelekwa Tanga wanakwenda kuchunguza ni kitu gani, huwezi

kusema mganga yuko hapahapa kwa nini atufanyie hapahapa na panga au na shoka. Lazima iende kwenye vipimo maalum na hii nayo ni kazi ya utaalam na kwa kweli ni lazima ifanyiwe hivyo hakuna cha siri wala hakuna dhuluma wala wizi ambaa unatokea, ni process tu ambayo inafanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, inatusaidia katika kupata dhahabu kwa sababu ya miamba ile ilivyo. Sehemu nyingine migodi ya kule haina matatizo hayo yote ni rahisi kabisa ku – separate dhahabu na ukapata asilimia 90 au 95 *of purity* yaani ya usafi, takataka zile nyingine zikawa ndogo sana ndiyo sababu inakuwa hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kidogo kuhusu kuongeza thamani ya vito. Mheshimiwa William Shellukindo na Kamati yake na Waheshimiwa Wabunge wengine walisema ni wakati umefika sasa tuongeze thamani ya madini yetu hasa vito kama *Tanzanite* ili tuweze kupata ajira na mapato makubwa na fedha nyingi kama Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi hii inaendelea Wizara imeunda *Gem Stone Board* ambayo na taratibu zake na sheria zake na ndiyo itakayoamua jiwe gani la vito kama ni safaya, rubi, *Tanzanite* liingizwe kwenye kundi hilo na baadaye tunazungumza sasa katika Serikali hasa na Waziri wa Fedha kuona kama atatusaidia kutupatia vivutio fulanifulani vyta kuweza kuwavutia wawekezaji waje hapa ambaa watatusaidia kutaka. Mitambo ije hapa kwa bei nafuu kama mlivyokuwa mkuzungumza Waheshimiwa Wabunge kwamba wachimbaji wadogowadogo wasaidiwe sasa kusaidiwa ni pamoja na kuweza kuleta mitambo ya kukata haya mawe, ku – *polish*, kutengeneza *jewellers* hapahapa nchini yote haya ni kuongeza thamani ya madini yetu.

Kwa madini makubwa ya thamani kama dhahabu tunazungumza na wawekezaji sasa hivi tuweze labda kuleta hata *gold refinery* iwe hapa nchini. Sasa hivi dhahabu yetu inapelekwa nje kwenda kusafishwa kule ndiyo tunalipwa pesa, dhahabu inapelekwa ikiwa *semi refined* halafu ikiishasafishwa ndiyo tunalipwa mrahaba wetu na kodi zingine ambazo zinastahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Mheshimiwa William Shellukindo ilizungumzia vilevile kwamba madini ya vito labda tuwakabidhi wananchi tu peke yao yaani wazalendo. Ni hoja nzuri sana, sasa hivi ukifika Melerani utakuta uchimbaji wa wachimbaji wadogo unakuwa mgumu kidogo kwa sababu kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge mmoja kazi hiyo ni rahisi unakwangua juujuu tu kwa kweli sasa wamemaliza kukwangua juu ni lazima uende chini na kwenda chini kwa kucha au beleshi siyo rahisi kwa hiyo, wanaumia wengi sana na wanahitaji msaada wa vitendea kazi vya kisasa ambavyo ni ghali.

Tunakuja kwenye ile *point* yetu Waheshimiwa Wabunge mtusaidie kuwahamasisha wachimbaji wadogo waungane kwenye vikundi vikampuni vidogovidogo ili waweze kwenda Benki wakakope wanunue vifaa waweze kuchimba kwa ufanisi zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, *AFGEM*, au *Tanzanite One*. Ni watu tu *individuals* waliungana walachanga pesa zao kama *share holders* wakaunda kampuni wakakosa sasa wanachimba, wao wanaweza kuchimba kwenda chini zaidi. Kuna kampuni samahani nitataja jina ya Bwana Mengi ambayo inaanza sasa hivi na yeze ni mchimbaji ambaye tunaweza kusema ni mchimbaji mkubwa lakini kuna wengine pale ambayo wako katika hatua hizo vilevile wanapanua shughuli zao, wamejiandikisha *they are registered at companies* na wanakopa wanaweza kufanya kazi hiyokwa ufanisi zaidi. Kwa hiyo wachimbaji wadogo tusiseme waendelee peke yao tu hivihivi ni lazima waungane ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi zaidi na kwa usalama zaidi na kwa faida zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwamba tuwakabidhi kazi hiyo sasa hivi tunasema kwenye vito. Mgeni hawezi kuja akafanya shughuli peke yake ni lazima afanye na Mtanzania kwa hiyo tumeanza tuna mbandika Mtanzania pale polepole kidogokidogo mwisho wake anasimama *on his own* tabu, yetu wengine ni kwamba wanakaa pale siku mbili jamaa kaishiwa au ana shida ya pesa anauza *shares* zake mara moja tu wala haja uvumilivu wa kungoja. Kazi ya kuchimba madini inatakiwa uvumilivu mkubwa sana lakini wengine wana *give up* mapema sana wanakata tamaa kwa hiyo wanunuliwa. Lakini sheria inasema lakini washirikiane na Watanzania.

Hii sera ya uwezeshaji ni sera ya Serikali ambayo sisi tunajaribu sana katika Sekta ya Madini kuihamasisha. Leseni tunawapa Watanzania wengi sana wengi wenu mnaleseni zenu hapa na tunawatafutia wabia ambao wanashirikiana katika kufanya *exploration* na mwisho wake kuchimba madini hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja nyingine ilikuwa nizungumze kwa ujumla ni hii ya *report* ya Dr. Kipokola. *Report* hii mimi namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kuunda Kamati hii mwaka jana kwa sababu kwa kweli imetusaidia sana sisi kule Wizarani na hasa Serikali kwa ujumla.

Hoja zilizokuwepo na wasiwasi na hisia potofu zingine zimeangaliwa vizuri sana na Dr. Kipokola na Timu yake na kama mlivyoona Waheshimiwa Wabunge kwenye *report* ile ambayo tulijjadili hapa wametoa ushauri mzuri sana na ninyi mmeuunga mkono katika sehemu mbalimbali na kama tulivyosema siku ile ya semina tutafuatilia ushauri wao kama Serikali na kuhakikisha kwamba yale ambayo tunaweza kuyatekeleza sasa hivi tunayatekeleza na yale ambayo tunaweza kuyaboresha tuyaboreshe.

Lakini wameondoa ukungu machoni mwetu ambao ulikuwa unatizingira kwa muda mrefu sana hasa hii ya kwamba labda tunaibiwa labda hatuko macho labda wanatudanganya kwa kweli nadhani hoja hizo sasa zimeelezwa vizuri na watu ambao ni *independent* siyo wafanyakazi wa Serikali hasa, walikuwa ni *independent processional*s ambao walifanya kazi hiyo.

Kwa hiyo, nawashauri Waheshimiwa Wabunge tena muingalie tena *report* hiyo na tunakubali ushauri ule kwamba sisi Serikali tufuatilie yale mapendekezo pale na kuyatekeleza yale ambayo yanaweza kutekelezeka ni mengi sana siwezi kuyataja hapa lakini ni ya busara na ni mazuri katika kukuza sekta yetu ya madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja ya *Mafuta House*. Serikali ni moja, ina Wizara nyingi na Mashirika mengi na mara kwa mara utakuta raslimali ya Shirika moja au ya Wizara moja inahamishwa kupelekwa kwingine.

Serikali ina utaratibu wake, Waziri wa Fedha ana mtu anamuita *Treasurer Registrar* ndiye mwenye mali zote zinazoitwa za Serikali kwa hiyo *Treasurer Registrar* Mheshimiwa Waziri wa Fedha akisema leo anataka jengo fulani au chuo fulani kwa manufaa ya Taifa *for the great good of the National* basi Serikali ni hiyo hiyo tunakaa tunaelewana tunakubaliana ili mradi tusiathiri shughuli za yule ambayo ananyang'anywa au anatoa raslimali hiyo.

Sasa mafuta House ilijengwa na *NHC* na *TPDC* walijikongoja na fedha zao, waliweka fedha nyingi sana yote haya ni mashirika ya Serikali 100%, wakafikia mahali wakakwamba kabisa vifaa vinaoza pale, ma – *lift* yapo, *equipment* nyingi lakini wameishiwa na pesa, wakatafuta mbia wa nje na ndani wakakosa tukapiga *report* sisi kama Wizara ambayo ni wajibu wetu tukaenda Serikalini tukasema tusaidiwe na Serikali ikatafuta katika mashirika yake nani ana uwezo wa kuweza kutukwamua *being one family* ni familia moja hiyo hiyo, ikaamuliwa kwamba *NSSF* kwa wakati huo au wakati ule wana fedha ambazo zinaweza kumaliza jengo hilo kwa manufaa ya Taifa zima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sasa uamuzi ukachukuliwa kwamba tuwape lile jengo na wamepewa jengo hilo lakini imekubalika vilevile kwamba *TPDC* kwa sababu jengo lile lilikuwa limesanifiwa kwa matumizi ya *TPDC* kama tunavyoambiwa ghorofa nadhani sehemu ya kwanza chini na ghorofa kama mbili au tatu hivi kuanzia chini zimekuwa *designed specifically for the use of TPDC* yaani kwa kazi za *TPDC* kuweka ramani zao zisioze, data zao na computer zao. Hiyo Serikali imesema *TPDC* waruhusiwe watumie sehemu hiyo ili kazi zao zisikwame hata kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo jinsi gani vitabu vinaandikwa, vitabu vya *TPDC*, *NHC* na vitabu vya *NSSF*, hilo tunamuachia Mheshimiwa Waziri na *Treasurer Registrar* wake wataamua kwa sababu kama nilivyo hiyo inatokea mara kwa mara na yanawazishwa tu kwa kitaaluma katika Serikali bila athari kwa shirika lolote lile.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TPDC* niendelee na *TPDC*, tuliambiwa na Kamati ya Mheshimiwa William Shellukindo kwamba haikupewa fedha za maendeleo, nataka kuendelea na ile dhana ya familia. *TPDC* pamoja na jengo lao hilo na kutafuta mafuta na sasa hivi wanapata *revenue* kidogo kutoka kwenye gesi bado hawana fedha za kutosha, huyu kijana hajaweza kusimama *on his own* lazima apate msaada kutoka Serikalini

tunarudi kwa Waziri wa Fedha sasa hivi tumeelewana kwamba turudi *TPDC* ije na bajeti yake ya ile miradi ya maendeleo. Maana *TPDC* ndiye mtafutaji wa mafuta ambaye leo ametupatia gesi kesho labda atatupatia mafuta ya petroli na kadhalika kwa hiyo miradi yao ya maendeleo ipewe fedha za kutosha na ninadhani Mheshimiwa Waziri wa Fedha amekubali kwamba wakipeleka *specific budget* ya maendeleo watapewa fedha ili shughuli zao ziweze kuendelea. (*Makofi*)

Kwa hiyo, watapata mahali pa kukaa, watapata fedha za maendeleo na hata mishahara ikiwashinda kulipa kwa siku moja kama tulivyokuwa tukifanya siku za nyuma basi tutawapa mishahara kama tulivyokuwa tukifanya. Kwa hiyo *TPDC* tunaipenda kama tunavyopenda mashirika yetu mengine na haikutupwa wala haikudharauliwa wala haikunyanyaswa ni taratibu tu za Serikali ambazo zimetumika katika *transfer* hiyo ya lile jengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dr. Hassy Kitine naomba nikutaje kwamba na wewe umechangia kwa hiyo samahani jina lako kidogo lilidondoka mahali fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika muda nilionao labda nigosie miwili au matatu ya jumla mengine ambayo ni kama tulivyosema lile la Kamati ya Mheshimiwa William Shellukindo hasa kwa wazalendo kupewa kipaumbele katika uchimbaji wa madini wa *Gem Stone* hilo ni ushauri mzuri na tumeshaanza na tutautekeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Ponsiano Nyami alizungumza kwa uchungu sana kuhusu mchanga na nimeelezea sababu zake na niko tayari kuelezea zaidi kama itakuwa lazima. Alizungumzia vilevile kwamba kuna ubaguzi kati ya wachimbaji, wengine tunawapa vivutio vizuri zaidi hawa wakubwa kuliko wachimbaji wadogo siyo kweli.

Wachimbaji wakubwa tunawapa vivutio ambavyo ni *very standard*, Dr. Kipokola amepita nchi zote zinazochimba madini akakuta kwamba vivutio tunavyotoa hapa Tanzania kwa wachimbaji wakubwa ni vilevile ambavyovinatolewa nchi nyingine ili tuweze kushindana vizuri. Lakini wachimbaji wadogo vivutio tunavyowapa na misaada tunayowapa tumeieleza na bado tunaendelea kuiboresha kutegemeana na uwezo wetu kama Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Isaac Cheyo Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kwa upande wangu ilikuwa inahu *MEREMETA*. *MEREMETA* kuacha kununua madini ya dhahabu na kuanza kuchimba huko Kiabakari, Serikali imeandaa utaratibu wa *MEREMETA* kuendelea na zoezi la kununua dhahabu na kutenganisha shughuli za uchimbaji na ununuzi.

Mbona migodi mingine haipeleki mchanga huko Japan, nimeeleza ni kwa sababu ya jiolojia iliyopo pale.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani nimalizie hapo na niwashukuru tena na mimi namshukuru sanasana Ndugu yangu Dr. Ibrahim Msabaha kwa msaada ambao amenipa miaka yote hiyo.

Nawashukuru wakubwa wangu Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa *wonderful gardens* ambayo ametupa sisi ambao tulichomekwa madarakani katika ngazi hizi alitushika vizuri sana na akatulea tukafika hapa tulipo.

Mimi nagombea tena mwaka huu na nitarudi na nikirudi nawataenia ninyi wengine kila la heri na ninyi mrudi, tukirudi bila shaka tutakuwa tunabdalishana vikao mimi nitakaa kule na ninyi wengine mtakaa huko na nitapata raha na ya kumtimua huyo atakayepewa Wizara ya Nishati na Madini. (*Makofî Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru wewe pia na ninawashukuru Waheshimiwa Wabunge na ninawataenia kila la kheri. Naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

(*Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa*)

KAMATI YA MATUMIZI

Matumizi ya Kawaida

Fungu 58 - Wizara ya Nishati na Madini

Kifungu 1001 - *Administration and General* Sh.1,917,423,800/=

MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie mambo miwili, Program ya 18 *sub vote* 101 kifungu cha 250100.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba Mheshimiwa Waziri anisaidie katika maeneo miwili yafuatayo:-

Katika majibu yake hapa sasa hivi ameeleza kwamba *TPDC* wataruhusiwa kutumia sehemu ya jengo la *Mafuta House* ambalo limejengwa kwa ajili ya matumizi ya *TPDC*. Ninachotaka kujua *TPDC* wanapewa eneo hilo kama wapangaji? Wanaazimwa? Au ni mali yao? Hilo moja.

La pili, ni kuhusu biashara ya mafuta ya gesi ya Songosongo. Kazi hii inatakiwa ifanywe na *TPDC* lakini hivi sasa Songas ndiyo wanatoa gesi wao ndiyo wanaauza, wanasantaza, wanakusanya pesa wanapeleka Hazina. *TPDC* hizi pesa hawazioni. Je, ndiyo utaratibu tuliokulaliana? Kama sivyo kwa nini iko hivyo?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kujibu maswali miwili ya Mheshimiwa Mbunge Mohamed Abdulaziz kama ifuatavyo:-

TPDC lile jengo walivyolewana mpaka sasa hivi na sijauona huo mkataba ni kwamba watapewa zile *floor* za ghorofa ambazo wanazihitaji kwa matumizi yao kama Shirika na lakini taratibu zilizoko kama watalipa kodi na ni kiasi gani hizo itabidi nikutafutie Mheshimiwa Mbunge kwa sababu kwa kweli sina hapa nilipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swal la pili, *TPDC* ni *shareholder* katika kuzalisha gesi ya Songsongo na wamewaajiri *PAN Africa* kuwa ndiyo wauzaji wa gesi hiyo na kama *share holder* *TPDC* inapata marupurupu yake malipo yake ambayo inastahili kama mbia mmojawapo katika kampuni hiyo ya kuzalisha gesi.

Kwa hiyo, hiyo ndiyo mikataba iliyopo na ndiyo utaratibu uliopo na mikataba ambayo imetiwa saini, *TPDC* inalipwa haki, Hazina inalipwa kodi zake na wabia wengine wote ambao wana hisa pale wanalipwa mapato yao kufuatana na mikataba iliyopo.

MHE. MOHAMED A. ABDULAZIZ: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naomba Mheshimiwa Waziri sjatosheka bado, kwa sababu nimesema pale mwanzo kwenye hotuba yangu kwamba majengo mengine ambayo watu yaliwashinda kama vile jengo la *NIC* Ubungo walipewa *share*, *TPDC* hawapewi *share* na Serikali ni hii hii moja kama Mheshimiwa Waziri alivyosema na kwamba Serikali ina nia nzuri ya kufanya kila mtu afanye kazi zake vizuri. Pale ziko *towers* tatu, kwa nini Serikali haitaki kuwapa *TPDC* lile jengo liwe *basement* wafanye kazi yao? Lazima wapangishwe? Kupangishwa ni hiari ya mtu. Leo unakwenda, kesho wanakuondoa. Kwa nini Serikali inashindwa kusema kwamba eneo lile sasa hivi ni mali ya *TPDC*? Kuna tatizo gani? Hilo ni moja. (*Makofii*)

La pili, narudia tena kama nilivyosema, kazi ya kuuza gesi ni ya *TPDC*, leo kazi hiyo inafanywa na *Songas*, si *TPDC* kwa nini? Ngoja tuulize vizuri hilo.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na hilo la pili la *Songas*. Kazi ya kuuza gesi siyo ya *TPDC*, kazi ya *TPDC* ni kama mbia, *TPDC* ndiye mwenye *title*, mwenye ile leseni tuseme lakini *TPDC* siyo mtaalam wa kuuza au kufanya biashara ya gesi. Yeye anamiliki sehemu ile ya gesi na anayeaza gesi ni *Pan Africa* siyo *Gongas*. *Songas* kazi yake ni kubadilisha gesi, ndiye mwenye ile mitambo, ndiye anayebadilisha gesi ile iwe umeme ili tuweze kupata umeme ambao tunauza hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kuna wadau wengi sana na wote wana shughuli maalum ambazo zinafanyika pale, kwa hiyo, Mikataba ambayo tumeweka na ni

standard kabisa Kimataifa, siyo kwamba ni *peculiar* kwa sisi wenyewe tu hapa. Ya kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata jibu kwamba *TPDC* hawatapangisha, watakaa bure pale katika jengo lile. Lakini ningependa nimsaidie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba kama nilivyosema shughuli hizi za kubadilishana *assets* katika Taifa letu zinatokea wakati wowote. sisi jengo hili hapa lilikuwa na *Local Government* nadhani tumeruhusiwa sisi kulitumia kama Bunge, ndiyo tumenunua, lakini ni Serikali kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kule Morogoro kilichokuwa Chuo cha *TANESCO* cha kuzalisha umeme, Serikali hii kwa busara zake kwa manufaa ya Taifa hili ikaona tunahitaji Chuo cha kuelimisha Watanzania kingine kipyaa na majengo yale kuyatumia kama Chuo cha *TANESCO* hatuyatumii kikamilifu. Kwa hiyo, kimekabidhiwa kwa *Muslim Development Foundation* ili watoto wetu wasome na Taifa hili liendelee. (*Makofi*)

MHE STEPHEN M. KAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mimi niko kwenye kifungu 58 *program* ya 10 *sub vote* 1001 kifungu kidogo 250100.

Nimechangia kwa maandishi na nimejaribu tu kutoa maoni, ningependa hapa kupata ufanuzi na maelezo ya Waziri mambo ambayo ningependa kuhusiana na suala hili la mchanga kwenda Japan. Ni kwamba mpaka sasa tunafahamu wote kwamba Umoja wa Afrika unapanuka na majukumu yake mengi hapo mwanzo yalikuwa ni suala la kuleta uhuru. Sasa hivi tunakwenda kiuchumi na mambo mengine ambayo yanatusaidia kuwa na *solidarity* kubwa.

Sasa kwenye hili nilitaka kujua kwamba Waziri na Wizara wametumia njia gani kutumia huo Umoja ili tuweze kupata mitambo hii hapa kwa kushirikiana na nchi nyingine ili tuweze kuzishughulikia hizo dhahabu zetu na michanga hapa nchini na nchi nyingine hapa Afrika badala ya kupeleka huko Japan kama wanavyofanya sasa?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumjibu Mheshimiwa Stephen Kazi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri wake Mheshimiwa Mbunge ni mzuri na tunajaribu katika mikutano yetu ya nchi zile ambazo zina madini kuwa na miradi ya aina hiyo lakini kwa kweli hatujafikia hapo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ndiyo tumeanza tu haijafika hata miaka 10 tangu tuanze kuchimba madini kwa dhati na kwa kisasa. Kwa hiyo, tuko katika hatua hizo za kusema sasa tuna madini ya kutosha tuwe na mtambo wetu labda wa kutambua *refine* dhahabu au wa kuchambua huo mchanga ambaao wanaupeleka nchi za nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini niseme kwa sehemu hizi ni sisi peke yetu tu ambaao tuna mgodi wenyewe dhahabu ya aina hiyo kule Bulyanhulu. Kwa hiyo, siyo rahisi

sana kumpata mwingine, labda atakuwa mbali sana na haitakuwa na faida kuanzisha mtambo huo mahali kama hapa. Ni rahisi zaidi kuupeleka kule. Hiyo moja.

Pili, tuisahau Waheshimiwa Wabunge kwamba hii migodi siyosisi tunaochimba pale ni wawekezaji, mtu umemwambia leseni hii hapa, nunua basi sasa ukianza kumwambia tena kwamba alipake rangi ya bluu au rangi nyeusi au atie maji asubuhi na jioni kwa kweli unamwingilia katika kazi zake. Sisi tunachoangalia ni kwamba maslahi yetu yanalindwa. Yeye anachimba kwa kutumia fedha yake, anakwenda kuchambua kule ambako teknolojia ipo na tunamshauri kwamba ukifanya hivi na sisi maslahi yetu yataongezeka na yeye mwenyewe atanufaika. Kwa hiyo, tutaliangalia hilo na ni ushauri mzuri tunaukubali.

MHE. HAROUB SAID MASOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, *Vote 58 Programme 10, Sub-vote 1001*. Mimi kwanza nimefarijika kutokana na jawabu alilolitoa Mheshimiwa Waziri kuhusu jengo la *Mafuta House*. Lakini labda tu nimuulize Mheshimiwa Waziri haya aliyoajibu hapa kutokana na msimamo wa Serikali, *TPDC* hawaelewi hayo? Kwa sababu ninavyoilewa mimi *TPDC* iko chini ya Wizara ya Nishati na Madini labda tu nimkumbushe Mheshimiwa Waziri kwamba katika kikao ambacho kilifanyika katika Ofisi ya Waziri Mkuu kikiwahusisha Wizara ya Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo, Wizara ya Fedha, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi, Wizara ya Nishati na Madini pamoja na viongozi wa Mashirika ya *NSSF*, *TPDC* na *NHC*. Serikali ndipo ilipoamua kukabidhi rasmi mradi huo kwa *NSSF*. Lakini masharti yaliyotoka hapo , (a) *NSSF* ilipe madeni yote ya mradi; (b) iangalie uwezekano wa kuendelea na ushauri pamoja na makandarasi waliopo ili kuharakisha utekelezaji wa mradi; (c) Mradi uanze kutekeleza mara moja. Lakini kubwa zaidi ni kwamba na (d) taratibu za kuhamisha umiliki wa jengo zianze mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri, *TPDC* wanakaidi kuuhamisha wakati hili ni agizo la Serikali, Mawaziri wote walikutana wakakubaliana mbele ya Waziri Mkuu. Sasa je, nani mkubwa baina ya Mawaziri wanne na Waziri Mkuu amba waliona kwa manufaa ya Serikali ifanyike hatua hiyo muhimu. Sasa je, hayo hayaeleweki?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho kabisa Mheshimiwa Waziri amesema haelewi makubaliano ya kuhusu upangaji. Sasa mimi labda si Waziri wala si msaidizi wa Waziri. Lakini najua makubaliano yaliyopita ambayo mpaka sasa hivi *TPDC* hawajakubali kuweka saini yao kuhusu makabidhiano hayo imeamuliwa mbele ya washauri na wakaguzi kwamba eneo lile la *ku-stock* vitu vyao muhimu wapewe bure milele na milele. Sasa je, Mheshimiwa Waziri tupe maelezo ya kina?

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa maelezo yake sijui ameyapata wapi. Lakini ukweli ndiyo huo kwamba *TPDC* wameruhusiwa kutumia pale mahali bure na hii ndiyo *position* niliyopewa sasa hivi hapa.

La pili, kusema kwamba wamekaidi Serikalini, Shirika haliwezi kukaidi amri ya Waziri na Waziri hawezi kukaidi kauli ya Waziri Mkuu. Kwa hiyo, hilo nakanusha kabisa *TPDC* wako hapa waonyeshe mkono kama walikataa ili tuwape tiketi zao za kurudi nyumbani. Hilo na Mheshimiwa Mbunge nakuhakikishia kwamba hawawezi kukaidi amri ambayo imetolewa na Serikali na watatii ili shughuli ziweze kuendelea na kukabidhiana kutafuata taratibu ambazo zimebekwa za kisheria na Serikali. (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Haroub Said Masoud, nimepewa na *ki-note* hapa kwamba *u-declare interest* fulani.

MHE. HAROUB SAID MASOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi nataka nimwambie tu Mheshimiwa Waziri kwamba nadhani huu ni wakati wa ukweli na uwazi. Mimi nilikopata nimepata ni Mjumbe wa Bodi ya *NSSF* kama ilivyokuwa humu ndani wamo vile vile Wajumbe wa Bodi ya *TPDC*. Sasa kinachosikitisha inaonyesha *TPDC* hawataki kuwaeleza Bodi yao ukweli na uwazi na ndiyo maana hata Mheshimiwa Waziri hakuelewa kitu hapo. Kweli hakiwezi kuwa chombo kama kile kinaidanganya Kamati ya Bunge ambayo ni ya Miundombinu badala ya kuwambia ukweli inapotosha umma. Hii ni aibu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, labda ninachotaka kujuu tu Mheshimiwa Waziri kasema miliki itafanywa, haraka lini? (*Makofi*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri nadhani ameleeza amepataje hiyo habari.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa maelezo hayo na mimi ahadi yangu ni kwamba tukitoka hapa tutawaagiza *TPDC* na *NSSF*, Waziri wa Kazi, Maendeleo ya Vijana na Michezo yupo hapa shughuli hii imalizike mapema iwezekanavyo ili tuendelee na kazi yetu ya kuendesha Mashirika yetu.

MWENYEKITI: Najaribu ku-*balance* Kusini, Kaskazini, Zanzibar na Kanda ya Katii. (*Kicheko*)

MHE. JOB Y. NDUGAI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuikumbuka Kanda ya Katii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni pale pale *vote 58 programme 10, sub vote 1001*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimpongeze kwanza Mheshimiwa Waziri kwa maelezo mazuri sana aliyojatoa yameondoa maswali yangu mengi sana. Mteja wa *TANESCO* akitaka kuvuta umeme akalazimika kutumia nguzo mbili, tatu kutoka pale alipo na pale *line* ilipoishia analazimika kwa taratibu za sasa za *TANESCO* kulipia nguzo, kulipia waya, kulipia vikombe na hili linakwenda kwenye huduma za vijiji vyetu huko, wana kisima chao cha maji ni karibu na huduma ya umeme inapopita, lakini wanaambiwa nguzo tatu, nne hivi kwa hiyo watalipia nguzo, watalipia waya, watalipia vikombe, watalipia vibarua watakaofanya kazi hiyo na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuliahidiwa kwamba *Net Group Solutions* ikija kutakuwa na maboresho makubwa sana ya *TANESCO*. Ni kwa nini *TANESCO* inafika mahali pa kuwatapeli wananchi kiasi hicho wanalipia fedha zote na vifaa vyote hivyo, halafu mali zote hizo zinabaki tena kuwa mali za *TANESCO*.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu hoja ya Mheshimiwa Job Ndugai, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, *TANESCO* haipaswi kuwatapeli wananchi na kwa mujibu wa tunavyojua sisi hawawatapeli. Lakini kama Mheshimiwa Mbunge ana taarifa mahsus kama ambavyo amezisema hapa nataka nimhakikishie tu kwamba tutakuwa tayari kuzifuatilia kwa karibu.

Lakini nataka nieleza jambo moja kuhusu usambazaji wa umeme. Kwa kawaida *TANESCO* wanafikisha umeme kwenye maeneo mbalimbali kama ambavyo nimesema kwa ufupi wakati nachangia mchango wangu hapa. Kama ni mradi fulani ambao wao wanalipia gharama zote. Lakini kutohana na hali mbaya ya kifedha katika miaka mitatu iliyopita kutohana na ukame haikuwezekana kuendelea na utaratibu huo na katika maeneo ambayo hawana mradi mahsus kama mteja anahitaji kufikishiwa umeme kwa haraka basi wanamtaka mteja yule alipie gharama zile ambazo katika hali ya kawaida zingechukuliwa na *TANESCO* kwa maana ya kuchangiwa na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika utaratibu huu wa kufikisha umeme kwa wateja Serikali inatoa ruzuku ya aina fulani kwa *TANESCO* hatulipi gharama halisi. Lakini kama mteja anahitaji umeme katika maeneo ambayo *TANESCO* haina mradi wa aina hiyo inabidi achangie. Sasa huo ndiyo mchango ambao sisi tunaufahamu na ili kupunguza matatizo kwa wateja wameweka utaratibu pia hata wa kulipia kwa awamu gharama zile ambazo wanatakiwa walipe ili kuweza kutoa unafuu wa aina fulani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kama nilivyosema awali anayoyasema Mheshimiwa Mbunge yeze hawesi kuwa amesimama tu akazungumza, kwa mambo ambayo ameyazungumza hapa tuko tayari kuzungumza naye mara ya kikao hiki tuone namna gani ya kusawazisha baadhi ya mambo.

MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Mimi niko kwenye *Vote 58, sub-vote 1001*, lakini kwa kuwa Mheshimiwa Daniel Yona ni kaka yangu sitaki kushika mshahara wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa nataka nifuatilie hili suala la kulipia umeme kwa awamu kwamba ilitangazwa na tukaona katika maeneo ya vijiji ambapo watu mapato yao ni madogo ilikuwa ni mwanya wa kuwawezesha kuunganisha umeme. Lakini wale waliolipa pale mwanzoni baadaye wameambiwa hawawezi kufungiwa umeme mpaka wawe wamelipa kiasi chote. Sasa nilikuwa nataka njue hivi ule utaratibu wa kulipa kwa awamu umefutwa au ni ukaidi tu wa *TANESCO* wa kutofauta maagizo ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, nilikuwa na *interest* kidogo sasa hili sikuliona vizuri kwenye bajeti. Mwaka jana mwezi Aprili, tulifanya marekebisho ya bajeti ya Serikali tukaajiri *Auditors* katika migodi ya madini ili tuweze kupata ukweli wa uzalishaji pamoja na mauzo ya madini kwa jumla. Sasa kwa kuwa *Auditors* wale ni ghali kidogo, ingekuwa ni vizuri tujue wamefanya kazi kwa kiasi gani na wametusaidia kwa kiasi gani ili tuweze kusema kwamba ile gharama ya kuwaajiri ilikuwa sawa kwamba kwa ajili yao tunapata mapato ya ziada ya kuhakikisha kwamba kuwaajiri ni faida kwetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la tatu, ambalo limenifanya nisimame labda wakati wake ulikuwa bado linahusu *IPTL* mchango wetu wa kubadilisha mfumo ule kama hao watu tunawalipa fedha bilioni 3.6 kwa mwezi. Inakuwaje tena sisi ndiyo tunaochukua jukumu la kununua mitambo na kubadilisha utaratibu na kulipa shilingi bilioni 60 also kwa ajili hiyo. Nilikuwa nataka nipate maelezo tu ili iniondolee maswali mengi kichwani kwangu. (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu maswali matatu ya Mheshimiwa Profesa Jumanne Maghembe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la kulipia umeme kwa awamu ni maagizo ambayo tayari yaliishachapishwa kwenye magazeti na kutangazwa kwenye vyombo vya habari. Ni kweli kwamba katika baadhi ya maeneo *Regional Managers* au *District Managers* hawakufuata kikamilifu maagizo hayo ninao mfano ambao mimi mwenyewe niliyatemebelea na nikapewa mfano huo. Tuliwaagiza Wakuu wa *TANESCO* wafuatilie na kwa mujibu wa taarifa wanazozitoa hivi sasa tutawaagiza sasa hivi wafuatilie hayo uliyoyasema ili tuhakikishe kwamba wananchi wanapata unafuu ambao Serikali ilitarajia wataupata kuhusu kulipia kufungiwa umeme kwa awamu ama tatu au 12 kwa maana ya miezi 12 katika mwaka mmoja. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu wakaguzi wa migodi. Napenda niseme tu kwamba bado hawajakamilisha kazi na watakopokamilisha nadhani tutaweza kupata faida ya kujua hali jinsi ilivyo katika migodi hiyo na imechelewa kidogo kwa sababu walipoanza walikumbana na matatizo ya kukataliwa na baadhi ya migodi hiyo na Serikali ilibidi iingilie kati kuhakikisha kwamba wanafanya kazi waliyotumwa na Serikali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, kuhusu *IPTL* kwanza kwa maana ya mahesabu mahsusni karibu shilingi bilioni 3 kwa maana ni shilingi bilioni 2.6 kwa mwezi kama *capacity charge*. Lakini la msingi ni lile nililolisema mwanzo wakati nachangia hapa kwamba Serikali imeamua kutafuta kila njia kuhakikisha kwamba mitambo hii inanunuliwa kuondokana na matatizo hayo ambayo ni mengi yaliyotokana na aina ya Mkataba wenyewe. Sasa nadhani kutokana na hali hiyo inaonekana kama ndiyo mtindo wa hizi Kampuni za binafsi za uzalishaji umeme katika maeneo mengi. Tumehudhuria mikutano mingi sana ya Mawaziri wa Nishati, lakini mahali ambapo wameingia hizi *IPPs* matatizo yanafanana uwekezaji kwenye sekta ya Nishati hususan umeme kama haya.

MHE. EDSON M. HALINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niulize maswali kwa Mheshimiwa Waziri kama mawili hivi.

La kwanza, mwaka jana niliuliza swali kwa nini umeme haujapelekwa Iyula, walnidanganya humu humu Bungeni kwamba tukimaliza Bunge nikirudi nyumbani nitakuta umeme tayari, matokeo yake nimekwenda nguzo zile zote zimeungua. Nimekaa nimekuja tena huku wakasimika nguzo. Lakini wakati wa kikao cha bajeti mwaka jana niliambiwa wewe sasa hivi kila kitu kipo kule itakamilika mwezi wa Oktoba. Lakini mpaka leo hakuna jibu na Mheshimiwa Waziri hajasema lolote. Sasa kudanganya Bungeni namna hii ni kudhalilisha Bunge na kutokuheshimu Serikali. Nataka wanieleze hivi wana maana gani kulidhalilisha Bunge au Serikali? Hilo la kwanza. (*Makofi*)

La pili, kuna watu wanatoka huko na vibali vya kutafuta madini wanafika tu wanaanza kung'oa mawe na kung'oa mazao ya watu na hili limetokea Maloji huko kwenye Mlima Ngamba na Mheshimiwa Waziri ana habari na hata Serikali imepata maelezo hayo kutoka kwa Mkuu wa Wilaya, lakin hayazungumzwi hayo. Wale watu sasa wahamie wapi bila kuzingatia utaratibu kama si kusababisha vurugu. Sasa waniambie wale watu watawapatia maeneo wapi?

MBUNGE FULANI: Wawalipe!

MHE. EDSON M. HALINGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ndiyo hilo nilitaka anijibu kwa kuwa Mheshimiwa Waziri ana habari yote na tulikwishazungumza analielewa, atoe maelezo ya kueleweka na wale watu wajue ni nini kinachotakiwa kufanyika sasa.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini, naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Edson Halinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Edson Halinga kwamba kauli au ahadi ambazo zimekuwa zikitolewa hapo nyuma kuhusu mradi wake ambao amekuwa akiufatilia kwa makini sana hazikuwa kauli au ahadi za hadaa. Tukitoa kauli au ahadi tunaitoa kutokana na taarifa ambazo tunazipata na kulingana na hali ya kifedha na upatikanaji wa vifaa kwa wakati ule. Lakini kama ilivyo Waswahili wanasema jitihada haishindi kudra. Kwamba unaweza ukatoa ahadi hiyo, lakin pakatokea mambo ambayo yakasababisha miradi ama mmoja au mingine ikasimama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyoeleza mwanzo kwa kweli tatizo kubwa la mradi wa Mheshimiwa Mbunge ni vifaa ambavyo *TANESCO* watavipata mara hali yao itakavyokuwa kidogo afadhali kutokana na ukame iliyotokea. Lakini si hivyo tu tulichofanya ni kwamba baada ya kupata mradi huu wa *ERT* ambao tunataraja kufadhiliwa na Benki ya Dunia. Miradi mingi hiyo ambayo imesimama na Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia ama zimewekwa nguzo tu hazijafungwa waya au mahali pengine kumechimbwa mashimo tu na kadhalika, miradi hii mingi imeingizwa katika mpango huo. Katika awamu ya kwanza karibuni Mikoa yote imehusishwa katika mradi huo wa *ERT*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Edson Halinga kwamba kwa kweli hatukumuahidi au hatukufutilia suala hili kwa mzaha mzaha tu hapana, tulilifanya kwa dhati. Lakini kama nilivyosema kutokana na hali ilivyojitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vibali vya madini na matatizo ya uharibifu wa mazingira ambayo ameyataja hapa ni kweli amewasilisha kwetu na sisi tumemwaagiza Afisa Kanda wa Madini afuutilie suala hilo mara moja na kuchukua hatua. Kwa hiyo, naamini katika muda mfupi ujao tutamfahamisha Mheshimiwa Edson Halinga hatua ambazo zitakuwa zimeishachukuliwa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, nimekuona sasa ulikuwa unasemaje, unaongezea jibu au! (*Kicheko*)

MHE. DR. HASSY H. B. KITINE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka kusema hivi, hiyo *concern* aliyoonyesha Mheshimiwa Edson Halinga ya wawekezaji katika Sekta ya Madini wanaokuja kufanya *exploration* na *search*. Tatizo siyo kwa Mheshimiwa Edson Halinga tu wanakuja wakitoka Dar es salaam wanapitiliza moja kwa moja mpaka kwenye sehemu wanazofanya kazi. Hakuna *DC* wala Mkuu wa Mkoa anayefahamu. Kwa hiyo, wananchi wanaauliza kwa mfano, Makete wameliniuliza mimi wanakuja wazungu hao wanafanya *exploration* wameniuliza mara nyingi wananchi ninashindwa kujibu kwa maana na *DC* anashindwa kujibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani Mheshimiwa Waziri au Naibu Waziri wajibu kwa maana ya nchi nzima. Sasa sijui kama wenzangu wana tatizo hilo vile vile. Ahsante.

MWENYEKITI: Ahsante sana, sasa namwita Mheshimiwa Raynald Mrope.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuonyesha *concern* yangu juu ya Wizara hii. Toka mwanzo kabisa niseme nina masikitiko makubwa dhidi ya Wizara hii kwa sababu kauli inazozitoa si kauli, si chochote, ni uongo tu mara kwa mara. Nasema hivyo kwa sababu mimi tarehe ...! (*Kicheko*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mbunge naomba ukae. Nadhani unaelewa kanuni kwa muda mrefu na wewe ni Mbunge wa siku nyingi. Kwa hiyo, hilo neno la uongo nadhani unajua haliruhuswi.

MHE. RAYNALD A. MROPE: Mheshimiwa Mwenyekiti, limefutwa. (*Makofifi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba tarehe 6 Agosti, 2003 Mheshimiwa Waziri aliahidi ndani ya Bunge hili kutokana na hoja binafsi niliyoitao tarehe 4 Agosti, 2003 kwamba angefikisha umeme katika vijiji vya Mwena, Chikundi, Chigugu, Chikukwe, Namakongwa na kadhalika. Naomba ninukuu alisema hivi: "Mheshimiwa Spika, nafurahia kumuarifu Mheshimiwa Mbunge kuwa miradi hii itakayogharimu kiasi cha

shilingi milioni 84 kinatarajiwa kutekelezwa katika kipindi cha mwaka 2003/2004.” Akapigiwa na Makofi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya hapo akaahidi kwamba atafikisha umeme toka Ndanda, Nagoho na Naganga kwa gharama ya shilingi milioni 660. Na hiyo ilipangiwu kufanyika katika bajeti ya Serikali ya mwaka 2004/2005 na kuendelea 2005/2006 akapigiwa makofi. Sasa mpaka leo kazi hii na ukweli kwake uko wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nashindwa kuelewa kauli inayotolewa humu Bungeni na Mawaziri maana yake ni nini? Ikiwa hili halijatekelezwa mpaka sasa. Wametekeleza kidogo kwa kuleta *transformers* katika vijiji hivyo lakini baada ya hapo hakuna kitu. Mimi nimekwenda ofisini kwao mara nyingi, nimekutana na *Regional Manager* nimweleza mpaka leo hakuna lolote lililotokea. Hili tatizo tulilifikisha na tukawa na mkutano mbele ya Waziri Mkuu. Halafu Mheshimiwa Waziri akaja akatoa kauli humu ndani ya Bunge halitekelezwi. Sasa mimi nimweleweje na wananchi wangu wa Masasi wamwelewe namna gani? Sasa naomba hili alieleze kiuwazi.

(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ni ya kwake muda wa kusema katika kipindi hiki ni dakika tano, tano. Kwa hiyo ni ya kwake. Sasa Mheshimiwa Waziri toa ufanuzi kwa hili na lile lingine la Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, alilolisema la ujumla ujumla.

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nianze na kujibu ushauri ambao Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, alioutoa kuhusu wachimbaji ambao wanakwenda tu na kuanza kufanya kazi. Lakini nianze labda na kumhakikishia Mheshimiwa Edson Halinga, nashukuru ameridhika kumwambia kwamba tumechukua hatua, tumetoa kitu kinachoitwa *default notice* kwa wale ambao tunawafikiria hawastahili kuwa pale ili wajieleze vizuri na huo ndiyo utaratibu tuliowekewa na sheria zetu.

Kwa hiyo, hatukulikalia kimya Mheshimiwa Edson Halinga, tumechukua hatua hiyo na siku zikishaisha zile za ile *notice* basi tutachukua hatua ifuatayo ikiwa ni pamoa na kuwanyang’anya wale waliopo tuwape wale ambao wanastahili kuwapo pale. Ndiyo hatua ambazo tunachukua Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, kwa wale ambao wanaingilia maeneo bila kufuata taratibu au hawatimizi masharti ambayo yanakuja pamoa na leseni tunazozitoa ni kwa nchi nzima tunafanya hivyo. *Zone Managers* wako pale kila mnapowaona watu wa aina hiyo tunaomba muwaarifu wale *Zone Managers* ili sisi Makao Makuu tuweze kulifanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa kumjibu Mheshimiwa rafiki yangu Mheshimiwa Raynald Mrope, mimi sitarudia lugha yake aliyotumia, lakini kwa kweli sisi hatudanganyi na yeye mwenyewe kama ukisikiliza alivyoninukuu tumetumia neno kutarajia, hakuna hata siku moja mimi kama Waziri nitasema nitapeleka umeme kesho

mahali fulani. Kwa sababu kwanza sina fedha hizo, pili, siyo kazi yangu mimi peke yangu ni kazi yangu labda mimi na Shirika la *TANESCO* au Serikali zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kwa kweli sijatoa ahadi ya kusema tutafikisha umeme kwenye viji vyake tarehe fulani, tarehe fulani tunachosema tunatarajia kwa sababu ni fedha ambazo aidha, tunaomba au tunapata kwenye bajeti na sina uhakika nazo kwa hiyo siwezi kutoa ahadi ambayo ni *categorical* au mia kwa mia kama Mheshimiwa Mbunge alivyosema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wapiga kura wake mimi naomba nimsaidie tu kwamba Mheshimiwa Raynald Mrope, anawatetea wapiga kura wake sana na amefanikiwa katika viji vyake ambavyo vilikuwa havijapata umeme tumeanza kufikisha ma-transformer na kwa hiyo kwa kweli ni Mbunge hodari arudishwe ili amalize kazi hiyo katika kipindi cha miaka mitano ijayo. (*Makofî/Kicheko*)

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MWENYEKITI: Kuhusu utaratibu.

MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO: Mheshimiwa Mwenyekiti, samahani kuhusu utaratibu chini ya Kanuni 55 natumia Kanuni ya 50 mambo yasiyoruhusiwa kusemwa Bungeni.

Wakati Mheshimiwa Haroub Said Masoud anatoa hoja yake alitoa kauli kwamba Kamati ya Miundombinu imedanganywa na watendaji wa *TPDC*. Kamati iliyoshughulikia suala hili ni Kamati ya Uwekezaji na Biashara na hatukudanganywa kama ni ushahidi wa kudanganywa aseme.

Kamati yetu imesema haikubaliani na utaratibu uliotumiwa na Serikali kutoa imani bure. Hatukusema Serikali inyang'anye *NSSF*. Tumetoa maelezo kwamba *NSSF* ni Shirika la watu wachache 360,000 si vizuri na si halali kuwakabidhi mali ya watu 35,000,000 na kwamba haitoi gawio kwa Serikali ni mali ya watu binafsi. Kwa hiyo, ni uamuzi wa Kamati hatukudanganya. Kama ana ushahidi wa kudanganywa basi tupate ushahidi. (*Makofî*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ni kweli Kanuni aliyoisema inazuia kusema mambo ambayo huna ushahidi nayo. Lakini niseme tu kwa hili siamini kama alikuwa na nia ya kuwdhalilisha wanakamati ile. Pengine alitaka *ku-emphasis* tu kwamba pengine walichoambiwa kule kwa kadri anavyojua yeye hayakuwa sahihi. Sasa sijui Mheshimiwa Haroub Said Masoud, kama una lolote la kusema.

MHE. HAROUB SAID MASOUD: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niseme tu kama Mheshimiwa aliyetoa hoja hiyo anasema kwamba kauli niliyoitumia mimi sio sahihi, basi mimi nasema *TPDC* wamesema kweli na kweli tupu. Lakini kwa nini wasiwaambie kwamba jengo lile eneo walilokubaliana wamepewa bure milele na

haikutamkwa hata na Waziri hapa isipokuwa hoja hiyo nilitoa mimi. Kwa hivyo, kama ni hayo basi nasema wamesema kweli na ukweli mtupu Serikali ina maamuzi yake. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Hoja hiyo ilishapita niliruhusu ili kupumua watu tu. Mheshimiwa Oscar Mloka, amesharidhika, sasa Mheshimiwa Lucas Selelii, wote mtapata nafasi na wote nimewaweka mmalizie ili mtroe hoja zenu zote. (*Makofi*)

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nimechangia kwa maandishi katika hoja ya Waziri wa Nishati na Madini. Nina mambo mawili. Pamoja na Mheshimiwa Stephen Kazi kuridhika juu ya kusafirisha mchanga Japan. Lakini mchanga ni madini na sheria inaruhusu Halmashauri za Mji na Wilaya kukusanya kodi ambayo inatokana na zao la mchanga. Sasa je, ada ya kufanya hivyo wanavyofanya Halmashauri ya Mji au Halmashauri ya Wilaya ya Kahama inalipwa fedha kiasi gani kutokana na mchanga huu kwa sababu ni pato halali la Halmashauri? (*Makofi*)

La pili, muda wote toka mwaka 1998 wakati tunapitisha Sheria ya Madini, Wabunge tunaotoka kwenye maeneo ya madini tulipinga juu ya Serikali kufanya mrabaha wa asilimia 3 kwa asilimia 5 kwa almasi. Muda wote Serikali wamekuwa wanang'ang'ania kwamba dunia nzima inafanya hivyo. Lakini tunazo habari za uhakika kwamba sehemu zingine mrabaha unafika hadi asilimia 10, 13 na kuendelea. Tunazo habari za uhakika kwamba katika maeneo mengine sehemu ya pato la fedha za mrabaha hulipwa Halmashauri zinazohusika katika maeneo ya madini. Je, ni lini sasa Serikali ya Tanzania itafikia kuziwezesha Halmashauri zinazotokana na madini kufikia kulipwa fedha ambazo zinatokana na madini kwa mrabaha na ni lini Serikali itaamua kuanza kufikiria upya mikataba mbalimbali ambayo imeingia na wachimbaji kupandisha ili hiyo raslimali iliyopo ardhini iweze kutufaidisha sisi wote kama Taifa? Ahsante.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Lucas Selelii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani tunaita mchanga kwa sababu ya ukosefu wa jina bora zaidi, pengine nitumie neno la Kiingereza. Kinachosafirishwa pale ni *copper concentrate*. Si mchanga kama mchanga wa barabarani ambao Halmashauri zetu wanatoza ushuru kama wanavyoweza. Hilo la kwanza.

Lakini la pili, kama hoja ni suala la Halmashauri kupata mapato fulani. Wakati nachangia ni wazi kwamba kuna mgongano wa aina fulani baina ya sheria zetu hizi na mikataba hii na ni jambo ambalo limefahamika. Alipokuwa anatoa Mheshimiwa Kabuzi Rwilomba, mfano wa dola laki mbili na tukasema kwamba kutokana na hali hiyo nadhani kuna mgongano wa aina fulani baina ya sheria zetu za ulipaji kodi na hii mikataba. Tukasema wakati wa kusawazisha mambo haya basi itawezekana pengine Halmashauri zetu zitapata chochote kutokana na fedha hizi ambazo zimeahidiwa katika baadhi ya mikataba.

Lakini sio hilo tu, kuhusu mrabaha na kwamba sehemu nyingine au nchi nyingine zinalipwa kwenye Halmashauri. Mimi nadhani inategemea na mfumo wa Serikali na mfumo wa utawala wa nchi. Hapa sisi katika kujenga umoja wa Kitaifa tunao utaratibu na mfumo wa makusanyo ya mapato katika sehemu moja au kuweka katika chungu kimoja na baadaye kugawa kwa mujibu wa mipango ya maendeleo ya mwaka hadi mwaka, kama inavyopitishwa na Bunge hili Tukufu kwa sehemu mbalimbali.

Sasa hii haiondoi hoja ya maeneo ya uchimbaji wa madini kwamba yapate kipaumbele mahsusui au uharibifu wa mazingira katika maeneo yale lazima yatiliwe maanani. Lakini ndiyo maana basi Serikali ikaunda Kamati ya suala zima la madini ambayo tumeipitia sisi hapa taarifa yake na ndiyo maana Serikali imeahidi kwamba itafanya kazi taarifa hii kikamilifu.

MHE. LUCAS L. SELELII: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. Namshukuru Naibu Waziri kwa kujibu kwa niaba. Mimi sijaauliza kwa niaba kwa nini asijibu Waziri mwenyewe? (*Makofî/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu mchanga ninaosema na *copper* huo ni mgodi wa dhahabu. Katika dhahabu kuna aina nyingi za udongo pamoja na mchanga pamoja na *copper concentrate* aliyoisema. Kwa nini sasa hata hiyo *copper concentrate* isiwekewe na yenyewe mrabaha ili tuweze kupata fedha kwa fedha ambazo tunakwenda kuzikusanya.

Lakini la pili, ni hili la mrabaha. Tunakubali kwamba Serikali inapata mrabaha lakini Serikali hiyo hiyo inaruhusu wachimbaji watoe wakitaka fedha kwa ajili ya maendeleo. Kwa nini isiwekwe sheria ikawalazimisha basi walau wakaingia kwa kiwango fulani cha fedha, fedha za maendeleo kuliko kufanya wanavyotaka, wakitaka au wasipende ili iwe ni lazima kisheria. Mimi naomba jibu Waziri mwenyewe. (*Makofî*)

MWENYEKITU: Ahsante. Mheshimiwa Mbunge nadhani mimi nimeichukua kama utani kati ya Mnyamwezi na Msukuma na Mzaramo. Lakini anayo haki ya yeye kujibu ningeshangaa angekuja Katibu Mkuu kujibu, pale asingeruhusiwa, lakini hawa wawili yoyote anaruhusiwa. (*Makofî*)

Sasa kama Mheshimiwa Naibu Waziri ungependa kuendelea wewe endelea tu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri napenda nijibu maswali ya Mheshimiwa Lucas Selelii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu *copper concentrate* labda nitumie neno hilo au mchanga kwa ajili ya wananchi wetu kutuelewa vizuri. Mchanga wa dhahabu unaosafirishwa nje na Mheshimiwa Mbunge anasema kila kitu pale kilipiwe mrabaha wake. Nataka nimfahamishe tu kwamba katika taarifa ambayo tumeiwasilisha kwenye Kamati ya Uwekezaji na Biashara tunesema wazi juu ya faida inayopatikana ya kifedha kutokana na uchambuzi unaofanywa huko nje kwenye *smelt* ambayo imepelekwa au

kwenye kinu cha kuchambulia na fedha ambazo zinapatikana na ndiyo maana basi Kamati ile ikaridhika na taarifa ambayo Serikali imetoa.

Mimi nadhani kwa kumsaidia Mheshimiwa Mbunge na mtani wangu Mheshimiwa Lucas Selelii, labda baada ya hapa tumpatie nakala ya taarifa ile ambayo tumeiwasilisha kwenye Kamati ambayo ina maelezo ya kina zaidi ili aweze kuyafahamu. Lakini kila kitu kinachokwenda kuchambuliwa malipo yanapatikana kwa Serikali kutokana na kazi hiyo kubwa inayofanywa huko nje.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala la maendeleo. Mara nyingi tumejibu swalii hapa Bungeni tukionyesha miradi inayotekelizwa katika maeneo mbalimbali ya migodi. Tukawa tunatoa mpaka takwimu za thamani na tumetembelea katika baadhi ya maeneo haya hatujasema kwamba inatosheleza. Kutokana na hilo kwamba Serikali au Wizara ikatoa maelekezo mahsusii kwenye Makampuni haya kwamba washirikiane na Halmashauri kila mwaka waulize Halmashauri kipaumbele chao ni nini na kutokana na kipaumbele ambayo Halmashauri inatoa wao wachangie kipaumbele kinachotolewa na Halmashauri hata kama maana yake ni wao wenye kusimamia miradi wao wenye ili mradi itekelezwe kutokana na mahitaji ya Halmashauri. Katika maeneo mengi haya yamekuwa yakifanyika lakini nirejee kusema yale ambayo nimesema mwanzo kwamba kwa kweli suala zima hili la uboreshaji wa maeneo ya migodi ya madini haya ndilo moja ya mambo ambayo yalitazamwa katika taarifa hii iliyokusanywa ya Dr. Kipokola na kama tulivyosema Serikali itafanya kazi.

MWENYEKITI: Ahsante, ninao wawili bado. Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni na Mheshimiwa Leonard Derefa. Kwa hiyo, naanza na Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni.

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi niko *vote 58 sub vote 1001*, mshahara wa Waziri na hasa Naibu Waziri Mheshimiwa Dr. Ibrahim Msabaha. (*Makofii/Kicheko*)

Mimi nimechangia kwa maandishi lakini nilipenda tu kujua kwamba baada ya kuwa tumeona asubuhi kwenye vyombo vya habari kwamba hii hotuba ilitolewa mapema tukadhani kwenye kitabu kutakuwa na takwimu za miradi ambayo inaendelea. Lakini bahati mbaya miradi yote ya umeme inayoendelea haikuonyeshwa kwenye kitabu hiki cha Mheshimiwa Waziri. Nilitaka tu kuhakikishiwa kwamba kuna miradi ya umeme wa kutoka Lamadi kwenda Nyashimo na kutoka Nyashimo kwenda Shigala na kutoka Lamadi kwenda *Mkula Hospital* kwenda *Mbangasamo ginnery*. Je, hii miradi ni sehemu ya hoja ya Mheshimiwa Waziri au iko wapi? Kwa sababu sikuiona kwenye hotuba yake hapa.

La pili, nilitaka tu kujua ni kwamba kuhusu bei za umeme kweli ni ghali sana na matazamio ya Watanzania wengi ni kwamba baada ya kuwe *Net Group Solution* imepewa kazi basi ingesaidia sana kuboresha pamoja na kupunguza gharama za umeme. Lakini mpaka sasa hivi gharama hizi hata kwenye kitabu cha Mheshimiwa Waziri hapa ziko (*on the higher side*) zimezidi kupanda juu. Sasa sielewi faida ya ufanisi wa Shirika

la *Net Group Solution*. Labda ni vyema Mheshimiwa Waziri akaelezea tu kwamba hawa wataendelea kuwepo hapa kwa muda gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu ni suala la migodi. Tumekuwa na migodi tunahodhi migodi ile lakini migodi tunawapa wawekezaji kwa asilimia mia kwa mia. Wakati tukienda Ghana, Serikali ya Ghana ina asilimia 20 *golden share*. Maamuzi yote muhimu sana lazima Serikali iyabariki. Sisi tunatoa migodi yote bure. Sasa hoja inakuja ni kwamba je, si muda muafaka tukajaribu kuliangalia hili na hasa naangalia katika angle ambayo Mheshimiwa Mwenyekiti tunapouza migodi hii wanapouza wawekezaji hawa wakiuja ile mambo ya *stamp duty* au namna gani Serikali haipati hata senti tano. Leo mtu amewekeza kwenye mgodi labda dola 150,000,000 akaiza mgodi ule kwa dola labda 300,000,000 Serikali haipati hata senti tano kwa sababu mauzo yanafanyika nje ya nchi na hao watu wanakuwa kwenye *stock exchange*. Sasa sielewi nchi inafaidika nini katika hili. Ningependa kupata majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini kwa sababu Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni ametaja na mshahara wangu mahsus, basi naona bora niharakishe kujibu kabla hajaninyang'anya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu miradi inayoendelea niseme tu kwamba isingewezekana kwa Mheshimiwa Waziri kuitaja yote katika kitabu. Namuahidi kwamba ni sehemu ya hotuba yake. Kama nilivyokuwa nimesema hapo awali maeneo mengi ambayo miradi iliyoanza hakikukamilika au ambayo imepangwa yameingizwa katika utaratibu wa *ERT*. Hiyo ni kuhusu miradi ambayo ameizungumzia Mheshimiwa Mbunge.

Pili, kweli ukilinganisha na hali ya wananchi wetu gharama za umeme ni kubwa. Lakini ukilinganisha na nchi zingine kama ambavyo Mheshimiwa Waziri ametoa hapa takwimu wakati anatoa mchango wake tunakaribiana karibiana hasa kwenye upande wa viwanda na sisi tuna unafuu kwenye upande wa bei za wananchi wa kawaida na zimekekwa ngazi mbalimbali za bei. Ni lengo la muda mrefu kwamba tutakapofikia hatua au tutakopofanikiwa kubadilisha mfumo wa uzalishaji ambao sasa hivi ni ghali mno na ambao ndio unaosababisha bei za umeme nazo kuendelea kuwa kubwa tutakapofikia uwezo wa kubadilisha mfumo huo na bei tunazotarajia kwamba zitashuka.

Nataka kutoa mfano mmoja tu kwamba katika maeneo yote ambayo tuna uzalishaji wa umeme usiouniganishwa na gridi unaotumia mafuta Shirika la *TANESCO* linatumia karibuni asilimia 37 ya mapato yake. Lakini inapata asilimia 7 tu na unaendeshaje maeneo haya kama si kwa kufidia maeneo mengine ya nchi na ndiyo maana pale tukasema bei za umeme zinakuwa ni za Kitaifa yaani za ujumla.

Kwa hiyo, ni suala kwa kweli la muda mrefu na ni sera ya Serikali na ni lengo la Serikali kuhakikisha kwamba tunafikia hapo. Ndiyo maana tunaharakisha katika kubadilisha mifumo ya uzalishaji umeme ili tuweze kufanikiwa. Halafu kuhusu migodi na kuwa na hisa. Hili ni jambo ambalo limezungumzwa katika taarifa ya Dr. Kipokola.

Nirejee tu kwamba taarifa ile itazingatiwa kwa ukamilifu. Lakini kuna jambo moja ambalo linapaswa pia kulifahamu. Kwamba hivi sasa kuna mgodi hapa nchini ambao Serikali ina hisa *Williamson* ina hisa asilimia 25. Unapokuwa na hisa unatakiwa pia uendane au utimize majukumu yanayoendana na kuwa na hisa.

Kwa hiyo, mgodi unapotaka kuwekeza kulingana na mpango wa maendeleo wa mgodi ukiambiwa uchangie na wewe inabidi uchangie. Ndiyo maana basi tukasema kwanza kwa upande mmoja kwa sababu Serikali imejitoa katika suala la kuingia kwenye biashara moja kwa moja. Lakini kwa upande mwengine kwa ajili ya wajibu huu tukasema ni vizuri tukavishawishi na kuvipa uwezo vyombo vyetu viingie katika kazi kama hii. Kwa mfano, *STAMICO* nimetoa mfano mwanzo, *TPDC, NDC* na kadhalika ili wao waweze kuingia na hasa katika ngazi za awali za utafiti ili waweze kuja kupata hisa katika uwekezaji na iwe rahisi wao kutuwakilisha sisi kama Taifa. Ni muhimu tunafahamu lakini napenda niseme tu hata kwa hali iliyoko hivi sasa hii migodi tumekuwa tukitoa takwimu mbalimbali hapa juu ya umuhimu ya hii migodi katika Taifa letu na katika suala zima la uwekezaji. Nadhani kama ambapo Mheshimiwa Waziri amesema nadhani sasa hivi ni nchi ya tatu Afrika katika uzalishaji wa madini.

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI: Mheshimiwa Mwenyekiti, labda tu Mheshimiwa Waziri aweze kufafanua kidogo si biashara. Unapokuwa na raslimali wewe tayari una mtaji.

MBUNGE FULANI: Eeeh, ndiyo!

MHE. DR. RAPHAEL M. CHEGENI: Sasa mimi sielewi anaposema ni biashara. Biashara gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa la msingi na hoja yangu ni kwamba kwa nini Watanzania wasimiliki ile migodi angalau kwa asilimia fulani. Hiyo ni sehemu yao ya mtaji wao. Mwekezaji alete fedha yake awekeze pale, halafu Mtanzania aweze kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nimeuliza suala kwamba Serikali imepata mapato kiasi gani kwa migodi hii *ku-change hands* yaani kubadilika kutoka kwa mmiliki mmoja kwenda kwa mmiliki mwengine. Hilo hajalijibu, naomba alijibu vile vile. (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimfafanulie ndugu yangu Mheshimiwa Dr. Raphael Chegeni kama ifuatavyo:-

Suala zima la raslimali na suala zima la umilikaji nililisema hapa wakati nasema kwa ujumla kwamba limo katika taarifa ya Dr. Kipokola. Nikasema kwamba Serikali italishughulikia kikamilifu. Nadhani pengine hakusikia wakati nazungumza hilo, lakini ndiyo ilikuwa jibu langu kwa maana ni hoja ambayo si kwamba hatuifahamu. Ni hoja nzito inafahamika lakini wakati umefika sasa wa kuchambua zile taarifa na kujua lipi ambalo linaweza likatekelezwa kwa wakati. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie kwamba

tunatilia maanani sana umuhimu wa umilikaji wa raslimali kwa mujibu wa taratibu zilizopo.

Kuhusu suala la kiasi gani kinapatikana. Mimi nadhani hili suala la takwimu. Mheshimiwa Dr. Chegeni atakuwa anafahamu kwamba *errors of fact* ni mbaya sana yaani kutoa takwimu ambazo sio sahihi. Kwa heshima yake na Bunge lako Tukufu ningependa tumpatие takwimu hizi mara baada ya Bunge lako ambazo ni sahihi kabisa.

MHE. LEONARD N. DEREFA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa pengine naona ndugu yangu Dr. Chegeni kama ameyauliza. Lakini na mimi labda nitayagusia. Mimi wakati nimechangia kwa maandishi ninaongelea kuhusiana na *vote 58 halafu sub-vote 1001* mshahara wa Waziri.

Nilikuwa nimeulizia masuala kuhusiana na kwamba je, katika uwekezaji wa madini misingi ya uzalishaji yaani *factors of production* ni kwamba kuna ardhi ambayo ndiyo *prime* halafu kuna mitaji ambayo ndio inakuja kutoka nje halafu kuna *labour* ile *entrepreneurior function*. Nilikuwa nimeulizia kwamba hivi kweli nchi yetu mtu anakuja anafanya vitu vyake hapa halafu sisi anatuachia takataka kwa kweli hii ni utaratibu gani, hivi nchi yetu haina thamani? Nilikuwa nataka nipelezo anaacha mashimo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, nilikuwa nimechangia kwa maandishi na bahati nzuri nimeambatanisha. Kuna baadhi ya wapiga kura wangu wa Shinyanga Mjini ambao *TANESCO* inawanyanyasa. Kuna Bwana mmoja anaitwa Issa Iddi Mrisho anadaiwa na *TANESCO* shilingi 1,317,759.50, halafu Juma Rashidi anadaiwa shilingi 442,591.56. Kassim Abdallah anadaiwa shilingi 358,272.95. Hawa watu hawana kiwanda kama *TANESCO* ilikuwa na uzembe iliwezaje ikaona mtu anadaiwa hizo hela na haikukata umeme halafu madeni haya wameyapeleka kwa mkusanyaji wa madeni ambayo kwa kweli anawanyanyasa kweli yaani hakuna amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kweli haya madeni ni madeni halali au ni ujambazi wa aina fulani wanataka kubabaisha watu wangu. Nilikuwa nimemwomba anieleze sababu hatuwezi kwa kweli namna hii ndiyo tunatafuta matatizo yaani mtu ana nyumba tu shilingi 1,317,754 halafu hana kiwanda walikuwa wapi hawa watu, kwa nini hawakukata umeme mpaka unafika shilingi milioni hizo sio ujambazi huo. Kwa hiyo, nilitaka niombe maelezo sababu namna hii ndiyo tunavunja amani ambayo tunaitangaza kila siku. Ahsante. (*Makofî*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nishati na Madini naomba kujibu maswali ya Mheshimiwa Leonard Derefa, kama ifuatavyo.

Naomba nianze na hili la mwisho ambalo amelizungumza kwa uchungu mkubwa sana suala la wapiga kura wake kunyanyaswa kama alivyosema ye ye na *TANESCO*. Napenda niseme kwamba si sera ya Serikali wala ya *TANESCO* kunyanyasa wateja na kama kuna mtu anawanyanyasa tumewaaagiza na tunawaagiza tena hapa sasa hivi *TANESCO* kufuutilia suala hili haraka na Mheshimiwa Mbunge tutakupa matokeo yake

hana hana Bungeni katika kipindi cha wiki hii. Lakini nataka nisisitize tu kwamba unyanyasaji wa raia kama uliyoyasema ndivyo ulivyo haukulaliki na tutalifuatilia kwa nguvu zote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili kuhusu mashimo yanayoachwa kwanza nataka niseme lile la msingi ambalo nimekuwa nikilirudia rudia. Ndugu zangu nataka muamini kwamba taarifa ile ya Dr. Kipokola itafanyiwa kazi. Lakini pia kama nyongeza tunao utaratibu wa kuhakikisha kwamba wachimba madini wanafuata utaratibu wa kutunza mazingira kiasi kwamba tumeanzisha mpaka utaratibu wa kupeana zawadi au kutoa zawadi ya Rais kwa Kampuni inayotunza mazingira vizuri. Kila mwenye mgodi anapoanzisha anatakiwa pia atoe mpango wa kulinda mazingira yaani *Environmental Impact Assessment*. Sasa haya ndiyo yanayofanyika.

Kuhusu faida zote kwa ujumla za madini nadhani kama nilivyosema awali hili ni suala pana zaidi na ambalo majibu yake kama nilivyosema tutalishughulikia kwa mujibu wa taarifa na ripoti ambazo zimeshapatikana.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts</i>	361,343,100/=
Kifungu 1003 - <i>Policy and Planning</i>	254,240,800/=
Kifungu 2001 - <i>Minerals</i>	2,890,527,100/=
Kifungu 2002 - <i>Madini Institute</i>	1,103,800,000/=
Kifungu 2003 - <i>Research and Laboratory Service</i>	1,150,241,500/=
Kifungu 2004 - <i>TANSORT London</i>	1,200,000,000/=

(*Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 3001 - *Energy and Petroleum*.... 21,675,550,200/=

MHE. DR. MILTON M. MAHANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hiyo *vote 58* programu 30. Wakati nachangia kwa maandishi niliulizia kuhusu mradi wa umeme kutoka Pugu kwenda Chanika na Mheshimiwa Waziri wala Naibu wake hakuweza kujibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chanika kwa kweli ukiacha kwamba suala la *DC* labda na utawala ni eneo ambalo limekuwa kama Makao Makuu ya Wilaya fulani fulani. Wakazi ni wengi pale ndio soko la mihogo yote kutoka Chanika, Msongola, Mvuti na Wilaya ya Kisarawe na Wilaya ua Mkuranga. Kwa kweli ni *centre* kubwa na wana matatizo makubwa sana ya umeme. Kwa miaka minne au mitano mradi ule umeshindwa kusogea kutoka pale Pugu kufika Chanika pamoja na kwamba mwanzoni wananchi walikuwa wamegoma kukata mazao yao lakini baadaye tumetafuta fedha kwa nguvu sana na kwa taabu tukapata milioni mbili na nusu tukawafidia wenyewe.

Lakini baada ya kuwafidia mwaka mzima na kitu *TANESCO* hawajatimiza ahadi ya kufikisha umeme Chanika. Nilitaka kujua na niliomba kwamba waniahidi Chanika watapata umeme kabla ya mwezi Oktoba mwaka huu. (*Makofî/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi huo wa umeme kama isingekuwa sababu ambayo na Mheshimiwa Mbunge mwenyewe ameigusia kwamba hapo awali palikuwa na watu kukataa kataa kidogo, ungekuwa pengine umeshatekelezwa miaka ya nyuma.

Lakini haikuwezekana kwa sababu hiyo na baadaye wananchi walipo kubali *TANESCO* nayo ikiwa uwezo wa kuutekeleza huu mradi haina. (*Makofî*)

Lakini napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi huu sasa uko katika mpango wa *ERT* kwa kuorodheshwa mahsusii sio kwa kutajwa.

Kwa hiyo, nadhani anaweza akitoka hapa na nadhani wananchi wa Jimbo lake wanasikia kwamba Mheshimiwa Mbunge amepata kauli hii kutoka Serikalini na najua amekuwa akilifuatilia hili sana, kwamba uko katika *ERT* mwakani.

(*Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 58 - Wizara ya Nishati na Madini

Kifungu 1001 - <i>Administration and General</i>	384,000,000/=
Kifungu 1003 - <i>Policy Planning</i>	100,000,000/=
Kifungu 2001 - <i>Minerals</i>	3,218,250,000/=

(*Vifungu vilichotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote*)

Kifungu 3001 - *Energy and Petroleum* 97,659,254,500/=

MHE. PHILIP S. MARMO: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, kwa ajili ya muda nilimwomba Mheshimiwa Waziri au Naibu wake anieleze zile fedha za *electricity IV* ya kilometra 22 iliyotengewa Wilaya ya Mbulu imepelekwa wapi? Ni kifungu hicho *sub vote 3001*.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niamini kwamba Mheshimiwa Philip Marmo anazungumzia suala ambalo amelizungumza nasi, la Kijiji cha Daudi na Dongobeshi, kama ndivyo hivyo kwa sababu amezungumzia Wilaya ya Mbulu tu, napenda niseme tu kwamba kwa ukweli kabisa kwenye mradi ule hapakuwa na fedha mahususi kwa ajili ile isipokuwa Mheshimiwa Mbunge aliahidiwa kwamba zingeweza zikatafutwa hapa na pale zikaweza kufanya kazi hiyo nasema kama anaulizia suala lile la maeneo yale ambayo nimeyataja.

Lakini kwa bahati mbaya baadaye fedha zile hazikupatikana lakini tumemwahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba mradi ule muhimu anaoutetea na ni haki yake kuutetea utashughulikiwa chini ya mpango huo ambao nimeutaja wa *ERT*. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira kama ambavyo amefanya huko nyuma katika kuhakikisha kwamba mradi huu unatekelezwa kuanzia hapo mwakani.

MHE. LEKULE M. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba na mimi kuulizia, nilipochangia nilisema kwamba Serikali imetoa muda mrefu ahadi kwamba umeme utapelekwa Namanga na Longido na kama hawakubali nilivyowafuata.

Je, Rais alipotoa ahadi kwa wananchi wa Longido kwamba watapatiwa umeme, miaka kumi imefika huu umeme haujapelekwa Longido, naomba Serikali inipe majibu kwamba huo umeme wa Longido unautaratibu gani? (*Makofi*)

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza napenda nimthibitishie Mheshimiwa Lekule Laizer kwamba maelekezo na maagizo na ahadi ya Rais yanakuwa ni maagizo ya kutekeleza kulingana na upatikanaji wa fedha.

Eneo alilolitaja Mheshimiwa Mbunge yapo maeneo mengine kama hayo hapa nchini ambayo Mheshimiwa Rais ameyataja na viongozi wetu wengine wakuu wameyataja na Wizara imekuwa ikifuatilia kwa karibu kuhakikisha kwamba ahadi hizi zinatekelezwa lakini kama ambavyo nimesema awali kutokana na hali ya kifedha ambayo imetokea hapa katikati haikuwezekana kutekelezwa na ndiyo maana Serikali au Wizara ikahakikisha kwamba inatafuta njia mbadala ya kutafuta ufadhili kutoka nje ili kutekeleza miradi hii mingi ambayo ama imeanza, haijaisha au kuna ahadai ambazo zimetolewa hazijatekelezwa.

Huu mradi ambao nimesema wanafadhiliwa na Benki ya Dunia. Kama nilivyosema uko katika kila Mkoa na katika Mkao ambako Mheshimiwa Mbunge anatoka hiyo sehemu ya Longido umo katika mpango wa *ERT*.

Nadhani walichotoka kufanya sasa hivi tulikuwa tunashauriana na Mheshimiwa Waziri kwamba pengine wakikamilisha ile orodha basi tuhakikishe tunawapatia Waheshimiwa Wabunge ili waweze kujua katika maeneo yao ni maeneo gani ambayo yatashughulikiwa na *ERT*.

MHE. STEPHEN M. KAZI: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho hicho nimejaribu kuchangia kwa maandishi na kuzungumzia suala la eneo ambalo limerukwa Mwanza kwenye kijiji cha Kishiri ambako mpaka sasa wangekuwa wameshafunga umeme, lakini sioni katika *provision* sijui ananielezaji juu ya jambo hilo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeomba angalau wawaarifu Ofisi ya Mwanza wachukue hatua kwenye jambo hilo kama liko ndani ya uwezo wa mara moja

NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ye ye mwenyewe alivyosema, kama inawezekana, kwa hiyo mimi nadhani tukimaliza hapa tutafuatana na Mheshimiwa Stephen Kazi kesho tuwasiliane na *TANESCO* tuone kama kuna uwezekanaao wa kufanya hiyo kazi ambayo amesema kulingana na uwezo uliopo.

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Matumizi bila mabadiliko yoyote)

(Bunge lilirudia)

T A A R I F A

WAZIRI WA NISHATI NA MADINI: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuwa Kamati ya Matumizi imepitia Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2005/2006, kifungu kwa kifungu na kuyapitisha bila mabadiliko yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu liidhinishe Makisio ya bajeti ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2005/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja (*Makofi*)

WAZIRI WA MAWASILIANO NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. (*Makofi*)

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Makadirio ya Wizara ya Nishati na Madini kwa mwaka 2005/2006
yalipitishwa na Bunge)*

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nilitaka tu kushauri upande wa Serikali, hii Kamati naoana inarudiwa rudiwa, hii Kamati tuliyomaliza inaitwa Kamati ya Matumizi. Kamati ya Bunge Zima ni ile wakati wa Miswaada, kwa hiyo naona wale wanaofuatia wakumbuke hilo.

Baada ya maelezo hayo sasa naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu kamili asubuhi.

*(Saa 01.39 usiku Bunge lilahirishwa mpaka siku ya Jumatano
Tarehe 13 Julai, 2005 saa tatu asubuhi)*